**Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA NNE

**Kikao cha Thelathini na Moja – Tarehe 27 Julai, 2006**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI**: Waheshimiwa Wabunge kikao chetu cha thelathini na moja kinaanza.

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI:**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):** Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Chuo cha Usimamizi wa Fedha kwa Mwaka 2004/2005 *(The Annual Report and Accounts of the Institute of Finance Management for the year 2004/2005)*

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba kwa Mwaka kwa Fedha 2006/2007.

**MHE. PINDI H. CHANA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA):** Maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba kwa Mwaka wa Fedha Uliopita, Pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2006/2007.

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI: (MHE DR. WILBROD P. SLAA):** Maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba kwa Mwaka wa Fedha Uliopita, Pamoja na Maoni Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2006/2007

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 287

**Siku ya Uchaguzi Mkuu Nchini**

**MHE. DKT. WILBROD P. SLAA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Ibara ya 65(1) ya Katiba ya Nchi imeweka kipindi cha uhai wa Bunge kuwa ni miaka 5; na kwa kuwa Uchaguzi Mkuu wa Tanzania mwaka 2005 ulifanyika siku ya Jumatano tarehe 14 Desemba, 2005 tofauti na chaguzi nyingine zilizowahi kufanyika na kwa kuwa siku hiyo haifungamani na siku yoyote ya Ibada kwa madhehebu ya Kikristo nay a kiislamu kwa maana ya Ijumaa, Jumapili, au siku ya Sabato na Watanzania wote walishiriki uchaguzi bila matatizo:-

(a) Je, Serikali imejifunza nini juu ya Uchaguzi Mkuu uliofanyika siku ya Jumatano, hasa ukizingatiwa kuwa sheria ya uchaguzi inataka vituo vifunguliwe saa 1 asubuhi muda ambao kwa kawaida watu wengi wamekuwa kwenye Ibada kwa maana ya watu kuwahi kufika vituo na kupiga kura kabla ya muda haujamlizika?

(b) Kwa kuwa miaka mitano ya uhai wa Bunge Kikatiba itaangukia siku ya Jumatano mwaka 2010 Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusu kuendelea na utamaduni huo mzuri wa kuwa na siku ya katikati ya juma (Jumatano) kwa ajili ya kupiga kura?

**NAIBU WAZIRI. OFISI YA MKUU, MAAFA NA KAMPENI DHIDI YA UKIMWI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Wilbrod Peter Slaa, Mbunge wa Karatu, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli Uchaguzi Mkuu wa Tanzania mwaka 2005, ulifanyika siku ya Jumatano tarehe 14 Desemba, 2005 kwa mujibu wa Sheria ya uchaguzi Na. 1 ya mwaka 1985. Sheria inatamka bayana kwamba Tume ya Taifa ya Uchaguzi, itapanga tarehe ya uchaguzi sio chini ya siku sitini na sio zaidi ya siku tisini tangu uteuzi wa wagombea ulipofanyika. Kwa kutilia maanani kwamba siku za katikati ya wiki siku za kazi, imekuwa utamaduni wa kupanga siku ya kupiga kura kuwa siku ya Jumapili.

Utaratibu huo umeendelea kwa chaguzi nyingi bila tatizo lolote. Watanzania waliokuwa na haki ya kupiga kura waliweza kujipangia saa na kuhudhuria ibada na pia muda wa kupiga kura bila matatizo yoyote. Uchaguzi uliopitia, uliandaliwa katika utaratibu huo na ilipangwa tarehe 30 Oktoba, 2005. Siku hiyo ilibadilika, baada ya kutokea kifo cha Mgombea Umakamu wa Rais kupitia CHADEMA. Uchaguzi uliahirishwa kwa mujibu wa Sheria ya Uchaguzi na Tume kupanga siku ya Jumatano tarehe 14 Desemba, 2005. Ili kuwezesha Watanzania kupiga kura zao ilibidi Serikali itangaze siku hiyo kuwa ya mapumziko. Hata hivyo, Serikali haitarajii kutumia utaratibu huo kwa kuwa hakuna sheria ya nchi inayotaja siku ya upigaji kura kuwa siku ya mapumziko.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wanajua kwamba siku ya mwisho wa uhai wa Bunge hili ndio mwanzo wa kupiga hesabu za kujua siku ya uchaguzi wa Bunge na Rais imeweka taratibu za kufuata ili kupanga siku hiyo na imetoa mamlaka ya kupanga siku ya Uchaguzi kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba majukumu ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi yako bayana, ni vizuri taratibu hizo zikafuatwa na kuiachia Tume ipange siku hiyo, ikizingatiwa kuwa kuna mambo mengi ya kutilia maanani, kwa mfano upatikanaji wa vifaa vya kupigia kura na kuvisambaza kunakohusika.

**MHE. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili madogo aidha namshukuru sana ndugu yangu, Naibu Waziri kwa majibu yake. Kwa kuwa Waziri ameeleza kwamba tatizo ni sheria, au sheria iliyoko ndivyo inayvotamka na kwa kuwa sheria ni kitu cha kusaidia wananchi kutekeleza majukumu yao vizuri, na kwa kuwa uzoefu wa mwaka huu umeonyesha watu wameenda kupiga kura katikati ya wiki siku ambayo haina madhara mengine yoyote, na wakapiga kura hiyo kwa utulivu mkubwa zaidi.

Je, Serikali iko tayari kutafakari, nakuona kupata mawazo ya nchi kama siku hiyo ya katikati ya wiki ni siku nzuri zaidi?

La pili kwa kuwa taratibu za tume kweli zinajulikana na Tume ndio inayofanya na kupanga siku ya uchaguzi, lakini kwa kuwa Tume pia inapaswa kuzingatia maoni ya wananchi, na kwa kuwa katika kuuliza swali hili nilitafuta baadhi ya maoni ya wananchi. Je, Tume sasa iko tayari kusikiliza maoni ya wananchi, ili kuweze kufikia uamuzi, kutokana na maoni ya Watanzania?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana ya Naibu ningependa kujibu ifuatavyo, ni kweli uchaguzi wa mwaka jana kumekuwa na mabadiliko ya tarehe za kupiga kura, na ni kweli mwaka jana tumepata uzoefu tofauti kuliko tulivyoupata miaka mingine ya nyuma. Lakini kama nilivyosema kwenye swali lingine hapa ndani, kwamba bado Serikali inaendelea na kujaribu kuona namna gani bora, na siku gani bora ya kupiga kura. Lakini pamoja na majibu hayo nipende tu kusema kwa miaka 40 mfululizo hatujawa na matatizo. Sasa inatupa matatizo kama Jumapili, ni tatizo kwa madhehebu fulani, Jumamosi bado ni tatizo kwa dhehebu lingine, Ijumaa ni tatizo kwa dhehebu lingine, sasa hatujui Jumatano pengine dhehebu lingine, sasa tutaendelea kufanya uchambuzi kuona ni siku gani nzuri.

Lakini kwa sababu kwa miaka 40 hatujawa na tatizo, hapo sisi ndio tutakuwa mahala pa kuanzia, niwahakikishie, nimwakikishie Mheshimiwa Mbunge na Watanzania wote kwa ujumla kwamba Serikali haina nia kuwaletea bughudha katika kupiga, tunataka wapige kura, siku ambayo wote wametulia, siku ambayo haina tatizo, lakini tutafanya uchambuzi kama jibu likiangukia jumapili, tutaomba watusamehe. Kama jibu litaangukia Ijumaa, tutaomba radhi, lakini nia ni kila mtu aweze kupiga kura kwa uhuru na bila wasiwasi wowote.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kuniona, kwa kuwa uchaguzi wa mwaka wa 2005 uliahirishwa kutokana na matatizo ya Mwenyezi Mungu, na mwenzetu aliyetangulia mbele ya haki. Lakini kwa kuwa utaratibu wa uchaguzi, mara nyingi unakuwepo siku ya jumapili katika mwezi wa 10, ambapo uhai wa Bunge na Rais, huwa ni miezi 60.

Je, kwa kuwa uchaguzi huu ulifanyika Desemba, Serikali inasemaji ju ya uhai wa Bunge pamoja na Rais, utakuwa ni miezi 60 au utakuwa umeongezeka?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana ilikuwa ni dharura, na wote tuliona ni dharura, tulipata bahati mbaya ya kufiwa na mmoja wa wagombea, hatimaye tukalazimika kufuatana na taratibu zetu, kubadilisha tarehe.

Mimi siamini kama lile litakuwa la wakati wote hapana, na kwa mwaka jana Waheshimiwa Wabunge ambao walikuwepo wakati ule waliona nini kilifanyika kwa upande wa Serikali, na mimi naamini kwa wale ambao walikuwa Wabunge, hawana malalamiko yoyote kwa hali tuliyofanya mwaka jana.

Lakini narudia tena, utaratibu utaangaliwa ambao utahakikisha kwamba mambo yanakwenda vizuri kwa kadri inavyotakiwa yaende. Mimi siamini kila mwaka tutakuwa na dharura, lakini ikitokea basi tutaangalia wakati huo wa dharura itapojitokeza. Lakini nchi itakwenda vizuri na wala mtu asiwe na wasiwasi.

Na. 288

**Tume ya Waziri Mkuu**

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR** aliuliza:-

Kwa kuwa, Tume ya Waziri Mkuu Mstaafu iliyoongozwa na Mwenyekiti Mheshimiwa Omar Shaaban Kwaangw' ilibainisha baadhi ya kero kama vile mishahara midogo, ukosefu wa likizo, walimu kukosa vitambulisho vya Bima, walimu kutopewa posho ya kujikimu wanapokuwa wamesafiri kikazi na madai mengine.

(a) Je, tangu Tume hiyo itoe taarifa yake ni kwa kiasi gani matatizo hayo yamepungua?

(b) Je, ni lipi kubwa ambalo mpaka leo Serikali haijalitekeleza?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mzee Ngwali Zuber Mbunge wa Mkwajuni lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Tume ya Mheshimiwa Omar Kwaangw' ilibainisha kero mbalimbali za walimu. Baada ya Tume hiyo kutoa taarifa yake, Serikali imechukua hatua mbalimbali kupunguza matatizo ya walimu. Matatizo yaliyobainiswa ni pamoja na kutolipwa fedha za uhamisho, masomo, matibabu, uhamisho wa mara kwa mara ambao hauna msingi wowote na mengineyo. Matatizo hayo kwa kiasi kikubwa yameshughulikiwa kama mlivyoona kwa miaka ya hivi karibuni malimbikizo mbalimbali ya walimu yamelipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu tatizo la madai ya walimu kulimbikizwa, maagizo yafuatayo yalitolewa na Serikali:

- Halmashauri ziliagizwa kuhakikisha kuwa zinatenga fedha zitakazokidhi mahitaji ya walimu kwa ajili ya likizo, matibabu, kujikimu, masomo ili kuepuka malimbikizoya madeni kwa watumishi na walimu pia. Kutokana na maelekezo hayo Serikali imeongeza fedha za ruzuku ya matumizi mengine.

- Aidha, Wakurugenzi watendaji wa Wilaya, Miji/Manispaa/Majiji wameagizwa kutotumia au kulipa fedha kwa matumizi mengine kutoka vifungu vya fedha za elimu vilivyotengwa kwa ajili ya huduma za walimu.

- Aidha, Halmashauri zilitakiwa kutohamisha walimu kiholela bila sababu za msingi ili kupunguza gharama. Aidha kila mtumishi atakapohamishwa ni sharti alipwe haki zake za uhamisho.

- Vilevile Serikali imewachukulia hatua za kinidhamu kwa Wakurugenzi na Maafisa Elimu waliobainika kutumia vibaya fedha zilizotengwa kwa ajili ya Elimu. Pia suala la Mfuko wa Bima, Serikali imewasiliana na wahusika ili kuweka mkakati maalum utakaopunguza malalamiko ya wanachama ikiwa ni pamoja na kusogeza mfuko wa bima karibu na vijiji ambako wanachama wengi wapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo ya walimu wakiwemo watumishi wengine ni ya kiutendaji na Serikali inaendelea kuyashughulikia kama nilivyoeleza hapo juu. Aidha kama ilivyo kwa watumishi wengine Serikali inaangalia upya viwango vya mishahara. Suala hili linashughulikiwa ili kuona uwezekano wa kurekebisha mishahara ya watumishi wote. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza kwenye kipengele cha hapo juu, (a) hakuna tatizo lolote ambalo Serikali haijalishughulikia kabisa. Serikali imeziagiza Halmashauri kutolimbikiza madai ya watumishi wote, pia Wizara inafuatilia Halmashauri zitakazoendelea kulimbikiza madai ya watumishi na kuchukua hatua kwa maafisa wahasibu. Tume iliyoundwa na Rais kushughulikia suala la mishahara kwa watumishi ni hatua mojawapo ya Serikali ya kuangalia kero za watumishi ikiwa ni pamoja na walimu.

Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, yaliyoainishwa kwenye Tume hiyo yameshughulikiwa na yanazidi kushughulikiwa hatua kwa hatua.

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini tatizo bado lipo. Kwa kuwa wakurugenzi wengi bado hawajakamilisha au hawatimizi agizo la Serikali kuwa wasitumie vibaya fedha za walimu ambazo zinapelekwa katika Halmashauri, lakini bado zinatumika vibaya fedha hizi kwa wakurugenzi hawa.

Je, Mheshimiwa Waziri haoni kuwa hatua ambazo wamewachukulia wakurugenzi hao bado wengine hawajasikia wanaendelea na suala kama hili?

Swali lingine, kwa mfuko wa Bima kweli upo lakini walimu wa vijini bado wanasumbuka na vitambulisho na vitu vya afya viko mbali na maeneo ambayo wanaishi. Je, kwa hili Mheshimiwa Waziri atalizungumziaje, kuhusu hili ambalo walimu wasisumbuke katika kufuatilia huduma ya afya wakati wanapougua?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu kwamba tatizo la walimu lipo, kama tulivyokubali kwamba tatizo bado lipo. Lakini hatua mbalimbali zilichokuliwa nafikiri zitaweza kupunguza baadhi ya kero, kwa mfano Wakurugenzi wote wameshaandikiwa barua kwamba wahakikishe kwamba hakuna malimbikizo ya aina yoyote, na baadhi ya wakurugenzi wameshachukuliwa hatua kama mnavyoona. Baadhi ya maafisa elimu wanazidi kuchukuliwa hatua za kinidhamu, pamoja na hatua za kisheria, kama mlivyoona na mnavyosikia kwenye vyombo vya habari. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hayo yote tunayafahamu na tunayafuatilia kwa karibu, ili kupunguza kero mbalimbali kama sio kuzimaliza kabisa.

Kuhusu mfuko wa bima, ni kwamba suala hili tunalifuatilia na tunafahamu kwamba kweli walimu na wafanyakazi wengi walioko vijijini wanapata shida kuhusu kufuatilia huduma za bima, lakini suala hili linafuatiliwa kwa karibu, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunalifuatilia, tunalifahamu na tutatekeleza hatua kwa hatua ili kupunguza kero ya walimu pamoja na watumishi wengine. *(Makofi)*

Na. 289

**Utunzaji wa Kumbukumbu na Nyaraka za Masijala**

**MHE. ANNA R. LUPEMBE** aliuliza:-

Kwa kuwa, kwa miaka mingi walimu wa shule za msingi na sekondari wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi wamekuwa wakilalamika kuwa Idara hua Masijala haitunzi nyaraka zao vizuri na hazifikishwi kunakotakiwa kwa wakati:-

(a) Je, Serikali itarekebisha vipi tatizo hilo ambalo ni kero kubwa sana kwa walimu hasa wanapodai haki zao?

(b) Je, Serikali haioni kuwa watumishi hao wanastahili kuondolewa/kuadhibiiwa wanaohusika na kero hiyo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Anna Lupembe, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa kuw ana kumbukumbu sahihi siyo tu za watumishiwake, bali pia kumbukumbu za masuala yote ya Umma. Kwa kutambua hili, Serikali kwa kupitia Bunge lako Tukufu, ilitunga Sheria ya Utunzaji wa Kumbukumbu na Nyaraka (*Records and Archives Management Act)* Na. 3 ya mwaka 2002 kwa lengo la kuzipa uwezo zaidi ofisi za Umma kusimamia Utunzaji wa Kumbukumbu hai, tuli na zisizotumika kabisa.

Aidha, Serikali kupitia programu ya kuboresha utendaji kazi katika Utumishi wa Umma, imeanzisha mfumo mpya ya utunzaji kumbukumbu ambao tayari umeshaanza kutumika. Serikali pia imehusisha na kuboresha muundo wa Utumishi wa Maafisa kumbukumbu kwa lengo la kuimarisha na kuboresha taaluma ya utunzaji wa kumbukumbu katika ofisi za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa maelezo haya, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Anna Lupembe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ni miongoni mwa Wizara zilizopewa kipaumbele katika jitahada za kuweka mazingira mazuri ya kupunguza kero ya utunzaji na upatikanaji wa kumbukumbu na nyaraka za walimu katika Masijala ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, ambapo hatua zifuatazo zimechukuliwa:-

(i) Kuchambua na kuondoa katika masijala majalada ya watumishi ambao hawako katika utumishi ili kubaki na majalada hai.

(ii) Kuhuisha kumbukumbu na nyaraka muhimu za watumishi kwa kuzingatia picha za elektroniki (*Scanning*) ili ziweze kupatikana kwa urahisi pale zinapohitajika kwa ajili ya maamuzi mbalimbali yanayohusu mtumishi wakati akiwa kazini na anapostaafu.

(iii) Kutoa mafunzo kwa watumishi wa Wizara ili waweze kutumia mfumo mpya wa utunzaji kumbukumbu.

Wizara nyingine ambazo zipo katika mpango huu ni pamoja na kilimo cha Ushirika, Maliasili na Utalii, Afya na Ustawi wa Jamii, Idara ya Mahakama, na Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Zoezi hili ni la kudumu na litafanyika kwa awamu hadi Wizara, Idara zinazojitegemea na Taasisi zote za Serikali zitakapokuwa na mfumo bora wa utunzaji kumbukumbu na nyaraka.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya 2002, kifungu cha 6(1)(b) kifungu kidogo (3) waajiri wamepewa mamlaka kamili ya kuajiri na kushughulikia masuala ya nidhamu kwa watumishi walio chini yao.

Hivyo, nawahimiza waajiri wote kushughulikia watumishi wote wazembe kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu zilizopo. Kwa kufanya hivi tutaimarisha uwajibikaji katika Utumishi wa Umma.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante Naibu Waziri kwa kunijibu swali langu nzuri, kwa kuwa watumishi wakija kutoka mikoani wanaangaika sana Wizarani wanaangaika, wanapata kero.

Je, Serikali ina mikakati gani kurekebisha kero hizo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu katika jibu langu msingi kwamba waajiri wamepewa mamlaka ya kushughulikia masuala ya nidhamu, ikiwa ni pamoja na uzembe.

Kwa hiyo, kwa wale wote ambao wanafika katika Wizara na wakawa wanazungushwa au hawashughulikiwi kwa wakati, bado wanao viongozi, kuna viongozi katika Wizara hizo ambao wanaweza wakawaona na wakawaelezea matatizo yao ili waweze kushughulikiwa.

Na. 290

**Rushwa Katika Nchi**

**MHE. PONSIANO D. NYAMI** aliuliza:-

Kwa kuwa, lengo la Serikali kuanzisha chombo cha *PCB* ni kupambana na madhara ya rushwa nchini;

(a) Je, mpaka sasa ni mikoa mingapi na ipi ambyao inaongoza kwa vitendo vya rushwa na ni ipi inayoongoza kwa kiwango cha chini katika tatizo la rushwa?

(b) Je, ki-uwiano ni kundi lipi kati ya watumishi wa juu, kati, chini, viongozi na wananchi wanaoongoza kwa vitendo vya rushwa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nyami, Mbunge wa Nkasi, swali lake lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Kulingana na takwimu za TAKURU kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka 2003 hadi 2005, Hali ya Rushwa nchini inaonyesha kama ifuatavyo:-

Mwaka 2003, Idara zilizokuwa zinaongoza kwa kulalamikiwa ni Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa yaani Halmashauri za Jiji, Miji na Wilaya zikifuatiwa na Jeshi la Polisi, Mahakama, Elimu na Afya. Mwaka 2004, Idara zilioongoza ni Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa yaani zilizoongoza ni Tawala za Mikoa yaani Halmashauri za Jiji, Miji na Wilaya, Jeshi la Polisi, Elimu, Mahakama na Sekta Binafsi.

Mwaka 2005, Tawala za Mikoa na Serikali za mitaa yaani Halmashauri Jiji, Miji na Wilaya ziliongoza, zikifuatiwa na Jeshi la Polis, Mahakama, Elimu na Vyama vya Siasa. Aidha, takwimu za 2005/2006 zinaonyesha kuwa mkoa uliokuwa unaongoza kwa kupokea malalamiko mengi kuhusiana na vitendo vya rushwa ni Kagera 558 na mkoa uliokuwa na idadi ndogo ya malalamiko ni Kigoma 35.

Mikoa mingine ambayo malalamiko yalipokelewa ni kama ifuatavyo:-

Shinyanga malalamiko 485, Mkoa wa Mwanza tulipokea malalamiko 331, Mkoa wa Mtwara tulipokea malalamiko 331 pia, Mkoa wa Tabora tulipokea malalamiko 312, Mkoa wa Tanga malalamiko 284, Mkoa wa Iringa malalamiko 249, Mkoa wa Morogoro malalamiko 248, Mkoa wa Dar es Salaam malalamiko 239, Mkoa wa Ruvuma malalaniko 202, Mkoa wa Pwani malalamiko 196, Mkoa wa Mbeya malalamiko 191, Mkoa wa Mara malalamko 187, Mkoa wa Arusha malalamiko 180, Mkoa wa Manyara malalamiko 86 na Mkoa wa Lindi malalamiko 76.

Idadi ya malalamiko yaliyopokelewa Makao Makuu kutoka kwa watu binafsi, Idara na Taasisi mbalimbali bila kuzingatia mikoa yaliyotoka yalikuwa ni malalamiko 59.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo kuna malalamiko mengi ya rushwa dhidi ya Mikoa au Idara siyo kigezo sahihi kuwa Mikoa au Idara hizo zinaongoza kwa kupokea rushwa kwani huenda ikawa kipimo kimojawapo kuwa ni wananchi katika maeneo hayo

wana uelewa mkubwa zaidi kuhusu haki zao na wana ujasiri wa kutoa taarifa dhidi ya watumishi wanaojihusisha na vitendo vya rushwa. Pia nyakati nyingine matukio ya makosa ya kawaida ya jinai yanayoweza kushughulikiwa na Polisi pia huwasilishwa kwa Taasisi ya Kuzuia Rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na takwimu za malalamiko au tuhuma za rushwa zilizokwisha kuchunguzwa tangu mwaka 2003 kiuwiano kundi la Watumishi wa kati na chini ndiyo wanaoongoza kwa vitendo vya rushwa, hii inatokana na malalamiko au tuhuma za wananchi kuhusu huduma zinazotolewa na Watumishi na Idara hizo.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina maswali mawili ya nyongeza.

La kwanza, kwa kuwa rushwa haiwezi kumalizika kwa kutegemea Serikali peke yake na kutegemea Sheria ambazo tunazitunga katika Bunge hili je isingekuwa vizuri kwa Serikali sasa kutumia madhahebu mbalimbali ya dini na kuyawezesha ili wafanya kazi hiyo sambamba na maamuzi yetu ya Serikali?

La pili, kwa kuwa taasisi ya Kimataifa inayoitwa *Transparent International* imeeleza wazi katika tovuti mbalimbali ya kwamba Tanzania inaoongoza katika rushwa kubwakubwa na hii inatokana na mikataba ambayo inakuwa ni ya siri na *tenders* zenyewe ambazo hazieleweki.

Kutokana na hilo Serikali itakubali ya kwamba ili kusafisha na kulipa Taifa letu jina zuri hasa katika awamu hii ya nne, Serikali kuanzia sasa mikataba iwe inapitia katika Bunge hili ili kujenga sifa ya nchi hii?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Paul Kimiti, Mbunge wa Sumbawanga Mjini, kama ifuatavyo:-

Kwanza baada ya Serikali ya awamu ya tatu kuunda Tume ya Jaji Joseph Warioba ilichukua uamuzi wa kuunda Kitengo cha Utawala Bora katika Ofisi ya Rais Ikulu Kitengo ambacho kinaratibu matukio yote yanayohusiana na rushwa nchi nzima.

Kitengo hicho sasa kinapanuliwa ili kiweze kupata taarifa kutoka mashirika yasiyo ya Kiserikali ikiwa ni pamoja na madhahebu kama alivyosema, makampuni ya biashara, Halmashauri mbalimbali kwa kuunda Vitengo vya Maadili katika maeneo hayo.

Swali la pili la Mheshimiwa Paul P. Kimiti kuhusu taarifa ya Taasis ya Kimataifa isiyo ya Kiserikali *Transparency International* yenye Makao yake makuu kule Berlin kwamba Tanzania inaongoza katika rushwa kubwakubwa, napenda kusema kwamba pamoja na kumheshimu sana Ndugu yangu Kimiti kwamba hii siyo kweli hata kidogo.

Katika Afrika Tanzania ni mojawapo katika nchi ambayo inadhaniwa kwamba pamoja na kwamba kuna rushwa lakini huwezi ukalinganisha na nchi nyingine za Afrika katika Kanda hii ya Afrika Mashariki na Kanda ya *SADC* kwa ujumla wake na ndiyo maana mashirika yote makubwa ya Kimataifa yamekuwa yakichukulia Tanzania kama nchi ya mfano katika kupambana na rushwa na ishara mojawapo ni kwamba hivi karibuni Mheshimiwa Rais wetu aliombwa kwenye Umoja wa Mataifa kuzindua kitabu cha Utawala Bora katika Karne ya 21na kupambana na Rushwa kwa kutambua jitihada zetu. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge kabla hatujahamia Wizara ya Maliasili na Utalii niwafahamishe kwamba leo tuna maswali mengi kuliko kawaida kwa hiyo nitaomba maswali mafupi na majibu mafupi ili tuweze kumaliza.

Tunahamia Wizara ya Maliasili na Utalii, kwa hiyo sasa namwita Mheshimiwa Herbert Mntangi.

Na. 291

**Wananchi Kufaidika na Mauzo ya Mitiki**

**MHE. HERBERT J. MNTANGI** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali imetangaza tenda ya ununuzi wa magogo ya miti aina ya TIKI iliyopandwa zaidi ya miaka 15 iliyopita katika Shamba la Longuza, Tarafa ya Amani Wilaya ya Muheza na kwa kuwa eneo hilo pia lina mito mikubwa na midogo inayotoka katika vyanzo vya maji ndani ya Hifadhi ya Msitu wa Amani, mfano Mto Ziggi.

(a) Je, Serikali imeandaa utaratibu gani utakaowawezesha wananchi wanaoishi karibu na eneo la msitu huo wanufaike na mauzo ya miti hiyo walioshiriki kuipanda na kuitunza?

(b) Je, kuna mpango gani wa kupanda miti baada ya mavuno ya sasa kwa nia ya kuhifadhi mazingira na mito inayopita kwenye eneo hilo?

(c) Je, Wanakijiji walishirikishwa vipi katika mpango mzima wa uvunaji wa msitu huo ulioanza hata kabla tenda haijatengazwa?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii naomba kujibu swali la Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mbunge wa Muheza, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mashamba ya Mitiki ya Longuza yalipandwa wakati wa Serikali ya Kikoloni mwaka 1959 na baada ya Uhuru mnamo mwaka 1961. Mashamba hayo yana ukubwa wa hekta 2,400. Tarehe 10/02/2006 na tarehe 11/02/2006 Wizara yangu kupitia magazeti ya *The Guardian*, Uhuru na Majira ilitangaza kuuza kwa zabuni miti ya Mitiki iliyopo kwenye shamba la Longuza yenye meta za ujazo 26,218.871 katika eneo lenye ukubwa wa hekta 98. Wananchi wanaoishi karibu na msitu wa Longuza wamekuwa wakipata manufaa mbalimbali kutokana na Msitu huo, kama vile ajira na elimu ya kustawisha miti aina ya mitiki, mpaka sasa wamepanda mitiki ambayo imewapatia manufaa makubwa baada ya kuiuza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upandaji miti utafanyika katika sehemu zote ambazo zitavunwa katika msitu wa Longuza. Upandaji miti baada ya kuvuna ni sehemu mpango wa muda mrefu wa Shamba la Miti la Longuza kama ilivyo kwa mashamba mengine ya miti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanaoishi karibu na eneo la msitu huo wataendelea kupata ajira kutokana na shughuli za uvunaji, kushiriki katika uuzaji na uvujani katika eneo maalum litakalotengwa kwa ajili ya wananchi wa kawaida na wenye mitaji midogo na watayatumia matawi ya miti hiyo kama kuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla tenda ya uvunaji wa mitiki kutanganzwa ambayo ilikuwa tarehe 10/02/2006 na tarehe 11/02/2006 kama nilivyoeleza awali miti iliyovunwa haikuwa mitiki bali ni Terminalia ambayo iliuzwa kwa taratibu za kawaida za kufuata *Management Plan* kwa miti iliyofikia muda wake wa kuvunwa.

Wizara haitauza miti ya Longuza kwa wafanyabiashara wakubwa pekee. Sehemu mbalimbali zimetengwa katika shamba hilo ambalo miti yake itauzwa kwa wananchi wenye mitaji midogo. Miti hiyo itauzwa kwa vikundi, vijiji au watu binafsi watakaoleta maombi yao kuonyesha nia ya kuuza hiyo mitiki.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na ninaomba nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyoyatoa. Hata hivyo nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Kama alivyoeleza Mheshimiwa Naibu Waziri inaonekana wananchi wale wananufaika tu kwa suala la ajira lakini ajira ni wajibu wao kwa sababu wanatumia nguvu zao vilevile wanatumia muda wao kupata kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo ningeomba Mheshimiwa Waziri atusaidie kama atakuwa anafahamu ni kiasi gani ambacho kimetengwa kwa ajili ya kuwawezesha wananchi wale wenye kipato kidogokidogo kuweza kuvuna lakini vilevile anisaidie kutambua ni Halmashauri ya Wilaya ya Muheza pamoja na Serikali za Vijiji vinavyolizunguka eneo lile watanufaika vipi na mauzo ya magogo hayo hasa ukizingatia kwamba Wizara hiihii huwa inatoa 5% kwa wananchi mbalimbali wanaoishi katika maeneo ya mashamba ya Mbuga za Wanyama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili ni kwamba Wizara hii ya Maliasili na Utalii bado inadaiwa fidia kubwa na wananchi wanaoishi katika eneo hilohilo la Longuza ndani ya Kata ya Kisiwani.

Je, Mheshimiwa Waziri anaweza akanithibitishia kwamba baada ya mauzo hayo atatenga fedha ili kulipa fidia kwa wananchi hao ili kuondoa kero inayowasumbua?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Herbert Mntangi kama ifuatavyo:-

Kiasi kilichotengwa kwa ajili ya wananchi na wenye mitaji midogomidogo yote iko katika *Management Plan* ya Shamba hilo. Katika *Management Plan* imewekwa kwamba miti hiyo itauzwa kwa awamu pia itauzwa tena kwa *tender* kwa watu ambao wana mitaji mikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Mntangi baada ya kipindi hiki Ofisini nimwonyeshe ile *Management Plan* na kiasi ambacho wananchi watauziwa kwa sababu ipo katika awamu mbalimbali.

Vilevile amependa kufahamu iwapo wananchi wana madai wataweza kulipwa. Ningependa kumfahamisha Mheshimiwa Mntangi kwamba hivi karibuni mwezi huu katika madai ya fidia tayari imeshapelekwa milioni 150 ambayo italipwa kama fidia kwa wananchi hao na sehemu iliyobaki ni mategemeo ya Wizara yangu kulipa mapema iwezekanavyo ili tuweze kumaliza kero hiyo, tunajua ni haki ya wananchi kupata fidia yao.

Kuhusu kunufaika kwa wananchi kutokana na mauzo ya mitiki ni kweli kwamba wananchi wanaoishi karibu na mapori ya asili wanapata asilimia fulani. Lakini hawa wanaoishi karibu pembeni na mashamba ya Serikali mpaka sasa hivi hakuna mpango wa kuweza kuwapa asilimia ya mauzo ya miti, hata hivyo ni wazo zuri tumelipokea na tutalifanyia kazi.

Na. 292

**Mahitaji ya Umeme Vijijini**

**MHE. JACOB DALALI SHIBILITI** aliuliza:-

Kwa kuwa, umeme ni muhimu sana kwa maendeleo ya wananchi na pia ni Nishati nzuri inayozuia uharibifu wa mazingira na kwa kuwa, tayari nguzo za umeme ziliisha simikwa toka kijiji cha Inolelwa kupitia Buhingo, Seeke, Nyamayinza, Mbalama, Isesa na Nyang'homango hadi Ihelele kwenye mradi wa Maji kwenda Kahama na Shinyanga.

(a) Je, ufungaji wa waya za umeme ambazo zipo tayari utaanza lini?

(b) Je, vijiji nilivyovitaja vitafaidika na umeme huo?

(c) Je, baada ya hapo vijiji jirani na hivyo navyo vitapatiwa umeme?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Jacob Dalali Shibiliti, Mbunge wa Misungwi, naomba nitoe maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji alivyovitatja Mheshimiwa Mbunge vipo kwenye njia ya umeme iliyopimwa na Mkandarasi wa Kichina anayefanya kazi katika mradi wa maji wa Ihelele. Kutokana na mahitaji makubwa ya umeme katika mitambo ya Ihelele umeme ambao ulitegemewa kutokea kijiji cha Inonelwa hadi Ihelele usingetosha mpaka kijengwe kituo cha kupoza umeme Mabuki chenye uwezo wa *kV 220/33, MVA/15.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango ya sasa ni kutoa umeme kutoka kituo cha umeme cha Bulyanhulu kwa kuongezea transfoma ya *MVA 10* na kujenga njia ya umeme kupitia Nyamtukuza na kuweka waya maalum chini ya ziwa na kufikisha umeme kwenye pampu za maji za Ihelele. Inategemewa kuwa njia za awali ya Inonelwa na Ihelele itajengwa na kukamilika mara baada ya kitu kipya cha umeme kujengwa katika kijiji cha Mabuki.

Baada ya maelezo hayo sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge lenye sehemu a, b na c kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza hapo awali, kazi hii itatekelezwa baada ya kupata fedha za ujenzi wa kituo cha Mabuki. Vijiji alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge pamoja vijiji vilivyo jirani vitafaidika na umeme huo mara baada ya ujenzi kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango ya utekelezaji wa mradi wa umeme kati ya Bulyanhulu kupitia Nyamtukutuza hadi kwenye pampu ya maji ya Ihelele inaendelea na tayari Wizara ya Maji ilitangaza Zabuni za ujezi.

Hata hivyo kati ya kampuni tano zilizobainishwa ni kampuni mbili tu zilizowasilisha mapendekezo yake baada ya tathmini ya zabuni kufanyika kampuni moja ilichaguliwa na kampuni hiyo ilipatiwa *Letter of Acceptance* wiki iliyopita. Kwa sasa kampuni iliyochaguliwa inasubiriwa kuleta maoni yake ili kuwezesha mkataba wa ujenzi wa njia hiyo ya umeme usainiwe.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru tu Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo nina imani yamewatia moyo wananchi wa maeneo niliyoyataja ya Buhingo, Nyamahinza mpaka Ihelele kwamba pindi kituo kitakapojengwa Mabuki watanufaika na sehemu hizo.

Sasa ningependa niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, kutoka Mwanza kuja Usafara kipo kijiji kimoja cha Nyangomango kina matatizo makubwa ya umeme na kinahitaji nguzo kati ya 12 hivi ili kuweza kupata umeme.

Je, Naibu Waziri ananiahidi nini kwa wananchi wa Nyangomango katika kijiji hiki?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Shibiliti kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi la Mheshimiwa Mbunge tumelipokea tungeomba kwamba Mheshimmiwa Mbunge awasiliane na Ofisi yetu aje tukae naye tuongee ili tuweze kuangalia namna ya kuweza kushughulikia mpango huu.

Na. 293

**Mahitaji ya Umeme Solwa.**

**MHE. AHMED ALLY SALUM** aliuliza:-

Kwa kuwa, moja kati ya majukumu ya Serikali ni katika kuboresha na kuendeleza maisha ya vijijini pamoja na kupeleka miundombinu mbalimbali ikiwemo umeme ili kurahisisha, kukuza kilimo na biashara, na kwa kuwa Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne aliahidi kupeleka umeme kwa wananchi wa Jimbo hili:-

Je, ni lini umeme utaanza kupelekwa Solwa kama Mheshimiwa Rais alivyoahidi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ahmed Ally Salum, Mbunge wa Solwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Shirika la Umeme (*TANESCO*) ina mpango wa kupeleka umeme katika Jimbo la Solwa kuptia mpango wa *Energizing Rural*

*Transformation* yaani *(ERT).* Mradi huu utafadhiliwa na Benki ya Dunia na Serikali ya Tanzania. Majadiliano na Benki ya Dunia kwa lengo la kukamilisha masharti yaliyowekwa na Benki bado yanaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa kupeleka umeme Solwa utahusisha ujenzi wa laini ya Kilovoti 33 ya kilomita 60, na kujenga njia ndogo ya umeme ya voti 400 yenye urefu wa kilomita 10. Kazi nyingine ni uwekaji wa *transfoma* mbili za kupotea, moja ya *KVA 50* na nyingine ya *KVA 100.* Gharama ya mradi huu inakadiriwa kuwa shilingi milioni 970.

**MHE. AHMED ALLY SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri katika Kata ya Samuye umeme umepita vizuri sana lakini wananchi wa pale hawana umeme na hasa hasa Kituo cha Afya cha Samuye hakina umeme kwa muda mrafu sana na kinahudumia Tarafa nzima ya Kata ya Samuye. Vilevile katika Kata ya Tinde kuna hule ya Sekondari ya Kituli haina umeme kwa muda mrefu sana na ina wanafuzi wengi sana.

Je, ningependa kujua Wizara kwa nini isipeleke umeme sana kwenye maeneo haya husika kabla ya mpango wa *IRT* kuanza?

Mpango huu wa *IRT* katika Jimbo la Solwa utaanza lini na itapita katika Kata zipi za Jimbo la Solwa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ahmed Ally Salum, Mbunge wa Solwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilivyoeleza katika jibu langu la msingi Serikali itapeleka umeme katika Jimbo la Solwa kwa kupitia mpango wa *IRT* na maeneo yote ambayo ameyataja ni maeneo ya muhimu kama vile maeneo yote mengine katika Jimbo la Solwa na tutahakikisha chini ya Mpango wa *IRT* umeme huo utafika.

Ameuliza umeme wa *IRT* utafika lini katika Jimbo la Solwa. Upelekaji wa umeme Solwa umepangwa kuanza katika awamu ya tatu ya mradi wa *IRT* ambao unategemewa kuanza katika mwaka wa fedha wa 2009/2010.

Kata ambazo zitapata umeme, ni kama ifuatavyo umeme utapita njia ya *Old Shinyanga* na kupitia Kata ya Shilabela, Iselemagazi na Solwa. (*Makofi*)

Na. 294

**Upatikanaji wa Tiketi za Shirika la Reli**

**MHE. MOHAMED RAJAB SOUD (K.n.y. MHE. HAFIDH ALI TAHIR)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Watanzania wanayo haki ya kuishi sehemu yoyote wanayotaka ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa kuwa, pamoja na maeneo mengine katika Jimbo la Dimani wapo watu kutoka Mikoa ya Shinyanga, Tabora na Mwanza ambao hupata usumbufu mkubwa wanapohitaji kwenda makwao kutokana na urasimu wa upatikanaji wa tiketi kutoka Shirika la Reli Tanzania.

Je, Serikali haioni kwamba wakati umefika sasa Shirika hilo kufungua Ofisi yake Zanzibar ili kuwezesha watu kupata tiketi zao huko badala ya kusafiri hadi Dar es Salaam kuweka *booking* na kurudi Zanzibar na baadaye kurudi Dar es Salaam kwa ajili ya safari?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, Mbunge wa Dimani, kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa, Shirika la Reli liko katika hatua za mwisho za ukodishwaji, tunaahidi kuyapeleka mawazo ya Mheshimiwa Mbunge kwa mkodishaji ili aweze kuyapa uzito unaofaa. (*Makofi*)

Na. 295

**Huduma ya Vyoo Barabarani.**

**MHE. DR. HARISSON G. MWAKYEMBE** aliuliza:-

Kwa kuwa, mtindo wa kusimamisha mabasi ya safari ndefu njiani na kuwataka abiria washuke Kuchimba Dawa porini umeshamiri na kuzoeleka kama suala la kawaida katika jamii na kwa kuwa mtindo huu unawashirikisha watoto wadogo, wengine kwa mara ya ya wkanza katika maisha yao kwenda haja ndogo na kubwa na wazazi wao au watu wazima pamoja, hivyo kumomonyoa polepole heshima na maadili ya Kiafrika kati ya watoto na watu wazima.

(a) Je, Serikali haioni kuwa muda umefika kwa wenye mabasi ya safari ndefu ambao vyombo vyao vyao vya usafiri havina vyoo ndani kuchangia ujenzi wa vyoo na

utunzani wake kwenye vituo kadhaa vya barabarani ili kuliondolea taifa tabia hii ya aibu ya Kuchimba Dawa kiushirika?

(b) Je, kwa nini Serikali haiweki kama sharti kwa wajenzi wa vituo lukuki vya mafuta kandokando mwa barabara zote kuu nchini kujenga idadi maalum ya vyoo kama huduma ya lazima ya biashara yao kwa ajilii ya abiria na watu wote wanaosafiri kwa magari?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Harisson George Mwakyembe, Mbunge wa Kyela, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwamba kuna umuhimu wa kujenga vyoo kwa ajili ya kuhudumia abiria wanaosafiri safari ndefu za mabasi pamoja na kulinda heshima, maadili na mazingira yetu kwa ujumla, badala ya mtindo wa Kuchimba Dawa Porini.(*Makofi*)

Kama ilivyo kwa Mataifa yaliyoendelea ambayo yanajenga vyoo na maengesho kwa ajili ya abiria wanaosafiri, nchi yetu tayari imeanza kuiga tabia ambapo kwenye mipango yake ya ujenzi wa barabara inapanga kujenga vyoo. Kwa mfano, kwenye barabara ya Makuyuni – Ngorongoro yenye urefu wa kilometa 77, vyoo vitatu vimejengwa. Serikali itajitahidi kutekeleza mpango wa ujenzi wa vyoo na tayari wahandisi wa *TANROARDS* na wa Wizara wameelekezwa kuzingatia suala hili katika kuchora barabara zote mpua za lami na changarawe na kitaifa ili kuondoa aibu na kumpatia msafiri raha na maisha bora.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la kushauri vituo vya mafuta kujenga au kupanua huduma hiyo, Wizara itawasiliana na mamlaka zinazotoa vibali vya ujenzi wa vituo hivyo ili ushauri huu uweze kuizingatiwa.

Na. 296

**Maendeleo Duni kwa Wakulima wa Mikoa ya Kusini**

**MHE. MOHAMMED SAID SINANI** aliuliza:-

Kwa kuwa, maendeleo ya uchumi wa Wakulima wa Mikoa ya Kusini yapo duni sana kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo ile ya kuwa mstari wa mbele katika vita vya kuwakomboa nduguzetu wa Msumbiji, na kwa kuwa, wananchi hao ambao wengi wao ni wakulima ambao wanashindwa kumiliki zana za kilimo kama Matrekta na kadhalika:-

Je, Serikali itawasaidiaje wananchi hao kuinua hali zao za maisha kwa kuwapatia hizo zana za kisasa za kilimo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Said Sinani, Mbunge wa Mtwara Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuwawezesha wakulima nchini kupata zana bora, wakiwemo wa Mikoa ya Kusini, Serikali kupitia Mfuko wa Taifa wa Pembejeo inatoa mikopo yenye masharti nafuu kwa wakulima kwa ajili ya kununua matrekta mapya na zana zake. Kiwango cha chini cha mkopo ni shilingi milioni 35 ambacho hutakiwa kurejeshwa katika kipindi cha miaka mitatu kwa riba ya kati ya asilimia 8 hadi 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia mwaka 2003/2004 hadi 2005/2006, jumla ya matrekta 96 yenye thamani ya shilingi bilioni 3.1 yamekwisha kukopeshwa kwa nchi mzima. Kati ya hayo matrekta 11 yamekopeshwa kwa taasisi ya watu binafsi katika Mikoa ya Kusini.

Kwa mfano, dayosisi ya Anglikana, Jimbo la Masasi imepata mkopo wa matrekta matatu na zana zake zenye thamani ya shilingi milioni 105 na Dayosisi ya Jimbo Kuu la Songea imepata mkopo wa matrekta matano yenye thamani ya shilingi milioni 114 ili kuanzisha vituo vya kukodisha matrekta. Serikali pia imetoa mikopo yenye thamani ya shiligni 85.7 milioni kwa watu binafsi kutoka Wizara za Mikoa ya Mtwara na Ruvuma kwa ajili ya kununulia matrekta na zana zake ili waweze kulima katika mashamba yao na kuwakodishia wengine.

Aidha, wakulima binafsi kutoka Mkoa wa Ruvuma wamepatiwa mikopo ya kukarabati matrekta yao yenye thamani ya shilingi 10.5 milioni. Hivyo jumla ya shilingi milioni 315 zimekwisha kutolewa kwa mkopo katika kuwawezesha wakulima wa Mikoa ya Kusini kupata zana bora za kisasa.

Serikali pia imekarabati vituo 55 vya maksai katika Wilaya mbalimbali nchini. Vituo vinavyoendelea kukarabatiwa katika mikoa ya Kusini ni Chipuputa (Masasi), Lilungu (Mtwara Mjini), Lilambo (Songea Vijijini), Utiri (Mbinga) na Masonya (Tunduru). Vituo hivi vimepatiwa zana mbalimbali na wakulima walio jirani na vituo hivyo wanaendelea kpaa mafunzo juu ya matumizi ya zana bora. Jumla ya shilingi milioni 46 zimetumika katika kuendeleza mpango wa matumizi ya wanyamakazi katika Mkoa hiyo ya Kusini. Aidha, vikundi 8 vyenye wakulima 210 vimefadhiliwa na mradi wa PADEP katika Wilaya ya Masasi na vimepatiwa zana za wanyamakazi zenye thamani ya shilingi milioni 16.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa 2006/2007, Serikali itaanza kutoa mikopo ya kununua zana zinazokokotwa na wanyamakazi kupitia Mfuko wa Taifa wa Pembajeo. Vifaa vitakavyopatiwa mikopo ni pamoja na plau, mikokoteni, ripa, majembe ya palizi na matuta.

**MHE. ABDULKARIM ESMAIL HASSAN SHAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa, Wizara ya Kilimo imejitahidi sana kupeleka baadhi ya vituo vya ukodishaji wa matrekta katika Wilaya nilizozitaja je hivi sasa ina mpango gani wa kupeleka vituo kama hivyo katika baadhi ya Wilaya ambayo haijapeleka hususan Mafia ambayo imetengeka kijiografia na ambayo kwa kipindi kirefu haijapata miradi mingi zaidi ya ule mradi wa afya wa Mabusha na Matende?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA(MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Shah Mbunge wa Mafia kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeeleza hapa katika majibu yangu kwamba Mfuko huu wa Taifa wa Pembejeo unatoa mikopo mbalimbali pamoja na ile ya pembejeo za kilimo, kununulia matrekta pamoja na ukarabati wa matrekta madogo na utaratibu wa upatikanaji wa wa mikopo hii ni kuomba kutitia kwenye Halmashauri zinazohusika na kwa hiyo ningemwomba tu Mheshimiwa Mbunge ashirikiane na Halmashauri yake ya Mafia na kushirikiana na Wizara yetu ya Kilimo,Chakula na Ushirika kuweza kuwela maombi na sisi tutakuwa tayari kuyashughulikia.

Na. 297

**Mawasiliano ya Simu za Mkononi**

**MHE. RAYNALD A. MROPE** aliuliza:-

Kwa kuwa mawasiliano ya simu za mkononi yameonekana kuwa ya muhimu sana, kwa kila mtu; na kwa kuwa mitandao ya simu hizo imesambaa sehemu nyingi hapa nchini:-

(a) Je, kwa nini Serikali isifute kabisa kodi ya ongezeko la thamani *(VAT)* inayotozwa kwa simu hizo wakati zinapoingizwa nchini ili kutimiza mojawapo ya malengo ya maisha bora kwa kila Mtanzania?

(b) Kwa mantiki hiyo hiyo, je kwa nini Serikali isipunguze kiwango cha kodi ya mauzo (*Sales Tax*) kinachotozwa kwa watumiaji wa huduma hiyo muhimu ili iweze kupatikana kwa urahisi katika maeneo mengi zaidi hapa nchini?

(c) Je, kwa nini Serikali isiwawezeshe wawekezaji wa ndani ili nao waweze kutoa huduma hiyo muhimu badala ya kuwaachia wawekezaji wa nje pekee kama ilivyo sasa?

**WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Raynald A. Mrope, Mbunge wa Masasi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na umuhimu wa mawasiliano, siyo busara kufuta kabisa Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)* inayotozwa kwa simu za mkononi zinapoingizwa nchini na kisha kuomba fedha kutoka kwa wahisani kwa ajili ya kuendesha mipango yetu ya Serikali. Katika kipindi cha Julai, 2005 hadi mwezi Aprili, 2006, Serikali imekusanya jumla ya shilingi milioni 7,817 kama *VAT,* mapato ya shilingi milioni 13,761 kama ushuru wa bidhaa kutoka makampuni ya simu za mkononi. Kwa kutumia kigezo cha kodi hiyo iliyokusanywa katika kipindi hicho, ni wazi kwamba endapo Serikali itafuta kodi hizo, itakuwa imejikosesha mapato yasiyopungua shilingi milioni 21,580 na hivyo italazimika Serikali kuendelea kuomba misaada zaidi kutoka kwa nchi wahisani. Ni vizuri Serikali ikakusanya kodi hizo na kisha kuzitumia kueneza mawasiliano katika Wilaya na hata vijijini ili kutimiza moja ya malengo ya maisha bora kwa kila Mtanzania.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inauona umuhimu wa kuwapatia wananchi simu za mkononi (*cellular phone handsets*) kwa gharama nafuu na urahisi wa upatikanaji wa huduma hiyo katika maeneo mengi zaidi. Ili kutoa unafuu wa kodi Serikali ilifuta Ushuru wa Forodha wa asilimia 25 uliokuwa unatozwa kwenye simu za mikononi mnamo mwaka 2003/2004.

Hata hivyo, kwa kuzingatia ukweli kuwa tunahitaji kupanua vianzo vyetu vya mapato ya ndani, uagizaji au ununuzi wa simu za mkononi hauna msamaha wa kodi ya *VAT* ya asilimia 20 na ushuru wa bidhaa kwa matumizi ya simu hizo (*air-time*) ambapo kiwango cha sasa ni asilimia 5. Kiwango hiki kinakusudiwa kuongezwa hadi kufikia asilimia 7. Wenzetu Kenya na Uganda wanatoza kodi ya ushuru wa bidhaa (*air-time*) wa asilimia 10. Kwa hiyo, Tanzania bado inatoza kodi kidogo ukilinganisha na wenzetu ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kutambua umuhimu wa mawasiliano imekuwa ikitoa vivutio mbalimbali katika sekta hii muhimu kama vile msamaha wa Ushuru wa Forodha kwa bidhaa zote (*capital goods*) zinazoagizwa na makampuni ya simu za mkononi kwa ajili ya uwekezaji, hii ikiwa ni pamoja na vifaa vya kusafirisha na kupokea mawimbi (*Transmission and Teception Apparatus*) kwa ajili ya kueneza mawasiliano kwa wateja wao. Kwa bahati mbaya au nzuri wawekezaji wengi waliojitokeza kuwekeza katika sekta hii ni wawekezaji wa kigeni. Ni azma ya

Serikali kuona kuwa wawekezaji wa ndani nao wanaweza kuwekeza si katika sekta hii tu, bali pamoja na sekta nyinginezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa uwekezaji huu unahitaji mitaji mikubwa, Serikali imejizatiti katika kuweka miundombinu muhimu, kutoa vivutio mbalimbali kwa wawekezaji na kuweka mikakati ya uwekezaji kupitia sera zake mbalimbali, ikiwemo Sera ya Uwezeshaji.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Pamoja na majibu marefu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ningependa tu kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, biashara duniani sasa hivi inafanyika zaidi kwa kutumia mtandao wa *Internet,* na kutokana na gharama kubwa za simu katika nchi yetu hasa *VAT*. Inakuwa vigumu Mikoani kuweza kutumia *Internet* kwa sababu ukichukulia mfano wa *TTCL* ina-*charge* shilingi 50,000 kwa mwezi na ukiangalia nchi nyingi zina-*charge* si zaidi ya shilingi 10,000. Je, kwa mtaji huu Tanzania kweli itaweza kushindana katika biashara huria?

**WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali hilo tunalipokea tutalifanyia kazi na tutamjibu kwa maandishi.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yameisha na muda wetu wa maswali umeisha. Naomba nitoe matangazo yafuatayo:-

Tangazo la kwanza, mtaona *Speakers Gallery* tunao wageni pale ikiwa ni pamoja na Majaji wanne wa *Law Reform Commission* kama wapo wanaweza kusimama. Tunawashukuru. *(Makofi)*

Pia nimeambiwa kwamba kuna Makamishna wa Tume ya Haki za Binadamu lakini sijawaona. Nimeambiwa kuwa Majaji wawili wa Mahakama Kuu hapa Dodoma. Karibuni. Pia nimeambiwa wako Wakuu wa Idara katika Mahakama Kuu Kanda ya Kati hapa Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Baada ya hapo, kuna taarifa ya Kikao kutoka kwa Mheshimiwa Gideon Cheyo Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi kwamba Wajumbe wa Kamati yake wakutane leo Alhamisi kuanzia saa 5.00 asubuhi, kikao hicho kitafanyika katika ukumbi wa Kamati namba 227 ghorofa ya pili.

Waheshimiwa Wabunge kwa ujumla mwakilishi wa Kampuni ya Magari ya Toyota yupo hapa anapatikana chumba Namba 8. Kwa wale wadau wanaombwa kufika hapo baada ya saa 7.00 mchana.

Pia ningeomba kumtambulisha Mheshimiwa Diwani Sinamudi kutoka Kata ya Mlali, Kongwa ambaye ni mgeni wa Mheshimiwa George Lubeleje. Karibu sana. *(Makofi)*

Pia tunao vijana wa kutoka Shule ya Sekondari ya Kikuyu vijana 50 na walimu wao watatu ambao ni wageni wetu. Mnaweza kusimama. Karibuni sana. *(Makofi)*

Nitakaowataja wanaombwa baada ya saa 7.00 mchana wakutane hapo nje na Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa shughuli maalum ambayo wameagizwa kuifanya. Hawa ambao nitawataja Mheshimiwa Joel Bendera, Mheshimiwa Abdulkarim Shah, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Lawrence Masha, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Anna Lupembe, Mheshimiwa William Ngeleja, Mheshimiwa Janeth Massaburi na Mheshimiwa Mohammed Soud. Saa 7.00 nje hapo.

Tangazo la mwisho, kutoka kwa Mheshimiwa Joel Bendera Kocha wa Bunge *Sports Club*. Anawataka wachezaji wa Timu ya Bunge kuendelea na mazoezi kwa bidii kwa maandalizi ya mechi mbili muhimu. Siku ya Jumamosi tarehe 29 Julai, 2006 mechi itakayokuwa kwenye Uwanja wa Mgambo Mpwapwa na tarehe 5 Agosti, 2006 mechi itakayofanyika katika uwanja wa Kongwa Mjini.

Mheshimiwa George Lubeleje anawaomba wakazi wa Ving'hawe, Mazai na Ilolo katika Mji wa Mpwapwa kuja kuona jinsi ambavyo timu ya Bunge ilivyo na uwezo mkubwa wa kucheza kandanda. *(Makofi)*

Lakini vilevile tunawaomba wananchi wa Kongwa wafurike tarehe 5 Agosti, 2006 kuwaona Waheshimiwa Wabunge wanavyoweza kucheza mpira wa miguu. Baada ya matangazo hayo, tunaendelea.

Waheshimiwa Wabunge, samahani, wako watoto wa Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, simameni hapo mlipo, wako wawili pale. Karibuni sana. *(Makofi)*

Katibu hatua inayofuata kwenye *Order Paper.*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2006/2007
### Wizara ya Katiba na Sheria

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na Taarifa iliyowasilishwa mapema leo Bungeni na Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, naomba kutoa hoja kwamba Bunge sasa likubali kujadili na hatimaye kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria, kwa mwaka wa fedha 2006/2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kueleza maudhui ya hotuba yangu, naomba nitumie fursa hii kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kumpongeza Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Awamu ya Nne. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM) Taifa. Napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Rais kwa imani yake kwangu kwa kuniteua kuiongoza Wizara hii nyeti yenye kusimamia haki ambayo ni msingi wa maendeleo na uelewano ndani ya taifa. Nampongeza pia Rais Mstaafu Mheshimiwa Benjamin William Mkapa kwa kuongeza nchi yetu na kuweka misingi imara kwa Serikali ya Awamu ya Nne. Namtakia afya njema na maisha marefu. Wahenga walisema imani huzaa imani, nami naahidi kulitumikia Taifa kwa kumsaidia kwa uaminifu mkubwa Rais wa awamu ya nne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuitumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Sheni kwa kuchaguliwa kwake kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na pia kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Amani Abeid Karume kwa kuchaguliwa tena kuwa Rais wa Zanzibar kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza rasmi Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, kwa kuteuliwa kwake na Rais kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, uteuzi ambao ulithibitishwa kwa kura nyingi za kihistoria na Bunge hili Tukufu. Aidha, nampongeza Waziri Mkuu Mstaafu Mheshimiwa Frederick Tluwaye Sumaye kwa kazi nzuri aliyoifanya kwa kipindi chote cha uongozi wake katika Awamu ya Tatu. Nawatakia viongozi wetu wote hao kheri na fanaka katika utekeleza majukumu yao katika safu za juu kabisa za uongozi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Spika, Mheshimiwa Samuel Sitta na Naibu Spika Mheshimiwa Anna Makinda, Mbunge wa Njombe kwa kuteuliwa kwake kushika nafasi hiyo akiwa Mbunge mwanamke wa kwanza kushika wadhifa huo katika historia ya Bunge letu. Mwenyekiti Jenista Mhagama. Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukupongeza wewe kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti na leo kukalia kiti wakati nawasilisha hoja yangu. Uongozi wenu hauna mashaka. Pongezi nyingi ningependa

kuzitoa kwa Wabunge wote wa kuchaguliwa na wa kuteuliwa. Ninapenda kuwaambia kuwa wote tuko katika Jahazi moja la kuleta maendeleo, hivyo nawaahidi ushirikiano wangu wa dhati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wenzangu na Naibu Mawaziri wote kwa kuteuliwa kwao kuziongoza Wizara walizokabidhiwa. Uwezo na uzoefu wao utaendelea kuimarisha utendaji na uwajibikaji ndani ya Serikali na taasisi zake. Napenda kwa namna ya pekee kumpongeza na kumshukuru Naibu Waziri wangu kwanza kwa kushinda katika Jimbo lake na kwa uteuzi wake na kwa msaada wake kwangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru wananchi wa Hanang, kwa kunichagua kwa kura nyingi sana kuwa Mbunge wao. Ushirikiano walionipa wakati wa kampeni na uchaguzi. Tutauendeleza katika kuleta maendeleo ya Jimbo letu ili kila mmoja wetu awe na maisha bora. Vilevile ninawashukuru kwa dhati wanawake wa Mikoa ya Arusha na Manyara kwa kunichagua kama Mbunge wao wa Viti Maalum kwa vipindi viwili mfululizo tangu mwaka 1995 hadi mwaka 2005 na kwa upendo wao kwangu hadi leo. Sitapenda kuisahau familia yangu akiwemo mume wangu Profesa Joseph Nagu na watoto wetu pamoja na Ndugu na Marafiki. *(Makofi)*

Mwisho, si kwa umuhimu napenda kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Fatma Maghimbi, Msemaji Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria kwa upande wa Upinzani. *(Makofi)*

Kabla ya kuelezea majukumu ya Wizara napenda nieleze muundo wa Wizara ya Katiba na Sheria. Ninafanya hivyo kwa sababu muundo wa Wizara unayo nafasi kubwa ya kurahisisha utekelezaji wa majukumu yake. Inafaa Waheshimiwa Wabunge wauelewe ili waweze kuichangia hotuba hii na kutoa mapendekezo yatakayotusaidia kuboresha utendaji wetu katika kufanikisha malengo muhimu ya Serikali kama yalivyowekwa kwenye Katiba ya Nchi na yaliyofafanuliwa vizuri na Mheshimiwa Rais katika hotuba yake wakati wa uzinduzi wa Bunge hili tarehe 30 Desemba, 2005. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni nchi inayofuata misingi ya demokrasia na haki ya kijamii kwa mujibu wa Katiba yetu. Misingi hiyo inatekelezwa kwa kuzingatia kwamba:-

(a) Wananchi ndio msingi wa mamlaka yote, na Serikali itapata madaraka na mamlaka yake yote kutoka kwa wananchi kwa mujibu wa Katiba hii;
(b) Lengo kuu la Serikali litakuwa ni ustawi wa wananchi;
(c) Serikali itawajibika kwa wananchi; na
(d) Wananchi watashiriki katika shughuli za Serikali yao kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii.

Ili misingi hiyo ya demokrasia na haki ya kijamii iweze kutekelezwa kwa dhati, Katiba inataka vyombo vyote vya Serikali kuelekeza sera na shughuli za vyombo hivyo kuhakikisha malengo 11 yaliyoainishwa katika Ibara ya 9 ya Katiba yamefikiwa kikamilifu. Aidha, vyombo hivyo vinapaswa kuhakikisha kwamba utekelezaji wa shughuli zake unazingatia amani, utulivu na umoja wa Kitaifa ili kukuza na kudumisha heshima ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli na mipango yote ya Serikali inaelekezwa katika kufikia malengo yake muhimu kama yalivyowekwa kwenye Katiba. Ili malengo hayo yaweze kutekelezwa na vyombo vya Serikali kwa manufaa yanayotarajiwa si budi vyombo hivyo viwe na muundo unaorahisisha utendaji bora na uwajibikaji. Wizara yangu inashughulikia masuala mtambuka kwa sekta zote za Serikali, hivyo muundo wake unasaidia utekelezaji wa majukumu ya Serikali nzima. Bila shaka Bunge lako litakubaliana nami kwamba muundo wa Wizara hii ni wa kipekee kwa kuwa unajumuisha taasisi kadhaa zinazojitegemea na zilizo huru kiutendaji kama ifuatavyo:-

(a) **Mahakama ya Tanzania.**

Mahakama ya Tanzania ni moja ya mihimili mitatu ya dola yenye mamlaka ya kutekeleza utoaji haki. Chombo hiki kinasimamiwa na Jaji Mkuu. Ngazi mbalimbali za Mahakama ya Tanzania ni kama ifuatavyo:-

(i) Mahakama ya Rufani ya Tanzania;
(ii) Mahakama Kuu inayojumuisha Masjala ya Mahakama Kuu, Kitengo cha Mahakama ya Biashara kinachoshughulikia mashauri ya biashara na Kitengo cha Mahakama ya Ardhi kinachoshughulikia migogoro ya ardhi;
(iii) Mahakama za Hakimu Mkazi;
(iv) Mahakama za Wilaya; na
(v) Mahakama za Mwanzo.

Aidha, katika kuendesha shughuli za Mahakama, yupo Msajili wa Mahakama ya Rufani, Msajili wa Mahakamu Kuu na Wasajili wengine. Vilevile zipo Kurugenzi mbili ambazo ni Kurugenzi ya Mahakama za Mwanzo na Kurugenzi ya Mahakama ya Wilaya hadi Mahakama ya Rufani.

(b) **Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali**

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inajumuisha pia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali yenye Idara saba, Idara tano kati ya hizo zikiwa ni za Kitaaluma ambazo ni:-

(i) Kurugenzi ya Mashtaka;
(ii) Idara ya Madai na Sheria za Kimataifa;
(iii) Idara ya Uandishi wa Sheria;
(iv) Idara ya Katiba na Haki za Binadamu; na
(v) Wakala wa Serikali wa Usajili, Ufilisi na Udhamini "*Registration Insolvency and Trusteeship Agency" (RITA)* iliyokuwa Idara ya kabidhi Wasii Mkuu wa Serikali.

(c) **Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kila mmoja wetu anavyofahamu, haki za binadamu zinafuatana na wajibu wa mwananchi. Hakuna haki bila wajibu kama kusivyokuwa na wajibu bila haki. Mambo hayo mawili yamewekwa wazi katika Katiba yetu. Kama ilivyo kwa 'mpiga kasia', akipiga kasia lake upande mmoja tu wa mtumbwi wake, mtumbwi hautasonga mbele, bali utazunguka hapo hapo alipo. Mtumbwi utasonga mbele kama atapiga kasia sehemu zote za kulia na kushoto za mtumbwi. Kulia ni haki, na kushoto ni wajibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ni uhamasishaji wa Hifadhi ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Katika kutekeleza jukumu hilo, Tume hupokea malalamiko na kufanya uchunguzi kuhusu ukiukwaji wa haki za binadamu na wajibu kwa jamii kwa mujibu wa sheria za nchi. Lengo lake ni kujenga misingi ya utawala bora na kutoa ushauri kwa Serikali na vyombo vya umma na sekta binafsi kuhusu Haki za Binadamu na Utawala Bora. Aidha, katika eneo hili Wizara ina jukumu la kujenga taswira nzuri ya nchi yetu katika Jumuiya ya Kimataifa kwa kuandaa taarifa za mwenendo wa Haki za Binadamu hapa nchini na kuziwasilisha katika Baraza la Umoja wa Mataifa.

(d) **Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania**

Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu jingine la Wizara yangu linahusu Utafiti wa Sheria mbalimbali unaofanywa na Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania. Baada ya kufanya utafiti, Tume hutoa mapendekezo ya kutungwa kwa Sheria mpya; kufutwa kwa sheria ambazo zimepitwa na wakati au kutoa mapendekezo ya marekebisho ya sheria hizo ili ziendane na wakati. Aidha, Tume inalo jukumu la kutoa elimu ya sheria kwa jamii, kutoa ushauri na kupendekeza sheria zinazolinda maslahi ya Taifa.Zipo Idara za kutoa huduma katika Mahakama, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Tume zote mbili; ambazo ni Idara ya Utawala na Utumishi; Sera, Mipango na Habari; na vitengo vya Uhasibu na Ukaguzi wa Ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dira ya Wizara. Wizara inaongozwa na dira yake ya "Haki Sawa kwa Wote na kwa Wakati." Dira hii inalenga kuleta demokrasia na Haki katika Jamii, Usawa na Utawala wa Sheria, mambo ambayo yatatokana na kuwepo kwa huduma bora za kisheria kwa wananchi zinazopatikana kwa wote na kwa wakati. Wizara pia inasimamia na kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025 (*National Development Vision 2025*), Dira ambayo inalenga na kusisitiza kuwepo kwa Sheria madhubuti zinazosimamia raslimali na

umiliki wake, shughuli za uzalishaji mali na mgawanyo wa mapato, kujenga utamaduni wa uwajibikaji, ushirikishwaji pamoja na kupiga vita rushwa na maovu mengine katika jamii. Aidha, Dira, inalenga katika kujenga utawala bora, kuheshimu na kuhifadhi Haki za Binadamu kama zilivyoainishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hivyo kuleta na kudumisha amani, utulivu na umoja miongoni mwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wajibu wa taasisi na asasi katika sekta ni kuhakikisha kwamba haki za kimsingi za binadamu na haki za kisheria zinapatikana kwa wote kwa wakati na kwa usawa. Katika kutekeleza utoaji haki mambo yafuatayo yanahitajika:-

(a) Utoaji wa haki ufanyike kwa wakati;
(b) Kupatikana kwa huduma za Kisheria kwa gharama nafuu;
(c) Kuwa na watumishi na wataalam wenye maadili ya hali ya juu; na
(d) Kuwa na mfumo wa utoaji haki wenye kuzingatia na kushiriki mabadiliko na mahitaji ya jamii katika nyanja ya siasa, uchumi, teknolojia na jamii.

Iwapo hayo yote yataweza kufanyika kikamilifu, yatavifanya vyombo vya utoaji haki nchini viwe kimbilio la kila mtu mwenye kiu ya haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Majukumu ya Wizara. Majukumu ya Wizara yangu yanalenga katika kutekeleza matakwa ya Katiba, Dira ya Taifa ya 2025 ya Wizara na Ilani za Uchaguzi. Kwanza, lipo jukumu la utoaji haki, ambalo linasimamiwa na Mahakama ya Tanzania. Mashauri yote ya madai na ya jinai husikilizwa na kutolewa uamuzi katika ngazi mbalimbali za Mahakama kuanzia Mahakama ya Mwanzo hadi Mahakama ya Rufani, ambayo ndiyo Mahakama ya Juu kwa ajili ya kutolewa maamuzi. *(Makofi)*

Pili, yapo majukumu mbalimbali yanayotekelezwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Majukumu hayo 11 yameainishwa kwenye Sheria ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya mwaka 2005 ambayo ni:-

(a) Kutoa ushauri wa kisheria kwa Serikali na taasisi zake;
(b) Uandishi wa sheria;
(c) Kusimamia na kuendesha mashtaka;
(d) Kuiwakilisha au kuitetea Serikali inapodaiwa au inapodai Mahakamani;
(e) Kushiriki katika majadiliano ya mikataba inayoihusu Serikali;
(f) Kutoa ushauri kwa Wizara, Idara na Taasisi nyingine za Serikali;
(g) Kuendesha mashauri ya Kikatiba Mahakamani;
(h) Kuisimamia Serikali katika chunguzi zinazohusiana na malalamiko ya uvunjaji wa Haki za Binadamu zinazowasilishwa kwenye Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora;
(i) Kuratibu masuala ya Katiba na Haki za Binadamu;

(j) Kusimamia masuala ya mirathi, kuandikisha vizazi na vifo, usajili wa ndoa na talaka, ufilisi, kusajili wadhamini, udhamini wa mali isiyokuwa na mwenyewe, uasili wa watoto na kadhalika; na

(k) Kuandaa, kuwasilisha na kutetea taarifa za mwenendo wa Haki za Binadamu nchini Tanzania katika mabaraza mbalimbali ya Haki za Binadamu ya Umoja wa Mataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu mengine ya Wizara yangu ni kufanya utafiti kuhusu Sheria mbalimbali zinazohusu jamii ya Kitanzania na hatimaye kuchapisha taarifa zenye mapendekezo kuhusu njia bora za kulinda, kuhifadhi jamii na kuendeleza maslahi ya Taifa letu.

Aidha, Wizara inatoa elimu ya sheria kwa wananchi kupitia Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania. Kwa kupitia Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Wizara imeendeleza jukumu la kuhamasisha na kuhifadhi haki za binadamu pamoja na kulinda misingi ya utawala bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Changomoto zinazoikabili Wizara. Ingawa Wizara yangu imejitahidi kutekeleza dira yetu na majukumu kwa nguvu zote, bado yapo mambo mengi ambayo hayajapata ufumbuzi wa uhakika. Vyombo vyetu vya utoaji haki vinajitahidi lakini havijafikia kiwango cha kuwa kimbilio la wote wanaotaka haki likiwa ndilo lengo kuu la Dira yetu. Mambo yanayochangia kutofikia kiwango hicho ni:-

(a) Ucheleweshaji wa kutatua migogoro na kutoa haki ambao unachangia kuwepo kwa mlundikano wa kesi za jinai za madai.

(b) Uwezo mdogo wa wananchi walio wengi kuvifikia vyombo vya kutoa haki na huduma za kisheria;

(c) Rushwa na tabia zisizozingatia matakwa ya taaluma kwa baadhi ya wafanyakazi na watumishi katika Sekta ya Sheria;

(d) Mfumo wa Sheria kwa kiasi fulani ni wa kizamani na una utaratibu na kanuni zilizopitwa na wakati na ambazo hazikidhi mabadiliko katika jamii, kisiasa, kiuchumi na teknolojia;

(e) Uelewa mdogo wa wananchi kwa mfumo uliopo wa sheria na Mahakama nchini;

(f) Uhaba wa ujuzi, utaalamu na hamasa ya kazi kwa wafanyakazi wa Sekta ya Sheria nchini; na

(g) Upungufu wa watumishi waliopata mafunzo kamili na mazingira ya kazi yasiyoridhisha kwa wafanyakazi wengi katika sekta ya sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto zilizoainishwa kimsingi zinatokana na ufinyu wa bajeti inayotengwa kila mwaka wa fedha. Mara nyingi na kwa kipindi kirefu, kiasi kianchotolewa huwa hakilingani na mahitaji halisi ya Wizara. Hata hivyo, kwa kulitambua tatizo hili, Serikali imekuwa inaongeza kiwango cha bajeti kila mwaka kwa kadri ya uwezo wake wa kifedha kama inavyosomeka katika Jedwali namba1.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua kwamba tatizo la ufinyu wa bajeti haliwezi kufutika mapema kutokana na udogo wa pato la Taifa, Wizara yangu ilibuni Programu ya Kuboresha Sekta ya Sheria ambapo Mkakati wake wa Muda wa Kati kwa mwaka 2005/2006 hadi 2007/2008 ulizinduliwa tarehe 22 Machi, 2005. Madhumuni ya programu hii ni kuweka mazingira bora ya upatikanaji wa haki. Programu hii inahusisha taasisi na asasi zote za Sekta ya Sheria. Utekelezaji wake ulianza mwaka wa fedha 2005/2006. Matatizo yote yaliyotajwa hapo juu yatashughulikiwa kwa kutumia mfuko wa pamoja *(basket funding)* chini ya programu hii; bajeti ya Serikali; raslimali nyingine na ubunifu wa viongozi na wataalaam katika utendaji kazi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Kipindi cha Mwaka 2005/2006. Katika kutekeleza mpango wa Bajeti kwa kipindi cha Mwaka 2005/2006 Wizara yangu iliongozwa na Programu ya Kuboresha Sekta ya Sheria chini ya Mkakati wa Muda wa Kati 2005/2006 – 2007/2008 ambayo imezingatia Ilani ya Uchaguzi ya CCM wa Mwaka 2000 hadi 2005 pamoja na Dira ya Taifa ya Maendeleo kwa lengo la kudumisha umoja wa Kitaifa, amani na utulivu nchini Tanzania. Chini ya programu hii, maeneo sita yamepangwa kuboreshwa na kutekelezwa kama ifuatavyo:-

(a) Sheria, Kanuni na Taratibu;

(b) Haki kwa Wanyonge na Wasiojiweza;

(c) Haki za Binadamu na Misingi ya Utawala Bora;

(d) Elimu na Taaluma ya Uanasheria;

(e) Kujenga uwezo wa Taasisi katika Kutoa Huduma; na

(f) Uendeshaji Uratibu na Usimamizi wa Utekelezaji waProgramu.Utekelezaji huo umezingatia pia ahadi za Wizara yangu Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Programu ya Kuboresha Sekta ya Sheria imelenga katika kuimarisha uwezo wa kutoa huduma kwa taasisi kuu zinazotoa huduma za Kisheria. Mambo yaliyofanyika ni kama ifuatavyo:-

(a) Vimeanzishwa vitengo *(division)* ndani ya Mahakama Kuu kwa madhumuni ya kushughulikia utoaji haki kwa masuala mahsusi ya kisheria. Kwa utaratibu huu, vimeanzishwa vitengo vya Mahakama Kuu inayoshughulikia mashauri ya Biashara na

mashauri ya Ardhi. Si muda mrefu ujao Kitengo cha Mahakama Kuu kitakachohusika na mashauri ya kazi kitaanzishwa;

(b) Kwa madhumuni ya kuharakisha ufumbuzi wa mashauri ya madai, umeanzishwa utaratibu mbadala wa kutatua migogoro, yaani *Alternative Dispute Resolution (ADR)* katika Mahakama Kuu. Mahakama za Hakimu Mkazi na Mahakama za Wilaya. Utaratibu huu unasaidia kutatua migogoro kabla ya kusikilizwa kwa ukamilifu na Mahakama na hivyo kupunguza mlundikano wa mashauri Mahakamani;

(c) Zimeanzishwa Kamati za Maadili katika ngazi ya Mkoa na Wilaya kwa madhumuni ya kushughulikia malalamiko dhidi ya Mahakimu wa ngazi hizo. Aidha, Tume za Utumishi wa Mahakama zimeunganishwa na kuwa Tume moja. Kamati ya Maadili ya Majaji imeanzishwa ili kushughulikia nidhamu ya Majaji. Tume pamoja na Kamati za Maadili zimeundwa chini ya Sheria ya Utumishi wa Mahakama ya 2005 yaani *Judicial Service Act, No 2/2005;*

(d) Majengo ya Mahakama yameendelea kufanyiwa ukarabati na mengine kujengwa;

(e) Ili kurahisisha mawasiliano, mkakati wa kuweka mtandao wa mawasiliano katika taasisi zote zinazotekeleza programu ya kuboresha Sekta ya Sheria umeandaliwa; na

(f) Umeandaliwa mpango endelevu wa miaka mitano 2004/2005 – 2008/2009 wa namna ya kuboresha miundombinu katika Mahakama za Mwanzo nchini. Katika Bajeti ya kila mwaka, Mahakama hutengewa fedha kwa ajili ya kutekeleza mpango huu kwa awamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwisho wa mwaka wa fedha 2005/2006, programu hii imepata mafanikio yafuatayo:-

(a) Katika kuboresha mfumo wa Sheria, Tume ya Kurekebisha Sheria imejengewa uwezo zaidi wa kupitia na kutafiti sheria mbalimbali kwa madhumuni ya kuziboresha. Watumishi wa Tume wamepewa mafunzo katika taaluma ya Utafiti wa Sheria na kupewa vitendea kazi;

(b) Imetungwa Sheria mpya ya Makampuni ya mwaka 2002 na Kanuni zake. Sheria hiyo imeanza kutumika mwezi Machi, mwaka 2006;(c)Limetolewa chapisho jipya la mwaka 2002 la Sheria za Tanzania likiwa na Marekebisho yote;

(d) Limetolewa chapisho jipya la vitabu vya taarifa za keshi (*Tanzania Law Reports)* zilizoamuliwa na Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufaa za kuanzia mwaka 1983 – 1997. Matoleo ya vitabu hivyo yanasaidia Wanasheria na Mahakama katika kurejea na kutatua migogoro inayofanana na maamuzi ya Mahakama katika matoleo hayo;

(e) Limetolewa chapisho jipya la kanuni za Magereza la mwaka 2003 baada ya kuhuishwa;

(f) Umefanyika uchambuzi wa kina na kubainisha mikakati ya kutenganisha masuala ya upelelezi na msuala ya uendeshaji wa mashtaka utakaoanza kutekelezwa mwaka huu wa fedha;

(g) Vipindi vya *radio* na televisheni vinavyotangazwa redioni kwa jina la "Ijue Mahakama yako" vimefufuliwa kwa madhumini ya kujenga uelewa kwa wananchi kuhusu majukumu ya kimahakama na namna ya kuifikia haki; na

(h) Tafiti kadhaa zilifanyika ili kuainisha maeneo yatakayoongeza kasi ya mageuzi katika Sekta ya Sheria kama ifuatavyo:-

(i) Kufanya mapitio ya sheria na kuhuisha kanuni na taratibu zinazoongoza taasisi za kisheria ili kukidhi mabadiliko yanayoendelea nchini;

(ii) Kuboresha usimamizi na mgawanyo wa kazi katika taasisi za kisheria ili kuboresha usimamizi wa uwajibikaji;

(iii) Kutenganisha majukumu ya utoaji haki na ya kiutawala ili kuongeza ufanisi katika utoa haki;

(iv) Kuangalia kanuni na taratibu *"Retention Scheme"* ya asasi za kisheria;
(v) Kuhuisha mafunzo na wajibu wa mtumishi katika kutekeleza malengo na majukumu ya asasi husika;

(i) Mfumo wa kusimamia haki za watoto umeboreshwa. Marekebisho yamefanywa katika jengo la Mahakama ya Watoto Kisutu, Dar es Salaam;

(j) Rasimu ya Sera ya Sekta ya Sheria imeandaliwa; na

(k) Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ilianzishwa mwaka 2003 ili kusimamia masuala ya kulinda haki za binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuboresha taaluma ya Uanasheria, uchambuzi yakinifu umefanywa ili kubainisha hatua zitakazowezesha kuimarishwa kwa mafunzo ya sheria kwenye vyuo vyetu vinavyofundisha masomo ya sheria. Mkakati pia umeandaliwa kwenye vyuo vya Magereza na Polisi ili kuwawezesha wahitimu wa vyuo hivyo watekeleze majukumu yao kwa kuzingatia misingi ya haki za binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia mwaka wa fedha 2004/2005 Wizara ilianza kufanya maandalizi ya Mradi chini ya Programu ya Uwajibikaji, Uwazi na Uadilifu

Tanzania *(Accountability, Transparency and Integrity Project)* unaofadhiliwa na Benki Kuu. Huu ni mradi wa kuendeleza Utawala Bora Nchini. Mradi huu unalenga katika utoaji wa misaada ya kiufundi na hatua nyingine za kujenga uwezo wa kuboresha ufanisi wa utendaji kazi kwa Taasisi mbalimbali zinazotekeleza Mpango wa Utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Utawala Bora (*National Anti-Corruption Strategy and Action Plan (NASAP).* Mingi ya misaada hii itatolewa kama ushauri, mafunzo, usambazaji wa habari na zana, uandishi wa sheria, taratibu na kanuni, vifaa, samani, magari pamoja na miundombinu michache. Mradi huu utatusaidia kutatua changamoto hizo. Hivyo, utekelezaji wa Mradi huu utarahisisha kuyafikia malengo ya sera yetu. Jedwali namba 4. Ni orodha ya majengo yaliyojengwa na kufanyiwa ukarabati kuanzia mwaka wa fedha 2004/2005 hadi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi huu utasaidia vilevile katika kugharamia ujenzi wa majengo mapya, ukarabati wa majengo yaliyopo, ubomoaji wa majengo yaliyopo na kujenga mapya kwa baadhi ya Mahakama zilizopewa kipaumbele, baadhi ya Mahakama za Mwanzo, za Wilaya, za Hakimu Mkazi, Kanda za Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani zitanufaika na mradi huu. Kwa jumla mradi utagharamia ujenzi wa Makao Makuu ya Wizara ya Katiba na Sheria, Chuo cha Sheria (*Law School*); Jengo la Mahakama ya Rufaa Tanzania, Ujenzi wa Mahakama Kuu 13; ujenzi wa Mahakama za Hakimu Mkazi kwa Mikoa 12, ujenzi wa jengo moja au mawili ya Mahakama ya Wilaya kwa Wilaya zilizoainishwa. Vilevile mradi utashughulikia ujenzi wa jengo moja la Mahakama ya Mwanzo katika kila Tarafa nchini.

Orodha kamili ilivyoonyeshwa katika Jedwali namba 3. Jambo muhimu la kuzingatia ni kwamba, chini ya mradi huu, ujenzi au ubomoaji wa majengo hayo unafanywa kwa utaratibu maalum na makubaliano na wadau wote. Sera ya Mahakama inayolenga kusogeza huduma za Mahakama karibu na wananchi, inakusudia kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kuwa na jengo la Mahakama Kuu katika kila Mkoa;
(b) Kujenga Mahakama ya Hakimu Mkazi katika kila Mkoa;
(c) Kuwa na jengo la Mahakama ya Wilaya katika kila Wilaya; na
(d) Ujenzi wa Mahakama ya Mwanzo katika kila Tarafa.

Mabaraza ya Kata yanayosimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa yatakuwa kiungo muhimu cha kusaidia kufikisha huduma za utoaji haki vijijini na kwenye Kata nchini kwa kutumia njia za usulushi kwa kufuata sheria, mila na desturi za sehemu zinazohusika kwa mambo ambayo Mabaraza hayo yana mamlaka nazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha chini ya Programu hii upo mradi wa Maboresho ya Sekta Sheria kwa ajili ya Maendeleo ya Uchumi (*Improving the Legal Framework*) Madhumuni ya mradi huu unaofadhiliwa kwa pamoja na Serikali ya Ujerumani na Serikali ya Tanzania na ulioanza kutekelezwa Julai, 2004 ni kuhuisha Sheria na taratibu za kisheria ili zikidhi mabadiliko ya kiuchumi. Mradi huu umeanza

kutekelezwa kwa kutoa mafunzo kwa wakuu wa Taasisi zinazotekeleza Programu ya Kuboresha Sekta ya Sheria ili kuleta mabadiliko katika uongozi (*change Management Training*). Mafunzo haya yamegharamiwa na Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Ujerumani.

Vilevile Waratibu wa Programu katika Taasisi na Asasi zinazotekeleza Mradi wamepatiwa mafunzo ya usimamizi wa programu na wamepewa vitendea kazi kama vile kompyuta na mpakato (*laptops*) ili kurahisisha utekelezaji wa majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu pia imetoa mafunzo kwa waratibu wa programu ya jinsi ya kuandaa taarifa za utekelezaji wa majukumu katika mradi itakayotekelezwa katika Taasisi zao, yaani (*Project Implemenntation Progress Reports)*. Mafunzo haya yalilenga kuwandaa waratibu hao na kuwawezesha kuwajibika katika kutoa taarifa za utekelezaji wa kazi pamoja na matumizi ya fedha za mradi. Aidha, mnamo tarehe 25/4/2006 Wizara imeweza kufanya kongamano la Majaji, Mawakili wa Serikali, Mawakili wa kujitegemea na Wanasheria mbalimbali kujadili mwenendo wa sheria za madai nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maboresho ya Sekta ya Sheria yanaendelea pia kufanyika chini ya Programu ya Kuboresha Mazingira ya Biashara Tanzania *(MKUMBITA – BEST)* kwa kutekeleza kipengele cha utatuzi wa migogoro ya kibiashara kwa lengo la kuharakisha na kuboresha utatuzi wa migogoro hiyo ili kuleta ufanisi katika uendeshaji wa migogoro ya kibiashara Mahakamani. Hadi sasa waratibu wa programu hii wameteuliwa. Mpango wa utekelezaji na taratibu za kuajiri zimeandaliwa. Hatua za kuteua Mshauri wa kitaalamu katika eneo hili zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uendeshaji wa Kesi na Kupungua Mlundikano wa Kesi Mahakamani. Wizara yangu imeendelea kuchukua hatua madhubuti za kuboresha uendeshaji mashauri na kupunguza mlundikanano wa kesi Mahakamani. Kama Waheshimiwa Wabunge watakavyokumbuka, mwaka 2005 Bunge lako Tukufu lilifanya marekebisho katika sheria za Mwenendo wa Jinai na Mwenendo wa Madai ili kuweka ukomo wa siku 60 kwa Majaji na Mahakimu kuandika hukumu. Uamuzi huo umeanza kuonyesha mafanikio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hatua za kupunguza mlundikano wa kesi, Serikali pia imeshughulikia tatizo la mlundikano wa mahabusu katika magereza. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kufanya ziara katika magereza ili kusikiliza matatizo ya mahabusu na wafungwa na kuchukua hatua zinazostahili. Ziara hizo zimefanywa kwa kushirikisha kwa pamoja mawakili wa Serikali wafawidhi wa kila kanda, Mahakimu wakazi na Majaji wa Mahakama Kuu na wakuu wa upelelezi wa Mikoa wa Makosa ya Jinai. Zoezi hili limezaa mafanikio makubwa kwa kubainisha mahabusu waliokaa gerezani kwa muda mrefu kwa makosa madogo madogo yasiyostahili, na limetoa chagizo katika kuongeza kasi ya upelelezi wa baadhi ya makosa na kutoa msukumo kwa baadhi ya kesi kukamilisha haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha mfumo wa utoaji haki, Kamati ya Kusukuma Kesi ziliendelea kuimarishwa pamoja na kuendeleza utaratibu wa kila Jaji na

Hakimu kujipangia ratiba ya usikilizaji wa mashauri *(Individual Calendar*). Aidha, suala la Ukaguzi na ufuatiliaji lilipewa kipaumbele. Ukaguzi na ufuatiliaji ulifanyika katika ofisi zote za Kanda za Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikai kwa ajili ya kuangalia utoaji haki na kutembelea Mahakama, hasa Mahakama za Mwanzo; ubora wa ushauri wa kisheria unaotolewa pamoja na uendeshaji wa mashtaka, kesi za madai, na za kikatiba na Haki za Binadamu. Pia Wizara imefuatilia kwa karibu utekelezaji wa mpango na bajeti ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali na manunuzi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kupunguza kero za wananchi kuhusu utoaji haki, Mahakama imeendeleza zoezi la ukaguzi wa Mahakama za Wilaya na hasa za Mwanzo. Ukaguzi umeimarika zaidi baada ya Mahakama zote za Mikoa 21 kupatiwa magari. Magari mengine 16 tayari yamenunuliwa na kusambazwa katika Wilaya kwa ajili ya Ukaguzi wa Mahakama za Mwanzo. Utaratibu unakamilishwa kununua mengine 31.

Aidha, Mahakama ya Rufani ya Tanzania, mwaka 2005/2006 imeweza kuendesha vikao 14, kama vile ilivyofanya mwaka 2004/2005. Mahakama hii ambayo hadi hivi karibuni ilikuwa na majaji 8 imeweza kuongeza idadi ya rufani ilizosikiliza na kuamua kutoka 277 hadi 577 ilizosikiliza katika mwaka 2004/2005.

Hili ni ongezeko la karibu asilimia 108. Pamoja na jitihada hizo bado mzigo wa kazi katika Mahakama ya Rufani ni mkubwa, kwani idadi ya rufani zote za madai na jinai zilizofunguliwa zimeendelea kuongezeka kufikia 640 ikilinganishwa na rufaa 277 zilizofunguliwa katika kipindi cha mwaka 2004/2005. Idadi ya Majaji wa Rufani sasa imefikia kumi na moja baada ya uteuzi wa Majaji 3 walioteuliwa siku chache zilizopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2005/2006, Mahakama kuu ambayo hadi karibuni ilikuwa na majaji 37, imeweza kuendesha vikao 100 katika nchi nzima ikilinganishwa na vikao 97 vilivyoendeshwa mwaka 2004/2005.

Katika vikao hivyo, Mahakama Kuu imeweza kusikiliza na kuamua kesi 6,379 ikilinganishwa na kesi 6,183 katika kipindi cha mwaka 2004/2005, ambalo ni ongezeko la takriban asilimia 3 sawa na ongezeko la kesi 196. Hata hivyo, Mahakama Kuu imeelemewa sana na mzigo wa kazi, kwani kesi mpya zilizofunguliwa katika kipindi hicho ni 9,308 na kesi zilizobaki ni 13,296.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama ya Biashara imefanikiwa kumaliza mashauri 91 kati ya mashauri 115 yaliyokuwepo Mahakamani, hii ni sawa na asilimia 79 ya mashauri yote yaliyofunguliwa kwenye Kanda ya Dar es Salaam na Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kitengo cha Ardhi cha Mahakama Kuu ya Tanzania kulipokea jumla ya Migogoro ya Ardhi 1,263 kwa nchi nzima. Kati ya migogoro hiyo, 476 imemalizika na 787 inaendelea kushughulikiwa. Taarifa kamili ya migogoro ya ardhi iliyofunguliwa na kushughulikiwa na Mahakama imeonyeshwa kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mahakama za Hakimu Mkazi na Mahakama za Wilaya pia ufanisi umeongezeka katika utendaji wake. Katika kipindi cha mwaka 2005/2006 Mahakama hizo zimeweza kusikiliza jumla ya mashauri ya jinai na madai 48,805 ikilinganishwa na mashauri kama hayo 46,603 katika kipindi cha mwaka 2004/2005, hili ni ongezeko la kesi 2,202 sawa na asilimia 4.7. Mzigo wa kazi katika Mahakama hizi pia ni mkubwa, kwani hadi kufikia mwezi Mei, 2006 kesi mpya 44,863 tayari zimefunguliwa ambapo kesi 47,552 zilifunguliwa katika mwaka mzima wa 2004/2005.

Kesi zilizobaki ni 24,557. Utaratibu wa kuajiri Mahakimu wakazi 37 wapya umekamilika ili kukabiliana na mzigo huo wa kazi. Lengo lilikuwa kuajiri mahakimu wa kada hiyo 63 lakini haikuwezekana kutokana na kutopatikana kwa wenye sifa. Tayari Mahakimu wakazi 36 wameajiriwa. Taarifa kamili ya kesi zilizoshughulikiwa zimeonyeshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uendeshaji wa Kesi za Madai. Wizara yangu kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iliendelea kushughulikia kesi mbalimbali za madai zilizoihusu Serikali, kesi za jinai, pamoja na Katiba kwa kiwango kinachoridhisha. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Mei, 2006 kulikuwa na kesi za madai 933, zinazoihusu Serikali katika Mahakama Kuu. Kati ya hizo, jumla ya kesi 284 zimeshughulikiwa na kesi 649 bado zinaendelea kusikilizwa. Katika Mahakama ya Rufani kulikuwa na rufaa 70, kati ya hizo rufaa 23 zimeshughulikiwa na nyingine 47 bado zinaendelea kusikilizwa. Kesi mpya 223 za madai zimefunguliwa dhidi ya Serikali katika Mahakama Kuu, kesi 31 zimemalizika na kesi 192 bado zinaendelea kusikilizwa katika hatua mbalimbali. Bado zipo rufaa 26 katika Mahakama ya Rufani ambazo bado hazijaanza kusikilizwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa, katika kipindi cha mwaka 2005/2006 kufuatia zoezi la Uchaguzi Mkuu mwezi Desemba, mwaka 2005 kulikuwapo na kesi 36 za uchaguzi zilizofunguliwa katika Mahakama Kuu ya Tanzania. Kati ya hizo kesi 5 zimemalizika au kufutwa na Mahakama baada ya wadai kushindwa kutimiza masharti na kesi nyingine 31 bado zinaendelea kusikilizwa. Wizara yangu kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeendelea kusimamia kesi hizo kwa niaba ya Wasimamizi wa Uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Usimamizi wa Kesi za Katiba. Utekelezaji wa majukumu ya Haki za Binadamu uliendelea vizuri. Mashauri ya Katiba 18 yalifunguliwa na mashauri 2 yamemalizika na 1 liliondolewa Mahakamani. Mashauri yaliyobaki yanaendelea kusikilizwa. Chunguzi nne (4) za malalamiko ya uvunjwaji wa haki za binadamu zinaendelea kusikilizwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uendeshaji wa Mashtaka. Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka imeendelea kutekeleza, kusimamia na kuboresha huduma zake chini ya sheria na taratibu zilizopo. Ofisi hiyo imeendelea na jukumu la kuiwakilisha Serikali katika Mahakama ya Rufani, Mahakama Kuu na wakati mwingine Mahakama za Hakimu Mkazi kwa kesi zote za jinai ambapo ama Serikali imeshitaki au inajibu rufani, Ofisi hii

imeweza kuiwakilisha Serikali katika vikao vyote vilivyopangwa na Mahakama ya Rufani na Mahakama Kuu, ambapo imeweza kuendesha jumla ya kesi za jinai 822, rufaa za jinai 1327 na kesi za usikilizaji wa awali 895. Aidha, jumla ya rufaa za jinai 310 ziliendeshwa katika Mahakama ya Rufani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utoaji wa haki, Mahakama imekuwa inatekeleza jukumu hilo bega kwa bega na Mawakili wa Serikali wakiwepo mawakili binafsi ambao pia ni maofisa wa Mahakama. Idadi ya Mawakili wa kujitegemea imeongezeka baada ya Mawakili wapya kusajiliwa. Hivi sasa, jumla ya Mawakili wote nchini ni 1012. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ushauri na Ushiriki katika Mikataba ya Kimataifa. Wizara imetoa ushauri na kushiriki katika masuala mbali mbali ya mikataba ya kitaifa na kimataifa, mikataba hiyo ni ile ya kibiashara baina ya Mashirika ya Kimataifa na Serikali, mikataba ya ushirikiano kati ya nchi yetu na nchi nyingine.

Pia ilishiriki katika mikataba ya utekelezaji wa majukumu ya Serikali katika mikataba inayohusu Haki za Binadamu na Utawala Bora, hususan Mkataba wa Haki za Binadamu na Watu wa Afrika *(African Charter on Human and Peoples Rights)* na Mkataba wa Haki za Kiraia na Kisiasa *(International Covenant on Civil and Political Rights).* Hili lilikuwa ni kwa Wizara kuungana na timu za wataalmu kutoka Wizara mbalimbali za majadiliano na ilishiriki kikamilifu kuandaa rasimu za taarifa muhimu kuhusu mikataba hiyo ambazo zilitakiwa kuwasilishwa kwenye mamlaka ya vyombo vinavyohusika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Oktoba, 2005 Wizara yangu ilishiriki katika Majadiliano yaliyofanyika Gevena-Uswisi, yaliyohusu Taarifa iliyowasilishwa kwenye Kamati ya Mkataba kuhusu kuondoa aina zote za Ubaguzi. Taarifa hii ilielezea hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Serikali katika kuondoa aina husika za ubaguzi nchini. Wizara ilishiriki katika majadiliano ya kuanzisha Itifaki ya Umoja wa Afrika ya kusimamia Demokrasia, Uchaguzi na Utawala Bora, na majadiliano ya kuziunganisha Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu *(African Court on Human and Peoples Rights)* na Mahakama ya Afrika ya Haki *(African Court of Justice).* Mkutano huu ulikuwa na umuhimu wa pekee kwa kuwa Tanzania iliomba na kuungwa mkono kuwa Makao ya Mahakama hiyo mpya inayojulikana kama *The African Court of Justice and Human Rights.* Kuwepo kwa Mahakama hiyo nchini kutasaidia kuongeza imani kwa Jumuiya ya Kimataifa kwamba nchi yetu inajali Haki za Binadamu. Napenda kutoa taarifa rasmi kwamba Wakuu wa Nchi wanachama wa Umoja wa Afrika katika mkutano wao uliofanyika huko Banjul, Mji Mkuu wa Gambia waliridhia Tanzania kuwa Makao Makuu ya Mahakama hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu imeendelea kutekeleza shughuli za uandishi wa sheria katika kipindi cha mwaka 2005/2006. Jumla ya Miswada 7 iliandaliwa na kupitishwa na Bunge lako tukufu. Hali kadhalika, Wizara imesimamia uandishi wa Sheria ndogo 305 zilizochapishwa katika Gazeti la Serikali, na Sheria moja imetafsiriwa katika Kiswahili. Sheria hiyo ni ya Mazingira, Namba 20 ya mwaka 2004. Aidha, Wizara yangu kupitia Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, imefanya utafiti na kukamilisha na kuwasilisha kwangu taarifa katika maeneo ya upatikanaji wa Habari;

Teknolojia ya Habari katika Biashara na Utawala wa Serikali wa Serikali yaani *e-commerce* na *e-government*; na kuanzisha nchini Haki ya Uraia wa Nchi Mbili yaani *Dual Citizenship.* Tunatarajia kuziwasilisha taarifa hizo Bungeni hivi karibuni

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchunguzi wa malalamiko yanayohusu uvunjwaji wa haki za binadamu, Wizara yangu kupitia Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora imetembelea vijiji na Taasisi mbalimbali katika Wilaya 38 Tanzania Bara ili kuwaelimisha wananchi na watendaji kuhusu haki za msingi za binadamu, misingi ya utawala bora na uzingatiaji wake. Katika kipindi cha 2005 hadi Mei 31, 2006 Tume ilikuwa na malalamiko 8,436. kati ya hayo malalamiko mapya ni 2,793 na yaliyokuwa yanaendelea kutoka miaka ya nyuma ni 5,619 katika kipindi cha 2005/2006. Hata hivyo, Tume haijaweza kufanya kazi kikamilifu Zanzibar kwa sababu za kikatiba. Suala hili limepatiwa ufumbuzi na Wizara inakusudia kuleta Muswada wa sheria hapa Bungeni utakaokuwa na mapendekezo ambayo kama yatakubaliwa na Bunge yataiwezesha Tume kuanza kufanya kazi Tanzania Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka huu wa fedha, Wizara yangu kupitia Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora imetembelea Magereza 38 na Vituo vya Polisi 87 katika Wilaya 38 za Mikoa 19 ya Tanzania Bara ili kuona kama Haki za Binadamu na misingi ya utawala bora inaheshimiwa na kulindwa. Tume ilipokea malalamiko kutoka kwa wafungwa na mahabusu. Malalamiko yaliyofikishwa Serikalini yanashughulikiwa na mengi yamefanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uimarishaji wa Ofisi ya Kabidhi wasii Mkuu, shughuli za usajili wa vizazi, vifo, ndoa na talaka, udhamini na ufilisi zimeendelea kufanyika. Katika kipindi cha mwaka 2005/2006, Ofisi ya Kabidhi Wasii ilikusanya maduhuli ya Sh.383,154,712.53 kutokana na shughuli za usajili.

Ofisi hiyo imeweza kufanya usajili wa vizazi 284,907, vifo 41,554 na ndoa 10,536 na ukaguzi katika Wilaya 85 ulifanyika ili kuimarisha utendaji kazi. Ninayo furaha kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa ofisi hii tayari imezinduliwa rasmi kuwa wakala wa Serikali, kwa mujibu wa Programme ya Kuboresha Miundo ya Wizara. Wakala huo unaitwa *Registration, Insolvency and Trusteeship Agency (RITA).* Uzinduzi huo utaongeza ufanisi na kuimarisha utendaji wake wa kazi katika ukusanyaji wa maduhuli na utoaji wa huduma za usajili wa vizazi na vifo, ndoa na talaka na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uimarishaji wa utoaji haki, Wizara yangu inaendelea na mchakato wa kutenganisha shughuli za mashtaka na zile za upelelezi wa makosa ya jinai. Utekelezaji wa mpango huu unalenga kuiwezesha ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kutekeleza jukumu lake la msingi la kuendesha na kusimamia mashtaka yote nchini. Lengo la mpango huu ni kuviondolea vyombo vya upelelezi vya polisi na asasi nyingine jukumu la uendeshaji wa mashtaka. Hivyo, kuziwezesha asasi hizo kubaki na majukumu yao ya msingi ambayo ni kukamata wahalifu na kupeleleza uhalifu. Majaribio ya mpango huu yatafanyika katika Mikoa sita ambayo ni Dar es Salaam Mwanza, Tanga, Arusha, Shinyanga na Ruvuma. Aidha, hatua za awali kuhusu mapendekezo ya muundo wa ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka zimechukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mfunzo na ajira, ili kuongeza ufanisi katika utoaji haki, Mahakama iliamua kuinua kiwango cha elimu kwa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo wasiokuwa na Stashahada ya Sheria. Hatua hiyo ilisababisha wengi wao kujiunga na mafunzo ya Stashahada ya Sheria. Katika kuendeleza azma hiyo, tayari Mahakimu 85 wanaendelea na mafunzo ya Stashahada ya Sheria. *(Makofi)*

Vile vile, makarani 18 wanapatiwa mafunzo ya cheti cha Sheria katika Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto. Katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mawakili wa Serikali 29 walihudhuria mafunzo ya aina mbalimbali yatakayowasaidia kuwa na utaalamu maalum katika maeneo yao ya kazi. Katika miaka miwili iliyiopita, Wizara imefanikiwa kuajiri Mawakili wa Serikali wapya 48. Wizara ilipanga kutoa mafunzo ya muda mrefu, mfupi, semina na warsha ndani na nje ya nchi kwa Mawakili wa Serikali na Watumishi wa Kada nyingine kama ifuatavyo:-

(a) Mawakili wa Serikali waliopata mafunzo ya muda mrefu ya shahada ya uzamili katika sheria ni 11 na muda mfupi katika taaluma ya sheria ni 18;

(b) Makatibu muhtasi 2 wamepewa mafunzo ya muda mfupi ili kuendeleza uwezo wao na kuboresha ufanisi.

(c) Watumishi wa Kada nyingine waliohudhuria mafunzo ya muda mrefu katika ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni 15 na mafunzo ya muda mfupi ni 31. Hata hivyo, lengo la Wizara la kutoa mafunzo kwa mawakili wengi zaidi halikufanikiwa kutokana na ufinyu wa bajeti.

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora imeajiri watumishi wapya 85. Mafunzo kuhusu Haki za Binadamu, kompyuta, sheria, uhasibu, elimu ya jamii, ukutubi na utafiti yalifanyika ili kuwasaidia Makamishna na watumishi katika kutimiza wajibu wao. Watumishi 7 walipelekwa katika mafunzo ya fani mbalimbali ya muda mrefu ikiwemo fani ya sheria. Watumishi 29 walipelekwa kwenye mafunzo ya muda mfupi na watumishi wengine walihudhuria semina ili kuboresha utendaji wao wa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuongeza ufanisi na uwezo wake, Tume ya Kurekebisha Sheria imewapeleka mafunzoni watumishi ishirini na wawili (22) katika nyanja mbalimbali, kama vile Utawala Bora, Rushwa na Maadili, Elimu ya Kupambana na Maambukizi ya UKIMWI na Sheria kuhusu utumishi wa umma. Kati ya waliohudhuria mafunzo hayo wanawake walikuwa kumi na wanne (14) na wanaume wanane (8).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uboreshaji wa mazingira, Wizara yangu iliboresha mazingira ya kazi katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Wizara ilifanikiwa kununua majengo kwa ajili ya Ofisi za Kanda za Songea na Mtwara. Aidha, Makao Makuu ya Wizara yamepanuka kwa kupata ofisi nyingine za kupanga katika jengo la Sukari. Kanda mpya ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imefunguliwa katika Mkoa wa Iringa na Sumbawanga, Mkoa wa Rukwa.

Upungufu mkubwa wa majnego ya mahakama pamoja na uchakavu wa majengo yaliyopo ni changamoto kubwa. Waheshimiwa Wabunge watakumbuka ahadi iliyotolewa na Serikali kuhusu ukarabati mkubwa wa majengo ya Mahakama na kujenga mapya. *(Makofi)*

Katika kutekeleza mpango huo, ukarabati wa majengo ya Mahakama umeendelea kwa kasi kubwa. Ukarabati wa jengo la iliyokuwa Hoteli ya Forodhani kwa ajili ya Mahakama ya Rufani umekwishakamilika. Ukarabati wa majengo ya kilichokuwa kiwanda cha kukata almasi Iringa umekamilika isipokuwa kwa marekebisho ya hitilafu ndogo ndogo. Tayari majengo hayo yamekwishaanza kutumika kwa ajili ya Mahakama Kuu na Mahakama ya Hakimu Mkazi ya Mkoa wa Iringa. Mahali hapo panajulikana kama Iringa *Judicial square* na palifunguliwa na Rais Mstaafu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa mwaka 2005. Vile vile, ukarabati wa jengo la Mahakama Kuu, Masjala ya Moshi unaendelea vizuri. *(Makofi)*

Aidha, mpango endelevu wa ukarabati wa majengo ya Mahakama ya Mwanzo kwa kutumia fedha zetu wenyewe, ambapo Serikali imekuwa ikitenga kiasi cha Shilingi bilioni moja (1,000,000,000/=) kila mwaka unaendelea. Mahakama za Mwanzo 51 zilikarabatiwa katika mwaka wa fedha 2005/2006 na ukarabati wa Mahakama nyingine 40 unaendelea katika Mikoa mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa jengo jipya kwa ajili ya Mahakama Kuu unaendelea Mjini Bukoba, Mkoani Kagera. Majengo matatu ya Mahakama za Wilaya yanaendelea kujengwa na mengine 13 ya Mahakama za Mwanzo yanaendelea kujengwa nchi nzima. Aidha, Wizara imenunua jengo moja Arusha litakalotumika kwa ajili ya Mahakama ya Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Wilaya ya Arusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ofisi nyingine 2 za Masjala ya Ardhi ya Mahakama Kuu ya Tanzania zimefunguliwa huko Sumbawanga na Iringa hivyo kufanya jumla ya masjala hizo kuwa 13. Masjala nyingine ziko katika Mikoa ya Arusha, Kagera, Dar es Salaam, Dodoma, Kagera, Mbeya, Moshi, Mtwara, Mwanza, Ruvuma, Tabora na Tanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu imeimarisha utendaji wake wa kazi kwa kuongeza upatikanaji wa vitendea kazi. Wizara imenunua magari 2 kwa ajili ya utafiti wa sheria na pia imenunua magari mawili; moja kwa ajili ya usimamizi wa shughuli za mashtaka na jingine kwa ajili ya kuimarisha shughuli za Uandishi wa Sheria. Aidha, Wizara imenunua vifaa vya ofisi kama vile kompyuta, nukushi *(fax),* mashine za kutolea nakala, kwa ajili ya kurahisisha utendaji wa Idara zake na kwa ajili ya Mahakama Kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu masuala mengine ya jumla, Wizara yangu imeendelea kupambana na rushwa kwa kuwahamasisha watumishi wake kwa njia za kuendesha warsha zilizowahusisha watumisha wa kada zote. Semina hizo zilifanyika Dar es Salaam na Morogoro, kwa ajili ya kuwaelimisha watumishi wa Wizara juu ya madhara ya rushwa na jinsi ya kupambana nayo. Aidha, Sheria imepitishwa kuanzisha rasmi Kamati za Maadili kwa ajili ya kufuatilia malalamiko ya rushwa. Kamati hizo zimeanzishwa katika ngazi ya Wilaya, Mikoa, Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ripoti rasmi ya hali ya maambukizi ya UKIMWI (*Situational analysis*) katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilizinduliwa tarehe 24 Machi 2006 na Mpango wa Utekelezaji wa ripoti hiyo umeandaliwa. Mpango huo utatekelezwa katika kipindi cha fedha cha mwaka 2006/2007. Wizara yangu imeendelea kushirikiana na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na Tume ya Kudhibiti UKIMWI ili kukusanya maoni kuhusu kutunga Sheria ya Kudhibiti na Kuzuia Maambukizi ya UKIMWI. Mafunzo yametolewa kwa watumishi wa jinsi ya kuzingatia masuala ya UKIMWI katika mipango ya bajeti, pamoja na kuwahamasisha kuhusu madhara ya maambukizi ya UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu inayaelewa na kuyatilia mkazo masuala ya jinsia. Hivyo, mafunzo ya masuala ya jinsia yameendelea kutolewa kwa watumishi waliopo katika Wizara, asasi na taasisi zilizopo katika Wizara yangu kuhusu jinsi ya kuzingatia masuala ya jinsia katika bajeti na mipango. Kwa mwaka wa fedha uliopita Wizara imeratibu na kusimamia utekelezaji wa mradi wa Benki ya Dunia wa upembuzi yakinifu kuhusu mila mbaya dhidi ya wanawake yaani (*Legal and Gender Responsive Reform Project*). Napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza majaji na mahakimu wanawake ambao kwa kupitia chama chao, wameendelea kuhamasisha masuala ya jinsia katika mahakama. Napenda kuwahakikishia kuwa mwamko huo haupo katika Mahakama peke yake, bali pia katika asasi na taasisi zote zilizopo katika Wizara yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hifadhi ya mazingira ni jukumu letu sote. Wizara yangu ina wajibu wa kuboresha sheria, kanuni na taratibu za kuhifadhi mazingira. Wizara imekwisha tafsiri Sheria ya Mazingira namba 20 ya mwaka 2004 katika lugha ya Kiswahili ili kuwawezesha wananchi walio wengi kuielewa. *(Makofi)*

Katika kuhifadhi mazingira, Mahakama katika ngazi zote zimeendelea kutekeleza tamko la Morogoro la mwaka 1993 linalozihitaji Mahakama zote kutunza miti na maua, ili kuhifadhi mazingira na kuyafanya yawe na mandhari nzuri. Utekelezaji wa jambo hili unaendelea kwa ufanisi katika maeneo mengi ya Mahakama zetu. Katika maboresho ya sekta ya sheria zipo shughuli nyingi za ujenzi. Napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba shughuli hizo zitazingatia kwa makini hifadhi ya mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu ina jukumu la kuchambua taarifa mbalimbali zinazoandaliwa na Tume ya Kurekebisha Sheria kwa mujibu wa Sheria iliyoanzisha Tume hii. Katika kipindi cha mwaka 2005/2006, Wizara yangu ilifanya uchambuzi wa taarifa zifuatazo: "*Flow of Justice*", Sheria ya Rushwa, Sheria ya Polisi na Magereza, mapendekezo kuhusu kutengwa kwa Sheria ya *"Paralegals"* na Mapendekezo ya Kuhuisha Adhabu za Faini (*Currency Points*). Uchambuzi wa taarifa hizi unaendelea kufanywa na Wizara na Taasisi nyingine husika ili baadaye kama itaonekana inafaa hatua za kutunga sheria mpya na kufanya marekebisho katika sheria zilizopo zichukuliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyokwishaeleza, masuala makuu ya kikatiba yaliyojitokeza katika kipindi cha mwaka 2005/2006 ni pamoja na kukamilika kwa

Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005 ambapo Chama cha Mapinduzi kimepata ushindi wa kishindo na kupata ridhaa ya wananchi kutekeleza Ilani yake ya uchaguzi. Vile vile, Mahakama Kuu imetoa maamuzi mbalimbali kuhusu Katiba. Maamuzi hayo ni kama ifuatavyo: -

(a) Kufuta vifungu vya Katiba vyenye masharti yanayoelekeza kwamba wagombea wa Kiti cha Urais na Ubunge wawe wanachama na wawe wamependekezwa na Chama cha Siasa;

(b) Kufuta vipengele katika Sheria ya Uchaguzi, vilivyokuwa vinaruhusu matumizi ya takrima katika kampeni za uchaguzi na

(c) Kufuta kipengele katika Sheria ya Uchaguzi kilichokuwa kinaruhusu chaguzi ndogo kufanyika kwa baada ya miaka miwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali ilivyotangaza katika Bunge hili Tukufu, hatua zimechukuliwa kukata rufani dhidi ya uamuzi wa Mahakama Kuu kuhusu kufuta masharti ya Mgombea kuwa Mwanachama na Mgombea aliyependekezwa na Chama cha siasa na utaratibu wa kuendesha chaguzi ndogo. Vile vile, Serikali inafanya uchambuzi ili kuwa na mapendekezo ya Sheria itakayoweka utaratibu wa kisheria juu ya kugharamia kampeni za chaguzi ambao hautapingana na Sheria ya Rushwa ili kutekeleza maamuzi hayo ya Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Matatizo yaliyoathiri utekelezaji wa Mpango wa mwaka 2005/2006, kama nilivyokwisha kueleza kuhusu chimbuko na matatizo ya msingi yanayoikabili Wizara ya Katiba na Sheria, napenda nieleze kwamba katika kutekeleza Mpango wa Bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka wa fedha 2005/2006, matatizo hayo kwa kiasi kikubwa yameathiri na yanaendelea kuathiri utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Sikusudii kurudia kuyaorodhesha matatizo hayo. Inatosha kusema kwamba kati ya hayo, yapo matatizo makuu mawili ambayo Serikali itayapa kipaumbele katika kukabiliana nayo ili tuweze kufanikiwa katika Dira yetu ya Haki Sawa kwa Wote na kwa Wakati. Matatizo hayo ni: -

(a) Uwezo mdogo wa wananchi walio wengi kuvifikia vyombo vya kutoa haki na huduma za kisheria na

(b) Uelewa mdogo wa wananchi kwa mfumo uliopo wa sheria na Mahakama nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu imeendelea kutatua matatizo haya na yale na ya msingi katika Sekta kwa kujenga hoja ya kuongezewa Bajeti ya Serikali; kuvishirikisha vyama vya hiari na Mashirika yasiyo ya Serikali na pia kutafuta misaada kutoka kwa wafadhili na wahisani chini ya Programu ya Kuboresha Sekta ya Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango na Malengo ya mwaka 2006/2007, kwa mujibu wa Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005, chini ya Sekta ya Sheria, Wizara iliagizwa kuendelea na hatua zilizoanza kuchukuliwa ili kuboresha Sekta hiyo kusudi nayo itoe huduma bora zaidi kwa jamii. *(Makofi)*

Malengo ya Mkakati wa Muda wa kati wa Programu ya Kuboresha Sekta ya sheria tayari yameoanishwa na Mpango wa Serikali wa Muda wa kati wa Mipango na Matumizi ya Fedha yaani *Medium Term Expenditure Framework (MTEF)* kwa taasisi zote zinzotekeleza programu hii katika kipindi cha mwaka wa fedha 2005/2006 kwa ajili ya Mipango ya Bajeti ya mwaka wa fedha 2006/2007. Malengo hayo yamezingatia utekelezaji wa malengo ya Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2006/2007, Wizara itaendelea kutekeleza majukumu yake ya Kikatiba kwa kuzingatia mpango na malengo iliyojiwekea ambayo ndiyo msingi wa makadirio ya bajeti yetu. Majukumu hayo ya utoaji haki kwa wananchi na kuishauri Serikali yatatekelezwa sambamba na Programu ya Kuboresha Sekta ya Sheria. Aidha, utekelezaji wa majukumu hayo utazingatia Dira ya Wizara, Dira ya Taifa 2025 na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, chama kinachoongoza Serikali hivi sasa, kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Sekta ya Sheria, Waheshimiwa Wabunge watakubaliana nami kuwa jukumu la utoaji haki nchini linapaswa kutekelezwa kwa misingi ya sera madhubuti. Sera ni mwongozo wa kutekeleza majukumu mbalimbali kwa sekta inayohusika. Wizara yangu itakamilisha maandalizi ya Sera ya Taifa ya Sekta ya Sheria katika mwaka huu wa fedha na rasimu ya kwanza ya Sera hiyo imekamilika. Rasimu hiyo itawasilishwa kwenye warsha za wadau wa ngazi mbalimbali ili kupata maoni na mapendekezo yao kabla ya kuwasilisha Waraka wa Sera hiyo kwenye Baraza la Mawaziri kwa uamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuimarisha uendeshaji wa kesi na kupunguza mlundikano wa kesi Mahakamani, Wizara itaandaa programu maalum kwa ajili ya upunguzaji wa mlundikano wa kesi katika Mahakama zetu chini ya mradi mahsusi unaoitwa *Case Backlog Disposal Programme in the High Court* and *Resident Magistrates Courts.* Kazi ambayo itafanywa kwa majaribio baada ya kukamilishwa upembuzi yakinifu wa kitaalamu utakaofanywa katika mwaka huu wa fedha. Kazi hii itafadhiliwa na Benki ya Dunia kupitia programu ya *BEST* chini ya mradi wa kuharakisha mashauri ya kibiashara yaani *Commercial Disputes Resolution.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2006/2007, Wizara yangu imepanga kuboresha huduma za kisheria, kuimarisha usimamizi na uendeshaji wa mashauri nchini kwa lengo la kupunguza kero ya mlundikano wa mashauri Mahakamani. Mambo yafuatayo yatatekelezwa: -

(a) Kutenganisha shughuli za upelelezi zinazopaswa kufanywa na Polisi na shughuli za uendeshaji wa mashauri ya jinai Mahakamani ambazo kwa mujibu wa sheria zinasimamiwa na kuendeshwa na Mkurugenzi wa Mashtaka. Mpango huu utaanza kwa majaribio katika Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Mwanza, Ruvuma, Shinyanga na Tanga kabla haujatekelezwa kwa nchi nzima.

Tunatarajia kwamba kutenganisha kazi za upelekezi na uendeshaji wa mashauri ya Jinai kutaiwezesha Polisi kujihusisha tu katika upelelezi wa makosa ya Jinai na hivyo kutumia muda wao kwa kazi hiyo na kuondoa malalamiko ya ucheleweshaji wa upelelezi wa jinai yanayokwamisha kumalizika kwa kesi haraka na kusababisha mlundikano wa mahabusu.

Aidha, hatua hii itaondoa matumizi mabaya ya mfumo wa kutoa haki kama vile ubambikizaji wa kesi kwa raia wasio na hatia. Utaratibu huu wa kutenganisha majukumu hayo mawili unatumika katika nchi nyingi za Jumuiya ya Madola na unaaminika kwa kudumisha dhana ya watuhumiwa kushughulikiwa kwa misingi ya sheria kuliko ile ya mpelelezi kuwa mwendesha mashtaka yanayohusu upelelezi alioufanya yeye mwenyewe au maafisa wenzake.

Katika kutekeleza mchakato huu, Wizara yangu itawaajiri Mawakili wa Serikali 104, kununua magari 6 na kununua majengo 6 kwa ajili ya matumizi ya ofisi na vitendea kazi katika maeneo ambayo mpango huo utatekelezwa.

(b)Kuhakikisha kwamba Majaji na Mahakimu wanasikiliza mashauri yaliyofikishwa mbele yao kwa haraka na kwa haki. Kwa ajili hiyo, Mahakama ya Tanzania imeweka mkakati wa kusikiliza Tanzania imeweka mkakati wa kusikiliza na kumaliza mashauri angalau kati ya 6 na 7 katika kila mashauri 10 yanayopelekwa na kuandikishwa mahakamani. Mahakama pia imepanga kuajiri Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo 100, Mahakimu Wakazi 70 na pia kuteua Majaji zaidi.

Aidha, Mahakama ya Rufani imepanga kuongeza vikao vya Mahakama kutoka 9 hadi 17 kwa mwaka, vikao vya Mahakama Kuu kutoka 100 hadi 196 na kufanya vikao vya Mahakama kila siku kwenye Mahakama za Hakimu Mkazi, Mahakama za Wilaya na Mahakama za Mwanzo na kufanya vikao 4 vya Kamati za Kusukuma Kesi (*Case Flow Management Committee*) kwenye kila ngazi za Mahakama nchini;

(c) Kuendeleza utaratibu wa kila Jaji na Hakimu kujipangia kalenda binafsi ya kusikiliza kesi (*Individual Calendar*) na kuhakikisha kwamba utaratibu huo hautumiki vibaya na kusababisha kero ya ucheleweshaji wa kesi tena;

(d) Kuzipatia Mahakama vitendea kazi, ikiwa ni pamoja na vifaa vya ofisi kama karatasi za kuandikia, usafiri na majengo zaidi ya Mahakama. Aidha, ili kukabiliana na tatizo la uandaaji wa hukumu, vitanunuliwa vifaa vya kunasa kumbukumbu za mwenendo wa kesi katika Mahakama Kuu;

(e) Mahakama ya Biashara itafungua masjala katika kanda ya Mwanza na Mahakama ya Ardhi itafungua masjala 2 ndogo katika Mikoa ya Shinyanga na Mara; na

(f) Ujenzi wa majengo ya Mahakama za ngazi zote ambao utahusu kujenga majengo mapya, ukarabati wa majengo yaliyopo, ubomoaji wa majengo yaliyopo na kujenga mapya kwa baadhi ya Mahakama zilizopewa kipaumbele, baadhi ya Mahakama za Mwanzo, za Wilaya, za Hakimu Mkazi, Kanda za Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani. Kwa ujumla mradi utagharamia ujenzi wa Makao Makuu ya Wizara ya Katiba na Sheria; Chuo cha Sheria (*Law School*); Jengo la Mahakama ya Rufani Tanzania; ujenzi wa Mahakama Kuu 13; ujenzi wa Mahakama za Hakimu Mkazi wa Mikoa 12; ujenzi wa jengo moja au mawili ya Mahakama ya Wilaya kwa Wilaya zilizoainishwa.

Vile vile, mradi utashughulikia ujenzi wa jengo moja la Mahakama ya Mwanzo katika kila Tarafa nchini. Jambo muhimu la kuzingatia ni kwamba, chini ya mradi huu, ujenzi au ubomoaji wa majengo hayo utafanywa kwa utaratibu maalum na makubaliano na wadau wote. Kwa misingi hiyo, Sera ya Mahakama inalenga kusogeza huduma za Mahakama karibu na wananchi inakusudia kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kuwa na jengo la Mahakama Kuu katika kila Mkoa;

(ii) Kujenga Mahakama ya Hakimu Mkazi katika kila Mkoa;

(iii) Kuwa na jengo la Mahakama ya Wilaya katika kila Wilaya; na

(iv) Ujenzi wa Mahakama ya Mwanzo kwa kila Tarafa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utunzaji wa kumbukumbu katika masjala zetu ni changamoto ambayo inabidi iende sambamba na maendeleo katika teknolojia ya habari na mawasiliano *(teknohoma)*. Wizara yangu chini ya Programu ya Kuboresha Sekta ya Sheria imejizatiti kuboresha masjala zote, kwa kuweka taarifa zake katika vifaa vya kisasa na kufunga mfumo maalumu wa mawasiliano utakaoboresha mawasiliano baina ya masjala zote zilizo katika Sekta ya Sheria (*Modernization and computerization of registries and installation of case management software*).

Kwa kuanzia, Wizara yangu itaunganisha mfumo maalumu wa mawasiliano Mahakamani, kwa ajili ya kusimamia Kesi. Kazi hii itafanywa chini ya Mradi wa Kusaidia Uendeshaji wa Kesi za Madai Kwenye Mahakama (*Support Civil Procedure in the Judiciary*) unaofadhiliwa na Benki Kuu kupitia Programu ya Uboreshaji wa Mazingira ya Biashara Tanzania *(MKUMBITA – BEST)*.

Chini ya programu hii sheria zifuatazo zitarekebishwa:

(a) Sheria ya Mwenendo wa Kesi za Madai (*Civil Prodecure Act*);

(b) Sheria ya Ushahidi (*Evidence Act*);

(c) Sheria ya Mawakili (*Advocates Act*);

(d) Sheria ya Mahakama za Mahakimu (*Magistrates Courts Act*); na

(e) Sheria ya Madalali wa Mahakama (*Court Brokers and Process Servers Act.*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ushauri wa Kisheria, Uandishi na Utafiti wa Sheria. Katika mwaka wa fedha 2006/2007, Wizara itaendelea kutoa ushauri wa kisheria kwa Serikali kuhusu masuala mbalimbali ya kisheria za Kimataifa, masuala ya Mikataba, Katiba na kuiwakilisha katika mashauri mbalimbali ya madai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu itaendelea na Uandishi wa Miswada ya Sheria, Sheria ndogo zinazotungwa na Mamlaka nyingine pamoja na kutafsiri Sheria katika Kiswahili. Jumla ya Miswada 25, Sheria ndogo 500 zitaandikwa na Sheria 10 zitatafsiriwa katika lugha ya Kiswahili ili wananchi walio wengi waweze kuzielewa. Aidha, Jumla ya Sheria 30 zitafanyiwa Marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu kupitia Tume ya Kurekebisha Sheria itazifanyia utafiti, uchambuzi na kuhuisha Sheria zetu mbalimbali zilizopitwa na wakati kwa kukamilisha taarifa zinazohusu maeneo yafuatayo:-

(a) Ushindani wa haki katika biashara *(Competition Law);*

(b) Usimamizi wa haki za ugunduzi na uhamishaji wa teknolojia *(Industrial property and Transfer of technology);*

(c) Sheria za *mila (Customary Law);*

(d) Usimamizi wa mali asili kwa ujumla (*Natural Resources*); na

(e) Ulinzi wa Haki za Watu Wenye Ulemavu (*Disability Law*); na mapitio na utafiti wa kuainisha sheria itakayosimamia matumizi ya teknolojia ya chembechembe za asili za urithi *(DNA).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2006.07 Wizara yangu itaandaa taarifa ya Utekelezaji wa Mkataba wa Kimataifa juu ya Haki za Kiuchumi, Kijamiii na Kiutamaduni (*International Convenant on Economic, Social and Cultural Rights).* Wizara pia itaendelea kuiwakilisha Serikali katika mashauri ya Katiba Mahakamani na chunguzi zilizopo katika Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Aidha, Wizara inatarajia kutoa tafsiri nakala za Katiba ya Nchi kwa lugha ya Kiingereza na kutoa vitabu vidogo vya Katiba hiyo ili kuwa rahisi kuwa navyo mifukoni kurahisisha marejeo ya Katiba mahali popote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu pia itaendelea kumarisha utoaji wa elimu kwa umma kuhusu Haki za Binadamu. Jumla ya Wilaya 40 zitatembelewa na kuelimisha wananchi juu ya Haki za Binadamu na kutoa taarifa kuhusu utekelezaji wa mikataba mbalimbali ya Kimataifa juu ya Haki za Binadamu kwenye mamlaka zinazohusika.

Aidha, Wizara itaendelea kutembelea magereza 16 na vituo vya polisi, kwa madhumuni ya kukagua hali ya waliozuiliwa katika sehemu hizo kwa lengo la kuhakikisha kwamba Haki za Binadamu zinahifadhiwa na kudumishwa. Wizara, kupitia Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora itaendelea kupokea, kuchunguza na kushughulikia malalamiko yanayohusu uvunjwaji wa Haki za Binadamu na ukiukwaji wa misingi ya Utawala Bora. Katika Mkakati wa kuipeleka Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora karibu na watu, matawi 2 ya Ofisi za Tume yatafunguliwa huko mkoani Lindi na Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2006/07, Wizara itaendelea na jukumu la kuratibu utekelezaji wa Programu ya Kuboresha Sekta ya Sheria. Utekelezaji wa Programu hii utaweka mfumo thabiti wa kisheria na kuharakisha harakati za Serikali katika kuondoa umaskini, kupitia Dira ya Wizara ya Haki Sawa Kwa Wote na kwa Wakati. Waheshimiwa Wabunge wote mtakubaliana nami kwamba Sekta ya Sheria inagusa kila sekta ya Uchumi na ya Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli zote zinategemea sheria, taratibu za kisheria na utawala bora. Juhudi za kupunguza umaskini hutegemea sana amani, utulivu na uhakika wa usalama wa maisha na mali za wananchi. Upatikanaji wa mambo hayo ni lazima uendane na ustawi wa mazingira ya utawala unaotokana na utawala wa Sheria.

Utekelezaji wa Sera zote za Kiuchumi na Kijamii katika kuleta maendeleo ya nchi zinategemea Sekta ya Sheria. Kwa sababu hiyo utekelezaji wa malengo ya Programu ya Sekta ya Sheria utatiliwa mkazo ili kuboresha mazingira yatakayowezesha kupunguza matatizo ya utekelezaji wa Sera na Programu za Sekta nyingine za kiuchumi na kijamii, hususan uwekezaji na uzalishaji mali ili kupunguza na hatimaye kuondoa umaskini katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chini ya Programu ya Kuboresha Sekta ya Sheria, Wizara inatarajia kuimarisha ofisi ya uratibu wa Programu kwa kuajiri wataalamu zaidi kuendeleza rasilimali watu katika kusimamia Programu ya Kuboresha Sekta ya Sheria katika Taasisi na Asasi zinazotekeleza Programu hii kwa kuwapatia mafunzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya wasimamizi 45 kutoka Taasisi na Asasi za Sheria, wasimamizi 4 kutoka katika ofisi ya Programu na wakuu wote wa Taasisi na Asasi za Sekta ya Sheria, na maofisa 120 watapatiwa mafunzo ya mabadiliko ya utashi (*Change Management).* Aidha, mazingira ya kufanyia kazi kwa ofisi za kusimamia programu yataboreshwa kwa kupatiwa vitendea kazi bora zaidi na vya kutosha. Orodha kamili ya wadau ambao ni watekelezaji wakuu wa Programu pamoja na majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chini ya mfuko wa pamoja (*Basket Fund*) Programu itajenga majengo zaidi ya Mahakama na kuendelea kuyakarabati majengo yaliyopo. Kazi hii itafanyika kwa awamu. Aidha, jengo la Ofisi ya Makao Makuu ya Wizara ya Katiba na Sheria litajengwa kwa utaratibu huu. Waheshimiwa Wabunge, jambo la msingi la kuzingatia katika Programu hii ni kwamba chini ya mfuko wa pamoja, utekelezaji wa majukumu unategemea sana michango ya pamoja kati ya Serikali, Wafadhili wetu na Wananchi.

Mwongozo wa usimamizi wa mfumo wa usimamizi wa Programu utaandaliwa (*Monitoring and Evaluation System).* Vifaa vya kutendea kazi katika maktaba 3 za Kisheria vitaboreshwa na mfumo wa kusimamia habari utafungwa. Aidha, mitaala ya kufundishia Sheria itaandaliwa, mafunzo kwa watumishi kuhusu usimamizi wa Programu yatatolewa na utaandaliwa mfumo wa mtandao utakaounganisha mawasiliano kati ya Taasisi zilizomo kwenye Sekta ya Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuongeza ufanisi katika Sekta ya Sheria na hivyo kuboresha utoaji huduma kwa wateja na wananchi kwa ujumla, Wizara yangu imetenga bajeti kwa ajili ya kuteuliwa majaji 20 katika mwaka huu wa fedha. Ongezeko hilo la majaji pamoja na mikakati mingine itasaidia sana kupunguza kesi nyingi zilizopo Mahakama Kuu zinazosubiri kusikilizwa. Aidha, Wizara yangu inakusudia kuwapeleka watumishi wa kada zote kwenye mafunzo ya muda mfupi na mrefu katika taaluma zao na ujuzi maalumu unaohitajika hususan kuwasomesha Mahakimu 6 na Mawakili 10 katika viwango vya Shahada ya Uzamili, Mahakimu na watendaji 99 katika mafunzo ya *Diploma* ya Juu, *Diploma* na cheti, na watumishi wa Mahakama wa kada zilizosalia wapatao 234 katika mafunzo ya muda mfupi ya fani mbalimbali. Aidha, Wizara itaajiri watumishi wapya 57 hasa Mawakili wa Serikali 27 na watumishi wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Uendeshaji wa Mashtaka itatoa mafunzo ya muda mrefu, mfupi, semina na warsha ndani na nje ya nchi. Mawakili wa Serikali 6 watapata mafunzo ya muda mrefu yaani shahada za uzamili katika sheria na Mawakili 50 watapata mafunzo ya muda mfupi katika taaluma ya sheria. Aidha, Idara itatoa mafunzo ya muda mfupi kwa makatibu muhtasi 5, ili kuendeleza uwezo wao na kuboresha ufanisi. Halikadhalika mafunzo ya muda mfupi kwa mawakili 30 waajiriwa wapya *(induction course)* yatatolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Haki za Binadamu inatarajia kuajiri watumishi 81 na itatoa mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi 6. Waheshimiwa Makamishna watahudhuria mafunzo kuhusu namna mbadala ya kutatua migogoro (*Alternative Dispute Resolution)* na namna ya kusikiliza mashauri na kuandika maamuzi. Watumishi katika kada ya uchunguzi watahudhuria mafunzo kuhusu Haki za Binadamu na Utawala Bora na utekelezaji wa sheria. Katika mwaka wa fedha 2006/2007, Tume inatarajia kusomesha watumishi katika maeneo ya makosa ya jinai kwa kutumia mtandao wa kompyuta (*e-Crime*) na Usimamizi wa fedha na uongozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2006/2007, Wizara yangu imelenga kuendelea na uboreshaji na uimarishaji wa vyombo vya utoaji haki nchini. Azma hiyo itatekelezwa kwa kuboresha mazingira ya kazi katika Ofisi zote za Mahakama, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na Tume ya Kurekebisha Sheria kwa kuzipatia vitendea kazi vya kisasa na bora zaidi pamoja na vyombo vya usafiri hususan usafiri kwa mahakimu wa Mahakama za Mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu itaendelea na juhudi za utoaji haki nchini kwa kuimarisha vyombo na mfumo wa utoaji haki katika mwaka wa fedha 2006/07. Usimamizi na ukaguzi katika ofisi za Kanda za Mahakama na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali utaimarishwa. Kila robo mwaka Ofisi zitakaguliwa. Aidha, Wizara itafuatilia utekelezaji wa Mpango na Bajeti, Ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali na taratibu za manunuzi katika Ofisi za Kanda za Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mahakama za ngazi zote kwa lengo la kuongeza uwajibikaji kwa wananchi katika utekelezaji wa Mipango yetu na matumizi ya fedha za umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha ujao, Wizara itaendelea kuungana na timu mbalimbali za Serikali za majadiliano *Government Negotiating Teams (GNT)* katika kujadili Mikataba mbalimbali itakayofungwa na Serikali.

Lengo litakuwa ni kuhakikisha kuwa maslahi ya nchi yanalindwa kisheria katika mikataba hiyo. Ni matumaini yangu kwamba utaalam wa kisheria wa Mawakili wa Serikali watakaohusika, utaungana na ule wa Wataalam wengine katika fani zinazohusika na maeneo yatakayojadiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uzoefu tulioupata siku za nyuma yapo mambo ya msingi ya kufanya na hatua za kuchukua ili kuboresha ushiriki wetu katika majadiliano ya mikataba ya Serikali. Baadhi ya hatua hizo ni kama ifuatavyo:-

(a) Kuhakikisha kwamba kunafanyika maandalizi ya kutosha ya pamoja kwa sekta na idara zote zinazohusika na mkataba unaohusika na kuhakikisha kwamba kuna mkakati wa majadiliano wa timu hizo ikiwa ni pamoja na mambo ambayo hayatakuwa na mjadala;

(b) Kuhakikisha kwamba Mawakili wa Serikali katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mawakili wa Serikali walio katika Wizara na Idara za Serikali wanapewa elimu ya fani ya majadiliano katika maeneo maalum kama vile madini, gesi asilia, mafuta, kodi, mambo ya fedha, uhakiki wa miradi (*project evaluation and implementation*) na kadhalika.

(c) Kuongeza usimamizi wa hatua zote za majadiliano wa mikataba ili kuweza kubaini matatizo kabla ya mkataba kusainiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuchukua nafasi hii kuzishauri Wizara na Idara za Serikali kuwapa mafunzo ya kuwaongezea ujuzi mawakili waliopo kwenye ajira zao kwenye maeneo hayo muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2005, Bunge lilipitisha Sheria ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Sheria hii inampatia Mwanasheria Mkuu wa Serikali mamlaka ya kusimamia kwa ufanisi zaidi kazi za ushauri wa kisheria Serikalini. Sheria hiyo imeanza kufanya kazi nahatua kadhaa za kuitekeleza zimeanza. Katika mwaka huu wa fedha, tutakamilisha taratibu za kuwatambua na kuwasajili Mawakili wa Serikali na Wanasheria wengine wanaofanya kazi katika Wizara na Taasisi nyingine za Serikali. Baada ya zoezi hilo, Mwanasheria Mkuu ataweza kutoa maelekezo mahsusi na ya jumla kwa Wanasheria Serikalini ili kusimamia utekelezaji wao wa majukumu ya kisheria. Hii yote itawezesha Wanasheria ndani ya Serikali waweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi na kwa viwango katika kulinda maslahi ya Serikali na ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Kabidhi Wasii Mkuu imekuwa Wakala wa Serikali na kuzinduliwa tarehe 23/06/2006. Lengo la kuifanya ofisi hii kuwa wakala ni kuimarisha ili uweze kutoa huduma bora kwa wananchi chini ya Wakala wa Serikali, *Registration, Insolvency and Trusteeship Agency (RITA).* Itaendelea kusajili vizazi na vifo, ndoa na talaka, kusimamia ufilisi, kusajili wadhamini, udhamini wa mali isiyokuwa na mwenyewe na uasili wa watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu itaendelea na jitihada za kukabiliana na janga la UKIMWI kwa kutoa elimu ya kuepukana na maambukizi ya UKIMWI kwa watumishi na kutekeleza mpango ulioandaliwa kuhusiana na athariza UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rushwa ni adui wa haki na maendeleo. Wizara yangu itaendelea kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Kupambana na Rushwa. Wizara yangu itajadili Taarifa ya Tume ya Kurekebisha Sheria kuhusu Sheria ya Kuzuia Rushwa na kwa kushirikiana na Taasisi ya Kuzuia Rushwa kuandaa rasimu ya kwanza kwa ajili ya kujadiliwa na Baraza la Mawaziri na kutayarisha sheria itakayowasilishwa Bungeni katika kikao cha Novemba, 2006.

Aidha, Wizara itaimarisha ukaguzi wa Kanda na Mahakama kwa ngazi zote ili kusimamia ufanisi na utendaji wa shughuli zote za Ofisi na kuhakikisha kuwa Mkataba kwa Mteja unatekelezwa kwa makini ili kuziba mianya ya rushwa katika utendaji kazi Serikalini. Wizara pia itaendesha na kutoa mafunzo ya maadili na madhara ya vitendo vya rushwa kwa watumishi wote katika ofisi zote za Kanda na katika Mahakama. Aidha, Wizara yangu itazingatia masuala ya Jinsia na Uhifadhi wa Mazingira katika mipango yake hususan kuendelea kuimarisha mradi wa *Legal and Gender Responsive Project* na kutoa mafunzo kwa watumishi wa Wizara juu ya Sera ya Mazingira na Mkakati wa kuhifadhi Mazingira; vyanzo vya maji na ardhi, uliotolewa na Ofisi ya Makamu wa Rais ili Mkakati huu uweze kueleweka na kutekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhitimisha hotuba yangu napenda nitoe shukrani zangu za dhati kwa viongozi wa Wizara walionitangulia. Aliyekuwa Waziri Mheshimiwa Harith Bakari Mwapachu, Mbunge wa Tanga Mjini na sasa Waziri wa Usalama wa Raia; aliyekuwa Mwanasheria Mkuu Mheshimiwa Andrew John Chenge, Mbunge wa Bariadi Mashariki na sasa Waziri wa Afrika Mashariki. Na aliyekuwa Naibu Mwanasheria Mkuu na Katibu Mkuu Mheshimiwa Johnson Paulo Mwanyika, ambaye sasa ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuweka misingi imara ya utekelezaji wa Sheria na maslahi ya wafanyakazi. Ninafarijika kuwa ninayo hazina kubwa ya kupata ushauri kila ninapohitaji. Nawashukuru na naomba tuzidi kushirikiana. Nawashukuru sana viongozi wa Mahakama, Mheshimiwa Barnabas Samatta, Jaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania na Mheshimiwa Amir Manento, Jaji Kiongozi kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakinipatia tangu nilipoteuliwa kuwa Waziri katika Wizara hii. *(Makofi)*

Nawashukuru pia Mheshimiwa Jaji Robert Kisanga, Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora; Mheshimiwa Jaji Anthony Bahati, Mwenyekiti wa Tume ya Kurekebisha Sheria na Mheshimiwa Balozi Bi Mwanaidi Maajar aliyekuwa Mwenyekiti wa Shirika la Sheria Tanzania ambao pia wamenipatia ushirikiano mkubwa na ninafarijika kuwa ninayo hazina kubwa ya kupata ushauri kila ninapouhitaji.

Nawapongeza watendaji mbalimbali katika Wizara, nikianza na Bwana Vincent Kitubio Damian Lyimo kwa kuteuliwa kuwa Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Katibu Mkuu. Tayari amekwishaonyesha uwezo wake mkubwa wa kusimamia maboresho katika Sekta kama alivyofanya Mheshimiwa Mwanyika aliyemtangulia. Napenda vile vile kumpongeza Bibi Crecencia Makuru kwa kuteuliwa kuwa Katibu wa Tume ya Kurekebisha Sheria na Bwana Dickson Ernest Maimu kuwa Mtendaji Mkuu wa *RITA*. Vile vile napenda kumpongeza Bwana Casmir Sumba Kyuki kwa kuteuliwa kuwa Mwandishi Mkuu wa Sheria. Bila shaka Bwana Kyuki atafanya kila jitihada kuziba pengo lililoachwa na Marehemu Siegfried Kato Byarugaba Lushagara aliyekuwa Mwandishi Mkuu wetu wa Sheria kwa siku nyingi. Nawashukuru watendaji wengine wakuu waliopo, katika Wizara yangu, Bwana Augustine Mwarija, Msajili wa Mahakama ya Rufani, Bwana Gadi Mjemmas, Katibu Mtendaji wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na Bi Daria Bigeye, Kaimu Mshauri Mkuu wa Shirika la Sheria Tanzania. Wao pamoja na viongozi wengine na wafanyakazi wote katika Wizara yangu wameniwezesha kutekeleza majukumu kikamilifu na hata leo nimeweza kusimama mbele yenu kusoma hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Engera Anold Kileo, Mheshimiwa Natalia Kimaro na Mheshimwia Edward Rutakangwa, kwa kuteuliwa kwao hivi karibuni kuwa Majaji wa Mahakama ya Rufani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa shukrani za dhati kwa nchi wahisani na Taasisi za Kimataifa ambazo zimeendelea kutoa misaada mbali mbali ya kuiendeleza Sekta ya Sheria nchini kama ifuatavyo:- Serikali ya Denmark, Finland, Sweden, Ubelgiji, Ujerumani, Marekeni, Ireland, Uingereza, Norway na Uholanzi; na Mashirika

ya Kimataifa ya Benki ya Dunia, *DANIDA, UNDP, USAID, UNICEF, GTZ, CIDA (Canada)* na *SIDA (Sweden)*. (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio haya, bado zipo changamoto mbalimbali kama ifuatavyo:-

(a) Bado upo ucheleweshaji katika utoaji wa haki. Upo mlundikano wa mashauri Mahakamani ambao ni kero kwa wananchi na Mahakama zenyewe. Waheshimiwa Wabunge wanakerwa na ucheleweshaji huu ambao pia unakwenda kinyume na kasi na viwango vinavyotakiwa kutenda haki.

(b) Bado wananchi wengi wanashindwa kuifikia huduma ya Mahakama, aidha kwa kutokujua haki zao au kutokuwa na uwezo kutokana na umaskini walio nao, au Mahakama kuwa mbali au vikwazo vya lugha iliyoandikwa katika sheria, dhana ya mila potofu aua rushwa na kadhalika.

Ufinyu wa bajeti unaosababisha kutofanyika kwa vikao vya kuendesha kesi, kuwalipa mashahidi, posho za wazee wa baraza, vitendea kazi kwa Majaji, Mahakimu wa ngazi zote na Mawakili wa Serikali na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika muda mfupi niliokaa kwenye Wizara hii, nimeona jinsi Wizara ilivyo na majukumu mazito yanayogusa nyanja zote za kiuchumi, kijamii kisiasa na kiutamaduni. Kwa jinsi shughuli zake zilivyo nyingi, ninaishukuru Serikali kutenga rasilimali zaidi katika mwaka huu wa fedha ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Katika kufanikisha azma ya Serikali ya kuwa na Utawala wa Sheria na Utawala bora, ni mategemeo yangu kwamba Serikali itaendelea kuwa na mtazamo wa kipekee kuipa kipaumbele Wizara hii ambayo ni muhimu katika kufanikisha utekelezaji wa malengo ya Dira ya Taifa pamoja na Malengo ya Millenia kama yalivyozingatiwa katika Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini Tanzania (MKUKUTA). Hii ni kutokana na ukweli kwamba Sekta ya Sheria inaweka mazingira mazuri ya mfumo na Utawala wa Sheria ulio imara kwa wawekezaji wa ndani na nje kuwekeza na vile vile Watanzania na wageni kufanya shughuli zao bila wasiwasi na hivyo kukuza uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba kiwango cha fedha za matumizi ya kawaida kilichotengwa kwa Wizara yangu kwa mafungu yote ni juu kidogo kwa viwango vya mwaka 2005/06, hi ni kutokana na ongezeko katika mishahara ya watumishi na pia katika fedha za Matumizi ya Maendeleo. Katika kipindi cha 2006/07 kiasi cha shilingi 66,849,887,000/= kimetengwa, ukilinganisha na shilingi 49,986,929,600/= ambacho kilitengwa katika mwaka wa fedha 2005/06, sawa na ongezeko la shilingi 16,862,957,400/= au asilimia 33.73.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na Waheshimiwa Wabunge, napenda niwahakikishie kwamba, utekelezaji wa Programu ya Kuboresha Sekta ya Sheria utaendelea kutekelezwa kwa nguvu na wadau mbali mbali katika mwaka huu wa fedha. Ni matarajio yangu

kwamba uwezo wetu utaongezewa kirasilimali na wafadhili na kwa wakati kufuatia kukamilika kwa taratibu zote za kuwa na mwongozo nilioutaja hapo awali pamoja na Hati ya Makubaliano. Vile vile, utekelezaji utaimarishwa na kukamilika kwa taratibu za kuwapata wataalamu katika ofisi ya Uratibu wa Programu katika Wizara yangu ambao ndio watakuwa Wasimamizi na Waratibu wa Programu hiyo. Ninawaombeni ushirikiano wenu katika utekelezaji wa majukumu haya kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka huu wa fedha 2006/07, kiasi cha shilingi 66,849,887,000/= zitahitajika kutekeleza shughuli zilizopangwa. Kati ya fedha hizo, fedha za Matumizi ya Kawaida ni shilingi 50,,027,746,000/= na fedha za Matumizi ya Maendeleo ni shilingi 16,822,141,000/=. Naliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe makadirio hayo ya fedha za Maendeleo na Matumizi ya kawaida kwa mafungu sita kama ifuatavyo:-

**Fungu 40: Mahakama:**

| | | |
|---|---|---|
| Matumizi ya Kawaida | shs. | 36,965,949,000/= |
| Matumizi ya Maendeleo (ndani) | shs. | 4,060,001,000/= |
| Matumizi ya Maendeleo (nje) | shs. | 300,000,000/= |
| **Jumla** | **shs** | **41,325,950,000/=** |

**Fungu 41: Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali**

| | | |
|---|---|---|
| Matumizi ya Kawaida | shs. | 7,667,198,000/= |
| Matumizi ya Maendeleo (ndani) | shs. | 466,000,000/= |
| Matumizi ya Maendeleo (nje) | shs. | 11,503,140,000/= |
| **Jumla** | **shs** | **19,636,338,000/=** |

**Fungu 55: Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora**

| | | |
|---|---|---|
| Matumizi ya Kawaida | shs. | 2,938,178,000/= |
| Matumizi ya Maendeleo (ndani) | shs. | NIL |
| Matumizi ya Maendeleo (nje) | shs. | 260,000,000/= |
| **Jumla** | **shs** | **3,198,178,000/=** |

**Fungu 59: Tume ya Kurekebisha Sheria**

| | | |
|---|---|---|
| Matumizi ya Kawaida | shs. | 785,972,000/= |
| Matumizi ya Maendeleo (ndani) | shs. | NIL |
| Matumizi ya Maendeleo (nje) | shs. | NIL |
| **Jumla** | **shs** | **785,972,000/=** |

**Fungu 64: Mahakama ya Biashara**

| | | |
|---|---|---|
| Matumizi ya Kawaida | shs. | 857,138,000/= |

Matumizi ya Maendeleo (ndani) shs. NIL
Matumizi ya Maendeleo (nje) shs. 233,000,000/=
**Jumla shs 1,090,138,000/=**

**Fungu 90: Mahakama ya Ardhi**

Matumizi ya Kawaida shs. 813,311,000/=
Matumizi ya Maendeleo shs. NIL
**Jumla shs 813,311,000/=**

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki cha mwaka wa fedha wa 2006/07, Wizara yangu inatarajia kukusanya kiasi cha shs.2,210,349,000/= kama maduhuli ya Serikali. Mchanganuo wa makusanyo ni kama ifutavyo:-

Fungu 40: Mahakama:shs. 751,306,000/=.

Fungu 41: Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali
shs. 621,401,000/=.
Fungu 55: Tume yaHaki za Binadamu na Utawala Bora
shs. 642,000/=

Fungu 59: Tume ya Kurekebisha Sheria Shs. -

Fungu 64: Mahakama ya Biashara Shs. 800,000,000/=

Fungu 90: Mahakama ya Ardhi Shs. 37,000,000/=

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:**Waheshimiwa Wabunge kabla hatujaendelea tunao wageni wa Waheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mheshimiwa Ali Ameir na Mheshimiwa Vuai Abdallah wageni hao wanatoka Zanzibar ni Madiwani 23 wa CCM na viongozi wa CCM wa Majimbo ya Mwanakwerekwe, Fuoni na Magogoni wanaoongozwa na Ndugu Matogo Juma Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi Unguja. Mnaweza kusimama wote.

Ahsante sana. (*Makofi)*

**MHE. PINDI H. CHANA(k.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni Na. 81(1), Kanuni za Bunge, Toleo la 2004, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2005/2006 na Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2006/2007 na kuliomba Bunge lako Tukufu liipokee na kuijadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuipelekea kazi ya kuchambua Bajeti ya Wizara hii, Kamati yangu ilikutana Dar es Salaam tarehe 30 Mei, 2006, kutekeleza kazi hii na kupokea maelezo ya Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria yaliyowasilishwa na Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, (Mb.), Waziri wa Katiba na Sheria. Katika maelezo hayo, Kamati ilijulishwa juu ya muundo wa Wizara ambao unahusisha Mahakama ya Tanzania ambayo ni muhimili mmojawapo wa dola, na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali yenye idara saba, tano kati ya hizo zikiwa za kitaaluma na mbili za huduma. Muundo huo pia unahusisha asasi huru ambazo ni Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na Tume ya Kurekebisha Sheria.

Aidha, Kamati ilijulishwa kuwa Wizara inaongozwa na dira inayolenga kuwa na Maendeleo ya Haki ya Jamii, Usawa na Utawala wa Sheria. Pia Kamati ilifahamishwa juu ya majukumu mbalimbali ya Wizara hiyo likiwemo jukumu la utoaji haki linalosimamiwa na Mahakama ya Tanzania. Majukumu mengine ni ushauri wa kisheria kwa Serikali na taasisi zake, uandishi wa sheria, na kadhalika kazi ambazo zinasimamiwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Kamati ilipokea taarifa ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati uliotolewa katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2005/2006. Ushauri huu ulikuwa kama ifuatavyo: (1) Kuiomba Serikali ifuatilie tatizo la wafungwa waliohukumiwa adhabu ya kifo na ikiwezekana imshauri Rais atoe msamaha kwa watu waliokaa muda mrefu gerezani badala ya kuwaacha waishi katika hali hiyo; (2) Kuiomba Wizara iendelee kulitafutia ufumbuzi tatizo la usafiri linalowakumba Mahakimu ikiwezekana kutafuta wakopeshaji wenye masharti nafuu; na (3) Kuiomba Wizara ijitahidi kuboresha maslahi ya mahakimu wote nchini na kuwapatia vivutio zaidi vya kazi hususan mahakimu wanaofanya kazi katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulithibitishia Bunge lako Tukufu kwamba baadhi ya ushauri wetu umetekelezwa. Aidha, Serikali imeahidi kuendelea kuyafanyia kazi mapendekezo yetu mengine hatua kwa hatua. Pamoja na hayo, bado Kamati inasisitiza kuwa Serikali iendelee kushughulikia tatizo la usafiri kwa mahakimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, Kamati ilipokea taarifa ya Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa kipindi cha Mwaka 2005/2006 ambapo ilielezwa juu ya utekelezaji wa Programu ya Kuboresha Sekta ya Sheria chini ya Mkakati wa Muda wa Kati 2005/2006-2007/2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine lilihusu Uendeshaji wa Kesi na Kupunguza Mlundikano wa Kesi Mahakamani. Kamati ilijulishwa juu ya jitihada mbalimbali zilizofanywa na Mahakama hadi Aprili, 2006 kushughulikia kesi na kupunguza mlundikano huo. Kazi hii ilifanywa na Mahakama za Mwanzo, Mahakama za Wilaya/Mahakama za Hakimu Wakazi, Mahakama ya Biashara, Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani. Napenda nitumie nafasi hii pia kuzipongeza mahakama zote kwa jitihada zinazofanywa kupunguza mlundikano huo na kuhakikisha kuwa uendeshaji wa kesi unafanyika haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Ushauri wa Kisheria, Uendeshaji wa Mashtaka, Uandishi wa Sheria na Utafiti wa Sheria, Kamati ilijulishwa kuwa hizi ni jumla ya shughuli mbalimbali zinazofanywa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kupitia Idara zake nilizozitaja awali. Katika kutekeleza jukumu hili, Kamati ilielezwa kuwa katika kipindi kilichopita, Ofisi hii ilishiriki katika majadiliano ya kuanzishwa kwa Protokali ya Umoja wa Afrika ya Kusimamia Demokrasia, Uchaguzi na Utawala Bora, Majadiliano ya kuziunganisha Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Mahakama ya Afrika ya Haki na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali ya hayo na kwa faida ya Bunge lako Tukufu, kati ya tarehe 14 – 24 Machi, 2006, Kamati yangu ilifanya ziara fupi kutembelea asasi na wizara kadhaa inazozisimamia kwa ajili ya kupata maelezo kuhusu majukumu yanayofanywa na vyombo hivyo. Kati ya wizara na asasi hizo ni Wizara ya Katiba na Sheria, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Tume ya Kurekebisha Sheria, Kabidhi Wasii Mkuu na Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipotembelea Ofisi ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali, ilionyeshwa mtandao uliobuniwa na Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali na Mwanasheria Mkuu wa Serikali wenye lengo la kuharakisha uchapishaji wa miswada ya sheria. Kamati ilielezwa kuwa mfumo huu utakaoanza kazi miezi michache ijayo, utaharakisha uchapishwaji wa miswada ya sheria kwa vile kazi hiyo sasa itakuwa ikifanyika moja kwa moja kwa kutumia mtandao wa kompyuta. Haya ni mafanikio mazuri katika sekta ya Uandishi wa Sheria na natumaini yatatatua tatizo la muda mrefu la ucheleweshwaji wa miswada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora mbali ya kusikia mafanikio yaliyopatikana, pia Kamati ilisikia matatizo kadhaa yanayoikabili Tume hiyo. Matatizo hayo ni pamoja na Tume kupata ushirikiano mdogo kutoka kwenye vyombo na asasi zinazolalamikiwa na wananchi. Katika suala hili Kamati ilijulishwa kuwa vyombo hivyo vimekuwa vikichukua muda mrefu kuitikia malalamiko ya wananchi na hivyo kuchelewesha maamuzi ya Tume. Aidha, Tume iliomba kuwa Ripoti zake zijadiliwe na Bunge ili kuwawezesha Waheshimiwa Wabunge kufahamu majukumu mbalimbali ya Tume. Kwa kuelewa umuhimu wa Tume hii, Kamati inashauri kuwa Ripoti za Tume hii zifanyiwe kazi na kupelekwa Bungeni.

Kwa upande wa Tume ya Kurekebisha Sheria, Kamati ilibahatika kufahamu kazi mbalimbali zinazofanywa na Tume hii. Hata hivyo, ilibainika kuwa Tume hushindwa

kutekeleza majukumu yake kikamilifu hususan kufanya utafiti wa sheria na kutoa huduma ya ushauri wa kisheria kwa wananchi kutokana na ufinyu wa Bajeti ambao unatokana na ukomo (*ceiling*) wa Bajeti unaowekwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali ya Tume ya Kurekebisha Sheria, Kamati ilijulishwa juu ya Uimarishaji wa Ofisi ya Kabidhi Wasii Mkuu ambayo kama nilivyodokeza hapo awali Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ilipata fursa ya kuitembelea na kujionea hali halisi ya Ofisi hiyo. Kutokana na matatizo makubwa yanayoikabili Ofisi hii, Kamati inaunga mkono kwa dhati Programu ya kuifanya iwe wakala wa Serikali. Kwa kufanya hivyo Kamati inaamini kuwa itajiendesha vizuri na kusimamia ukusanyaji wa maduhuli kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimegusia maeneo haya machache ili kulipa picha Bunge lako Tukufu juu ya mafanikio na matatizo kadhaa yanayoikabili Wizara hii ambayo Kamati iliyashuhudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengine ambayo Kamati ilijulishwa yalihusu mikakati iliyowekwa na Mahakama katika Uimarishaji wa Utoaji Haki, Mafunzo na Ajira kwa Mahakimu, Makarani wa Mahakama na Mawakili wa Serikali na Uboreshaji wa Mazingira ya kazi katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mahakama. Ilifahamika kuwa uboreshaji huu unahusu ukarabati na ununuzi wa majengo na vitendea kazi kwa ajili ya ofisi zote za Wizara.

Mwisho, Kamati ilielezwa juu ya masuala ya jumla yanayohusu uandaaji wa Sera ya Sekta ya Sheria na Maamuzi yaliyotolewa na Mahakama Kuu kuhusu Katiba likiwemo suala la Mahakama kufuta vipengele katika Sheria ya Uchaguzi vilivyokuwa vinaruhusu wagombea kujigharamia katika kampeni za uchaguzi na hatua ambazo Serikali imechukua dhidi ya uamuzi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Kamati ilipokea maelezo juu ya matatizo yaliyoathiri Utekelezaji wa Mpango wa Mwaka 2005/2006 licha ya mafanikio yaliyopatikana. Ilifahamika kuwa katika ujumla wake matatizo haya yalitokana na ufinyu wa bajeti inayotengwa kila mwaka na kiasi kinachotengwa kutotolewa kwa wakati na hivyo kuathiri kwa kiwango kikubwa suala la utoaji na usimamizi wa haki na utawala wa sheria.Katika Mwaka wa Fedha 2006/2007, Kamati ilijulishwa juu ya majukumu mbalimbali yatakayotekelezwa na Wizara na kazi zilizopangwa kufanyika. Mwisho, Kamati iliombwa kupitisha Maombi ya Fedha kwa mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo ya Wizara, Kamati ilipata fursa ya kutoa maoni na ushauri katika maeneo mbalimbali yakiwemo yaliyohusu mahakama na sekta ya sheria kwa ujumla. Kwanza, napenda nikiri kuwa Wizara hii ina majukumu mengi ambayo kutokana na uzito wake, Kamati inashauri kuwa katika Bajeti ijayo Serikali ijitahidi kuitengea fedha za kutosha na kuipatia fedha hizo kwa wakati ili iweze kutekeleza majukumu hayo ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakumbukwa kuwa katika Uchaguzi Mkuu wa 2005 aliyekuwa Mgombea Mwenza wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Hayati Jumbe Rajab Jumbe, alifariki ghafla siku chache kabla ya kufanyika kwa Uchaguzi Mkuu nchini Tanzania, 30 Oktoba, 2005. Kufuatia kifo chake ilibidi kampeni za wagombea zisitishwe kwa muda na uchaguzi uahirishwe hadi 14 Disemba, 2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukio hilo ambalo halikutarajiwa liliiathiri Serikali, Tume ya Uchaguzi, vyama vya siasa na wagombea wa nafasi mbalimbali kufikia hatua ambayo ama baadhi ya vyama vilishindwa kuendelea na kampeni au baadhi ya wagombea walilazimika kujipanga upya kwa kukosa fedha na nyenzo muhimu kwa ajili ya uchaguzi. Kutokana na athari zilizojitokeza, Kamati inashauri kuwa Wizara ishirikiane na Tume ya Uchaguzi kuipitia upya Sheria ya Uchaguzi na kuifanyia marekebisho ili kuweka utaratibu bora wa kukabiliana na tatizo kama hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza hapo mwanzo, miongoni mwa majukumu ya Wizara hii ni pamoja na kutoa ushauri wa kisheria na kushiriki katika majadiliano ya mikataba inayohusu Serikali. Kwa kutambua kuwa kuna malalamiko yanayotolewa na wananchi juu ya baadhi ya mikataba mibovu ambayo imeliingizia Taifa hasara kubwa, Kamati inashauri kuwa Serikali inapokusudia kuingia mkataba mpya, uwekwe utaratibu wa kisheria wa kuufanyia ukaguzi wa kina (*double check*) mkataba unaohusika ikiwezekana kuhusisha chombo au vyombo vingine vya kitaalamu zaidi na ikibidi hata wadau kuhakikisha kuwa mkataba unaohusika unajitosheleza na kwamba hauwezi kuliletea Taifa athari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyofahamu Mahakama kama muhimili mmojawapo wa dola, imepewa jukumu la utoaji haki nchini. Ili jukumu hili liweze kutekelezwa kikamilifu hapana budi huduma hii iwafikie wananchi wengi kuanzia vijijini. Hata hivyo, Kamati yangu imebaini kuwa maeneo mengi nchini hayana mahakama za mwanzo na hivyo kuwafanya baadhi ya wananchi waikose huduma hii muhimu au waifuate katika vijiji jirani. Kutokana na tatizo hili, Kamati inashauri kuwa Serikali ijaribu kuwahamasisha wananchi wengi ili washiriki katika ujenzi wa mahakama hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza kwa kifupi hapo mwanzo juu ya matatizo kadhaa yanayoikabili Tume ya Kurekebisha Sheria ambayo Kamati yangu iliyashuhudia wakati wa ziara yake, Kamati inashauri kuwa katika Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha ujao, Serikali iongeze Bajeti ya Tume ya Kurekebisha Sheria ili iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu na kuwafikia wananchi wengi hadi vijijini. Aidha, Wizara izifanyie kazi sheria zilizokwisharekebishwa na Tume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya magereza yetu nchini yana idadi kubwa ya watuhumiwa waliowekwa rumande ikilinganishwa na wafungwa. Hali hii imesababisha kuwepo kwa mlundikano wa watuhumiwa hao katika magereza hayo. Kwa sababu hiyo, Kamati inashauri kuwa Wizara ya Katiba na Sheria ishirikiane na Wizara ya Usalama wa Raia na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kutafuta mbinu za kupunguza mlundikano huo na kuharakisha uendeshaji wa kesi mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako Tukufu litakumbuka kuwa hivi karibuni kumeanzishwa Mkataba wa Afrika unaozitaka nchi za Kiafrika kuzingatia na kuheshimu misingi ya demokrasia na utawala bora (*African Peer Review Mechanism*). Kwa kuwa hadi hivi sasa Tanzania bado haijaridhia Mkataba huu, Kamati inashauri kuwa Serikali ifuatilie na kuhakikisha kuwa Tanzania inaridhia mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa jumla haya ndiyo maoni na ushauri wa Kamati yangu wakati ilipojadili Bajeti ya Wizara hii. Natumaini kuwa maeneo ambayo sikuweza kuyagusia, yatazungumziwa na Wajumbe wa Kamati hii watakapopata nafasi ya kuchangia hoja hii. *(Makofi)*

Aidha, Kamati yangu inapenda kukuhakikishia kuwa baada ya kuridhishwa na maelezo ya Wizara ya Katiba na Sheria, Kamati ilipitisha kwa kauli moja Maombi ya Fedha ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumalizia Taarifa hii kwa kukushukuru kwa kunipatia fursa hii kuwasilisha Taarifa ya Kamati. Vilevile napenda kumshukuru Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Johnson Mwanyika, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Mathias Chikawe, Naibu Waziri, Wizara ya Katiba na Sheria, Katibu Mkuu, Wakuu wa Idara na Vitengo, kwa kutoa maelezo na ufafanuzi wa kina mbele ya Kamati na kuiwezesha kuwasilisha Taarifa hii Bungeni. *(Makofi)*

Aidha, nachukua nafasi hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa kuonyesha umahiri wa hali ya juu wakati wa kuchambua Makadirio ya Wizara hii na kuboresha maeneo mbalimbali kama ilivyojidhihirisha katika Taarifa ya Kamati. Naomba niwataje kama ifuatavyo:-

Wajumbe wa Kamati ni Mheshimiwa George Malima Lubeleje, ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati na Mheshimiwa Tatu M. Ntimizi, ambaye ni Makamu Mwenyekiti. Wajumbe wengine ni Mheshimiwa Pindi H. Chana, Mheshimiwa Stephen J. Galinoma, Mheshimiwa Athumani S. Janguo, Mheshimiwa Rajab Hamad Juma, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Charles N. Keenja, Mheshimiwa Salim Yussuf Mohammed, Mheshimiwa John P. Lwanji, Mheshimiwa Fatma M. Maghimbi,Mheshimiwa Ramadhan A. Maneno, Mheshimiwa Halima J. Mdee, Mheshimiwa Nimrod E. Mkono, Mheshimiwa Abbas Z. Mtemvu na Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa. *(Makofi)*

Mwisho, napenda nimshukuru Katibu wa Bunge, Bwana Damian Foka, watumishi wote wa Ofisi ya Bunge, bila ya kuwasahau Makatibu wa Kamati hii, Ndugu Charles Mloka na Ernest Zulu, kwa kufanikisha shughuli za Kamati kufikia leo tunapohitimisha Taarifa yetu ya mwisho katika Mwaka huu wa Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha jumla ya sh. 66,849,887,000/= kama zilivyombwa na Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria kwa ajili ya Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Pindi Chana. Sasa kabla sijamwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani niwataarifu tu Waheshimiwa Wabunge ili mjiandae kwa wale watakaochangia hoja hii kwa hatua itayofuata ambao watakuwa ni waliochangia mara moja Mheshimiwa William Shellukindo, Dr. Wilbrod Slaa, Mheshimiwa Tatu Ntimizi, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, na Mheshimiwa Anna Komm. *(Makofi)*

Katika waliochangia mara mbili tutakuwa na Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Gosbert Blandes na kama muda utaruhusu Mheshimiwa Diana Chilolo, Yona Kevela, Mheshimiwa Juma N'hunga na Mheshimiwa Ania Chaurembo na tutakuwa tunakwenda hivyo. Kwa wale ambao watakuwa hawapo watachukua nafasi katika wale ambao wameomba.

Baada ya kufikia hapo sasa nimkaribishe Msemaji wa Upinzani, Mheshimiwa Fatma Maghimbi. *(Makofi)*

**MHE. FATMA M. MAGHIMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natanguliza shukrani zangu kwa kunipa fursa hii ya kutoa maoni kwa niaba ya Kambi ya Upinzani kuhusu Bajeti ya Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru wapiga kura wa Jimbo langu la Chake Chake kwa kunipa kura nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Dk. Mary M. Nagu na wasaidizi wake katika Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba kwa jitihada mbalimbali walizozifanya hadi leo hii katika kufikia dira ya Wizara. Hata hivyo, Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna maeneo kadhaa ambayo Serikali kupitia Wizara hii inatakiwa kuyafanyia kazi zaidi. Baadhi ya mambo hayo ni kama ambavyo nitayawasilisha katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na Mahakama. Kati ya sehemu zilizo na kazi ngumu ni Mahakama za Tanzania. Katika Mahakama, kila Jaji ana wastani wa kesi 900 anazotakiwa kuzishughulikia. Lakini katika ngazi zote za Mahakama kuna upungufu wa Mahakimu na Majaji . Matokeo yake huchukua muda kupata hukumu za kesi hasa zinazohusu ibara ya 12 mpaka 29 za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sheria inalazimisha katika baadhi ya kesi kuwe na jopo la Majaji watatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mlundikano huu wa kesi zisizofanyiwa kazi, pia unaleta athari kubwa sana Magerezani ambako kwa sasa kuna mlundikano mkubwa wa

wafungwa na mahabusu wanaosubiri kesi zao kusikilizwa. Mfano, kwa sasa kuna mahabusu zaidi ya 19,100 katika Magereza mbalimbali za Tanzania ikiwa ni zaidi ya asilimia 108 ya uwezo wa Magereza kwa Mujibu wa uchunguzi wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Washitakiwa wengine zaidi ya 30 wamekaa Mahabusu kwa zaidi ya miaka kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani, tunaitaka Serikali ifanye juhudi ya makusudi ya kuwapa mafunzo watumishi wa Idara hii kama Mahakimu na Makarani wa Mahakama. Pia, kuwasambazia sheria zinazofaa kutumika ili kutoa maamuzi yaliyo ya haki na kupunguza idadi ya kesi za rufaa katika Mahakama za juu zinazoleta msongamano wa kesi. Aidha, Mabaraza ya Kata na Mahakama za Mwanzo yapatiwe fungu la kutosha ili kuwasaidia wananchi waishio Vijijini fursa ya kuifikia haki kwa muda mfupi zaidi. Hii pia itasaidia kuondokana na maamuzi ya kesi ndogondogo katika Mahakama za Juu. Kwa sasa Mabaraza mengi ya Kata yaliyoundwa na Sheria ya Mabaraza ya Kata ya mwaka 1985 hayapo kinyume na hitaji la sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua kwa dhati juhudi ya Serikali ya kutatua tatizo hili sugu la mlundikano wa kesi Mahakamani kwa kuanza kutumia mfumo mbadala wa utatuzi wa kesi, yaani *Alternative Dispute Resolution* ambao ulianza kutumika hapa nchini kwetu miaka ya 1990.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo huu mbali na kuwa una miaka 15, haujafanikiwa kupunguza idadi ya mlundikano wa kesi katika Mahakama zetu. Hii ni kutokana na ukweli kuwa *ADR* inatumika katika Mahakama chache sana na ni katika baadhi tu ya siku katika wiki. Mfano, kwa Dar es Salaam, katika Mahakama ya Kisutu hufanyika siku ya Alhamisi tu.

Pia, utaratibu wa kiutawala ulioanzishwa wa kufuatilia mwenendo wa kesi, yaani *Case flow Management* nao unafanyika Mahakama ya Kisutu. Ule utaratibu wa kukamilisha upelelezi ndani ya siku sitini, yaani *60 days rule* ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai ya mwaka 1985 nao pia unaelekea haujatumika, kwani upelelezi huchukua muda mrefu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapendekeza juhudi hizi za *ADR* zifanywe pia katika maeneo mengine ili kuongeza nguvu katika kupunguza kesi na kero zitokanazo na ucheleweshwaji wa kesi hizo. Kama Tume ya Haki za Binadamu ilivyopendekeza katika taarifa ya Utafiti wake wa mwaka 2002/2003, Idara ya Mahakama inabidi ichukue hatua mapema za kutoa nakala za hukumu kwa wakati, kutoa maelekezo kwa wakata rufaa na kadhalika ili kupunguza wingi wa kesi na Mahabusu Magerezani. Tunaamini kuwa haki iliyocheleweshwa ni sawa tu na haki iliyonyimwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefarijika sana kumisikia Mheshimiwa Waziri anasema Ofisi ya Kabidhi Mkuu, Wasii Mkuu imekuwa Wakala kuanzia mwaka huu na itaitwa *RITA*. Kwa hiyo, sina lolote la kusema ikiwa pendekezo hili limeshapita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Idara ya Uandishi wa Sheria kwa kazi nzito wanayoifanya. Nafahamu kwa sasa tunatumia utaratibu mpya wa sheria ambazo zilifanyiwa mapitio mwaka 2002 na kuchapishwa katika juzuu kwa kutumia *JUTA and Company* iliyoko *South Africa.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na utaratibu huo wa kuzipangilia sheria zetu katika juzuu, bado kuna mapungufu mengi katika Idara hii. Baadhi yake ni makosa mengi ya uchapaji katika sheria nyingi. Nitatoa mfano. Katika Sheria ya Magereza, mwaka 1967 kifungu cha pili, pamoja na mambo mengine, kinazungumzia *"Convicted Criminal Prisoner"* kwa kukifanyia kifungu hiki marejeo ya kifungu cha 57 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai *(Criminal Procedure Act),* 1985; yaani vifungu hivi visomeke pamoja. Lakini ukienda katika kifungu cha 57, unakutana na mambo tofauti kabisa na yale yalioainishwa katika kifungu cha pili.

Katika kifungu hiki hiki cha pili ambacho ni cha ufafanuzi, kinasema *Visiting Officers* watakaoteuliwa kwa mujibu wa kifungu cha 100. Ukienda katika kifungu cha 100 unakutana na mambo tofauti kabisa na yale yaliotajwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, udhaifu mwingine uliopo katika Idara hii ni uandaaji wa sheria kwa lugha ya Kiingereza tu, ilhali Watanzania zaidi ya asilimia 50 hawajui lugha hii. Je, ni kwa nini basi sheria hizi zisiandikwe kwa Kiswahili? Nafahamu kuna sheria zisizozidi tano ambazo ziko kwa Kiswahili, yaani Sheria ya Ardhi ya Vijiji ya mwaka 1999; Sheria ya Mabaraza ya Kata ya mwaka 1985 na lile Tangazo la Serikali la Sheria za Mila za mwaka 1963. Kambi ya Upinzani inataka Serikali iliambie Bunge hili Tukufu ni mkakati gani wa makusudi wa kuandaa na kuchapisha Sheria kwa lugha ya Kiswahili kwa manufaa ya Watanzania? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ambalo ni tatizo kwa sasa, ni kuwa juzuu nilizozitaja hapo juu za sheria katika mpangilio mpya zimeishia mwaka 2002. Kwa hiyo, sheria zote zilizotungwa kuanzia mwaka 2003, haziko katika mfumo mmoja na zile zilizotungwa hadi mwaka 2002. Waziri atueleze ni lini basi Idara hii itaziweka katika mfumo uliokubalika wa sasa? Kwa vile kuzuu hizo hazipatikani hata kwenye Duka la Vitabu vya Serikali, Serikali ina mpango gani kuhakikisha vitabu hivyo vinapatikana kwa urahisi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Madai na Sheria za Kimataifa, Uwajibikaji Katika Mikataba ya Kimataifa. Mikataba mbalimbali ya kimataifa inatambulika nchini kwetu kupitia Ibara 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano. Serikali yetu imeridhia Mikataba mbalimbali ya kimataifa ambayo kati ya mambo mengine, Mikataba hii imeweka sharti la nchi wanachama kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa masharti yaliyowekwa katika Mikataba hiyo kwa kila baada ya muda ulioainishwa katika Mikataba hiyo. Kwa mfano, Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu *(African Charter on Human and Peoples Rights)* wa mwaka 1981, ambao Tanzania tuliuridhia mwaka 1984, unaagiza kutoa taarifa kwa Tume ya Haki za Binadamu kila baada ya miaka miwili, lakini hadi sasa imetoa taarifa moja tu kwa Tume hii ya Afrika toka mwaka 1984.

Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ihakikishe jukumu hili la kimataifa linatekelezwa kwa kuwa sisi siyo Kisiwa cha kutokufuata taratibu za Kimataifa. Uwasilishaji wa taarifa za namna hii haujafanyika katika kiwango cha kuridhisha hata katika mikataba mingine iliyoridhiwa, kama Mkataba wa Kimataifa wa Watoto wa 1989, Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa wa mwaka 1966 na mingineyo mingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mikataba muhimu ya kimataifa ambayo Serikali yetu hii haijairidhia na kuifanya kuwa sehemu ya Sheria za nchi ni *The Protocal to the African Charter on Human and Peoples' Rights on the Rights of Women in Africa of 2000* unaohusu haki za wanawake wa kiafrika.

*The Convention Against Torture and other Cruel, Inhuman or Degrading Treatment or Punishment of 1984* ambao unazihitaji nchi husika zijiwajibishe katika kuzuia ukatili. Mkataba huu umeridhiwa na nchi 129 kati ya nchi 189.

*The Second Optional Protocal to the International Convenant on Civil and Political Rights, 1989* ambao unahimiza kufutwa kwa adhabu ya kifo.

*The Optional Protocol to the International Covenant on Civil and Political Rights, 1966* ambao unaruhusu wananchi wa nchi husika katika mkataba huo kupeleka malalamiko yao ya haki za binadamu moja kwa moja katika Tume ya Umoja wa Mataifa ya Haki za Binadamu, yaani *UN Human Rights Committee.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Serikali hii kushirikishwa katika Mikutano mbalimbali ya Mikataba ya Kimataifa, ikiwa ni pamoja na ule Mkutano wa mwaka 2002 kuhusu ubaguzi wa rangi na wageni na pia pamoja na kupewa heshima ya kuwa Makao Makuu ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu *(African Court of Justice and Human Rights*), utekelezaji wa majukumu yake kimataifa umekuwa ni wa kusuasua sana. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuzingatia majukuu yake kimataifa ili kulinda na kuendeleza heshima ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Tume hii ambayo ilianzishwa na Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ya mwaka 2001 na kwa mujibu wa Ibara ya 131 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, iliwapatia Watanzania wengi matumaini makubwa sana kwamba ukiukwaji wa haki zao na masuala ya utawala bora yatapatiwa ufumbuzi kwa haraka na kwa umakini na hivyo haki zao zitalindwa na ukiukwaji utapungua ama kuondoka kabisa. Pia, namna ya kuwapata Watendaji hasa wale makamishna, ni mahiri sana. Timu ya kuwapata Watendaji hao ni nzito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, Makamishna waliopo ni wale ambao wanaaminika katika kutekeleza jukumu la Tume hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni za Paris *(Paris Principles of 1993)*, zinatamka kuwa *"It is not usual for a human rights commission to be granted authority to impose a*

*legally binding outcome on parties to a complaint. However, this does not mean that the settlement or appropriate remedial steps recommended by the commission can be ignored."* Hii ina maana kuwa uhalisi wa chombo kama hiki ni kuheshimu maamuzi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe pia kuwa, Tume hii, kwa mujibu wa sheria hiyo kifungu cha 20, inatakiwa kufanya utafiti wa kina, upelelezi na kukusanya ushahidi kama Mahakama nyingine kwa kuzingatia Sheria ya Ushahidi *(Evidence Act, Cap.6)*, Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai *(Criminal Procedure Act, Cap. 20)* na hatimaye kutoa uamuzi. Hivyo basi, uamuzi unaotolewa ni ule uliofuata kanuni za sheria. Lakini pamoja na hayo yote, cha kushangaza, Serikali imekuwa mstari wa mbele kwa kutokuheshimu maamuzi ya Tume hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano halisi, hali iliyotokea katika shauri la kesi ya Kijiji cha Nyamuma dhidi ya Mkuu wa Polisi na Mkuu wa Wilaya ya Serengeti, Tume hii kwa hakika kupitia wataalam wake, ilifanya uchunguzi wa kina, tena kwa kutumia hela nyingi sana za Serikali na kumaliza uchunguzi na ushahidi. Baada ya hapo, Tume iliona kuwa kuna ukiukwaji wa haki za binadamu na suala la utawala bora. Lakini mpaka sasa hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa katika kutoa fidia na kuwawajibisha waliotenda uovu. Tatizo lingine lililopo katika Tume hii ni kuwaleta wafanyakazi wa Tume ya Kudumu ya Uchunguzi *(Permanent Commission of Inquiry - PCE)* ambao wengi wao sio wanasheria. Kwa kuwa katika kifungu cha 20(2) cha Sheria ya Tume ya mwaka 2001 kinaelekeza kwamba uamuzi wa Tume ufikiwe kwa kuzingatia sheria, taratibu na kanuni kama zitumikazo Mahakamani. Basi, ni dhahiri kuwa kuwepo kwa watu ambao sio wanasheria katika safu ya kutoa maamuzi ni hatari katika mustakabali wa upatikanaji wa haki kupitia Tume hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, namwomba Mheshimiwa Waziri, atueleze amefikia wapi katika mikataba ya kimataifa ya haki za binadamu kwa mujibu wa kifungu cha 6 (1) (L) cha Sheria ya Tume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine ni suala la muda wa ajira ya Makamishna wa Tume ambao sheria ya Tume inatamka kuwa ni ya kipindi cha miaka mitatu ambayo Afisa anaweza kuendelea tena kwa kipindi kingine cha miaka isiyozidi mitatu. Muda huu ni mfupi sana kuliko mikataba ya kazi za Serikali ambayo ni miaka mitano.

Pia, Mkakati wa Kazi *(Strategic Plan)* wa Tume inaainisha mpango wa kazi wa miaka mitano. *The United Nations Paris Principles of 20$^{th}$ December, 1993*, ambazo ni Kanuni kwa Tume kama hii ya Kitaifa, zinaelekeza *"...to ensure a stable mandate for members of the National institution..."* (Kanuni ya sita). Hivyo, ajira ya muda mrefu ni moja ya njia ya kuhakikisha kuwa Watendaji katika Tume hii wanafanya kazi yao kwa kujiamini zaidi.

Nchi nyingine kama Uganda na Kenya, katika Tume zao kama hii ya Tanzania muda wa ajira unanzia miaka saba. Ni vyema tukajifunza kutoka kwao. Sambamba na hili, kuna hitaji la kuongeza idadi ya Makamishna ili kupunguza mzigo wa mashauri

ambayo kwa sasa yanafikia zaidi ya kesi 7,781. Mashauri zaidi ya 130 upande wa Zanzibar hayajashughulikiwi hata moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine ni mapungufu ya baadhi ya vifungu vya Sheria ya Tume ya mwaka 2001. Mfano, kifungu cha 28 (2) na (3) vinaweka urasimu usio wa lazima katika kutoa haki kwa mlalamikaji mbele ya Tume. Kifungu hiki cha 28 kinatoa utaratibu baada ya uchunguzi. Kinasema kuwa baada ya uchunguzi, Tume itawasilisha mapendekezo yake katika mamlaka husika ambayo inatakiwa na sheria kutekeleza ndani ya miezi mitatu na kama haitafanya hivyo, basi Tume yaweza kuipeleka mamlaka hiyo Mahakamani. Hii ina maana kuwa shauri hilo litatakiwa kuanza upya kwa kuwa sheria haielekezi rufaa kutoka katika Tume kwenda Mahakama za kawaida. Mbali na urasimu, pia udhaifu mwingine ni aina ya maamuzi ya Tume ambayo hayana msukumo wa moja kwa moja wa kisheria *(direct legal enforceability)* kama ilivyo Tume ya Uganda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juhudi za Tume hii ya Kurekebisha Sheria imekuwa ikipata vikwazo vya utekelezaji wa mapendekezo ya marekebisho ya sheria ilizozifanyia uchunguzi na kuainisha mapungufu yaliyopo. Mfano, Sheria ya Rushwa ya mwaka 1971 ilishafanyiwa udurusu (*review*) kupitia Tume hii. Lakini Bunge hili Tukufu halijafanya marekebisho yoyote ya sheria hii muhimu katika kupambana na tatizo la rushwa.

Aidha, hadi kufikia mwaka huu wa 2006, Tume hii imeshawasilisha Taarifa mbalimbali (yapata 21) za mapendekezo ya marekebisho ama utungwaji wa sheria kwa Wizara hizi ambazo zimependekeza mabadiliko ya sheria mbalimbali. Baadhi ya Tarifa hizo ni *Report on Delays in the Disposal of Civil Suits. Report on the Law of Marriage Act, Report on the Law of Succession/Inheritance, Report on the Law of the Child, Report on the Nyalali Commission 40 laws, Report on the Problem of Congestion in prisons, Report on the Impact of Criminal Justice System in Combating Thefts/Embezzlements in Government Institutions and Public Corporations, Report on Private Legal Practice, Report of Dual Citizenship, Report on Access to Information* na *Report on E-Commerce and Cyber/Computer Crimes*. Hakuna hata moja ambayo imetiliwa maanani na kufanyiwa kazi kiufasaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuiwezesha Tume hii, kuharakisha taarifa nyingine hasa zinazohusu *HIV/AIDS, Review of Customary Law (Declaration) Order 1963* na *Review of Legislation Relating to the Protection of Rights of Persons with Disabilities in Tanzania,* ambazo nafahamu ziko katika mchakato wa mwisho. Aidha, Kambi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri atupe kwa kirefu taarifa za uchambuzi wa mapendekzo ya Tume kwa kulijulisha Bunge lako Tukufu ni sheria ngapi zimefanyiwa marekebisho baada ya mapendekezo ya Tume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hili kundi la watu wenye ulemavu ambalo mpaka sasa halijapewa ulinzi na usimamizi wa kutosha wa sheria. Natambua kwamba, Katiba ya Jamhuri ya Muungano inatambua, katika Ibara ya 11, uwepo wa kundi hili ila sasa sheria zilizopo *kama Disabled Employment Act, 1982* na *Disabled Persons (Care and Maintanance) Act, 1982* hazitoi usimamizi wa kutosha. Mfano, sheria hii ya pili

niliyoitaja iliainisha kuwepo kwa mfuko kwa watu wenye ulemavu *(National Fund for Disability)*. Mfuko huu haujulikani kama upo na unafanya kazi kama sheria ilivyoelekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haijaridhia Mkataba wa Kimataifa wa Mafunzo ya Ufundi kwa Walemavu *(ILO Convention No. 159 on Vocational Rehabilitation and Employment of Disabled Persons, 1983)*. Kati ya madhara makubwa na mapungufu haya, ni unyanyapaa wa kundi hili la watu. Ukosefu wa sheria mahiri tena katika kipindi hiki cha ushindani wa kiuchumi, kutawaengua kabisa watu wa kundi hili katika wigo wa ajira endapo tutaendelea kutokuwa na sheria zinazotoa mwongozo wa kutosha kwa watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dira ya Wizara inaelekeza haki sawa kwa wote na kwa wakati. Moja ya jukumu kubwa la Wizara hii ni kujenga utamaduni wa uwajibikaji na vita dhidi ya rushwa. Aidha, vita dhidi ya rushwa hapa nchini ni ya kila Wizara, Idara na hata mtu mmoja mmoja katika nafasi yake. Kwa sasa, kwa mujibu wa tafiti za *Transparent International*, Tanzania inashikilia nafasi ya 96 kati ya nchi 159 katika suala hili la rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lililopo, ni kuwa sheria hii haitoi nguvu ya kutosha kwa TAKURU katika kupambana na rushwa. Mashitaka mengi yahusuyo rushwa kwa mujibu wa sheria hii yanatakiwa kuidhinishwa na Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai *(DPP),* ambaye pia ana mamlaka ya kufuta shauri lolote yaani *(enter nole proseque).* Kesi nyingi ambazo zimewasilishwa na TAKURU zimekwama kuendelea kwa ajili hii. Mfano, kati ya Januari, 1995 hadi katikati ya mwaka 2005, TAKURU ilipokea kesi 11,434. Lakini ni kesi 48 tu kati ya hizo ndizo zilizoendeshwa na TAKURU. Ni Mapendekezo ya Kambi ya Upinzani kuwa sheria hii irekebishwe kuipa Taasisi hii nguvu zaidi kama Tume ya Kurekebisha Sheria ilivyopendekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijamaliza, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali itoe ufafanuzi juu ya haya yafuatayo:-

(a) Bunge lako Tukufu lielezwe maendeleo ya mikakati mbalimbali iliyoko katika Wizara hasa juu *Legal Reform Sector.*

(b) Sheria Na.4 ya mwaka 1998 ifanyiwe marekebisho katika kifungu cha 21(2) kinacho husu ukeketaji wa mwanamke. Kwa sababu sheria hii inamlinda mwanamke hadi afikapo miaka 18 tu. Miaka 18 ndipo mwanamke anapohitaji kutokeketwa. Mwanamke anapokeketwa inamuathiri ki-saikolojia na pia kuna uwezekano mkubwa wa kupata magonjwa ya kuambukiza kama vile UKIMWI kwa sababu vyombo vinavyotumika katika ukeketaji sio salama.

(c) Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza ni kwanini sheria zetu zinapelekwa Afrika ya Kusini kwenye Kampuni ya *JUTA* kuziweka

katika *Juzuu*. Je, Mchapaji Mkuu wa Serikali hana uwezo wa kufanya kazi hiyo na kama hana uwezo, kwa nini asiwezeshwe? Je, Serikali inatumia gharama kiasi gani kwa kazi hiyo ya kuipeleka huko *South Africa*?*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesoma katika magazeti kwamba kumetokea wizi wa kughushi katika Balozi yetu nchini Italy wa fedha za kitanzania Shilingi bilioni mbili. Wizi wa kughushi kwa lugha ya kisheria ni *forgery* na wala sio *corruption*. Kambi ya Upinzani inataka ufafanuzi kuhusu haya yafutayo:-

Kwanini tuhuma hizo zisipelekwe Mahakamani badala ya kupelekwa TAKURU? Kama ni kweli kumetokea janga hilo huko Italy, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali iwaeleze Watanzania majina ya wahusika kutoka katika Wizara zifuatazo:-

Wizara ya Mambo ya Nje, Wizara ya Miundombinu, Wizara ya Fedha na *Negotiator* aliyekwenda kupatana manunuzi ya nyumba hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli za manunuzi ya nyumba katika Balozi zetu, huwa Wizara nilizozitaja zinahusika. Kambi ya Upinzani inataka kujua ni akina nani wanaohusika ili njia ya kuzirudisha fedha hizo ipatikane? Watanzania wana imani na Serikali hii ya Kasi mpya, Ari mpya na Nguvu mpya . Tunaomba iwe wazi juu ya hili ili tuweze kutofautisha kati ya Serikali hii na ile ya Awamu ya Tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, lakini kwa umuhimu sana, namshukuru Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa George Lubeleje pamoja na Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Tatu Ntimizi, kwa kazi yao nzuri sana wanayoifanya katika kuiongoza Kamati hii. Kwa kweli watu hawa wawili wote wana-*sense of human* na wametuweka pamoja tumekuwa kitu kimoja na Kamati inanidhamu ya hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, nawashukuru Wabunge wote kwa kunisikiliza. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI :** Mhesghimiwa Mwenyekiti, tunakushukuru Mheshimiwa Fatma Maghimbi, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara hii ya Katiba na Sheria.

Waheshimiwa Wabunge, mtaona kwamba kwa wale ambao wamepitia vitabu tunavyovitumia jioni, Wizara hii ya Katiba na Sheria ina *Vote* sita, *Vote* 40, 41, 59, 64 na 90. *Vote* kama ya 40 na 41 kwa matumizi ya kawaida na maendeleo zina *sub-votes* 25 na zaidi. Kwa hiyo, huenda tukakutwa na *guillotine*. Kwa hiyo, nawaandaeni hivyo, kwa maana hiyo huenda jioni tukaomba achangie Mbunge mmoja tu ili tutoe nafasi kwa majibu kutoka kwa Mtoa hoja na baadaye ule utaratibu mwingine uende kwa muda ambao utakuwa ni muafaka.

Baada ya kusema hayo, sasa nawaita wachangiaji, tukianza na Mheshimiwa William Shellukindo. Karibu.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa nafasi ili na mimi nitoe mchango wangu kidogo kwenye hoja hii ya Waziri wa Katiba na Sheria. Awali ya yote, napenda kumpongeza sana Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Mary Nagu kwa hotuba yake nzuri sana na ambayo ameiwasilisha kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maeneo machache ya kuchangia. La kwanza ni hili la Bajeti. Bajeti hasa ya muhimili huu wa kutoa haki na kusimamia haki, ningependa niunganishe Bajeti yake pamoja na muhimili mwingine wa Bunge. Vyombo hivi ni vyombo vikubwa sana katika Taifa letu. Kwa hiyo, wakati tunapotazama Bajeti yake, nadhani tufike mahali hii hali ya kuombaomba, kwamba tunaomba hiki, tunaomba hiki na kuna mtu mwingine wa kuamua kwamba leo hapana, leo utapata tatu, leo mbili, kunacheleweshа sana mambo ya utendaji katika vyombo hivyo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi napenda kushauri kabisa kwamba tufike mahali tuwe na uamuzi wa kudumu ambao hauna tabia ya kuombaomba na kupiga magoti. Kwa sababu kunarudisha nyuma kazi ambayo kwa mfano Bunge linatakiwa lisimamie Serikali, vyombo vya Mahakama vinatakiwa vitoe haki bila kutazama uso wa mtu yeyote. Sasa ukifikisha mahali pa kuombaomba, unavipunguzia hata ile nguvu yao ya kutekeleza bila kuzingatia kwamba huyu unamfahamu, huyu simfahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na ushauri kwamba, pengine tufike mahali tuzungumzie suala la asilimia ya mapato ya Serikali na pengine utaulizwa utaifikiaje hiyo? Kwa nini tusianze hapa tulipo? Kwa mfano, kama Bajeti ya vyombo hivi vya kutoa haki kwa jumla kwa maana chini ya Wizara hii ya Katiba na Sheria, Bajeti yake sasa ni karibu bilioni 80. Sasa, tunaanzia hapo, bilioni 80 ni asilimia ngapi ya mapato ya Serikali kwa sasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukijua hiyo *percent*, basi mwaka ujao hakuna haja ya kwenda kwingine, tunatumia *percent* hiyo hiyo kupata kiasi cha kuweza kupangia kazi katika vyombo hivyo. Muhimili huu wa Mahakama unaotoa na kusimamia haki pamoja na Bunge ambalo linatunga Sheria.

Tufike mahali habari ya kuombaomba kwa kweli tuiondoe, nchi nyingi hazifanyi hivyo. Zikiishakubaliana hivyo na ni watu ambao wanajua tuna majukumu ya kufanya, watapata fedha wakipanga majukumu yao jinsi wanavyoona wahudumie Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ninataka kuchangia ni kuhusu Chuo Cha Uongozi wa Mahakama Lushoto. Chuo kinafanya kazi nzuri sana na kiko katika mazingira mazuri sana ya kuweza kuwaweka Viongozi wakasoma kwa utulivu. Lakini nina wasiwasi kwamba kinatumika kweli kuondoa tatizo la uhaba wa Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo. Kwa sababu sasa hivi, Mahakimu wengi wa Mahakama za Mwanzo wanajitahidi kwenda kuchukua shahada ili waondoke pale waende juu.

Kwa huku chini nafasi inakuwepo wakati wote, mathalani katika Jimbo la Bumbuli, yako majengo ya Mahakama nne. Soni, Vuga, Bumbuli na Mgwashi. Lakini ni Mugwashi tu ndiyo ina Hakimu wa muda wote pale. Bumbuli, Soni na Vuga zinachangia Mahakimu wa Mwanzo pamoja na walioko Jimbo la Lushoto kwa maana hawapo katika mazingira yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, utakuta katika mwezi, anapanga pengine siku moja kwa jinsi alivyo na kazi nyingi. Sasa hatuwezi kwa kweli kuendelea hivi. Wananchi wana matatizo yao ya kila siku haya. Kwa mfano wanagombea mashamba, ardhi, wanamhitaji Hakimu huyu awepo jirani.

Kwa hiyo, mimi nadhani Chuo hiki kwa kweli pamoja na kukifanya kiwe ni cha ku-*upgrade skills*, lakini vile vile kiwe ni cha kufundisha Mahakimu hawa wa Mahakama za Mwanzo na kama Bajeti haitoshi, basi hilo liwe ni suala kwamba pengine hakuna Bajeti ya kuajiri Mahakimu hawa wa Mahakama za Mwanzo, kwa sababu kwa kweli haki zaidi ni kwa watu wengi kule waliko, wako Vijijini, sio Mijini. Huku juu utakuta ni kesi chache sana ambazo zinakwenda juu zaidi huko kwenye Mahakama za Wilaya, Mahakama Kuu na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia kutoa haki, nadhani na yale mazingira vile vile ya kumfundisha mtu ya kutoa haki, yawe yameandaliwa vizuri. Mimi nina pendekezo kwamba, kwa dhati kabisa, Wizara iangalie zile Mahakama za Mwanzo ambazo ziko jirani na Chuo cha Lushoto, ziwe ni za mfano wa Mahakama ya Mwanzo kwa maana ziboreshwe zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona wana mpango mzuri sana wa kuboresha na kujenga majengo ya Mahakama za kila Tarafa. Nimeona katika orodha katika jedwali Na.3, Wilaya ya Lushoto ni mojawapo. Wilaya ya Lushoto ina Tarafa tatu nikiwa na maana majengo ya Mahakama matatu yatajengwa na yajengwe vizuri kwa kweli kwa sababu haya yatatumika kwa ajili ya mafunzo ya kazi kwa Mahakimu hawa ambao watafundishwa pale. Kwa hiyo, ni vizuri tuanzie mfano pale Chuo kilipo ili yajengwe mazingira hata Hakimu akitoka pale, kule anakokwenda atajitahidi kuiga mfano ule wa Mahakama ambayo iko katika hali nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la usafiri kwa ajili ya usimamizi. Naipongeza sana Wizara kwamba imefikiria hili. Kwa kweli Mahakama za Mwanzo zinahitaji sana usimamizi wa Mahakimu wa Wilaya wanaosimamia. Lakini kama hawana magari ya kusafiria, itakuwa ni kazi bure na kwenye kutoa haki kwa kweli kuna lawama nyingi sana. Mahakimu wetu wa Mahakama za Mwanzo wanafanya kazi nzuri sana, lakini wanafanya kazi katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine, wanachukua tu mawazo ya kuona tuwatendeeje haki watu, anajikuta hana makaratasi, anamwambia mwananchi aje na makaratasi amwandikie hukumu. Inageuzwa hiyo kwa watu ambao pengine hawamtaki Hakimu huyu, wanageuza inakuwa ni rushwa. Sasa ni vizuri kwa kweli tuwaweke

mahali ambapo kazi zao zinakuwa sio za kuhisia hisia kwamba hapa pengine kuna mazingira ambayo yanajengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, usafiri ni muhimu sana na nimeona katika Bajeti hii, kuna magari 31 kwa ajili ya Mahakimu wa Wilaya kwa ajili ya usimamizi wa Mahakama za Mwanzo. Haya yapatikane haraka, Bajeti ikishapita msingojee ili tuwape nguvu na hamasa ya kufanya kazi kwa bidii zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna eneo lingine ambalo ni kero kubwa sana kwa wananchi, suala la kuandikisha vizazi, vifo, sio sana lakini vizazi sasa hivi ni kero kubwa sana. Ni kero kubwa kwa sababu, kwa mfano katika Wilaya ya Lushoto katika Kata zilizoko 32, ni Kata labda kama nne hivi ambazo hazina Shule ya Sekondari. Sasa, vijana hawa walioko Shule ya Sekondari akiendelea kutoka hapo, anatakiwa awe na Cheti za Kuzaliwa, vinginevyo hawezi kupokelewa kwenye Chuo chochote kile. Sasa tatizo hili tutalitatua vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi napendekeza kwamba Wizara ijaribu kutizama uwezekano, maadam mnaimarisha majengo ya Mahakama za Tarafa, basi hapo kwenye Tarafa pangekuwa ni Kituo cha kuandikisha vizazi na pengine kuwe na ratiba ya huyu mwandikishaji wa Wilaya kuweza kutembelea maeneo haya atusaidie kutatua matatizo. Sasa, hivi Waheshimiwa Wabunge, nina hakika hata katika Majimbo yao wanapata tatizo hilo. Anakujia mzazi anakwambia sijui mimi hicho cheti nitakipata wapi! Mtoto wangu amekubaliwa kwenda Kigonsela na Kigonsela kwenyewe hakujui na ameambiwa aende na chetia za kuzaliwa na hakipatikani mpaka uende Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nadhani hili kwa kweli lisimamiwe. Ni kero kubwa sana na maadam imeundwa *Executive Agency,* nadhani ipewe nyenzo iweze kuharakisha kufikisha huduma hii karibu na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa na haya machache tu ya kuchangia. Nitoe nafasi kwa wenzangu wengine waendelee kuchangia. Ahsante sana. Naunga mkono hoja hii kwa dhati. *(Makofi)*

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Aidha, naomba nitoe pongezi kwa timu nzima ya Waziri na timu yake yote na Taasisi zote zilizoko chini yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze tu kwa kusema kwamba Mheshimiwa Waziri bila shaka anatambua, ukiacha Polisi na Magereza, Idara yake ndiyo iliyo karibu zaidi na wananchi na hivyo Idara zake hizi hasa za Mahakama ndizo zinazoweza kuwa na kero kwa wananchi au zinaweza zikaondoa hizi kero kwa wananchi. Kwa hiyo, kadri zitakavyosimamiwa vizuri, haki itakavyolindwa ndiyo kadri hiyo Serikali itapendwa. Lakini Idara hizi zina uwezo mkubwa kabisa wa kusaidia kujenga chuki kati ya wananchi na Serikali yao tusipokuwa makini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hilo, naomba niseme pia kwamba namshukuru sana Mheshimiwa Waziri, ndani ya Bunge hili nilipiga kelele kuhusu Mahakimu wawili; Hakimu wa Endabashi na Hakimu mwingine wa Karatu anaitwa Shayo. Namshukuru Mheshimiwa Waziri kwamba Hakimu wa Endabashi ameondoka. Hapo tunaposema Serikali iwe sikivu.

Nadhani kwa kweli sasa Serikali imesikia ni kilio cha muda mrefu, watu wamepiga kelele, lakini kwa muda mrefu waliteseka sana. Naomba nisisitize kwamba wanapopiga kelele Wabunge, ningependa Serikali daima ifungue masikio kwa sababu Wabunge ni mdomo wa wananchi wanaoteseka. Sasa, Serikali isipochukua hatua kwa kilio hicho, Serikali isipofanya hata uchunguzi wake, kwa kweli wananchi wengi wanaumia. Ni imani yangu kwamba na yule wa Karatu ambaye amebaki Bwana Shayo naye hatua itafuata mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishawaambia sisemi mimi, fuateni ya kwangu, pelekeni timu ikachunguze. Watu wa haki za binadamu kule Arusha, Tasisi ya Haki za Binadamu imekwishafanya uchunguzi, imekuta maamuzi mengi yanayofanywa na Hakimu huyu ni kinyume na haki za binadamu. Sasa sijui Serikali inasubiri nini na kwa bahati mbaya Mahakimu tunao wachache sana Karatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nitoe tahadhari, hawa Mahakimu tunaowasema hivi kuwaondoa na kuwahamisha kuwapeleka mahali pengine ni kuhamisha pia mzigo. Kwa hiyo, mimi sipendi mzigo utoke Karatu uende mahali pengine. Watanzania wa huko wanakokwenda wanafanana na wa Karatu. Kwa hiyo, ningependa hatua za dhati zichukuliwe watu wa namna hii wanaoaibisha na kudhalilisha Mahakama zetu, sio tu wahamishwe toka mahali, lakini wachukuliwe hatua zinazostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, labda niseme la msingi nililonifanya nisimame na kuomba kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara nyingine tena, naomba nirudie ombi langu nililotoa ndani ya Bunge hili kuhusu hadhi, maslahi na haki za Majaji wetu na Mahakimu wetu. Leo napenda kuongelea kipengele kimoja tu. Nimepitia kwa makini sana taarifa ya Tume ya Mheshimiwa Bomani. Sijui kama Serikali, naona kuna vipengele vinaguswa hapa, bado inasemwa tu kwamba itafanywa, itafanywa lakini sijaona mkakati kamili wa kutekeleza vipengele vya hii taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Majaji ni watu pekee ambao katika Katiba yetu wana haki au ya kurudisha uhai wa mtu au ya kuuondoa kabisa, ambao ni Mwenyezi Mungu tu ndiye peke yake anaweza kuondoa lakini na Jaji amepewa kazi ya kushiriki katika kutoa uhai huu kisheria. Sasa hawa tusipowasaidia na tukawawekea mazingira, kwa kweli tunawaweka katika mazingira magumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa tuwaone hawa kama tunavyoona kuna *rare professions*, hawa tuwaone kama *rare profession* vilevile. Wana nafasi ya peke yao, hawana mtu wa kuwasemea kwa sababu humu Bungeni kwa bahati mbaya

wanawakilishwa na Mwahasheria Mkuu. Lakini Idara ya Mahakama haiingii, wala hata kwenye ile *Inter-ministerial* hata wao hawana hata Katibu Mkuu. Kwa hiyo, haki zao, maslahi yao hakuna mtu wa kutetea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Kamati tuliomba ikiwezekana, kuwe na mtu anayeingia kuwakilisha Mahakama wakati zinajadiliwa Bajeti zao ili haki zao zote, maslahi yao, maombi yao yaweze kufikiriwa. Tumekwenda kutembelea sisi Mahakama, tumekuta hali ya Mahakama zilivyo, ni jambo la ajabu Majaji unapokuta wanashirikiana katika *chamber,* wanakaa kwenye chumba kimoja au wanapishana. Ili mmoja asikilize kesi, mwenzake anatoka kwanza. Mwenzake anapomaliza, mwingine anaingia. Sasa hiyo inaungana pamoja na mlundikano wa kesi. Tutategemea kumaliza kesi vipi kama hatuwezi kuwapatia nafasi hizi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tungependa hao wazee wetu ambao wana kazi muhimu ya kutoa haki na ni kazi ngumu kweli kweli. Tusipowapa mazingira mahsusi ya aina hii, kwa kweli tunawajengea mazingira magumu sana ya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini, mimi najiuliza, hapa Bungeni sisi tukiongea, jioni tumeshaletewa karatasi, tunaambiwa tusahihishe zile karatasi zetu ya kile ambacho mimi nakiongea hapa sasa hivi, jioni iko tayari imeishachapishwa. Jaji unamweka pale au Hakimu, anamsikiliza mtuhumiwa, anamsikiliza Wakili, wakati huo huo anafikiria sheria, wakati huo huo anafikiria na makandokando ya sheria nyinginezo zilizoko. Anajaribu kuangalia hiki kinachotuhumiwa kama kweli kiko kinalingana na sheria hizi. Anapima kama yule anayesema anasema ukweli, kichwa chake kinafanya kazi, masikio yanafanya kazi, mkono unafanya kazi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu anaandika saa zote, akimaliza hayo, bado pia aandike na hukumu. Hukumu zetu nyingi za Mahakama Kuu, za Rufaa na hata za *Resident Magistrates* ni ma-*page* na ma-*page*. Huyu ni mtu mmoja tunamtaka afanye kazi zote hizo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani turudi kwenye ripoti ya Bomani, imetuambia kuna vyombo vya kisasa. Kama Bunge limeweza, tukaweka hapa tunayoongea sasa hivi, jioni yako tayari, ni kwa nini tusifikirie angalau kwenye Mahakama Kuu, kwenye Mahakama ya Rufaa tukaweka vyombo vya kisasa vikamsadia Jaji, wakati anasikiliza na chombo kile kinarekodi, baadaye na yeye akaweza kuandika hukumu yake kufuatana na kilichorekodiwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunampunguzia na inawezekana kabisa, sina hakika, lakini kuna taarifa zinasema Jaji kwa kukaa muda mrefu kwa kuandika tu ripoti, tunampunguzia maisha yake. Kumbuka mtu anaandika *page* 200, 300 ya hukumu, amejiinamia tu pale kwa mkono, kutokana na *notice* ambazo ameziandika Mahakamani. Hatufanyi haki kwa watu hawa, lakini pia hata sisi hatujitendei haki kwa sababu kesi zitaendelea kuchelewa hata kama tunawapangia utaratibu huu ambao Waziri ameueleza kwenye kitabu chake. Namna pekee ya kumsaidia, kuondoa msongamano huu *Backlog*

wala siyo *Cash flow*, ni vifaa vya kisasa vitakavyorekodi, vitakavyomsaidia Jaji aweze kuandika hukumu yake katika muda unaotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hili, nilipenda nilisisitize nirudie tena, yeyote ambaye amekwenda Mahakamani, anapaswa kweli kuwahurumia Majaji na Mahakimu wetu na kwa maana hii nawaongelea Mahakimu wa Ngazi zote hata wa *Primary Court*. Tunawahurumia kwa sababu mazingira yao ya kuandikia na kufanyia kazi ni magumu sana na ndio maana hata baadaye kuna malalamiko kwamba hukumu imebadilishwa. Hivi huyu ni mtu mmoja, ni malaika!

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua kwamba labda kuna wengine wanabadilisha kwa makusudi, lakini hata katika hali ya kawaida uweze kuwaelewa hawa watu wote, wameongea kwa saa nyingi, wewe uko peke yako unayaandika halafu utegemee uyarekodi na kuya-*produce*, kila mmoja alivyosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna malalamiko mengi yanayotokea kwamba hukumu imebadilishwa. Mimi sikusema hivyo, Hakimu ameandika jinsi alivyotaka. Tuondoe utaratibu huo kwa kuwawezesha wenzetu kwa kupata vifaa vya kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baada ya kusema hilo, niseme dogo sana kuhusu Mahakama ya Wilaya ya Karatu. Hili nimeliandika pia kwa maandishi, nimempelekea Waziri. Wilaya ya Karatu ina karibu miaka 10 sasa, lakini tuna mazingira ya ajabu sana, hatuna Mahakama ya Wilaya. Mahakama yetu ya Wilaya iko Mbulu, kilometa 76 toka Karatu, lakini kwa kuwa hatuna jengo la Mahabusu, juzi ilielezwa hapa Bungeni kwamba tulikuwa tunatumia *godown*. Kwa kweli kwa wale ambao hawaelewi, sio *godown* hizi mnazojua, ni *godown* zile za Wajerumani, zamani ambazo hazina madirisha. Nashukuru Waziri wa Mambo ya Ndani alipiga marufuku. Kwa hiyo mahabusu wetu wanapelekwa Arusha. Arusha ni kilometa 150. Sasa watoke Arusha, wapelekwe Mbulu kwenda kusikiliza kesi, kwa kweli ni usumbufu mkubwa sana. Ni kilometa zaidi ya 200, watu hawapelekwi kwa sababu Polisi nao mara wanasema hawana mafuta, hawana gari, kwa hiyo, siku zinapita, haki ya watu inanyimwa, inanyongwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyomwandikia Mheshimiwa Waziri, nitaomba nipate taarifa kamili kama katika hiki kitabu chako ukurasa nadhani ni wa 20 umesema kila Wilaya, lakini baadaye kwenye jedwali nimeona umeandika kwamba Arusha, moja, mbili kwa kila Wilaya. Sina hakika ina maana gani. Kwa hiyo, nitaomba nipate uhakika kama jengo hilo la Mahakama sasa litapatikana na wakati tunafikiria hivyo kama atafikiria ombi letu, angalau kesi zile zinazomhitaji Hakimu wa Wilaya zisikiliziwe Karatu, kuondoa usumbufu kwa sababu kinachotakiwa pale ni kutoa tu mafungu ya fedha kwa yule Hakimu wa Mbulu apange *Roster* yake aweze kufika Karatu azisikilizie kesi pale Karatu, angalau tutakuwa tumepunguza usumbufu kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hilo litakubalika, mimi nitashukuru kwa sababu lengo la Serikali daima ni kupunguza kero kwa watu wake kadri inavyowezekana na nadhani tukipunguza hivyo, tutakuwa tumepiga hatua kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwa kifupi sana pia juu ya sheria zetu mbalimbali. Ninashukuru kwamba Waziri amezungumza jinsi sheria zinavyotazamwa na kuleta mabadiliko mbalimbali ili tuendane na hii *spirit* ya mabadiliko ya sheria. Ninasema hili kwa sababu moja ya sababu kubwa kabisa ya malalamiko ya watu wetu ni sheria zilizoko ambazo hazikidhi tena hadhi ya wakati huu wa leo. Mengine ni ubinadamu wa kawaida na kwa hili nadhani Serikali ni moja ifanye kazi.

Kwa mfano, mdhamana, sheria yetu, *CPA* inayoongelea suala la mdhamana liko wazi kuanzia Polisi mpaka Mahakamani. Lakini wakati mwingine mazingira ya kutoa mdhamana inafanywa kuwa magumu bila sababu yoyote na matokeo yake watu wanakaa, hata mtu aliyeiba kuku, anafanyiwa ngumu, anakaa mahabusu na kuleta msongamano bila sababu. Tunamlisha kwa gharama kubwa. Sasa sijui hawa watu wanakuwa na sababu gani. Kunaweza kuwa na sababu binafsi, kunaweza kuwa na mtu kutokuelewa na kadhalika. Lakini kwa kweli katika hili, kwa mtu anayependa kufuatilia kifungu cha 148 mpaka cha 169 nadhani cha *CPA*, kiko karibu wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama tatizo ni sheria, basi haidhuru, tukubali tuzitazame upya hizi sheria, tuweke mazingira mazuri wale watu wanaohitaji mdhamana, tuweze kuwapatia mdhamana. Tuondoe msongamano kadri itakavyowezekana. Hakuna namna nyingine zaidi ya kurekebisha mazingira ya kisheria. Tukishaweka mazingira, tukawafundisha watu, tukapata watu waadilifu, Watendaji wetu waadilifu, Mahakimu, Majaji; sina hakika sana kule juu kama kuna malalamiko, lakini kule chini ni makubwa sana hasa kwenye Mahakama za Mwanzo. Wakati mwingine, hata kwenye Mahakama, mdhamana unanyimwa tu kwa sababu kuna mtu fulani anataka ukae ndani. Ndiyo maana mtu anaweza kupelekwa hata *weekend* akawekwa ndani mpaka Jumatatu ili tu asitoke kule ndani. Sasa haya tusipoyaangalia, hatuwezi kuondoa kero katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka niyaseme haya. Sitaki nigongewe kengele na kwa sababu muda ni mfupi, ningependa watu wengi zaidi waongee. Mimi nitashukuru kama Mheshimiwa Waziri atanisaidia haya na kama nitapata majibu ya yale ambayo nimeyauliza katika maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. TATU M. NTIMIZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na mimi kupata nafasi niweze kuboresha kidogo tu na kuomba maombi machache kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru ndugu yangu Mheshimiwa Dr. Mary M. Nagu kwa uwasilishi mzuri alioufanya, na nina hakika kafanya uwasilishi huo kutokana na msaada wa wenzake wote anaofanya kazi nao. Ni mtu ambaye ni mpenda watu, anapenda kushirikiana na watu. Nina hakika kazi hii ameifanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kusema lolote na mimi niungane na Waziri kuwapongeza walioteuliwa kuwa Majaji wa Mahakama ya Rufaa na hasa

nimpongeze Natalie Kimaro ambaye nimefanya naye kazi kwa muda wa miaka sio chini ya minne. Ni mama makini, mama mahiri, mwenye uwezo sana na ni mchapa kazi. Kwa kweli hata mimi nimefurahi sana mama huyu kupata hii nafasi aliyoipata hivi sasa. Wengine sikufanya nao kazi, lakini nina imani nao wanastahili heshima ile ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na naipokea hotuba ya Waziri kwa mikono miwili kabisa. Ni hotuba makini, mahiri na yenye ufasaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina moja tu ambalo ninasikitika na Idara ya Mahakama, kwenye Jimbo langu la Uchanguzi, miaka mitatu iliyopita nilikuwa naomba Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo Makao Makuu ya Jimbo. Kwa kuwa nilikuwa katika nafasi ile, haikuwa rahisi kuchangia huku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini, nilikwenda mpaka Mahakama Kuu kumwona anayehusika na utawala wa Mahakimu wa Mwanzo. Akanithibitishia kwamba nitapata, akaniuliza Je, kuna Jengo? Nikamwambia jengo lipo, wananchi wamekarabati na mimi mwenyewe Mbunge nilikuwa mstari wa mbele kukarabati ili nione sheria inatendeka katika Jimbo langu. Basi, nikapewa nafasi mpaka Mahakama Kuu Kanda ya Tabora. Nikaonana na Jaji, akanihakikishia kabisa kwamba nitapata. Nikamwambia njoo ukague eneo hilo ambalo Mahakama ipo. Akatuma wataalamu kuja kukagua, wakathibitisha kwamba ni kweli, marekebisho yote yamefanyika, utapatiwa. Mwaka ukapita, hakuna kilichofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Polisi kiko Makao Makuu ya Jimbo, wanatoka pale askari na washitakiwa kilometa 28 kuwapeleka Goweko ambako Hakimu wa Mwanzo yupo. Cha kushangaza, Mahakama ya Goweko wamepanga jengo la Mahakama kwa mtu binafsi. Hakimu anapanga, sasa kipi bora? Jengo ambalo liko tayari wananchi wamejitolea ili kazi ifanyike, au kwenda kupanga walikotaka Mahakama iwe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikasemekana nimepata Hakimu kutoka maeneo ya Usoke nafikiri au Nzega. Hakimu huyu anaitwa Kapaya, ni *reject*, hakutakiwa kule kwa tabia ya ulevi na kupenda kuombaomba. Faili lake sio zuri. Akaletwa, kuambiwa anapelekwa Igalula, akasema ni Kijijini. Akakataa Tabora Mjini miezi waliyoitaka wao wenyewe watawala wake. Baadae wakampeleka Goweko, wakashindwa kumleta pale kwenye jengo mahsusi, akapelekwa Goweko. Kule akawa *nuisance to himself*, wakamtoa wakamleta Kigwe. Kigwe na Igaula ni kilometa 22. Pale Kigwe ndio kaonyesha sasa asivyokuwa mahiri na mwadilifu kwenye kazi yake. Siku moja Diwani wa Kata hiyo aliniambia mama, Hakimu wetu siku moja kanywa pombe, kalala kwenye meza, watu wanashangilia jinsi anavyoonekana. Sasa, mimi nikasema nimekuwa Naibu Waziri kule, nimekuwa sasa Mbunge wa kawaida, hili jambo kweli litatekelezwa! Hapa ndio Makao Makuu ya Jimbo, hawaoni umuhimu wa kuwa na vyombo vya Dola hasa Mahakama katika Kijiji cha Igalula?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo langu lina wafugaji wengi na ndio wenye kuonewa sana. Kwa sababu mfugaji hataki matatizo, anabambikizwa kesi, lakini wakati

ule ule anaambiwa lete laki nne, laki tano ili asifike Mahakamani. Hivi kweli watu hawa watapata haki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanakamatwa na Wanamgambo, kesi *judgement* zinatolewa, zinakwenda kupelekwa kwa hawa Wasukuma, wanapewa laki nane, tisa, mpaka milioni ili akamatwe yule mshitakiwa aletwe huku, lakini havifikishwi mahali popote na aina ya Hakimu ndio huyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nililalamika Hakimu wa Mahakama ya Kigwe, Mzee mmoja kwa jina anaitwa Katuku mlevi mlevi, hujuma nyingi, wakasema wanamshughulikia kutokana na sheria inayohusu matatizo ya Mahakama ya Mwanzo. Lakini kaendelea kula pesa, kutokuwa mwadilifu, sasa ukafika umri wa kustaafu, sijui kama atapewa nyongeza ya kuendelea na kazi ili aendelee kufaidi pale, wananchi wangu waendelee kuwa na matatizo!

Sasa huyu Kapaya bado yuko pale Kigwe, kazi ndio hiyo na ulevi kathibitika watu wote wanamwona. Nikaambiwa na Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Wilaya ya Uyui, akasema anamleta mama mmoja ataripoti hapo, mpaka leo yule mama hajaonekana. Matokeo yake wameleta *furniture* katika hilo jengo, wameweka mlinzi karibu zaidi ya miezi sita analipwa, analinda jengo lisilotumika, lakini wako tayari kukodi majengo ili Mahakama ziendelee. Haki iko wapi? Je, tunaisadia Serikali kweli? Naambiwa kuleta Hakimu wa kutembea katika Mahakama mbali mbali, wanaogopa kumlipa *night*. Akikaa wiki moja atadai *night*. Je, huyu ambaye ni mlinzi, ina maana tumlipe Serikali ya Kijiji? Analipwa na nani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekarabati jengo lile, likaja likabomolewa lote kwa sababu hawakutaka Mahakama, yeyote mhalifu hataki Mahakama. Ikabidi tena Serikali igharimu kukarabati tena upya lakini jengo halifanyiwi kazi. Sasa mimi naona kama hakuna ulazima Mahakama Makao Makuu ya Jimbo, afadhali Mahakama ile iondolewe au lile jengo litumike kwa kazi nyingine ya Kiserikali, kwa sababu Hakimu haonekani na wala hakuna mtu anayetilia maanani kupata Hakimu pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Polisi nzuri kabisa inafanya kazi vizuri, lakini hawana usafiri. Inabidi siku nyingine kama ni kesi za muhimu, watoke kwa basi mpaka Tabora kilometa 45 au wapande treni kwa nauli zao wenyewe kuwapeleka washitakiwa. Kuna riski kwa sababu Mahakama hazipo. Wakikatisha pori kwenda Kigwe, pori lile, nyoka koboko njiani na mshitakiwa nyuma ya baiskeli. Hivi kweli hii haki tunayosema kwamba itafanyika, itafanyika wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Wizara, hii sina matatizo nayo, naifahamu kwa sababu nimefanya kazi miaka kumi katika kuhakikisha kwamba sheria inachukua mkondo wake. Ninafahamu matatizo ya washitakiwa, matatizo ya Mahakimu na Watendaji wote, lakini kama kweli hatutendei haki Jimbo la Igalula, mimi naona kwamba sio vyema lile jengo liendelee kulindwa. Ninaomba likabidhiwe Serikali Kuu ili ifanyike kazi nyingine ambayo itasaidia wananchi wangu wa Jimbo la Igalula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa leo kulikuwa na swali Na. 290 la Mheshimiwa Nyami kwa Utawala Bora. Katika majibu ya Mheshimiwa Waziri amesema, moja ya Idara inayolalamikiwa Mahakamani kwa kesi za rushwa ni Mahakama yenyewe pamoja na Idara mbalimbali. Napenda kusema kwamba, kutokana na kutokamilisha kazi zinazohitajika ili Mahakama ziendeshwe, ndiyo maana rushwa inakuwa sababu mojawapo katika utendaji wa Mahakama. Naomba sana tuwape nyenzo. Naomba sana tuwahimize wafanye hizo kazi. Naomba sana utawala uchukue nafasi yake. Kama kweli danadana itakuwa ni hii katika Jimbo la Igalula, labda tulikosea kuweka Jimbo la Igalula kuwa ni Jimbo na Makao Makuu yake. Suala hili sikutaka kulizungumza kwenye Ofisi kwa sababu nilitumia Ofisi kwa miaka mitatu, lakini sikupata jawabu. Nimeona leo nilizungumze hapa wakati hata wananchi wanasikia na Watendaji wote wanaohusika na haki wako hapa. Msaidieni Waziri suala la Igalula litatuliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunisikiliza, kwa kweli sitakuwa na raha na Jimbo langu kama hali hii itaendelea. Nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Tatu Ntimizi na wazungumzaji wanaofuata wakiokoa muda pia. Basi, tutazidi kushukuru zaidi. Mheshimiwa Mwanne Mchemba, atafuatiwa na Mheshimiwa Anna Komu.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nashukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia katika Wizara ya Katiba na Sheria kwa mambo machache sana. Inawezekana nikaokoa muda kama sitakuwa nimevutiwa na yale ninayoyaongea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitoe pongezi kwa mama yangu, dada yangu Dr. Mary Nagu. Nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Naibu Waziri, Mathias Chikawe, Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa hotuba yao nzuri sana yenye uchangamfu, yenye mwelekeo na inaeleweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina tatizo kubwa sana katika *Affiliation Bill* kuhusu wanawake. Kwa sababu mimi ni Mbunge wa Viti Maalum (Wanawake), nina nafasi ya pekee kuizungumzia hii sheria katika Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nauliza swali langu, tarehe 23 Juni, Wizara ilinijibu kwamba, ni kweli hii sheria haikufanyiwa marekebisho kwa muda mrefu. Sheria hii haikufanyiwa marekebisho tangu mwaka 1964. Kwa mtazamo huo, Serikali haikuona kipaumbele cha sheria hii ili kulinda haki ya mama mjamzito na watoto wanaozaliwa nje ya ndoa. Hilo ndiyo tatizo kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kuna ongezeko kubwa la watoto wa Mitaani na kuna ongezeko kubwa la utupwaji wa watoto wachanga. Hii yote inachangiwa na sheria hii kwa sababu haikufafanua vizuri ni jinsi gani hawa watu wanaweza wakabanwa, wakaeleweshwa na wakadhibitiwa ili angalau hivi vitendo viweze kukoma kabisa katika jamii hii. Miaka ya nyuma hii sheria ilikuwepo, lakini kiwango cha fidia ya mtoto au

mama mjamzito ilikuwa Shilingi 100 na amekiri katika taarifa yao wakati anawasilisha hapa tarehe 23 Juni.

Hivi, katika miaka yote hiyo, Serikali, Wizara ya Sheria na Katiba haioni kwamba waathirika wakuu ni akinamama? Hawaoni kwamba ni tatizo kubwa sana katika jamii? Kwa sababu, sasa hivi kumetokea wimbi moja zito sana, wanaume ambao ni baba zetu sisi tunawategemea na wao wanatutegemea, inapotokea mwanaume akaambiwa kwamba hii hali ya ujauzito ni ya kwako, majibu yake anasema: "Sina uhakika." Ndiyo majibu ya wanaume! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mtazamo huo kikaletwa chombo ambacho kinataka kupima damu baina ya mama na ya mtoto. Hivi Vijijini hiyo mashine ipo? Hata Mjini kweli tutaweza wanawake wote kwenda kupima ili kuhakikisha kwamba hii *group* ya mimba ya mama na huyu mtoto ni sawa! Naomba sheria hii irekebishwe. Mheshimiwa Mary Nagu, nina imani kubwa na yeye, naomba ashirikiane na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ili waweze kufanya kazi ya kutatua hili tatizo. Akinababa mpaka sasa hivi wameongeza sana hata nyumba ndogo, ni nyingi mno, watoto wanatelekezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baba anapokwenda mahali kwa mfano sasa hivi hapa Dodoma, eeh, wanaweza wakaachwa watoto hapa. Unafanyaje kama sheria haipo? Naomba mama yangu, liangalie hilo na liangalie kwa uchungu kama mwanamke, kwa uchungu kama mtunga sheria. Wewe una vyombo vyako, wanaume hawawezi kuipa kipaumbele sheria hii kwa sababu inawagusa. Sasa kwa sababu tumepata na majaji wanawake naomba waliangalie kwa kina na kwa uchungu. Mwanamke yeyote ni kikaango, hakichagui mboga na ndiyo maana methali ikasema kitanda hakizai haramu. Leo kwa nini wanakataa watoto wanaopewa bayana?

Mwanaume akifumaniwa, mwanamke anaridhika. Mwanaume akimfumania mwanamke kinachotokea sasa hapo akimwambia mwezi uliopita kwamba sioni katika hali yangu labda ni mjamzito, anasema: "Mtoto sina uhakika naye, tukapime." Haki iko wapi? Mama yangu, mimi nakuheshimu sana, lakini nisipopata majibu nitasikitika sana, naomba uliangalie sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ubakaji ni tatizo. Askari anapelekewa shitaka kwamba huyu ni mtuhumiwa wa ubakaji, Polisi anasema nenda kwa Daktari. Daktari anathibitisha, ikija kwenye Mahakama, Sheria ya Ubakaji inababaisha sana.

Naomba ifanyiwe marekebisho kama ni kweli, kwa sababu mtu anakamatwa, Daktari kathibitisha, hivi kwa nini mtu huyo anapigwa tarehe? Ni *red-handed,* mtu kakamatwa kabisa anabaka, au ananajisi, leo baada ya miaka 10 bado hukumu yake haijatolewa. Kama ndivyo hivyo, basi anayepatwa na tatizo hilo ahasiwe ili asiendelee. Ni kero katika jamii. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu wamechangia kuhusu Mahakama. Kwa kweli hali na mazingira wanayofanyia Mahakimu ni tatizo, hususan katika Mahakama za

Mwanzo za Tabora. Naomba Mheshimiwa Waziri akipata nafasi baada ya Bajeti yake, hebu aende kuangalia Mahakama za Mwanzo, kuna matatizo huko. Inawezekana ni tatizo la nchi nzima, hata mahali anapokaa Hakimu ukienda utamhurumia. Nenda hapa Dodoma kwa mfano.

Mimi wakati nikiwa Mjumbe wa Kamati ya Sheria na Katiba kipindi kilichopita, tulitembelea Mahakama nikasema: "Eeh, hawa watu hata kama wanakula hii hela, nayo inawala." Afya zao zitakuwa dhaifu miaka mingi inayokuja kwa sababu kuna vumbi, makabati hayapo na yaliyopo hayatoshi, kesi ni nyingi. Hivi hili nalo linataka mjadala!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiti cha Hakimu ni cha mbao, kinapigiliwa misumari. Hivi kweli sheria hii ipo? Halafu bado wanalalamikiwa kwamba wanapata rushwa. Ni mazingira ndiyo yanayosababisha. Karatasi hakuna. Atakapoambiwa nenda kalete karatasi ili nitoe hukumu, kitakachotokea pale ni kwamba Hakimu anadai rushwa. Hebu tuliangalie hili. Wapo wadhaifu, lakini wapo ambao wanatenda haki sawa sawa bila matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la hawa Majaji. Amezungumzia Mheshimiwa Dr. Slaa, sitaki kuliongelea tena, lakini kuna wale Wanasheria. Wanasheria wengi sasa hivi wanaikimbia Serikali wanakwenda kufungua Ofisi zao. Hawapo kutokana na mazingira yaliyopo kwa wanasheria hao. Mwanasheria anakimbia na koti lake barabarani kama analovaa Mheshimiwa Spika, hana usafiri. Heshima yake iko wapi? Anakimbia na mafaili ambayo anategemea kwenda kuitetea Serikali Mahakamani, kuitetea jamii, lakini hana usalama wa kumlinda, hata kigari tu hata pikipiki ya kumwezesha kumtoa pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mheshimiwa Waziri aliangalie sana tatizo hili ili angalau hawa nao waweze kuonekana ni watu kwa fani yao. Kama walivyosema wengine, hakuna wa kumtetea zaidi yetu sisi na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu. Hebu naomba hilo nalo waliangalie kwa umakini sana kuhusu vitendea kazi vya Idara hizi zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ili kengele isije ikanigongea. Nilitaka kusahau, lakini linanikera, ni suala la Mahakama ya Wilaya ya Sikonge. Wananchi wa Sikonge wanatoka Sikonge, ni kilometa kama 55 kuja Tabora kusikiliza kesi zao. Wanapochoka kwa sababu ya nauli na usumbufu, mtu anaacha hata kama alikuwa na haki zake.

Mheshimiwa Waziri, hili leo litatutenganisha mimi na wewe kwa kutopata majibu ya uhakika kuhusu Mahakama ya Sikonge itajengwa lini na imetengewa nini. Kwa sababu mimi nakwenda kule na ninajua umbali wake, kwa kweli ingekuwa sio rahisi kwangu kuliacha hili suala na wewe pia uzungumzie kwamba labda kwa kipengele kijacho au kwa wakati ujao. Naomba leo unipe jibu ili haya mambo yawe sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kwa haraka haraka ni suala zima la kuhusu pensheni. Nashukuru Serikali imerekebisha sheria mbalimbali za wastaafu waliochukua pesa zao kwa mkupuo ndani ya Serikali, lakini wapo ambao sheria haijawaona waliochukua kwa mkupuo katika Mashirika ya Umma. Hawa nao wanafikiriwaje?

Naomba waweze kufikiriwa kwenye hii sheria iliyowalinda hawa wastaafu wa Serikali. Waliokuwa kwenye Mashirika ya Umma kwa wakati ule, nao waangaliwe upya ili warejeshwe rejeshwe kwa kiasi kidogo ambacho Serikali itaweza kuwaonea huruma kwa sababu wastaafu ni wale wale, waliotumikia Serikali ni wale wale, ni kwa utofauti tu kwamba huyu ametumikia kushoto na huyu ametumikia kulia. Ninakuomba Mheshimiwa Waziri japo najua haya yote yanahitaji ufafanuzi mkubwa wa sheria. *(Makofi)*

Pia, niipongeze Serikali kwa kuiangalia Sheria ya Mirathi ya Ardhi, yaani Sheria ya Ardhi kwa Haki ya Akinamama. Nawapongeza pia, lakini bado kuna mila na desturi nyingine hazitambui kumrithisha mwanamke ardhi.

Hivi vyote naomba pia Mheshimiwa mama Mary Nagu ili aweze kuangalia kwamba ni jinsi gani atafafanua hiyo sheria ili iwafikie hata wanawake Vijijini wajue haki zao za msingi kwa jinsi gani Sheria ya Ardhi inavyoweza kuwalinda waweze kukopa, waweze kujiamini na waweze kujipangia maisha yao kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya, maisha bora kwa kila Mtanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. ANNA M. KOMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami leo nitoe yangu machache. Kwanza nikianza kwa kumpongeza ndugu yangu pale, Mheshimiwa Waziri kwa kutengeneza kitabu kizuri kinachofanana na hizo haki zenyewe. Nampongeza pia Naibu, Mwanasheria Mkuu na wale wote waliomsaidia katika kufanikisha shughuli hizi. Hapo hapo nikimwambia awe na kifua kwa sababu kutafuta haki inabidi na wewe uwe mpenda haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 38 wa kitabu unasema, naomba kunukuu: “Kwa mwaka wa fedha uliopita Wizara imeratibu na kusimamia utekelezaji wa mradi wa Benki ya Dunia wa upembuzi yakinifu kuhusu mila mbaya dhidi ya wanawake.” Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafurahi kwamba na mwenyewe Mheshimiwa Waziri ni mwanamke na alitokea kwenye Wizara wakati huo ikiambiwa inashughulikia wanawake. Lakini nikianza, kuna sheria chungu nzima ambazo zimepitwa na wakati. Sheria zinazoendelea kukandamiza hao wanawake, sheria zinazoendelea kumnyima haki mtoto, sheria hizo bado zipo na hazirekebishwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza, kuna Sheria ya Mirathi ya Kimila ya mwaka 1963. Hii sheria kwa kweli imepitwa na wakati kabisa, kwa sababu sheria hiyo mpaka leo inasema kumtunza mtoto ni Sh.100/=. Ukiitupa hapo chini Shilingi 100 hata huyo mtoto akipita haiokoti kwa sababu hata pipi hapati! Sasa hii Sh.100/= sijui inazungumziwaje! Hapo hapo mwanamke mpaka leo hana haki ya kusimamia mirathi kisheria. Nimechuma mimi na Komu miaka 30. Komu leo akifa hata siku moja mimi sitaruhusiwa kusimama kusema kwamba nadai haki, mirathi yangu. Sheria hiyo haipo! Hata kama nitaonewa huruma eti kwa sababu mama Komu atapepeta sana, tumruhusu basi asimamie, lakini je, sheria inaniruhusu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hivi vitu viende na wakati. Kuwe na sheria ya kuniruhusu na kuwepo na sheria ya kujua kwamba mtoto anahitaji haki kwa mzazi wake. Leo utakuta akinamama wanahangaika kudai haki za watoto, wanahangaika huku na huku, akienda Ustawi wa Jamii anapigwa tarehe utafikiri sijui anakwenda kudai nini.

Kinachompeleka pale, ana utitiri wa watoto wanne wamemsakama huko nyuma wamemfuata, mume keshamfukuza ndani ya nyumba, keshapigwa, keshang'olewa meno, katoka kwenye nyumba, hana pa kukaa, mume anaendelea kupeta ndani ya nyumba na anachukua mke mdogo anampeleka kwenye ile nyumba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yote hii ni kwa sababu hakuna chombo ambacho kinamsimamia huyu mama na kumwongoza na kumtafutia haki zake. Mimi ndiyo wa kutoka ndani ya nyumba, lakini mwanamme anaruhusiwa kubaki ndani ya nyumba. Niliuliza juzi, nikaambiwa kwa sababu mimi nasema: "Basi natoka, nakuachia nyumba yako." Haitoshi hiyo, kwamba nikisema hivyo ndiyo sina haki ya ile nyumba. Nitahangaishwa na haki yangu ya kuweza kurudi katika ile nyumba kwa sababu mwanamme ana uwezo, kuku tumefuga wote, atachukua pesa ya kuku aende akatafute kuhonga ili aendelee kubaki na haki. Kwa hiyo, kwa kweli inahuzunisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna sheria nyingine ya mwaka 1971 inaitwa Sheria ya Ndoa. Sheria hii inasema kwamba mtoto akiwa na miaka 14 anaweza kuolewa kwa ridhaa ya wazazi na mtoto huyo huyo akiwa na miaka 15 anaweze kuolewa kwa Sheria ya Mahakama. Hivi mimi nikikuta mtoto wa miaka 15 amekamatwa, niseme kabakwa au niseme ni mtu mzima hiari yake? Bado huyu ni mtoto! Hata wakati tukiolewa sisi tukiwa na umri wa miaka 18, bado tulikuwa watoto kwa sababu ndiyo unashindwa kutoa uamuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba ndugu yangu, Mheshimiwa Mary Nagu, sheria hizi zirekebishwe za haki ya mwanamke. Sheria zirekebishwe za haki ya ndoa, ziletwe hapa tuzipigie kelele, tuzizungumze hizi sheria zipite ili mwanamke awe na haki kwenye desturi zake, awe na haki kwenye mali anayochuma na mumewe, awe na haki ya kurithi, awe na haki ya kusema na pia asiozeshwe kwa nguvu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulitokea kesi juzi, msichana alipigwa mpaka akafa kisa, kwa nini kakataa kuolewa? Hivi kweli, yule baba kachukuliwa hatua gani? Hii ni sheria gani? Labda atahukumiwa kwa sababu yule mtoto alikufa. Lakini kama angekuwa hakufa, hakuna sheria. Baba yake si alisema aolewe!

Kwa hiyo, aolewe! Sasa, tuweke sheria za kuwakinga hawa watoto wetu, ule wakati wa kulazimishwa akina Anna Komu waolewe kwa nguvu, haupo tena umeshapitwa, haupo wakati huo. Sasa hivi mwanamke aseme mwenyewe: "Nataka kuolewa." Wewe kama mzazi uzungumze naye kwamba: "Hapana, huyu mume yuko hivi" na aelewe. Lakini anapokazania ni haki yake, siyo wewe kumkazania kwamba lazima aolewe. Kwa hiyo, naomba sheria hizi ziangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikimalizia, kuna Sheria ya Kubaka. Ndugu yangu aliyekaa hapa sasa hivi ameizungumza. Hii sheria ina utatanishi sana. Umebaka mtoto wa miaka sita umemharibu vibaya vibaya, ana *frustration* za maisha yake, pengine inaweza ikafika asizae, au mwanamme mwingine asimtake kwa sababu keshaharibikiwa. Mwanamme ana miaka 20, anafungwa miaka 30, akitoka jela ana miaka 50 ana nguvu yake ataoa msichana ataendelea. Yule msichana aliyefanyiwa yale ndiyo basi wakati wake umeshakwisha na umri wake umeishakwisha na maisha yake yamekwisha. Sheria hizi za kubakana zirudi tena maana wataendelea kuwabaka mpaka dakika ya mwisho. Huyo aliyekamatwa akihukumiwa miaka 30 kwenda jela, atakwenda hiyo miaka 30.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama juzi hapa Waziri alituambia siku hizi jela kuna wali na nyama mara nne kwa wiki. Kwa hiyo, nitatafuta njia nibake, nistarehe, halafu niende nikale nyama mimi. Nikitoka huko baada ya miaka 15 au 20 naoa, naendelea kuishi. Yule msichana je, tunamkingaje? Tutakomeshaje hili jambo ili watu waogope? Hivi tukikaa hapa ndani tunafikiri kwamba wenzetu Waarabu walivyoweka sheria za kukamata mapanga Ijumaa wanafanya wazimu? Inafika wakati mwanadamu anashindwa, anakuwa kama dudu, kila unavyomwambia haelewi, kila unavyomuweka haelewi, inabidi watu wakamate mapanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hatutaendelea kusema kwamba tunaweka hatua na sheria kali kwa hao wanaobaka watoto wetu, wanakwenda kubaya. Kwa hiyo, hizi sheria zirudiwe tena, ziangaliwe tena, muangalie tangu siku tulipotunga sheria mpaka leo kuna kesi ngapi, wamebakwa wangapi na wamekufa wangapi na walio kwenye mateso ya kubakwa ni wangapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, ninaomba nisaidiwe. Tena ninafurahi maana na baba yangu yupo leo atanisaidia kweli. Ningeomba nieleweshwe maana ya neno ujamaa, linanipa taabu. Kwa sababu Marehemu baba yetu Mzee Nyerere alipoleta ujamaa huu akauweka huku kwenye Katiba, ulikuwa ujamaa wa kweli kweli. Kila mmoja alikuwa anajua kweli tunaishi kwa ujamaa na kweli, Watanzania ni watu wa kujitegemea. Alituwekea Makampuni, Mashirika na mambo mengi tu tukaendelea kujitegemea. Ngozi yetu ilikuwa inatoka kwa ng'ombe wetu, inapelekwa kwenye viwanda vyetu, tumeajiriwa, tunatengeneza vitu vyetu, tunapeleka nje kuuza, tunajitegemea. Leo yako wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hapo hapo ukurasa wa 18 wa Katiba hii ndogo inasema hapa kwamba: "Lengo la Katiba hii ni kuwezesha ujenzi wa Jamhuri ya Muungano wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar au chochote kati ya vyombo vyake na udugu na amani kutokana na Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea ambayo inasisitiza utekelezaji wa misingi ya kijamaa kwa kuzingatia mazingira yaliyomo katika Jamhuri ya Muungano."

Sasa hapo kipengele (c) kinasema kwamba: "Shughuli za Serikali zinatekelezwa kwa njia ambayo itahakikisha kwamba utajiri wa Taifa unaendelezwa, unahifadhiwa, unatumiwa kwa manufaa ya wananchi wote kwa ujumla." Leo tumechukua utajiri wetu, tunakaribisha watu eti tunawaita hawa wanakuja kuwekeza. Leo madini yetu na utajiri

wetu ndiyo tumewapa wao, sisi tunaonekana ni vibarua wa kufanya kazi kwenye utajiri wetu. Unatunufaisha nini huu utajiri? Ikiwa kweli leo dhahabu, almasi, *tanzanite*, tumeweka watu wa kutoka nje ndiyo wao wamiliki, sisi ni vibarua wa kufanya kazi na nikionekana Mtanzania napitapita kwenye pembe za pale, napigwa risasi. Haki iko wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba tunachokizungumza na tunachokisoma kwenye huu msahafu watanisamehe, kwa sababu Katiba ya Nchi ndiyo inayotuongoza tuendane na jinsi Katiba inavyozungumza, tusiende kinyume na Katiba inavyozungumza, halafu tukatafuta vipengele vya kusema, maana mtu anakwenda kinyume halafu anatafuta uchochoro wa kupenya ili isije ikawa kwamba amekwenda kinyume. Tufanye yale ambayo yamo humu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ni Wizara nzuri kweli. Mama ninakuomba sana sheria nilizozisema zirekebishwe na ninaomba sana nipewe ufafanuzi wa ujamaa na ninaomba sana niambiwe kulikoni kuleta wageni kukamata mali zetu wakati sisi wenyewe tupo.

Ni kwa nini sisi tusishike zile mali na hao Wazungu kama hatuelewi vizuri tukawaita wakawa waajiriwa wakatuelewesha tufanye nini ili hata mimi nikiiba ni mali yangu na nikichukua mimi itamalizikia hapa hapa Tanzania. Nikichukua *tanzanite* itamalizikia hapa hapa, nikichukua dhahabu ni hapa hapa, lakini wenzetu wanapochukua wanakwenda kutajirisha makwao sisi tunabakia na mikono ya shingo tukisema kwenye miti hakuna wajenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Kwa sababu ya kuokoa muda, pongezi nimeshamaliza, nimeishampa Mtoa hoja pamoja na wataalam wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nikizungumza katika Wizara ya Madini nilikuwa na wasiwasi sana juu ya ndugu zetu Wanasheria na nikatoa hoja kwamba Bunge liunde Kamati ya kuchunguza. Lakini baadaye sikuendeleza hiyo hoja kwa sababu nilikuwa ninangoja kwenye Wizara hii ambayo inahusika moja kwa moja na Wanasheria na mikataba mbalimbali ambayo inafanywa. Kwa hiyo, sikusudii kuwa na maneno mengi kwa sababu *Hansard* ipo waliishasoma.

Lakini kwa kukumbusha tu ili kwenda vizuri, niligundua kwamba Sheria za Madini ambazo zimepitishwa na taratibu ambazo zimepitishwa katika madini, bado isingetosheleza kwa sababu bado maeneo mengine vile vile yana matatizo na utata kama ilivyo katika maeneo yetu. Yako maeneo ya *IPTL*, ukiangalia Mtibwa, *ATC*, *Net Group Solution* na ukiangalia hata mabenki. Mabenki yanafumka kwa sababu pengine sheria zetu zinawapa fursa kubwa zaidi wawekezaji kuliko kutupa sisi Watanzania. Sasa nimeona hapa ni mahali pazuri ambapo naweza kupewa ufafanuzi na ninaweza kupewa maelekezo katika Wizara hii ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi unapouliza juu ya Mikataba hii ya Serikali, Serikali inatuambia: "Hii ni siri ya Serikali." Lakini ninachojua ni kwamba, Bunge lako ndiyo msimamizi wa shughuli zote za Serikali kwa niaba ya wananchi na Katiba inatupa fursa hiyo. Kwanza kazi yetu kubwa ni kutunga sheria, lakini ya pili, inatupa fursa ya kuisimamia Serikali kwa niaba ya wananchi. Ukiangalia Katiba katika Ibara ya 63 (3) kinasema kwamba: "Kujadili na kuridhia mikataba yote." Sasa inakuwaje mikataba mingine iwe ni siri? Inakuwaje sisi tuweze kuisimamia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli napenda Wizara hii inipe ufafanuzi mzuri zaidi kwamba kwa nini Katiba inatupa uhuru wa kusimamia na kuishauri Serikali, inatupa fursa ya kujadili na kuridhia Mikataba yote je, hii Mikataba inayosemekana ni ya siri, iko kwenye Katiba gani nyingine? Ni Katiba hii hii au kuna Katiba nyingine inataja mikataba ambayo ni ya siri? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu nilizungumza siku ya madini, nisingehitaji kuzungumza sana juu ya hili, lakini napenda nikumbushe ili Waziri na Mwanasheria Mkuu waweze kusaidia kutoa maelekezo. Ningependa kurudia kwamba imefika wakati mzuri sasa Bunge lako hili liunde Kamati maalum ya kuchunguza mikataba yote ili maslahi ya Taifa yaweze kuwepo. Lakini vile vile, imefika wakati sasa Kamati za Kisekta ziweze kujadili mikataba yote kwa maslahi ya Taifa letu. Hilo ni la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni juu ya swali langu la nyongeza leo na linamhusu moja kwa moja Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Nimezungumza kwamba mwaka 2005, uchaguzi ulifanyika mwezi Desemba, badala ya mwezi Oktoba kama ambavyo tumezoea. Kwa sababu ya mapenzi ya Mungu, ukafanyika mwezi wa Desemba na nimezungumza kwamba uhai wa Bunge ni miaka mitano. Bahati mbaya wakati *Chief Whip* ananijibu, hakujibu sawasawa swali langu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma Katiba Ibara ya 65 kifungu (1) Katiba inatamka wazi na napenda kunukuu: "Bila kuathiri masharti mengine ya Katiba hii, maisha ya kila Bunge yatakuwa ni muda wa miaka mitano." Ibara ya 65 (2) inaeleza maana ya maisha ya Bunge, kwamba: "Maisha ya Bunge yanaanzia ule muda wa Bunge jipya lilipoitishwa."

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ningependa hoja hii iwekwe wazi na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Katiba inasema ni miaka mitano tokea Bunge jipya lilipoitishwa, siyo kama nilivyojibiwa na *Chief Whip* kwamba tutaangalia tutaona, au kama tunaangalia maana yake tubadilishe Katiba au kama tutaona maana yake tuvunje Katiba kwa sababu inatutaka tuishi miezi 60. Kwa hiyo, ningependa katika majumuisho, anijibu kwa ufasaha na wananchi wote waweze kuelewa kwamba maisha ya kila Bunge ni miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalo Jeshi la Sungusungu wale ambao wanatoka katika kanda ya Magharibi, Kanda ya Ziwa wanaweza kuniunga mkono. Sungusungu hawa wamefanya kazi nzuri sana hasa ya kukomesha wizi wa mifugo na wizi mdogo

mdogo na kila mtu kwa kweli hapa anastahili kuwapongeza kwa kazi nzuri ambayo wameifanya. *(Makofi)*

Lakini bahati mbaya sana Sungusungu hawapendwi na Mahakama na Polisi pamoja na kazi nzuri ambayo wameifanya sungusungu ya kurejesha amani. Maana ilifikia wakati kule kwetu unaweza kulala mlango wazi bila matatizo yoyote kwa kazi nzuri ambayo inafanywa na Sungusungu.

Bahati mbaya sana Idara ya Mahakama na Idara ya Polisi, hawaitaki kabisa Sungusungu. Mara nyingi Sungusungu wanapofanya kosa dogo tu hapo hapo Mahakama, hapo Polisi watasimamia bango na kuwakamata na kuwatia ndani. Hivi ninaposema, wapo Sungusungu wamewekwa ndani kwa miaka mitano, mitatu mfululizo na bado hawajapelekwa Mahakamani. Namna hiyo unadhoofisha nguvu za wananchi kujilinda wenyewe kwa sababu wanaona wakijilinda tu watakamatwa. *(Makofi)*

Mimi ningeomba Mahakama na nimefurahi sana watu wa Mahakama wapo, Jaji Mkuu yupo, Mwanasheria Mkuu yupo, wawaambie hawa ni wenzetu, hawa wanatusaidia sana katika Ulinzi, katika kuleta usalama na katika kurejesha amani katika maeneo yetu, ni wenzetu. Kweli matatizo yapo, makosa yapo lakini tuwasaidie kuonyesha sheria, tuwasaidia kuwafundisha sheria, tuwasaidie hata kuwaondoa katika matatizo yale.

Sungusungu hawa wana taratibu zao. Mimi huwa nasikiliza sana redio na kusoma magazeti wana taratibu za kuchukulia hatua mhalifu, mwizi, lakini huwa nashangaa sana magazeti na redio Mjini wanampokamata mwizi wanampiga, wanamchoma, wanamfanya wanavyotaka, baadaye askari au Mahakama wanasema huyu jambazi ameuwawa na wananchi wenye hasira kali. Lakini kule Kijijini kwenye Sungusungu akishakamatwa jambazi au mwizi yeyote akauwawa wanakamatwa Sungusungu. Hivi hawa wanakijiji wenyewe mnadhani hawana hasira kali? Wenye hasira kali wako Mjini tu, huko Kijijini wenye hasira kali hakuna! Hapana! Haiwezekani! Hawa nao wana hasira kali kama vile watu wa Mjini.

Kwa hiyo, tuwasaidie, yule ni jambazi, anajulikana jambazi, bahati mbaya ameuwawa. Kama vile inavyotokea Mjini, ameuwawa na watu wenye hasira kali na kule kwa Wungusungu itokee wawe ni watu wenye hasira kali na kweli Sungusungu na wenyewe wana hasira kali. *(Makofi)*

Mimi ningeomba Mahakama na Polisi wasaidie hawa Sungusungu na ningeshauri kabisa kwa kweli, hebu ifike mahali tuone kwamba hawa nao ni wabia katika kuleta amani. Yapo mambo mengine ambayo wanafanya hawa Sungusungu wakienda wale wakorofi, mkorofi hataki kuchangia majengo, mkorofi hataki kwenda kuzika wenzake, mkorofi hashiriki kwenye shughuli za kijamii, zipo taratibu ambazo Sungusungu wameziweka.

Wakishakwenda Mahakamani, yule mkorofi ndiye anaonekana wa maana kuliko wale wananchi walio wengi. Mimi nakubali nchi yetu kweli inaendeshwa kwa sheria, sina matatizo. Sheria zinatungwa na Bunge, lakini inaendeshwa vile vile na kanuni,

kanuni inatungwa na Waziri pamoja na watu wake, lakini inaendeshwa vile vile kwa taratibu.

Hivi hizi taratibu ambazo tumeziweka kule Vijijini kwamba, sisi wote lazima tuzikane, sisi wote lazima tushiriki mambo ya jamii, iweje mmoja akishindwa kufuata zile taratibu anaonekana yeye ni wa maana kuliko wengi? Haiwezekani! Akienda Mahakamani huyu, wanachukuliwa Sungusungu, wanawekwa ndani, wanafungwa kwamba wamekiuka Katiba ya Sheria, wamemnyima uhuru wa kuishi kwa raha. Ataishije kwa raha peke yake, sisi wengine tuna shida? Lazima tuwasaidie Sungusungu kwa sababu nao wanafuata taratibu vile vile. Yeye kama anavunja taratibu zetu ambazo tumekubaliana yeye ni mkorofi achukuliwe hatua kuliko kuwachukulia hatua walinzi wetu wa Sungusungu kwa sababu kama tunawachukulia hatua, mbona Kanisani hatuwachukulii hatua? *(Makofi)*

Sisi wote tunaamini Kanisani au Msikitini ukikiuka masharti kule Kanisani, wanakufungia sakramenti. Sijawahi kuona hata siku moja muumini amekwenda Mahakamani kumshtaki Padri kwamba ameninyima sakramenti. Kwa nini Sungusungu hawa wanapelekwa Mahakamani kwa sababu mhalifu mmoja tu amekiuka taratibu ambazo Kijiji kimejiwekea? Kwa hiyo, nilikuwa naomba Sungusungu hawa tuwasaidie na ningeomba Sungusungu wote walioko ndani watolewe nje. Wamefanyakazi nzuri sana kwa wale wote wanaotoka Kanda ya Ziwa Mikoa ya Mwanza, Shinyanga na Tabora wanaelewa kazi nzuri iliyofanywa na Sungusungu hawa. Naomba watolewe, wako wengi Magerezani na kesi zao haziendi. *(Makofi)*

Lakini lingine katika Sungusungu, ningeomba na yenyewe itambulike kama Jeshi. Kama utasema Jeshi la Mgambo, au utasema Jeshi la namna gani, lakini itambulike ili Sungusungu anapofanya ile kazi, angalau waweze kulipwa kifuta jasho. Wanapambana na wahalifu ambao wana silaha, hawa Sungusungu hawana silaha, silaha yao kubwa ni fimbo, kifua wazi na mishale, basi. Lakini wameweza kuwakomesha ambao wana bunduki wakashika adabu, kwa hiyo, ni watu wa kuthaminiwa sana kwa kufanya kazi vizuri, hivyo waweze kupewa kifuta jasho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, ni haya malipo ambayo yanatolewa kwa mtu aliyehukumiwa. Nimefuatilia kwa makini sana mjadala ambao unasema juu ya wabakaji. Lakini nina mfano hai, mtu anatuhumiwa ameiba kwa mfano pale Nzega, kuna mtu ambaye alituhumiwa ameiba ambaye alikuwa Mhasibu wa Mahakama, alituhumiwa lakini Mahakama ikamtia hatiani ikamfunga miaka kumi mwaka 1998, aliiba fedha za mirathi ya wananchi. Hizo fedha za mirathi hazijalipwa mpaka leo, eti mpaka aje arudi kutoka kifungoni ndiyo yale yale ambayo yanatoka hata kwa hawa wanaobaka anafungwa kwanza, ndiyo aje kutoa adhabu. Hii sheria, inaumiza hawa ambao wameathirika, hawa wananchi ambao wangelipwa fedha zao za mirathi walitakiwa walipwe kwanza ndiyo afungwe.

Wakati unamfunga ana mali, kwa nini ile mali isipigwe mnada ili aweze kulipa hawa wananchi, miaka 10 wanamsubiri toka mwaka 1998 wanamgonja mpaka mwaka 2008 akitoka ndio aje awalipe, haki iko wapi? Tunasema nchi hii inaendeshwa kwa haki, hujawatendea haki hawa, kwanza ni yatima, kwanza ni wajane, hela zao zimeliwa, baba

yao amefariki au mama yao amefariki, bado una fedha unasema kwamba mpaka arudi. Kwa nini basi Mahakama au Serikali isingelipa baadaye ije imdai kwa sababu wenyewe ndiyo wanamfahamu, wao wanamfahamu kuliko wananchi wale ambao ni wajane, yatima hawamfahamu yule mtumishi wameliwa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwaachia na wengine, naomba niishie hapa, lakini ningefurahi kupata majibu kwenye Kamati ya matumizi ya Bunge. Naelewa dada yangu, Mheshimiwa Mary Nagu ananifahamu lakini nimemwambia Chikawe kuku mzuri kumchinja, ni yule wa kwako. Ahsante sana. *(Kicheo/Makofi)*

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuweza kunipa nafasi ya kuweza kuchangia hotuba hii. Kwanza kabisa, nipongeze kwa hotuba nzuri ambayo imetolewa na Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria na mimi bila kuzunguka ni kwamba naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa leo naomba nianzie na utaratibu wa Mahakama zetu na utaratibu huu ni kuhusu utoaji wa hukumu za Mahakama na hasa Mahakama ya Rufaa *(Court of Appeal)* ni wazi kwamba hukumu ya Mahakama ya Rufaa kisheria inaitwa *precedent* ni kwamba hukumu ikishatolewa inakuwa ni sheria yenyewe na inakuwa inatumika na Mahakama za chini, yaani *High Court*, Mahakama ya Hakimu Mkazi, pamoja na Mahakama nyingine ndogo. Mahakama za chini ziweze kutoa maamuzi sahihi na mazuri ambayo yatakuwa *challenged,* lazima zihakikishe kwamba hazipingani na maamuzi ya Mahakama ya Rufaa.

Sasa hizi hukumu mara nyingi zimekuwa zikitolewa kwenye vitabu maalum vinaitwa *Law Reports*. Kwa kweli zimekuwa zikisaidia. Lakini kwa bahati mbaya ni kwamba Mahakama yetu ya Rufaa haijawezeshwa kutoa hukumu zake kwa wakati. Utakuta hukumu inatolewa siku kama ya leo na ni hukumu muhimu sana ambayo inatengeneza sheria, lakini inachukua miaka miwili/mitatu/mitano mpaka sita haijawa *reported* kwenye vitabu vyetu vya *Law Reports*.

Kwa maana hiyo, basi utakuta zile Mahakama za chini yake ikiwemo *High Court* pamoja na Mahakama za Hakimu Mkazi wakati mwingine zinatoa maamuzi ambayo yanapingana na maamuzi ya Mahakama ya Rufaa. Katika hili, nilitaka kushauri kwamba Wizara ijitahidi sana kuhakikisha kwamba hukumu za Mahakama ya Rufaa zinatolewa kwa wakati na zinaweza kuingizwa kwenye *Law Reports* pamoja na *Library* kwa wakati muafaka ili Mahakama zetu za chini ziweze kutumia hiyo *precedent* ya Mahakama ya Rufaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, nizungumzie mlundikano wa kesi Mahakamani. Mengi yamesemwa kuhusiana kuchelewa kwa kesi Mahakamani, Waheshimiwa Majaji, Waheshimiwa Mahakimu wamekuwa wakilaumiwa sana kwamba wanachelewesha kesi pale Mahakamani. Lakini ukweli nilitaka niseme kwamba Majaji wetu pamoja na Mahakimu na Mawakili wa Serikali wamekuwa wakifanya kazi nzuri sana na wanajitahidi isipokuwa wanafanya kazi katika mazingira magumu sana. Mlundikano wa kesi hizi Majaji wenyewe binafsi hawawezi kuondoa kwa sababu Majaji

wetu ni wachache sana na sijui ni sababu ambao inaifanya Serikali iwe na kigugumizi cha kutoteua Majaji wa kutosha kuendana na uwingi wa kesi ambazo ziko Mahakamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye *High Court Registry* ya pale Dar es Salaam utakuta wako Majaji kama saba na wengine majuzi wameteuliwa kutoka kwenye *High Court* ya Dar es Salaam nadhani na nyingine ya Moshi kwenda kwenye Mahakama ya Rufaa na mpaka sasa hivi bado hatujapata Majaji wengine. Lakini kesi zinafunguliwa kwa wingi sana kwa kweli Majaji wetu wanachoka wanahitaji waongezewe Majaji wengine. Kwa takwimu tulizonazo wako watu wengi sana ambao wako *competent* kwa ajili ya kuwa Majaji na hapa nasema kwamba tunao Mawakili wa Serikali Waandamizi wenye uzoefu, wengi sana ambao wanastahili kuteuliwa kuwa Majaji. Tunao Mahakimu ambao wanastahili kuwa Majaji na vile vile Mawakili wa Kujitegemea ambao wanastahili kuwa Majaji na mimi Wakili wa Kujitegemea siku nikiteuliwa sitakataa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo nilitaka nizungumzie nyenzo kwa ajili ya watumishi wetu wa Mahakama pamoja na Mawakili wa Serikali. Niliwahi kuwa Wakili wa Serikali, tatizo kubwa sana ambalo linawakumbuka watumishi wetu hawa kwa kweli Serikali imewasahau kwa muda mrefu sana. Iimewasahau kwamba wanafanyia kazi katika mazingira magumu, Wakili wa Serikali wa hapa Tanzania kwa kweli hathaminiwi hata kidogo. Mawakili wa Serikali, hawana nyumba, lakini wanaendesha kesi kubwa sana mnazosikia za mauaji, madawa ya kulevya pamoja na kesi nyingine nzito nzito.

Lakini hawa watu wanaishi Mitaani, Wakili wa Serikali hana nyumba na vile vile hana hata usafiri kama gari. Sasa utakuta Wakili wa Serikali akitaka kwenda Ofisini wakati mwingine inabidi aombe *rift* tena anaomba *rift* ya mtuhumiwa yule, ambaye anakwenda kum -*prosecute* kule Mahakamani. Sasa katika mazingira kama haya tunayafanya Mawakili wetu wa Serikali wapate kazi nzito sana katika kuendesha shughuli zao. *(Makofi)*

Nilikuwa napendekeza kwamba Serikali iangalie hili, ikiwezekana iwakopeshe magari ya kawaida ili Mawakili wetu wa Serikali wapate usafiri. Vile vile, nilikuwa nashauri Serikali ijitahidi sana kuwatafutia nyumba za kuwapangisha na ikiwezekana na Mawakili wetu wa Serikali wakopeshwe ikiwemo pamoja na Waheshimiwa Mahakimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni aibu kubwa sana kumkuta Mheshimiwa Hakimu Mkazi wa Mahakama yoyote anakwenda kupanga uchochoroni, huko uchochoroni anakaa pamoja na majambazi, anakaa pamoja na watuhumiwa ambao kesho yake wata-*appear* mbele yake wakiwa na kesi. Katika mazingira kama haya na uzingatia kwamba huyo Mheshimiwa Hakimu naye ni binadamu atafikia mahali atashindwa kutenda haki na tutabaki tunamlaumu bure.

Naiomba sana Serikali ijitahidi kuwapa nyumba Mahakimu wetu ili waweze kuwa katika mazingira ambayo ni huru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi tunao wanafunzi wengi ambao wamemaliza Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, *degree* ya Sheria. Hawa wanafunzi wengi wako Mitaani mpaka sasa hivi. Baadhi yao wameshapata nafasi za kuajiriwa na wengine wanasubiri waweze kufanya mitihani yao ya Uwakili ili waweze kuwa Mawakili wa kujitegemea.

Lakini nilikuwa nashauri kwamba kwa wale ambao bado wako Mitaani na ambao hawajapata kazi, basi Serikali iangalie uwezekano wa hawa vijana ambao ni ma-*graduates* kuwatumia katika Mahakama zetu hasa Mahakama Kuu hawa watumike kuwasaidia Waheshimiwa Majaji, wawasaidie katika kufanya *research* kwa sababu nafahamu kwamba Majaji wetu wana kazi nyingi mno na tunategemea Jaji atoe *judgement* ambayo ni ya *standard* wa Jaji. Sasa ili aweze kutoa *judgement* hiyo anahitaji kufanya *research* ya makini. Sasa vijana wetu hawa wakiweza kuajiriwa wataweza kusaidia sana Majaji wetu kufanya *research* na wenyewe watakuwa wamepata ajira kwa njia moja au nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nigusie suala la kupanda vyeo kwa Waheshimiwa Mawakili wa Serikali pamoja na Mahakimu. Limekuwepo tatizo la muda mrefu kwamba Mawakili wa Serikali walio wengi vyeo vyao vinachelewa kupanda. Hili lilishasemwa sana hata pamoja na Waheshimiwa Mahakimu. Mimi sijui ni kwa nini sababu gani ambayo inafanya mtumishi wa Serikali na hasa *state attorney* hasa Wakili wa Serikali, amefanya kazi kwa muda mrefu sana cheo chake asiweze kupanda. Mimi nilikuwa nashauri Waziri mwenye dhamana Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, nakuomba hili uliangalie kwa sababu kama mtu anafanyakazi na hapandi cheo kwa kweli anafika mahali anakata tamaa ya kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nigusie Mahakama za Wilaya ya Karagwe. Wilaya ya Karagwe inayo Mahakama ya Wilaya ambayo iko pale Kayanga, jengo lake ni siku nyingi sana nadhani aliacha Mkoloni nadhani alikuwa Mwingereza au Mjerumani, tunaomba lifanyiwe ukarabati na liwekwe katika hadhi ambayo hata mtu anayekwenda kusikiliza kesi yake pale ataona kwamba anaingia kwenye chombo cha kutenda haki kwa haki kwa sababu ni mahali pa heshima. *(Makofi)*

Sambamba na hilo tunazo Mahakama za Mwanzo nikianzia na Mahakama ya Kata ya Nyaishozi. Namkaribisha Waziri mwenye dhamana apitie siku huko akaangalie zile Mahakama zinavyofanana, Mahakama ya Nyaishozi ni ya siku nyingi imebomoka na haifai, sisemi kwamba aikarabati mimi nasema wajenge Mahakama nyingine ambayo inaendana na hadhi ya watu wa Kata ya Nyaishozi, Kata ya Nyabionza, Mahakama ya Nyabionza ya mwanzo ni mbovu naomba ijengwe mpya. Vile vile, Mahakama ya Kituntu, Mahakama ya Mwanzo ya Kayanga na Mahakama ya Mwanzo ya Isingiro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naangalia hapa kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ameelezea ujenzi wa majengo mapya lakini kwa upande wa Wilaya

ya Karagwe sijaona hata jengo moja kwa ajili ya Mahakama ya Mwanzo pamoja na Wilaya. Sasa nategemea wakati anajumuisha nadhani ataweza kunituliza kwamba angalau Mahakama za Mwanzo zitapata majengo mapya.

Pamoja na hiyo Mahakama yetu ya Karagwe inayo *in-charge* mmoja pale Wilayani ambaye anazungukia Mahakama zote za Wilaya. Lakini pale Wilayani Karagwe wana tatizo la usafiri wanalo gari moja aina ya Suzuki ambayo inabidi atumie Hakimu *in charge* kuzungukia Mahakama zote kwa ajili ya ukaguzi. Ni gari ya zamani sana, tunaomba Mahakama ipatiwe gari mpya yenye uwezo wa kuzunguka katika Wilaya nzima ya Karagwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kurudia kwamba naunga mkono hoja. Ahsante kwa kunipa nafasi *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Baada ya kumsikia Mheshimiwa Blandes Mheshimiwa Juma Nh'unga Mbunge wa Dole alinihakikishia kabisa kwamba dakika tano zinamtosha. Karibu Mheshimiwa.

**MHE. JUMA S. NH'UNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nichukue nafasi hii nikushukuru sana kwa kunipa hizo dakika chache na mimi nitajitahidi sana nitumie hizo hizo dakika chache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri na Mawaziri wenzake. Sasa kwa sababu dakika zenyewe chache na mimi nizitumie hivyo hivyo kwa uchache wake, nianze na Ilani ya Chama cha Mapinduzi ukurasa wa 132 Ibara ya 108 (b) Mzee Kingunge nadhani anajua hilo, inasema: "Kulipatia ufumbuzi suala la kuanzishwa kwa Mahakama ya Kadhi Tanzania Bara."

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa namsikiliza kwa makini sana Waziri alipokuwa anatoa hotuba yake. Mimi Mheshimiwa Waziri, anafahamu kabisa kwamba ni mshabiki wake mara nyingi anaposema huwa napenda kumsikiliza hata nikiwa nakunywa chai mara nyingi kikombe nakiweka pembeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikiliza kifungu kwa kifungu hotuba hii na ameisoma kitaalam sana. Hotuba tulizopewa sisi ni kubwa zaidi aliyosoma yeye baadhi yake hayamo. Kwa hiyo, sisi imeboreshwa tuna mengi zaidi lakini sikuliona hili suala la kuanzishwa kwa Mahakama ya Kadhi. Ni jambo ambalo limo kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano, amekuwa anazungumzia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi na amesema Wizara zote amezikabidhi Ilani za Uchaguzi. Sasa nataka nijue Mheshimiwa Waziri alipokabidhiwa Ilani ya Uchaguzi kifungu hiki hakukabidhiwa? Kwa sababu amejulikana kwamba yeye yuko karibu na Mzee Kingunge atamkumbusha tu au namna gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili la kuanzishwa Mahakama ya Kadhi limekuwa linanung'unikiwa kwa muda mrefu sana, shahidi yangu wa kwanza Mzee Kingunge. Mwaka 1998 Bunge baada ya minong'ono mingi liliunda Kamati Ndogo na niwie radhi, niwataje wajumbe.

Wajumbe wa kwanza alikuwa Mheshimiwa Arcado Ntagazwa wakati huo ndiyo Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria, Mzee Kingunge alikuwa - Mjumbe, Dr. Msabaha - Mjumbe, Mzee Manyanya - Mjumbe, Dr. Zainab Gama - Mjumbe, Mheshimiwa Yusuf Mohamed Yusuf - Mjumbe na mimi mwenyewe nikiwa Mjumbe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikiri tumefanya kazi nzuri kweli kweli muda wa miaka miwili, tumesaidiana vizuri sana na akiwemo mzee wangu Mheshimiwa Kigunge alitusaidia sana baadhi ya sehemu tulikwenda kutafuta maoni na mambo mbalimbali zilikuwa moto, lakini Mzee Kingunge kwa busara yake alipoza hizo nafasi. Sijui alipoza kwa imani gani, lakini alipoza, aliweza kusema na waliokuweko huko walimsikiliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo huo mwaka 2000 hii mwaka 1998 Kamati ilifanya kazi ikakamilisha, haikuwahi kuwasilisha katika Bunge. Lakini tena mwaka 2000 Spika akaiagiza Kamati ya Katiba na Sheria ilichunguze tena jambo hili na Kamati hiyo ikafanya kazi naye tena, ikatumia hela za Serikali.

Kamati ya mwanzo imefanya na ya safari hii ilikuwa na watu wengi zaidi kwa sababu kipindi hiki ilikuwa na watu 20, ikazunguka, baadhi ya wajumbe wamekwenda mpaka Msumbiji, wengine wamekwenda Kenya, wengine wamekwenda Uganda na nchi mbalimbali nasikia wengine walifika mpaka Uingereza. Wakamaliza kazi na taarifa hiyo iliwasilishwa katika Bunge na *Hansard* ninayo hii iliwasilishwa siku ya tarehe 11 Februari, 2005 na iliwasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Athumani Janguo. Lakini kwa bahati mbaya Bunge halikujadili jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano ina maneno inasema katika nchi ya Tanzania kama ilivyo nchi nyingine ambayo katiba ndio sheria mama, Katiba ya Tanzania inatoa uhuru wa kuabudu katika Ibara ya 19 (1) na (2), Ibara ya 19 inatamka kuwa kila mtu anastahili kuwa na uhuru wa mawazo, imani ya uchaguzi katika mambo ya dini pamoja na uhuru wa mtu kubadilisha dini au imani yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ibara ya 19 (1) kama ilivyo haina mipaka. Ibara ya 19 inasema bila ya kuathiri sheria zilizohusika na Jamhuri ya Muungano kazi ya kutangaza dini kufanywa ibada, kuenezwa dini, itakuwa ni huru na jambo la hiari ya mtu binafsi, ibara ya 19 kama ilivyo inatoa haki hiyo kwa kuweka mipaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama katiba imeshasema hivyo hili jambo la kutaka kuweka Mahakama ya kadhi linatisha nini, bahati nzuri leo nina gazeti hapa la rai mtu mmoja anaitwa *Prince Bagenda,* ameandika makala humu. Lakini bado sikupata maelezo yoyote, sikupata sababu zozote mpaka leo.

Sasa nilikuwa najiuliza kwamba labda Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake ndefu inawezekana atanijibu baadaye.

Kwa hiyo, sitaki niseme zaidi ya hilo. Ni dogo tu na nilikuwa nayo mengi lakini kwa heshima na taadhima kwa sababu umeniambia nizungumze dakika tano na kwa kawaida ya Wagogo na Wasukuma wanaposema wanakubaliana, haidhuru ni watani wa jadi, sitaki nivuke mipaka. Naomba kuunga mkono hoja na kuwatakia kila la heri na fanaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nh'unga ametupa somo la matumizi ya muda, tunakushukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge, tutakubaliana kwamba muda wetu unaelekea kwisha. Nitambulishe mgeni wa Mheshimiwa Batilda Buriani, ambaye Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, mwimbaji wa Injili kutoka Arusha anaitwa Betrice Muhone karibu sana. Huyu atakuwa na shughuli ya kuzindua albam yake Dodoma hoteli tarehe 5 Agosti, 2006.

Waheshimiwa Wabunge wote, mnakaribishwa kusikiliza na kujionea wenyewe. *(Makofi)*

Jingine nililotaka kusema ni kuhusu jioni kama nilivyosema mafungu yako mengi ili Waheshimiwa Wabunge msipate tatizo kwa muda huu wa kujiandaa hadi jioni, mafungu yetu yapo sita.

Litakuwepo fungu Na.40 la Mahakama, Fungu 41 la Mwanasheria Mkuu, Fungu Na. 55 la Tume ya Haki za Binadamu, Na. 59 ya Tume ya Kurekebisha Sheria, Fungu 64 ya Mahakama ya Biashara na Na. 90 ya Mahakama ya Ardhi.

Ili twende vizuri jioni, mwisho jioni Msemaji wetu atakuwa mmoja tu Mheshimiwa Diana Chilolo, baada ya hapo atafuatiwa na Naibu Waziri, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, baadaye Mtoa mada mwenyewe na kama Mheshimiwa Diana Chilolo atakuwa hayupo, Mheshimiwa Yono Kevela ajiandae.

Baada ya kusema hayo naomba sasa nisitishe shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilifungwa Mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuwa kitinda mimba katika kuchangia hoja ya Waziri wa Katiba na Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kukushukuru wewe, nitumie nafasi hii nimshukuru sana Ndugu yangu, mtani wangu Mheshimiwa Dr. Mary Nangu, Waziri wa Katiba na Sheria, ndugu yangu, Mheshimiwa Mathias Chikawe, Naibu Waziri na Mwanasheria Mkuu wa Serikali na si mwingine ni Mheshimiwa Johnson Mwanyika. Nawapongeza sana kwa kuandaa Bajeti nzuri na ambayo imewasilishwa kwa ufanisi mkubwa, wananchi wana imani sana na hotuba hiyo na hasa akinamama kwa sababu Waziri mwenye dhamana ni mwanamke mwenzao na wana matumaini sana na Waziri, Mheshimiwa Dr. Mary Nagu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo basi nitumie nafasi ya awali kuzungumzia suala la Mahakimu kukaa kituo kwa muda mrefu. Kwa kweli kuna tabia ya Mahakimu kukaa kituo kimoja cha kazi kwa muda wa miaka mingi sana tendo ambalo linawafanya Mahakimu hawa kuolewa na mazingira na kusahau wajibu wao uliowapeleka katika vituo hivyo na kuingia katika tabia ambazo haziwatendei haki raia wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mheshimiwa Mwenyekiti ni mama, nina hakika sasa Wizara imepata mtu. Nina hakika Mahakimu sasa imefika wakati muafaka kutawanywa waondoke kwenye maeneo waliokaa muda mrefu ili waweze kuwatendea raia wetu haki. Kwa sababu wanapokaa muda mrefu unakuta Hakimu ameoa hapo hapo, anakuwa na mkwe, anakuwa na wajomba, mashangazi, mashemeji.

Kwa hiyo, kila anayepelekwa Mahakamani ni ndugu. Kwa hiyo, matokeo yake haki huwa haitendeki na wengine kutokutendewa haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hilo basi sasa niongee kuhusu akinamama wajane na watoto. Kwa kuwa nimeshasema kwamba Wizara imeshapata mtu, sasa ni wakati muafaka akinamama wajane ambao wamehangaika miaka mingi kuhangaikia haki zao na huwa ni taabu kufanikiwa, sasa watafanikiwa kwa sababu Waziri mwenye dhamana ana uchungu sana na akinamama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, akina mama wengi wajane, wanapofiwa na waume zao, ni mara chache sana kutendewa haki katika Mahakama zetu. Inawezekana katika akinamama kumi waliofika Mahakamani kudai haki zao baada ya kufiwa na waume zao anayetendewa haki ni mmoja. Sasa ni wakati muafaka Mheshimiwa Waziri kuhakikisha unawabana Mahakimu wetu ili waweze kuwatendea haki akinamama wetu waweze kupata haki zao ili waweze kumudu maisha yao wakati waume zao wamefariki kwa sababu baada ya waume zao kufariki huwa wanaachiwa majukumu mazito sana ya kulea familia. Watoto wanahitaji nguo, kula, walale mahali pazuri, wanahitaji kusomeshwa, sasa bila kupata haki zao Mahakamani, wao ndugu wa marehemu walio wengi ni waroho wa mali mara nyingi hutumia kila aina ya mbinu kuhakikisha kwamba mali za marehemu, wajane hawapati. Sasa ni wakati muafaka akinamama wajane kupata haki zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya akinamama niongee kuhusu watoto wanaozaliwa nje ya ndoa. Wenzangu wamechangia sana, lakini kwa umuhimu wake na mimi nalazimika nilitamke, watoto wetu hawa hawana hatia, wanazaliwa kutokana na baba na mama kuamua kubeba mimba aidha, kwa kuamua ama kwa bahati mbaya. Sasa wanaponyimwa haki, hatuwatendei haki. Sheria ambayo imepitwa na wakati ni wakati sasa iletwe hapa Bungeni kama ulivyosema Mheshimiwa Waziri ilete haraka sana, ninaamini Bunge hili Tukufu litaipitisha haraka sana. Habari ya kuwapa watoto shilingi 100/= kwa mwezi, haki hiyo imeshapitwa na wakati. Mtoto shilingi 100/= itamsaidia nini. Haimsomeshi, hapati chakula na hapati mavazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli hapo hatuwatendei kabisa haki watoto wetu kwa sababu kuzaliwa kwao kwanza hawakuomba, wamezaliwa kwa sababu ya baba na mama kuamua kuwazaa. Kwa hiyo, sioni sababu ya baba kukwepa wajibu. Nina hakika kama Serikali itakuwa imeifanyia *amendment,* hii sheria akina baba wanaowakimbia watoto watawajibika kikamilifu katika kuwalea watoto hawa ambao wamezaliwa na wanastahili kupata haki kama watoto wengine wenye wazazi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuongea suala la watoto, sasa niongee suala la upungufu wa Mahakimu. Kwa kweli Mahakimu ni wachache. Sielewi kuna sababu gani za msingi Mahakimu kuwa wachache. Ukienda Mkoa wa Singida Mahakama za Mwanzo ni nyingi ajabu kuanzia Iramba, Singida Vijijini, Singida Mjini, Manyoni, Mahakama nyingi za Mwanzo hazina Mahakimu. Utakuta hakimu mmoja wa Mahakama ya Mwanzo anasimamia Mahakama mbili ama tatu. Hivi tunategemea Hakimu kutumikia Mahakama mbili ama tatu atafanya kazi kweli kikamilifu? Ukizingatia Hakimu huyu hata usafiri hana. Hakimu huyo huyo aamue mjini, ana Mahakama nyingine Makyungu, ana Mahakama nyingine Ikungi, niambie Hakimu anavyohangaika katika kutembea, usafiri hana. Nauli hana, mshahara wake ule ule anatumia nauli ya kwenda kuhudumia katika Mahakama zingine ambazo hazina Mahakimu.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Serikali sasa ni wakati muafaka kuhakikisha tunawasomesha vijana wengi wenye elimu zao waweze kushika Mahakama ambazo hazina Mahakimu na siyo Singida tu, hata mikoa yote ya Tanzania, Mahakimu ni wachache katika Mahakama za Mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuongea hilo sasa niongee kuhusu nyumba wanazoishi Mahakimu wetu. Mahakimu wanafanya kazi ambayo inawaweka katika mazingira magumu sana. Kwa sababu wanatoa hukumu, siyo kila mtuhumiwa hukumu anayopewa anaridhika nayo, wapo ambao wanadhani kwamba wameonewa. Sasa tunapowaacha Mahakimu uraiani hatuwatakii mema, tunawahatarishia maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Serikali, Wizara imepata mtu, mpeni Mama Mary Nagu pesa ili aweze kufanya kazi zake kikamilifu, Mahakimu wajengewe nyumba wakae katika hali ya usalama, waondokane na wasiwasi wa kuishi uraiani. Nina hakika wakikaa kwenye nyumba ambazo zimejitenga watatenda haki hawatakuwa na

wasiwasi katika maamuzi ambayo watakuwa wanayatoa katika kuwahukumu watuhumiwa wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuongea hilo, sasa niongee kuhusu akinamama ambao ni Mahakimu. Tunao akinamama wengi sana waliosoma, wenye uwezo wa juu sana. Mahakimu wetu, Wanasheria sasa ni wakati muafaka kwenda sambamba na azma ya Rais kuhakikisha akinamama wasomi kuongezwa kuongeza katika nafasi za juu. Sasa akinamama tuwape *promotion. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapandisheni vyeo, uwezo wanao na wamejitahidi kusoma, kuna kila sababu ya kuwakomboa akinamama, kama Rais wetu ameamua kuwaunga mkono akinamama na sisi tuonekane kwenye nafasi mbalimbali za uongozi naomba na kwenye eneo hili akinamama wapandishwe vyeo, tuongezewe Majaji. Mahakimu Mfawidhi wapatikane Mahakama za Mkoa akinamama wapo na wanaweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niongee kuhusu utaratibu unaotumika katika kuamua kesi kwenye Mahakama zetu za Wilaya na Mkoa. Lugha inayotumika katika kuendesha kesi katika Mahakama zetu za Wilaya na Mkoa ni kiingereza. Hivi ni Watanzania wangapi wanajua lugha ya kiingereza? Watanzania wengi wanapoteza haki zao kwa sababu ya kuchengwa na lugha. Kama kweli tumeki-*promote* Kiswahili sasa ni lugha ya Kimataifa kwa nini tusidumishe Kiswahili sisi wenyewe humu nchini? Naiomba Serikali sasa ni wakati muafaka kukidumisha Kiswahili, Mahakama zetu za Wilaya na Mkoa sasa zitumie Kiswahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria ziandikwe Kiswahili, nina hakika tukifanya hivyo si watuhumiwa, si watu wengi wanaokuwa na kesi Mahakamani watakaotumia Mawakili, watasimama wao wenyewe kwa sababu watakuwa na uwezo wa kujieleza. Naomba sana suala hili litazamwe kwa kina kabisa na ninatumaini Mheshimiwa Waziri, mtani wangu, kwa hili utatoa majibu hapa hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuongea hilo sasa, niongee kuhusu vitendea kazi. Kweli Wizara hii ina tatizo kabisa na suala la vitendea kazi hasa vifaa kwa Mahakimu wetu. Utakuta Mahakama zetu za Wilaya hata Mikoa bado wanatumia mashine za kupiga chapa *(typewriter),* kitu ambacho kimeshapitwa na wakati kabisa, wakati kuna ofisi nyingi, Taasisi nyingi utakuta kompyuta mbili, tatu, ziko kabatini. Wapeleekeni Mahakimu wetu wa Wilaya na Mikoa kompyuta ili wanapoamua kesi zao angalau nakala za hukumu waweze kuzitoa upesi na wahusika wapewe na vifaa vingine vingi wanavyovihitaji wapewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hilo sasa niongee kuhusu mishahara. Mahakimu wanapata mishahara midogo sana. Kweli hatuwatendei haki na tunawashawishi kupokea rushwa kwa sababu ya umaskini. Naomba tutazame mishahara yao kwa kina kabisa. Majukumu waliyokuwa nayo ni mazito. Nimeshasema mwanzo unakuta Hakimu ana Mahakama tatu, anatumia mshahara ule ule hana hela nyingine. Sasa kama mshahara huo huo, nauli, chakula, akiwa kazini, bado nyumbani, kusomesha

watoto, wataiba tu hawa, wakipewa rushwa watakataa wapi, watapokea. Naomba sana sasa Mahakimu wetu watazamwe upya kabisa viwango vyao vya mishahara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongee kuhusu posho za Wazee wa Baraza pamoja semina kwa ajili ya Wazee wa Baraza. Wazee wa Baraza kazi wanayofanya ni nzuri na muhimu sana kuwasaidia Mahakimu wetu. Lakini posho wanazopata ni ndogo. Pamoja na kwamba ni ndogo hata kupatikana kwake ni kwa taabu. Utakuta Mzee wa Baraza anayetumikia miezi mitatu mpaka sita posho yake bado inalimbikizwa tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kwa nini Wazee wa Baraza wasipewe posho zao kwa wakati muafaka? Mbona sisi tunalipwa mshahara wakati muafaka?

Mheshimiwa mwenyekiti, naomba jamani kila binadamu anahitaji haki yake ya msingi apate. Naomba posho hizi sasa zitolewe wakati muafaka na vile vile Wazee wa Baraza elimu hawana. Wapeni semina angalau wawe na upeo angalau mdogo wa kuwasaidia Mahakimu wetu. Wazee wa Baraza wanateuliwa wanapewa kazi hawajui hata waanzie wapi. Wanaenda tu ili mradi wako pale, wapeni semina wazee wa Baraza ili waweze kufanya kazi zao kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongee kuhusu sheria ya kuzuia ukeketaji. Sheria hii naiunga mkono, ni nzuri sana. Kwa sababu mabinti zetu wanaathirika kwa sababu ya ukeketaji. Lakini wanaofanya tendo hili la ukeketaji ni akina bibi kizee, akinamama waliochoka na wengi wao sasa hivi wako magereza. Hivi kumpeleka bibi kizee magereza ni kumfundisha ama kufanyaje?

Naomba sana ili mabibi kizee hao wasiendelee kufika magerezani ama Mahakamani wapeni elimu. Tunaomba fungu kabisa litengwe kwa ajili ya kutoa elimu kwa akinamama wazee wanaoendeleza ama akina baba wanaoendekeza mila hii potofu ya ukeketaji. Kwa sababu bila kutoa mila wataendelea kupelekwa Mahakamani na watakapofika Mahakamani mtu ana miaka 60, 70 unategemea akitoka huko afanyeje? Akitoka huko ni kifo. Sasa tunawafundisha ama tunawaua. Tunaomba elimu itolewe ya kutosha ili waweze kupata haki zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo basi natumaini nimeshaongea ambayo nilikuwa naona ni ya muhimu sana, niunge mkono hoja asilimia mia kwa mia. Mungu awatangulie Waziri wa Katiba na Sheria na wenzake wote waweze kutekeleza azma yao barabara, hongereni sana. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE:**Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na suala la rushwa ambalo Mheshimiwa Waziri aliongelea katika ukurasa wa 37 wa hotuba yake kwa wepesi sana. Tatizo la rushwa katika Mahakama zetu ni kubwa sana kuliko linavyoonyeshwa katika hotuba zetu. Jamii,

kwa kiasi kikubwa sana imepoteza imani ya kupata haki bila kuinunua. Mahakama inashangiliwa kwa kufuta takrima, lakini inashindwa kuondoa takrima katika *administration of justice.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, rushwa haitaondoka Mahakamani kwa kupitia semina au warsha anazoziongelea Mheshimiwa Waziri au kwa hizo Kamati za Maadili. Rushwa itaondoka ikiwa Mahakama zenyewe (kwa maana ya Majaji na Mahakimu) zitakiri kuwa rushwa inatawala sehemu kubwa ya maamuzi yake na wananchi wanajua hilo. Heshima ya Mahakama inapotea kwa kasi. Hivyo njia iliyobaki ni Mahakama kujisafisha zenyewe kabla wananchi hawajachoka na kuamua kuyamaliza mambo wenyewe. Zoezi hili la kujisafisha lianzie Mahakama ya Rufani na kushuka chini na lisitegemee ushahidi wa kiwango cha juu. Tetesi zinazojirudia zinatosha kumpumzisha Jaji au Hakimu kwani *integrity* ya *judiciary* iko kwenye hati hati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefurahia taarifa ya uteuzi zaidi wa Majaji. Lakini ufanisi hautotokana na idadi kubwa peke yake ya Majaji. Upo ulazima na umuhimu kwa kila Jaji wa Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani kuwa na *Research Assistant* wake. Mzigo mkubwa wanaoubeba Majaji wa kusikiliza kesi na kutoa maamuzi ya kufuatwa na Mahakama zingine ni mkubwa mno kuwapa Majaji muda wa ziada na nguvu ya kutosha kwenda maktaba na kufanya utafiti wa kina. Wasaidizi niliowasema, watasaidia sana kuboresha mfumo mzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kuipongeza Serikali kwa uamuzi wa kutenganisha shughuli za mashtaka na zile za upelelezi wa makosa ya jinai. Ikumbukwe kwa shughuli hizo ziliunganishwa huko nyuma kutokana na uhaba wa wataalamu wa kutosha katika fani ya sheria. Leo tatizo hilo hatuna na hivyo hatuna sababu kwenda mwendo wa kinyonga kulikamilisha zoezi hili. Naunga mkono hoja.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie hoja hii kwa kuanza na Mahakama na Majaji ni watu ambao ndio wenye uamuzi kwa mujibu wa sheria kumuamulia mtuhumiwa kufungwa, kusamehewa ama faini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama zetu zimetawaliwa na rushwa hasa Mahakama za Mwanzo. Hii inatokana na kwamba kwanza kesi haziendeshwi kwa mpango unaotakiwa na hatimaye mshtakiwa hulazimika kutoa rushwa ili Jaji amalize kesi na pili, askari ambao ndio wapelelezi wa kesi huchukuwa muda mrefu kukamilisha taarifa za ushahidi na kupelekea mtuhumiwa huyo amebambikizwa tu kesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna Hakimu wa Mahakama za Mwanzo ambaye hapokei rushwa, hivyo nashauri taaluma zaidi itolewe kwa wananchi ili wajue haki zao na wajibu wao na waeleweshwe sheria. Watanzania wamenyimwa haki yao ya kujua hata Katiba ya nchi yao licha sheria nyingine, basi waelimishwe angalau waweze kujikomboa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Majaji wapewe nyenzo zote zitakazowawezesha kufanya kazi katika mazingira mazuri. Majaji wahamie katika maeneo ya Mahakama wanazozitumika ili tuondokane na mtindo wa kwenda kesini

mtuhumiwa na kuambiwa kwamba Hakimu/Jaji leo hayupo amesafiri. Majaji wengi hutumia siku za mwisho wa wiki kuungana na familia zao na hivyo husababisha kuondoka katika mazingira ya kazi. Jaji anaondoka Alhamisi harejei mpaka Jumanne au Jumatano, wakati alishampangia kesi mshtakiwa siku moja kati ya zile ambazo hayupo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utawala Bora na Haki za Binadamu hii ni idara muhimu na nyeti sana. Lakini bado katika nchi yetu kuna vyombo ambavyo vinakiuka huo Utawala Bora na Haki za Binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara hii ikae na vyombo vya ulinzi kwa sababu polisi wanawavunjia sana Watanzania haki zao. Askari huwabambikizia kesi raia na hatimaye kutiwa hatiani. Ama kuwapiga na kuwanyanyasa kabla ya kuwafikisha kwenye chombo husika (Mahakama). Naomba Wizara ijitahidi kusimamia Utawala Bora na kuona kwamba Haki za Binadamu zinalindwa na kuheshimiwa kwa mujibu wa Mkataba wa Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MHE. PHILIP S. MARMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jedwali namba tano, kesi za migogoro ya ardhi siyo sahihi. Yaonekana Manyara hakuna kesi wakati Mbulu pekee yake ina mashauri zaidi ya mia moja katika hatua mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbulu ina tatizo la pekee ambapo Mahakimu (Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo na Wilaya na Polisi) huzichangamkia sana kesi za migogoro ya ardhi. Wiki mbili zilizopita nilitembelea Gereza la Mbulu, idadi ya mahabusu na wafungwa walioko gerezani kutokana na mashauri ya ardhi ni zaidi ya 20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali, Mahakimu wa Mbulu hawaitambui Sheria za Ardhi za mwaka 1999? Hawafahamu kuwa mashauri yote ya ardhi sasa yanashughulikiwa na mabaraza na Mahakama Kuu ya Ardhi? Je, Msajili wa Mahakama Kuu, Arusha ataweza kuchunguza mashauri yote ya ardhi yaliyoko katika Mahakama mbalimbali za Mbulu, kwa hakika hali hii haisababishwi na uvamizi wa kijamii *(criminal trespass)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi siwafahamu Mahakimu walioko Wilayani kwangu ama kwa sura au majina lakini mara zote vyombo vya dola pamoja na wananchi huniletea hali ya utoaji wa haki katika Mahakama zilizopo Wilayani kwetu. Naungana na wananchi wa Tarafa ya Dongobesh kwa sifa nyingi wanazompa Hakimu wa Dongobesh. Rekodi zinaonyesha Mahakama hii haipokei Mashauri ya Ardhi. Kero kubwa iko katika Mahakama ya Mwanzo Dandi na mahabusu na wafungwa niliowataja hapo awali wamefikishwa huko kutokana na Mashauri ya Ardhi hutokea katika Mahakama ya Dandi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo ambalo siyo zuri kuhusu Hakimu wa Dandi kwa vile rekodi zinaonyesha kuwa rufaa kutoka Mahakama yake zikifika Wilayani, Hakimu wa Wilaya mara nyingi hupata kigugumizi kuzishughulikia kuanzia katika hatua za kupata nakala za hukumu hadi upangaji rufaa hizo ili kusikilizwa. Hisia

za wananchi na baadhi ya vyombo vya Serikali ni kwa vile Hakimu wa Dandi na yule wa Wilaya wanatoka eneo moja nchini Tanzania. Naomba suala hili liangaliwe.

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuwa na afya njema na kuniwezesha kuchangia hotuba hii.

Kwanza nampongeza Waziri na Naibu wake na watendaji wote na walioashirikiana wote kwa kuweza kutunga hotuba hii nzuri. Nampongeza Mwenyekiti wa Kamati na wajumbe wote na pia namshukuru Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa hotuba yake nzuri. Namshukuru Waziri Mkuu nakushukuru wewe Spika kwa kuliongoza Bunge hili kwa umahiri na kiwango na *speed*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nachangia kuhusu Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Tume hii ikumbuke kuwa inawajibu wa kufanya upelelezi na kukusanya ushahidi kama Mahakama nyingine kwa kuzingatia sheria.

Leo kuna masikitiko makubwa kwenye kukiukwa haki za binadamu, mtu anakamatwa anawekwa ndani kwa muda hata miaka mitano mpaka zaidi mhusika huyo ndani ni mahabusu tu bado hajapata hukumu eti upelelezi unaendelea, yeye anaendelea kuteseka baadaye anaambiwa sasa anapewa hukumu juu ya kesi yake anapelekwa Chuo cha Mafunzo miaka mitano je, ile aliyokaa mahabusu yote ile haimo kwenye hesabu yake? Je, hiyo ni haki ya binadamu au mhusika huyo baada ya upelelezi kaonekana hana hatia anatolewa gerezani? Ni kwa nini huyo halipwi fidia? Serikali naomba iliangalie suala hili na nijibiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake kwa kweli tunasikitika, mume amenioa na tumezaa watoto na tumekaa kwa maelewano na kupendana lakini Mungu amechukua roho yake amekufa. Sasa hawa ndugu wa mume wanakuja wanakutoa kwenye nyumba na matusi na kukunyanyasa na wewe watoto wako ni wadogo je, wewe uende wapi? Sasa Serikali iangalie sheria upya kwa mwanamke.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuitumia fursa hii kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, Mheshimiwa Mathias Chikawe, Naibu Waziri, Mheshimiwa Johnson Paulo Mwanyika, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Katibu Mkuu, Jaji Mkuu Mheshimiwa Barnabas Samatta na watendaji/watumishi wa Wizara hii walioshiriki kwa hatua na ngazi yoyote katika uandaaji wa hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hotuba nzuri yenye maudhui na nia thabiti ya kuleta maendeleo ya kimapinduzi katika Wizara hii. Ninawapongeza sana na kwa niaba yangu binafsi na kwa niaba ya wapiga kura wangu wa Jimbo la Kwimba, naunga mkono hoja hii.

Pamoja na kuiunga mkono hoja hii lakini napenda kutumia fursa hii kutoa maoni yangu katika maeneo kadhaa ya hotuba hii kama ifuatavyo:-

Kwanza, nawapongeza Wizara kwa hatua mbalimbali inazozifanya kuimarisha uendeshaji wa kesi na kupunguza mrundikano wa kesi Mahakamani. Pamoja na kuwa

mafanikio hayajafikiwa asilimia mia lakini juhudi hizi zinaonesha ni thabiti ya kuondoa dosari hii ambayo ni kero kwa wananchi. Kila pale inapowezekana basi nashauri kasi iongezwe ili mwelekeo huu usije ukawakatisha tamaa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa mpango wake wa ujenzi wa Mahakama. Katika hotuba ya Wizara nimeona Wizara ina mpango wa kujenga majengo ya Mahakama za Wilaya na Tarafa, naipongeza sana. Hata hivyo kutokana na ukweli kuwa fedha iliyotengwa haiwezi kuikamilisha kazi hii kwa mara moja.

Mimi naomba nifahamishwe kwa nini Wizara haikupanga ijenge kwa mara moja majengo ya Mahakama za Mkoa tu kwanza, hatua hiyo ikafuatwa na ujenzi wa Mahakama za Wilaya zote na hatua ya tatu ambayo ingefanywa kwa mwaka wa tatu ikajenga majengo ya Mahakama za Tarafa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mawazo yangu kwanza Wizara ingekuwa imetenda haki sawa kwa Mikoa, Wilaya na Tarafa zote. Kama ungakuwa ni mpango wa miaka mitatu kila ambaye angetakiwa kusubiri angeweza kuvumilia kusubiri ili hatimaye nchi ikawa na Mahakama za aina moja, mchoro mmoja na hadhi sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisikiliza wananchi wengi kama kuna malalamiko yoyote kwa Wizara hii, hayatakuwa sana juu ya sheria na majengo ya Mahakama zetu. Malalamiko mengi yatakuwa juu ya Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo. Mahakimu hawa ndiyo wanaokutana na wananchi siku hadi siku. Tatizo linalowakumba Mahakimu hawa ni tuhuma za rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Wizara hii ipitie tabia na mienendo ya maisha ya Mahakimu hawa! Wizara ilinganishe mapato ya Hakimu kulinganisha na kipindi chake cha kazi. Itakuwaje Hakimu hana shamba, hana biashara nyingine yoyote awe na ng'ombe 30 hadi 100 baada ya kuwa kazini kwa kipindi cha miaka miwili mpaka mitano hivi. Je, mshahara wake utamudu hayo na kuhifadhi familia yake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa kuifanya ofisi hii kuwa wakala. Nashauri kuwa ofisi hii iwe na matawi hadi vizazi na vifo. Nazidi kushauri kuwa iwapo kuwa na ofisi hizo hadi kwenye Kata itakuwa vigumu, nashauri ofisi hii ikasimu uwezo wake wa kusajili vizazi na vifo kwenye vituo vya afya watoto wanakozaliwa na vifo vingi vinakotokea. Taarifa hizi zipelekwe kwenye ofisi hii kwa utaratibu na majumlisho. Naona ni vyema vyeti hivi vitolewe katika zahanati, vituo vya afya na hospitali kwa vile hawa ndio wanashuhudia matumizi hayo wakati yakitokewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nihitimishe mchango wangu kwa kuuliza maswali kadhaa, hivi sasa jengo hili liko Bomani na Jengo la Kizamani na ni la kizamani kwa maana zote. Sehemu ya Mahakama, ni finyu, watumishi wamebanana, Mahakimu hawana nafasi za kufanya kazi kwa uhuru. Sasa hivi kuna mpango wa kujenga jengo la Mahakama ya Wilaya, Hakimu Mfawidhi atajisikiaje? Nashauri ujenzi wa majengo hayo yapate hadhi na kwa Kwimba waanze na Mahakama wa Wilaya.

Mwisho, nashukuru Wizara inanunua magari na kuyapeleka kwenye vituo mbalimbali. Mimi nashauri iwapo kule yanakopelekwa kutakuwa na gari kuu kuu basi Mkuu wa kituo hicho apewe kipaumbele, kulinunua gari hilo, akishindwa basi liweze kupigwa mnada. Serikali yetu haina uwezo wa kutoa motisha kwa watumishi wetu wengi wakiwemo watumishi wa kada hizi. Naomba hii iwe mojawapo ya motisha na hasa kwa watumishi wasiokuwa na tuhuma nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

**MHE. WILSON M. MASILINGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya katika mazingira magumu ya kazi. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa uwasilishaji mzuri sana wa hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kuendelea kuongeza bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria. Hii inadhihirishwa na mtiririko wa bajeti katika jedwali namba moja, 2000/2001 – hadi 2006/2007. Nashauri Serikali iongeze bajeti kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya Wizara na hasa Mahakama kadri mapato ya Serikali yanavyoongezeka. Mahakama na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali vipewe kipaumbele kama afya, elimu, kilimo na ulinzi na usalama. Bila haki hakuna amani. Bila amani, kukuza uchumi na kuondoa umaskini haiwezekani kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kuishukuru Serikali kufuatia uboreshaji wa Mahakama Kuu Kanda ya Bukoba na miradi ya kujenga Mahakama mwaka huu wa fedha. Lakini baada ya kushukuru nakumbushia maombi ya wananchi kujenga Mahakama za Mwanzo Tarafa za Nshamba na Kimwani, kujenga Mahakama ya kisasa ya Wilaya ya Muleba. Aidha, tunakumbushia maombi ya kupewa Hakimu Mkazi Wilaya ya Muleba, kwa sasa anatoka Bukoba na kurudi! Huu ni usumbufu kwa wananchi wa Muleba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Majaji wapya wa Mahakama ya Rufaa na watumishi wengine wote wapya. Naunga mkono tena hoja.

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, Naibu wake pamoja na watendaji wa Wizara ya Katiba na Sheria kwa kutayarisha hotuba nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia katika hotuba hii kwa kujadili mojawapo ya majukumu ya Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania hususan jukumu la kutoa elimu ya sheria kwa jamii, kutoa ushauri na kupendekeza sheria zinazolinda maslahi ya Taifa kama ilivyoainishwa kwenye ukurasa wa nane wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri, mtoa hoja.

Napenda kuishauri Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania ianzishe programu maalum ya kuwaelimisha wananchi juu ya sheria za umiliki wa ardhi Tanzania.

Programu hii ilenge kuwaelimisha wananchi kuhusu taratibu za umilikishwaji wa ardhi. Nalisema hili kwa sababu migogoro ya ardhi iliyopo, mingi imechangiwa na ufahamu mdogo wa wananchi kuhusu mambo ya kuzingatia kabla ya kumilikishwa ardhi. Mambo haya yakieleweka vizuri kwa wananchi yatasaidia sana kupunguza migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo ambayo napendekeza Tume iwaelimishe wananchi ni pamoja na kupata kibali cha maandishi kutoka kwa Afisa wa Ardhi wa eneo husika kabla ya kufanyika mauziano na taratibu zinazofuatwa kubatilishwa umiliki wa hati ya ardhi (kwa sasa taarifa/*notice* ya siku 90).

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo napenda kuchangia ni uanzishwaji wa Wakala wa Serikali *(Registration Insolvency and Trusteeship Agency (RITA)*. Naipongeza sana Serikali kwa kuanzisha wakala huu, nadhani sasa utendaji wa Taasisi hii utaboreka kama inavyotarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizi, naiomba Serikali kupitia Wizara hii sasa ipeleke ofisi au Msajili wa Taasisi hii katika Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema. Kwa muda mrefu sasa Wilaya ya Sengerema imekuwa haina afisa anayeshughulikia masuala ya vizazi, vifo, talaka, ndoa, udhamini na ufilisi. Huduma hii kwa sasa imekuwa ikitolewa kwa msaada na afisa wa Halmashauri ya Geita. Ukosefu wa afisa huyu Sengerema umesababisha kero kubwa sana kwa wananchi wa Wilaya ya Sengerema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, napendekeza Wizara ipitie na ilete Bungeni marekebisho ya sheria zifuatazo ili kuendana na hali halisi na malengo ya Serikali kuhusu kupunguza umaskini Tanzania.

(i) Sheria ya Madini, marekebisho yazingatie maelekezo ya Mheshimiwa Rais kuhusu ulipwaji wa *Corporate Tax* na *Development Agreements* kwa kila palipo na machimbo ya madini.

(ii) Sheria ya Mawasiliano irekebishwe ili kudhibtii wanaoendesha *internet café* waweke *blocking websites* kuzuia picha za ngono. Jambo hili linawezekana kabisa katika dunia hii ya utandawazi hasa kutumia wataalam wa mitandao ya kompyuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa heshima na taadhima nimpongeze kwa dhati kabisa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Rufiji tumeipokea hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwa matumaini makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ya kwanza ni kusifu utendaji kazi wa Wizara hii. Hata hivyo, hapa na pale kunahitajika kutazamwa vema. Watumishi wa

ngazi ya *PCM* wanapata maslahi duni sana ukilinganisha na uzito na unyeti wa kazi zao na mchango wao katika jamii. Ni ukweli ulio wazi kwamba Idara ya Mahakama ndio mhimili mkubwa wa dhana nzima ya Utawala Bora katika nchi yetu. Naomba Wizara hii wafikirie Mahakimu wetu wa *Primary Courts* ili wapate maslahi bora zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ya pili ni kwamba Utete ndio Makao Makuu ya Wilaya ya Rufiji. Katika kutoa huduma za *District Magistrate,* Mahakama ya Utete haina *Resident District Magistrate.* Tuna mmoja tu ambaye vile vile anafanya kazi katika kituo cha Kibiti. Athari zake ni nyingi, lakini iliyo kubwa ni ucheleweshaji wa kesi nyingi sana. Kwa vile kila jambo likiwa adimu basi kuna hatari ya kujipenyeza vitendo vya upendeleo/rushwa, naomba Wizara hii kuwa Mahakama ya Wilaya Utete, Rufiji ipate Hakimu wake wa Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya tatu ni kwamba, naomba Idara ya Mahakama Rufiji ipatiwe usafiri (gari) wa uhakika. Hakimu wa Wilaya ana hadhi kubwa na anatoa hukumu mbalimbali. Huyu Hakimu kama anaonekana anatangatanga kutafuta usafiri, basi anaweza akapatwa na matatizo ya kijamii au kisasi kwa wale waliowahukumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nazidi kuwapongeza na naunga mkono hoja mkono kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na ofisi yake yote kwa kazi nzuri wanayofanya katika mazingira duni na magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachangia machache kama ifuatavyo:-

Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 20 ameeleza sera ya Mahakama. Katika kipengele (c), amezungumzia kuwa na jengo la Mahakama ya Wilaya katika Wilaya na (d) ujenzi wa Mahakama ya Mwanzo katika Tarafa zote.

Aidha, katika ukurasa wa 79 Mheshimiwa Waziri ameorodhesha Wilaya ambazo hazina majengo ya Wilaya, mojawapo ikiwa Kilindi. Sasa ningependa katika majibu yake jioni nielezwe kama Kilindi iko kwenye mpango kulingana na sera hasa ukizingatia Wilaya inaelekea umri wa miaka minne na wananchi wanalazimika kusafiri kilometa 90 kwenda Handeni ambapo siyo tu ni usumbufu, bali gharama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 20 umezungumzia Mabaraza ya Kata kuwa kiungo muhimu kufikisha huduma ya haki vijijini. Je, amewawezesha kitaaluma au wana uwezo huo? Serikali inafanya jitihada gani kusaidia hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile Hakimu wa Wilaya anatoka Handeni, suala la kumfuata na kazi kuwa nyingi ni gharama sana, hivyo kesi huahirishwa kwa kukosa usafiri wa kumleta Hakimu huyo. Pia kwa sababu eneo la Kilindi ni kubwa kijiografia, ni muhimu na Kilindi ikapewa gari la kutumiwa na Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo, ukurasa wa 24 wahusika. Naomba katika majibu nipate maelezo endapo katika hayo magari 31 yaliyoagizwa kama Kilindi tutapewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba pia tupatiwe watumishi. Sisi wananchi kama tulivyoonyesha nia yetu ya kuimarisha Mahakama, tumefyatua matofali na eneo la Mahakama limetengwa. Aidha, pia katika Tarafa tumekusudia kuchangia nguvu zetu kuimarisha na kuhakikisha Mahakama za Mwanzo zinakuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aAidha, Mheshimiwa Waziri akizingatia barua niliyomuandikia mimi binafsi mwezi Aprili, 2006 nikimweleza na kumwomba hayo yote hapo juu, naomba katika majibu atupe tamko lake, kwani tayari tumekwishapata mchoro wa jengo la Wilaya kutoka Tanga. Wananchi wawe na imani kuwa nguvu zao haziendi bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kwa uwezo mkubwa Mheshimiwa Waziri atatoa majibu muafaka. Ahsante.

**MHE. DAMAS P. NAKEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimpongeze Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, kwa hotuba yake nzuri.

Pamoja na hotuba nzuri ya Mheshimiwa Waziri, napenda kuchangia katika kuboresha hoja nzima kwa manufaa ya wananchi na jamii kwa ujumla. Kuna msemo wa kiingereza unasema *justice delayed is justice denied* yani haki ya mtu inapocheleweshwa ndiyo kunyimwa kwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii sasa imezoeleka katika nchi yetu kutokana na uhaba au uchache wa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo. Naomba Serikali itafute kila njia kupatikana kwa Mahakimu kama inavyofanya kwa walimu na madaktari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo langu la Babati Vijijini, kwa muda mrefu kumekuwa na upungufu wa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo. Mahakama hizo ni Bashanet, Ufana na Dareda. Wananchi wa maeneo hayo husafiri masafa marefu, kilometa kati ya 35 na 70. Naomba sana Serikali ituletee Mahakimu kwenye Mahakama hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aya ya 73 kifungu (f) ya hotuba ya Waziri inaelezea azma ya Serikali kujenga Mahakama kila Tarafa. Naomba katika mwaka huu wa fedha Tarafa ya Dareda iwepo katika mpango huo. Mpango huu pia uhusishe ukarabati wa Mahakama za Bashanet na Ufana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Waziri wa Katiba na Sheria kwa asilimia mia moja.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake pamoja na watendaji wao wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, askari wengi wamalizapo kazi hupata usumbufu wa kupata ajira. Nashauri Wizara ije na sheria ya kuanzishwa upelelezi na uendeshaji binafsi ili askari wetu waliostaafu waweze kupata ajira ya uhakika. Aidha, itahimiza na

kusukuma mwenendo wa mashtaka kwa vile wananchi wenye uwezo wao watatumia vyombo hivyo kama vile vikosi vya ulinzi vya binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba wakati wa majumuisho Mheshimiwa Waziri alielezee Bunge hili juu ya msimamo wa Serikali katika kuanzisha Mahakama ya Kadhi ambayo Serikali ilianza kuifanya kazi hiyo. Ieleweke kuwa Mahakama ya Kadhi ipo katika sehemu ya Jamhuri (Zanzibar). (Baba yangu alikuwa mmoja wa Makadhi wakati wa 1964 hadi 1988 alipofariki). Kenya, Uganda na Msumbiji zipo Mahakama za Kadhi, tatizo ni nini? Naomba maelezo ya kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali ije na programu ya Miswada ambayo itawasilishwa Bungeni ili Bunge liweze kuwa na ratiba inayoeleweka kwa kupanga ratiba ya shughuli zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na kumtakia kila la kheri Mheshimiwa Waziri katika kutekeleza majukumu yake.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia kwa maandishi hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Waziri wa Katiba na Sheria, Naibu Waziri, watendaji wa Wizara pamoja na washiriki wote kwa kuandaa hotuba nzuri, yenye mpangilio mzuri, yenye kueleweka na inayoonyesha utekelezaji wa majukumu na mipango ya baadaye.

Aidha, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria kwa kazi zake nzuri alizotangulia kufanya katika Wizara nyingine na kazi ambazo anaendelea kuzifanya katika Wizara hii mpya aliyokabidhiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa mapendekezo yangu kuhusu haki ya wajane na watoto yatima. Aidha, naiomba Wizara iangalie upya suala la mirathi kwa wajane. Katika shughuli zangu mkoani Mtwara, nimekuwa nikijihusisha na kuboresha hali za watoto walioko katika mazingira magumu. Mojawapo ya vyanzo vinavyosababisha hali ya mazingira magumu ni hali ya unyanyasaji wa wajane mara tu baada ya kuachwa na waume zao. Unyanyasaji huu ni pamoja na kunyang'anywa nyumba pamoja na mali nyingine za familia ya marehemu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na tatizo hili, mke wa marehemu pamoja na watoto hulazimika kuhama na kwenda kupanga chumba mitaani na kuanza maisha mapya ya kufanya biashara ndogo ndogo kwa ajili ya kujikimu. Kwa kuwa haya ni maisha mapya kabisa, hali huendelea kuwa ngumu ikiwa ni pamoja na watoto kukosa huduma za elimu (sare za shule, ada na hata mali ya kumpeleka mtoto shule pamoja na vifaa vya darasani kama vitabu na madaftari).

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilifuatilia sababu za mjane kunyang'anywa nyumba ikaonekana kuwa chanzo ni pale ambapo marehemu katika kipindi cha uhai wake

alikuwa ameandikisha jina la mtoto wake wa kiume kama ndiye mmiliki wa mali zake hasa nyumba na kumbe jina la mtoto huyu hufanana na la babu yake (baba wa marehemu). Wakati mwingine marehemu kipindi cha uhai wake aliandika jina la baba yake katika hati ya nyumba na kiwanja. Hivyo ndugu wa marehemu hung'ang'ania kuwa nyumba ni ya ukoo na kwa sababu hii Mahakama huamua kesi kwa kufuata kilichoandikwa katika hati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kutoa pendekezo la kuanzishwa kwa Kamati za Haki za Binadamu kwa ngazi zote katika Taifa letu. Aidha, naomba Wizara ilizingatie sana wazo hilo na kuanza utaratibu huu mapema ili kuharakisha utendaji haki miongoni mwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kuwa Kamati hizi zitakapoanzishwa zitatumika na Mahakama kutafuta ukweli, basi tatizo la kukosekana ushahidi litapungua au kutoweka kabisa na haki itatendeka ipasavyo si tu katika mirathi, bali hata katika matatizo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ikumbukwe kuwa mume anapoandikisha nyumba ya familia yake kwa jina la baba yake mzazi ni ukiukwaji wa haki za binadamu. Kwa sababu hiyo, imekuwa ikitokea migogoro kwa wanandoa juu ya tatizo hili. Kwa kuwa mara nyingi wanawake ni wanyenyekevu na kwa kuamini kuwa hakuna unyanyasaji wowote unaoweza kutokea siku za baadaye, basi wanawake huamua kuepusha ugomvi kwa kukaa kimya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishauri Wizara itafute utaratibu mzuri wa kuhakikisha kuwa wajane na watoto wao wanatendewa haki ili kupunguza tatizo la umaskini usiokuwa wa lazima.

Aidha, naiomba Wizara ifanye jitihada za kuielimisha jamii juu ya suala hili, hasa akina baba juu ya matatizo ya ukiukaji wa haki na akinamama juu ya haki ya familia zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, sheria inayomlinda mtoto nje ya ndoa naomba tuige sheria ya Marekani kwamba mtoto atakayezaliwa nje ya ndoa wazazi wote wawili wamtunze mtoto huyo. Inapotokea mtoto akakataliwa na mzazi mmoja, mzazi huyo sheria imlazimishe kumtunza wala asisingizie dini. Dini hairuhusu, mtoto ametokea, basi sheria imruhusu/ imlazimishe kumlea na sheria ya malezi itegemee sana kipato cha mzazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo, napendekeza elimu ya Mahakimu ipandishwe kusiwe na Mahakimu wenye *Certificate.* Kwa nini, kwa sababu ngazi hii kuna uonevu wa hali ya juu, hawajali hata *ethics* za utaalamu

wao. Sheria nyingi hasa zenye mabadiliko hawazijui. Haiwezekani kesi inatajwa, inasikilizwa, mshitakiwa anaarifiwa mapema kuleta mashahidi, mtuhumiwa hasa anayepakaziwa kesi anajikuta yuko Mahakamani, kesi inatajwa, inasikilizwa kwa kutumia mashahidi wa mlalamikaji na baada ya siku moja hukumu inatolewa. Mahakimu hawa ndiyo wala rushwa wakubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba wale wote wenye *Certificate* wapelekwe masomoni na wasiendelee na kazi mpaka wapate *Diploma, Advanced Diploma* na *Degree.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge linadhibitiwa na wananchi, maamuzi ya matokeo ya uchaguzi wanadhibitiwa na vyama vyao, na Bungeni, Mbunge pia anadhibitiwa na Kamati ya Bunge inayoshughulikia nidhamu za Wabunge, Serikali inadhibitiwa na wananchi. Wakati wa uchaguzi, Bunge kama wajibu wa Bunge kusimamia na kushauri. Pia Serikali iliyoko madarakani inadhibitiwa na chama chake, lakini tukiitazama Mahakama inadhibitiwa na chombo kilichowekwa katika Idara ya Mahakama. Utaratibu huu si mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chombo cha kudhibiti utendaji wa Mahakama kinawahusu wataalam wa Mahakama, wanaweza kulindana. Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora hawana uwezo wa kuingilia hukumu iliyotolewa na Hakimu. Hakuna chombo kingine kinachowekwa kufuatilia mwenendo wa wafanyakazi wa Mahakama. Uhuru mkubwa waliopewa Idara ya Mahakama umesababisha watu wasiwe na sehemu ya kupeleka malalamiko yao ukiacha utaratibu wa Rufaa. Mahakama imefanya wananchi wawe na manung'uniko na Mahakama. Naomba kiundwe chombo nje ya utaratibu wa Mahakama cha kufuatilia shughuli za Mahakama.

**MHE. FELIX N. KIJIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia hotuba ya Wizara ya Katiba na Sheria katika vipengele vifuatavyo:-

Moja, uchache wa Mahakimu kwenye Mahakama kunachangia kwa kiasi kikubwa kuwapo kwa mrundikano wa kesi na pamoja na msongamano wa mahahusu kwenye magereza na vituo vya polisi. Kutokana na hali hii, majengo ya Mahakama ambayo yalikuwa yakitumika kuendesha kesi ama kutolea hukumu, majengo hayo yamebaki bila kutumika hadi sasa. Kutokana na sababu hii inabidi kuwasafirisha watuhumiwa hadi kwenye Mahakama kama ya Wilaya. Tatizo linaloathiri zoezi hili ni uhaba wa magari ya polisi yanayotakiwa kuwasafirisha hayapo.

Pili, adhabu kwa wanaojihusisha na dawa za kulevya. Sasa hivi kumeongezeka kwa wimbi la vikundi vya vijana wanaojihusisha na dawa za kulevya. Madhara yake ni kwa Watanzania kuwa na vikundi vinavyofanya uhalifu mbalimbali baada ya kutumia dawa hizo. Hata hivyo, vijana wanaojihusisha na biashara hiyo wanapokamatwa kwenye viwanja vya ndege kila wanaporudi kutoka nje ama kutoka nje ya nchi, hawachukuliwi hatua yoyote baada ya kuwabana na kuhakikisha dawa hizo zinatoka kwa ajili hiyo ya kutokuwepo kwa adhabu ya kuwabana hata kama

ushahidi upo kumechangia kwa kiasi kikubwa kuongezeka kwa biashara hii haramu, je, Wizara imejipanga vipi kuhusu kutunga sheria ya kuwabana hao wanaofanya biashara haramu?

Tatu, ni kuhusu ujenzi wa nyumba za Mahakama. Maeneo yaliyo mengi hapa nchini yamekumbwa na tatizo la kutokuwa na Mahakama pamoja na nyumba za kuishi watumishi wa Mahakama. Hii imekuwa ni changamoto kubwa kwa Mahakimu kutokuripoti kwenye vituo vya kazi na kuacha maeneo yakiwa hayana Mahakimu, je, Serikali/Wizara imejipanga vipi kuhusu hali hii katika bajeti ya mwaka 2006/2007?

**MHE. STEPHEN J. GALINOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara hii kwa hotuba nzuri na pia kwa utendaji mzuri japo katika mazingira mapya na magumu. Hatua inazokusudia kuchukua, mkizitekeleza, nina uhakika mwakani kutakuwa na matatizo machache. Nawatakia kila la kheri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo napenda kuzungumzia kwa kifupi juu ya mambo mawili.

Moja, nimeona kwamba ukarabati wa Mahakama ya Tarafa umeachwa kabisa Tarafa zangu tatu za Kalenga, Maboga na Mlolo. Tarafa zote tatu zina Mahakama zilizojengwa na wakoloni na yako katika hali mbaya, afadhali kidogo Mlolo na Maboga au Kifimzelo. Lakini Kalenga inatisha na ndiyo Makao Makuu siyo tu ya Tarafa, bali Jimbo na kitovu cha Uhehe. Jengo liko pamoja na makumbusho yanayotembelewa na watalii ambao utashangaa kuliona jengo hilo la Mahakama likiwa kama gofu. Naomba angalau jengo la Kalenga likarabatiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, *adoption/*uasili kifungu 92 cha hotuba kama tujuavyo UKIMWI ni kiwanda cha kuzalisha yatima kwa kasi ya kutisha. Sambamba na hatua za kukabiliana na balaa hili, nashauri sheria yetu kuhusu *adoption* ilegezwe ili watoto wengi ambao ni yatima waweze kuwa *adopted* kwa wingi zaidi kuliko ilivyo hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naunga mkono hoja hii na nawatakia bajeti yao ipitishwe sina migogoro.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Waziri mwenye dhamana ya Katiba na Sheria, Mheshimia Dr. Mary Nagu, Naibu Waziri Mheshimiwa Mathias Chikawe na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri ya kuandaa bajeti ya mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninao mchango kama ifuatavyo, matatizo ya Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo husababisha watu wengi kukosa haki zao na pengine hata uvunjaji wa sheria za nchi huko vijijini, mfano, Jimbo langu la uchaguzi la Iramba Magharibi, Mahakama za Kaselya, Urughu, Kisiriri, Ntwike hazina Mahakimu wala hazina watumishi wa kutunza mazingira za Mahakama hawajaajiriwa hivyo hufanya kazi kama vibarua, ni jambo la hatari kwani Mahakama hutunza majalada

muhimu, zana zinazohusiana na mwenendo wa kesi, hivyo kwa bajeti ya mwaka huu naomba Mahakama hizo nilizozitaja zipatiwe Mahakimu ikiwa pamoja na ajira kwa wahudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, vitendea kazi vitolewa kwa Mahakimu hasa kwa kuwapatia pikipiki na kadhalika ili Mahakimu hawa wafanye kazi kwa mazingira yanayowafanya wajisikie wapo salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, Mahakimu na makarani wala rushwa wadhibitiwe ipasavyo ili kuiletea heshima Idara ya Mahakama ambao ni mhimili mojawapo katika kuongoza nchi na nne, mrundikano wa kesi Mahakamani utafutiwe ufumbuzi ni kwa nini kesi zimerundikana, Mahakimu watoro wabainishwe na ikiwezekana wachukuliwe hatua kali ikiwa ni pamoja na kuwafukuza kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, Wilaya ya Iramba tuongezewe Mahakimu watatu wa Mahakama za Wilaya ili tuwe na idadi ya Mahakimu wanne pamoja na huyu mmoja tuliye naye, kuongezeka kwa idadi kutaleta tija katika kufanya kazi hasa kwa chombo hiki muhimu cha sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sita ni kuhusu Katiba, wale wavunjaji wa Katiba ya nchi wadhibitiwe na sheria hasa wale wanaotumia Vyama vya Siasa, kitumiwe kipengele ndani ya Katiba kinachowadhibiti watu wa aina hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DR. LUKA J. SIYAME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kutoa shukrani zangu za pekee kwa Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria kwa umahiri wake mkubwa katika kuwasilisha hotuba yake ya Makadirio ya Fedha za Matumizi ya Wizara yake kwa mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia nimpongeza kipekee Naibu Waziri wa Katiba wa Sheria, Mheshimiwa Mathias Chikawe, kwa juhudi zake kubwa katika utekelezaji wa kazi zake na hivyo kuleta ufanisi mkubwa katika Wizara yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza pia Katibu Mkuu na watendaji wakuu wa Wizara ya Katiba na Sheria kwa kazi yao nzuri na hasa katika kukamilisha hotuba iliyofikishwa mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla kuendelea na maelezo yangu mengine naomba kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Mbozi Magharibi lina Tarafa tatu zenye Makao yake Makuu katika vijiji vya Kamsamba, Msangano na Ndalambo. Tokea enzi za ukoloni hadi miaka ya 1980 kulikuwa na Mahakama za Mwanzo na Mahakimu wa Mahakama hizo katika Tarafa zote tatu, kutokana na umbali kutoka Mji wa Vwawa ambayo ni Makao Makuu ya Wilaya ya Mbozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu zisizoeleweka, Mahakimu wakati wa miaka ya 1980 waliondolewa kwenya Mahakama zote tatu na kibaya zaidi Mahakama ya Mwanzo ya Tarafa ya Msangano nayo ilivunjwa, hivyo Tarafa hiyo kubakia bila huduma zozote za Mahakama hadi leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa Mahakimu kutoka Vwawa hutembelea Mahakama za Mwanzo za Kamsamba umbali wa kilometa zaidi ya 120 na Ndalambo umbali wa zaidi ya kilometa 80 kutoka Vwawa mara mbili au tatu tu kwa mwaka na wananchi wa Tarafa ya Msangano umbali wa kama kati ya kilometa 60 na umbali kilometa 120 kutoka Vwawa hulazimika kwenda kufungua kesi zao Vwawa pamoja na kwamba sehemu hii ina miundombinu ya barabara mibaya sana na hakuna usafiri wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Msangano walikuwa wanafyatua matofali kwa ajili ya ujenzi wa jengo jipya la Mahakama ya Mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi ya wananchi wa Jimbo la Mbozi Magharibi, moja, kupatiwa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo kwenye Tarafa za Kamsamba, Msangano na Ndalambo na pili, kuidhinisha ujenzi mpya wa Mahakama ya Mwanzo katika Tarafa ya Msangano kwani wananchi wako tayari kwa kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, narudia tena kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. MKIWA ADAM KIMWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia hotuba ya Wizara hii, kwanza napenda kuchangia eneo la Mahakama. Mahakama za Mwanzo kuna matatizo sana, kwanza vitendea kazi hawana hasa karatasi kwa ajili ya kuandikia mwenendo wa kesi. Kama huna pesa ya karatasi kesi yako itakuwa ngumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wasaidizi wa Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo yaani Wazee wa Baraza. Wazee hawa ni tatizo sana, hata kama Hakimu ameamua uamuzi sahihi, lakini wazee hawa wakipinga basi Hakimu hana nguvu tena.

Mheshimiwa Waziri naomba hili liangaliwe upya na Hakimu aweze kupata nguvu ya hukumu, kwani wazee hawa kwanza huwa wamechoka kimaisha, hivyo kwa hongo ndogo tu wanaweza kubadilisha hukumu ambayo ingekuwa sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mahakama nyingi za nyumba baadhi yake hakuna uhalali wa baadhi ya kesi katika Mahakama moja ya nyumba ambayo iko katika Jiji la Mwanza, kuna baadhi ya kesi ambazo hazisikilizwi na hutolewa maamuzi tu. Mfano kulikuwa na kesi moja ya ndoa na ikawa katika Mahakama ya Wilaya, lakini ikatoka hukumu Mahakama ya Nyumba ya kumhamisha mke eti ni mpangaji, anatuma Mahakama ya Wilaya ikaziwe hukumu. Kesi haikusikilizwa, mke hakuitwa kueleza, ile hukumu inatolewa, uhalali uko wapi, Mahakama hii ni hatari sana. Kwanza hata haki au sheria haiko hivyo. Huyu ni ambaye anatambuliwa. Je, ambaye hajatambuliwa hali za Mahakama za nyumba sio nzuri baadhi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia makarani wengi wa Mahakama za Wilaya siyo waadilifu na mara unapotaka kufungua kesi usumbufu huwa mwingi sana. Ukitaka nakala ya hukumu ndiyo basi, unaweza kusota hata mwezi mzima bila kupata nakala hiyo, hatimaye watu ambao wanataka kuomba Rufaa hukata tamaa kabisa. Mheshimiwa Waziri naomba makarani hawa na utaratibu wa kazi zao watekeleze majukumu yao kupitia sauti ya Wizara.

Kuhusu sheria za mitaa, katika mitaa au vitongoji kuna ma-*WEO* na ma-*VEO,* watu hawa ni watu ambao wengine huwa wanataka kuwa miungu watu. Kama kuna sheria ya watu hawa, naomba iboreshwe kwani watu hawa wamekuwa ni matatizo matupu kwani huko vijijini watu hawa hutumia nguvu zao na sio sheria kufikia kuchukua hata mali za wanavijiji eti kufanya faini. Hivi kweli kuna faini kwa *WEO* na anaruhusiwa kutoza fani ya kiwango gani? Naomba kupata maelezo kwa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sheria ya ardhi. Hapa ndipo pagumu sana na wananchi wengi hawajui sheria hii, hata mimi sielewi vizuri. Mfano mtu ana shamba lake zaidi ya miaka 40, lakini wanapokuja watu ambao wanapima viwanja huchukua kupima shamba lote na huenda likatoa viwanja nane au kumi, lakini mwenye shamba hupewa kiwanja kimoja na analipwa shilingi 300,000/=. Halafu kiwanja hicho hicho anauziwa shilingi 360,000. Hapo amelipwa au amedhulumiwa maana viwanja saba vimechukuliwa na kimoja kauziwa mwenye shamba. Kama kalipwa shilingi 300,000 halafu unamtoza shilingi 360,000. Hapa sheria ya ardhi inasemaje? Naomba jibu la uhakika, ili wananchi wanaotendewa hayo wasikie haki yao iko wapi. Hii ni hatari kwa wananchi kutoelezwa sheria ya ardhi ili waijue ili kuepusha dhuluma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kumpongeza Waziri wa Katiba na Sheria pamoja na Naibu Waziri wake kwa hotuba yao nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kama ifuatavyo, mgawanyo wa kazi za mahakama kati ya Mahakimu na makarani pamoja na watumishi wa Mahakama. Kwa nini Mahakimu walio wengi hutegea kufika Mahakamani na kufika kwa muda wanaotaka na wanapofika wanaendelea kuahirisha kesi hata ambazo zinastahili kuzungumzwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni nani anawawajibisha hawa Mahakimu na kuwafuatilia kama wanatimiza siku yake kwa kufanya kazi kwa saa zinazotakiwa? Je, ni wangapi wamepatikana na kosa la kutokutimiza masharti yake ya kufanya kazi kwa saa anazopatia mshahara? Wamewajibishwaje au wamechukuliwa hatua gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini kesi nyingi huchukua muda mrefu? Je, ni nani anafuatilia mlolongo wa kesi zote ambazo zimetoka muda mrefu. Kwa nini kesi huamishwa hamishwa mara hakimu huyu au yule? Je, ni hatua gani zinachukuliwa dhidi ya usumbufu wa aina hiyo kwa wahusika wote?

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuzungumzia juu ya rushwa. Rushwa hudhulumu haki ya mtu na Mahakama zetu zimekithiri kwa rushwa hiyo kupelekea haki kutokutendeka. Je, Wizara inamkakati gani juu ya rushwa Mahakamani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria inasema nini juu ya wanandoa wanaoachana na hali wakiwa na watoto chini ya umri wa miaka saba? Je, kuhusu mgao wa mali, sheria inasemaje Na hukumu ya talaka inapotokea mali zinatakiwa zigawanywe kwa muda gani na je, endapo kesi hiyo ikachukua muda mrefu na hatimaye watoto walio chini ya miaka saba wakaendelea kuwepo upande mmoja, je, Wizara (sheria) inasemaje, juu yao, je, si kuwanyima haki yao ya msingi kama binadamu, je, haki au sheria inasemaje juu ya haki ya watoto?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafadhali sana naomba majibu ili nipate kuelewa. Naomba kuwasilisha.

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote katika Wizara hii hasa ukizingatia kuwa Wizara inaongozwa na mama, anaonyesha jinsi gani alivyo na uwezo wa kusimamia na kuamua mambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ni nzuri, naamini kama Mungu akijalia hali za wataalamu na wananchi wetu zitaboreka. Napenda kuchangia mambo kadhaa katika hotuba hii, mchango wangu napenda ujikite katika vipengele vifuatazo vikienda sambamba na Jimbo/Wilaya ya Bukombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukosefu wa mahakama, naomba Serikali itujengee Mahakama kwani hata kiwanja tayari kipo, Serikali tunaiomba ichukue umuhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Hakimu Mfawidhi wa Wilaya, Bukombe tumekuwa tunasumbuka mno kwani kesi zote za Kiwilaya hulazimika kwenda Kahama na hali hii inasababisha msongamano wa kesi kwa sababu anahudumia Wilaya mbili zenye wakazi zaidi ya milioni moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *labour office* naomba Serikali ifanye kila linalowezekana ili *labour office* tupate Bukombe. Hii itapunguza gharama *unnecessary cost* za kwenda na kurudi Kahama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kesi kuchukua muda mrefu, naiomba Serikali irekebishe utaratibu ili kesi ziwahishwe. Pamekuwepo na ucheleweshaji wa kesi pengine kwa sababu zao binafsi. Pia ubambikizaji wa kesi za mauaji nao unatesa sana wananchi wetu. Naiomba Serikali ilifuatilie hili kwa makini hata Wilaya ya Bukombe unaofanywa na askari polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo wanakaa kituo kimoja kwa muda mrefu sana, hivi watafanyaje kazi? Mfano wapo Mahakimu ndani ya Jimbo/Wilaya yangu tangu miaka ya 1993 hadi leo kituo kimoja. Naomba Mheshimiwa Waziri alifuatilie kwangu nao wabadilishwe vituo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazee wa mahakama, naomba Serikali iniambie mpango/mkakati iliyonaYo kuhusiana na wazee hawa. Katika Mahakama ya Runzewe, Ushirombo, Masumbwe na Mbugwe Wilayani Bukombe wamenilalamikimia hawalipwi hela zao.

Je, Serikali inafahamu hili na kama inafahamu mbona imekaa kimya? Waishi vipi kwa njia ya rushwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwandishi mmoja alisema nanukuu: *"God does not give success, he gives ideas. Ideas when well investeda can alter the destury of a nation,"* mwisho wa kunukuu. Serikali kama itafuatilia mawazo na michango ya Waheshimiwa Wabunge naamini tutajenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba Serikali ifuatilie kwa makini matatizo ya Bukombe niliyoainisha hapo juu pamoja na kesi ambazo zimekaa muda mrefu bila majawabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, Mungu mbariki Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote. *Amin.*

**MHE. HEMED MOHAMED HEMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema nimwombe Mwenyenzi Mungu aniwezeshe kutoa mchango wangu katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea naomba kumpongeza Waziri wa Katiba na Sheria Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, pamoja na wasaidizi wake kwa hotuba yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanza naomba nianze katika maeneo ya Mahakama, mzigo mkubwa katika Wizara hii uko katika Mahakama. Katika Mahakama zetu nchini tukubali kuna uhaba mkubwa wa Mahakimu na Majaji jambo ambalo hupelekea mrundikanao wa kesi Mahakamani. Matokeo haya hutoa shida kubwa kwa Mahakimu na Majaji husababisha mrundikano wa mahabusu na wafungwa wanaosubiri kesi zao kusikilizwa na kupata maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo hili ndilo linalosababisha mrundikano wa mahabusu magerezani, kuwakusanya watuhumiwa pamoja na wahukumiwa kinyume cha utaratibu ni kwenda kinyume na haki za binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaeleweka Serikali iko mbioni kutatua tatizo hili ambalo linapelekea kuwa sugu. Pamoja na kazi za Wizara naomba kujua utaratibu uliopo ndani ya chombo cha sheria juu ya ndoa zetu. Nchi yetu huozeshana kimila na kidini. Kwa upande wa kidini kuna utofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili pia kuna hukumu za kidini pale ambapo ndoa imevunjika ama mmoja wapo amefariki dunia. Ni utaratibu gani Wizara inatoa haki

za wenye kuachana kindoa ama aliyefiwa kimali wakati kesi ikija Mahakamani. Namwomba Waziri anipatie jibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utawala bora na haki za binadamu ushirikishwaji na uwakilishi, dhana ya kushiriki kikamilifu kama msingi wa utawala bora imepewa nguvu Kikatiba ambapo inalindwa kama haki ya msingi ya binadamu. Katiba ya nchi inatamka kuwa kila raia anayo haki na uhuru wa kushiriki kwa ukamilifu katika kufikia uamuzi juu ya mambo yanayomhusu yeye, maisha yake au yanayolihusu Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo wasiwasi mkubwa katika nchi yetu hasa pale Serikali inapopanga idadi ya walemavu katika Bunge letu Tukufu mlemavu ni mtu kama mtu mwingine katika jamii. Kumpangia ni kuashiria kumnyima haki yake ya kimsingi. Watanzania tumewafanya walemavu na wakongwe kuwa si watu wa kawaida. Walemavu wanadiriki kupewa majina yasiyo yao, wakongwe huuliwa bure kimila. Vipi Serikali linalipa uzito suala hili. Ni vyema basi sasa Wizara iwapangie sheria wenzetu hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni vyema Serikali iwapatie vitendea kazi wahusika Mahakamani.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kusema naunga mkono hoja, hata hivyo pamoja na kuunga mkono hoja hii ambayo imetayarishwa kiumakini mkubwa nina mambo machache ambayo yanapaswa kuangaliwa kwa makini.

Tatizo la uchache wa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo. Wilaya ya Kahama ni miongoni mwa Wilaya zenye eneo kubwa la kiutawala. Wilaya hii ina tatizo kubwa la uhaba wa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo jambo ambalo huwafanya wale waliopo kufanyakazi katika mazingira magumu. Maeneo wanayohudumia ni makubwa lakini vitendea kazi (usafiri) hawana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii imesababisha kuwapo kwa tatizo kubwa la rushwa, Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo wanalalamikiwa kwa rushwa, sambamba na shutuma hizo (rushwa) Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo sasa wamefumua mtindo mpya wa kutoa hati za kupekua watu ambazo wamekuwa wakizitoa kwa watu binafsi au mgambo kufanya kazi ya upekuzi. Katika mazingira hayo yamejitokeza malalamiko mengi wananchi wa Kahama hususan wafugaji wanaporwa mali zao (fedha na mifugo) chini ya utaratibu huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la mrundikano wa kesi, Wilaya ya Kahama ina tatizo kubwa la mrundikanao wa kesi hii inatokana na mambo mawili.

(i) Kesi nyingi kuwa za kubambikiza na polisi kushindwa kuleta ushahidi.

(ii) Hakimu wa Wilaya ya Kahama, huyu amehudumia Wilaya mbili za Kahama na Bukombe. Naiomba Serikali isaidie kutatua tatizo hili kwa kujenga Mahakama ya Wilaya ya Bukombe. Hii itaondoa pia tatizo la msongamano wa mahabusu na wafungwa

katika Gereza la Kahama lenye uwezo wa kuchukua watuhumiwa 70 lakini sasa lina mahabusu/wafugwa 600.

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi ya kutoa mchango wangu kwa njia ya ushauri kwa hoja hii katika msuala yafuatayo:-

(i) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Waziri wa Katiba na Sheria kwa hotuba nzuri.

(ii) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Mikumi na nadhani jambo hili limelalamikiwa kwa kipindi kirefu nchi nzima ni kwamba Serikali ichukue hatua madhubuti za kusimamia malipo kwa wakati ya washauri wa Baraza katika Mahakama za Mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, washauri wengi kwa kutolipwa poshi zoa kwa wakati wamelazimika kutotenda haki katika ushauri wao kutokana na kufanya upendeleo kwa mshtaki au mshtakiwa aliyetoa chochote rushwa, kwa baadhi ya washauri wa Mahakama za Mwanzo. Malimbikizo ya malipo ya washauri wa Mahakama katika Kata za Kidodi na Mikumi yanafikia hadi zaidi ya mwaka mmoja.

(iii) Mheshimiwa Mwenyekiti,kukua kwa miradi ya MKUKUTA, MKURABITA na mengine itakua kuanzishwa kwa Benki nyingi ndogo ndogo *(SACCOS)* katika kata mbalimbali nchini. Kutokana na kuongezeka kwa vitendo vya ujambazi wa kutumia silaha mijini na vijijini ni vema Serikali itunge sheria itakayoongoza taratibu kanuni na masharti ya kiusalama kuhusiana na *location* zilizo *secure, safe* na madhubuti kiujenzi zenye lengo la kuhakikisha usalama wa fedha za wananchi wengi ambao fedha zao zitakuwa zimehifadhiwa katika *SACCOS* zao. Sheria hii inalazimisha wahusika kujenga au kupanga majengo ambayo ni madhubuti la sivyo matuko ya wizi mara kwa mara ya uvunjwaji wa majengo yasiyo imara yatawavunja moyo na kuondoa imani ya wananchi wenye nia ya kuweka akiba katika *SACCOS* mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mchango wangu huu mdogo naunga mkono hoja hii ya Waziri wa Katiba na Sheria kwa asilimia mia moja.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa hatua mbalimbali inazofanya na kuchukua kuboresha Mahakama za Wilaya na Mahakama za Mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Haki za Binadamu inafanya kazi nzuri mpaka sasa ila ipanue shughuli zake kufikia ngazi za kata na vijiji ili mwananchi waweze kuelewa dhana ya utawala bora na haki za binadamu ili waondokane na unyonge wa kuonewa bila sababu na watendaji.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, kwa kuwasilisha vizuri hoja yake imeeleweka. Napendekeza yafuatayo:-

Mahakama za Mwanzo nchini zipewe uzito wa kipekee maana yake kwanza majengo ya Mahakama hizo yote yakarabatiwe na ikibidi yajengwe upya. Naipongeza Serikali kwa kukarabati *Kamachumu Primary Court* na sasa naiomba Serikali ilitupie macho jengo la Mahakama ya Mwanzo Muhutwe. Muhutwe pia ipate jengo muhimu la maliwato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watumishi wa Mahakama hizo hasa Mahakimu waliopo japokuwa bado ni wachache, napendekeza hatua za kuwabadilisha zisiachwe. Mahakimu waendelee kupata mafunzo na waajiriwe moja kwa moja toka vyuoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakimu wa Mahakama ya Mwanzo Kamuchumu analalamikiwa sana kwa rushwa na kuchelewasha kesi. Napendekeza achunguzwe na ikibidi aondolewe haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama ya Mwanzo Muhutwe pia haina Hakimu. Naiomba Serikali ituletee Hakimu ili haki itendeke. Mahakama za Mwanzo zipewe usafiri ili kumaliza haraka zile kesi za kufuata huko. Hata hivyo wapewe mafuta maana kuna tabia ya watendaji kudai mafuta pale wanapokuwa na vyombo. Wasio kuwa na vyombo walalamikaji hulipa pesa za kufunga Mahakama ili kwenda kutembelea eneo linalolalamikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda Serikali inisaidie, hivi kesi iliyoanzia Mahakama ya Mwanzo ikaenda hadi Mahakama ya Rufaa na kutolewa hukumu inaweza kufunguliwa tana Mahakama ya Mwanzo? Je, inakuwaje mtu aliyeshinda kesi hii ikawa kila wakati anaitwa Mahakama ya Mwanzo au polisi ili mradi anasumbuliwa tu.

Naomba Serikali inipe jibu, nitahoji wakati wa vifungu maana hili ni moja ya mambo yanayonisumbua sana. Ninayo kesi ya Mzee Mukono *vs* Merius, imenisumbua sana. Mzee Mukono alishinda hiyo kesi lakini bado anasumbuliwa na Mahakama na polisi kwa kushitakiwa na Mzee Merius.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwasilishe.

**MHE. NURU A. BAFADHILI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Napenda nizungumzie kuhusu Mahakama. Hakimu anapokuwa Mahakamani anatakiwa atende haki pale inapostahili. Cha kushangaza kuna baadhi ya Mahakimu wanaacha kazi yao ya kuhukumu na wanajiingiza katika siasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema hivyo ni pale Hakimu anaposhabikia Chama fulani na kuthubutu kusema kuwa nanukuu: “Hizo kesi za hao wapinzani nipe mimi niwashughulikie,” mwisho wa kunukuu. Nasema hilo kwa vitendo vya Mahakimu wetu wanavyotenda kinyume cha maadili ya kazi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu rushwa, kwa kweli tunaiomba Serikali ilipigie sana kelele suala hili la rushwa. Kwa kweli kuna baadhi ya Mahakimu wanapenda sana hupokea rushwa. Mahakimu hao wanapokea rushwa lakini kupita kwa watu wengine. Kuna baadhi ya mahakimu huwatumia jamaa zao wa karibu katika kuomba rushwa kwa washitakiwa. Haiwi rahisi kumshinda Hakimu kwa rushwa kwa vile yeye hapokei mikononi mwake bali ana wakala wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuzungumzia kuhusu wazee wa Mahakama katika Mahakama za Mwanzo. Kwa kweli wazee hawa wana matatizo. Itokeapo mtu ana kesi hujifanya wao wanaweza moja kwa moja kuonana na Hakimu wao wanaweza moja kwa moja kuonana na Hakimu na kuimaliza kesi hiyo, atakapofanya hivyo pale ndipo anapodai rushwa. Hili lakini linasababishwa na wale wazee wa Mahakama kutolipwa.

Nashauri hawa wazee wapate malipo hutokana na kazi yao ya kushinda Mahakamani kuanzia asubuhi hadi jioni. Wazee hawa wanakuwa hawafanyi kazi zao za kuwapatia kipato kwa ajili ya kushinda Mahamani na kwa vile hana kipato ni lazima aombe rushwa ili waweze kuishi na familia zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa wakipatiwa malipo kwa kiasi fulani rushwa itapungua. Naomba kuwasilisha.

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuruhusu kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Katiba na Sheria. Kabla sijachangia naomba kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Mwanakwerekwe naunga mkono hoja hii ya asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza hotuba hii ingawa ina mapungufu machache tu, naanza kuchangia kuhusu mikataba ya madini ichunguzwe upya. Pia mkataba wa uwekezaji nao pia uchunguzwe na mambo hayo yote yaletwe Bungeni na kujadiliwa na kupitishwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Wabunge kufika muda wake iangaliwe upya. Kwa mfano likitokea jambo lolote kabla uchaguzi na Uchaguzi Mkuu akaahirishwa basi kuwa na kifungu kitachoruhusu Wabunge kuendelea na nafasi za hadi uchaguzi au kipindi husika na apate haki zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itasaidia hata kama litatokea tatizo kubwa basi nchi itakuwa na Bunge kamili ambalo litafanya kazi kwa wakati ule. Kuhusu wabakaji, watu hao ni watu ambao wanawapa matatizo watoto wetu. Kwa hii adhabu hii ya miaka 30 inastahili kuendelea, lakini ifanyiwe uchambuzi zaidi kwa sababu ubakaji ule wa kumdhalilisha anabakwa hata kama hafanyiwi kitendo. Lakini kwa yule ambaye ameenda nyumbani hadi chumbani usiku na akafanywa kitendo yule hata kama atalalamika kubakwa basi iwe adhabu nyingine kwani kaenda kwa hiari yake na ana akili timamu. Kwa hiyo, kuwe na vipimo. Ahsante sana.

**MHE. SIGFRID S. NG'ITU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Nimeona kuchangia kwa maandishi ni vizuri kwa vile hoja nimeikubali, vilevile nimefurahia mpango wa kukarabati Mahakama ya Mwanzo ya Madawa katika Jimbo langu. Kero iliyobakia tayari nilikwishaanza kunong'ona nong'ona na Naibu wako Mheshimiwa Mathias Chikawe na ambaye ni jirani yangu na ni kaka yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wananipigia kelele kuwa niombe kibali cha kuazima huduma za Mahakama ya Wilaya Msumbiji kwa vile ni majirani zetu. Pale Ruangwa kila kitu Kimahakama ya Wilaya ni Mkoa tu Lindi Mjini umbali wa kilometa 158 kwa hiyo, inabidi mkazi wa Ruangwa atembee umbali wote huo ili kufuata haki yake. Matokeo yake kule Lindi mahabusu zimejaa wana Ruangwa. Kwa vile hakuna mtu wanayemfahamu ili wapate dhamana. Gharama ni kubwa, nauli ni kama shilingi 4,000/= hadi 5,000/=. Chakula na malazi bado.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watuhumiwa na kesi za Mahakama ya Mwanzo hupelekwa Nachingwea kilometa 47. Pale hakuna jela au mahabusu. Inabidi umpelekee chakula kule Nachingwea. Hii ni ngumu sana ikiwemo gharama kubwa ya kupeleka gari kwenda kuwachukuwa asubuhi kuwaleta Mahakamani na tena kuwarudisha tena jioni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafadhali naomba uongee na Waziri mwenzako wa Usalama wa Raia ili pajengwe kituo cha polisi na amlete *OCD* na hasa kwa vile pale kituo cha polisi cha Wilaya na wewe jenga Mahakama ya Wilaya ili Hakimu wa Wilaya apatikane. Wana Ruangwa tunaomba haki zetu. Vinginevyo andaa utaratibu wa angalau Hakimu wa Wilaya awe anakuja kusikiliza kesi angalau mara moja tu kwa wiki, kwa kuanzia.

**MHE. AZIZA S. ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Kuhusu kupunguza kwa kesi Mahakamani, nadhani sasa kuna hoja ya kupunguza kero kwa wananchi kwa sababu kesi nyingi sana na muda wa kuamua kesi hiyo unakuwa ni mrefu sana. Lazima Serikali ilione hilo ili wananchi wafanye shughuli zao kwa muda kuliko kuwa Mahakamani kwa muda mrefu hata wengine kukatazwa kutoka nje ya Mkoa anaoishi na kushindwa kujipatia vipato vya kumudu maisha yake na familia yake hiyo si haki kwa binadamu kukosa uhuru kama huo na kubaki kuwa omba omba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu haki za wanawake, hapa ndipo pabaya zaidi hasa kesi hizo zinapowagusa wale wenye uwezo. Mwanamke anaponyanyasika na hata anapoachana na mwanaume, Mahakama huamua kuwa mwanamke huyo alipiwe kodi ya nyumba na mwanaume, ingawa walijenga wote na kuzaaa watoto. Lakini huyo mwanaume kubaki na nyumba na mwanamke kuondoka na watoto na kulipiwa kodi ya nyumba na huyo mwanaume. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kuelewa hukumu hiyo ina msaidia huyo mwanamke au inatoa njia panda ili baadaye asimlipie kodi hiyo au atakapofariki mwanaume huyo mwanamke akose haki yake ya kimsingi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kuna haja ya sheria kuwekwa ili mwanamke awe na haki ya kupata haki yake kama huyo mwanamke amezaa watoto hao na hata kama

hakuzaa maana kuzaa au kutozaa yote ni maisha yanapangwa na Mungu pia nae ana haki zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoa vipeperushi ili wanawake waelewe haki za kisheria katika nchi maana wanawake hawaelewi haki zao na kutoelewa haki zao ni tatizo la kudhulumika kabisa na hasa ukizingatia kuwa mfumo dume ulitawala.

Ni vigumu sana wanawake wa mijini na vijijini kuelewa haki zao kimsingi mategemeo yangu ni kuwa Wizara itaandaa utaratibu wakaelimisha haki za mwanamke na mwanamke kwa mwanamke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria ambazo zinamkataza msichana wa shule kutokuendelea na masomo anapopata mimba kuna haja ya kuileta hapa Bungeni na kuibadili. Kuna mifano mingi ambayo mnatoa kwa nchi fulani imefanya hivi na sisi tunafata kwa kuwa ina faida. Je, kuna uzito gani kufuata taratibu za Zanzibar kwa sheria kama hiyo na kuileta hapa kwetu ili na sisi twende sambasamba?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hati za vizazi na vifo, tusiwanyime haki wananchi wetu kwa kutoandaa sisi wenyewe utaratibu mzuri wa hati za kuzaliwa kwa wananchi ni mojawapo ya kuwanyima haki zao na hasa husababisha mapenyo ya rushwa na ambayo Mheshimiwa Waziri atangazie wananchi kuwa wanapokwenda kwa sasa hivi kuomba hati hizo kisheria kinahitajika nini? Ili waelewe wakati hiyo mikakati inaendelea, rushwa imetawala hapo. Ni vyema kuwaambia wananchi ukweli wa kupata hati hizo na mategemeo yangu litafahamika na Waziri ataeleza leo wananchi ukweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii muhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujalia kuwa wazima na salama na kukutana hapa kila siku ya kazi. Mimi nitachangia mambo matatu tu. Kwanza ni kuhusu Tume ya Kurekebisha Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume hii tumeipa kazi nzuri ya kurekebisha sheria ili ziendane na wakati. Sasa napenda nipate maelezo kwa Mheshimiwa Waziri, kwa nini Tume hii baada ya kumaliza kufanyia marekebisho sheria, kwa nini zinacheleweshwa kuletwa Bungeni na kufanyiwa marekebisho. Zinawekwa kwenye makabati ya Waziri muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili napenda kuelezea kuhusu ucheleweshaji wa kesi Mahakamani kwa visingizo kuwa ushahidi au uchunguzi haujakamilika kunakotolewa na polisi na Mahakama kukubali na kuwaacha watuhumiwa kuendelea kusoto rumande au kuwa na kesi muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini Majaji na Mahakimu wetu wanakuwa wanasikiliza amri za polisi zaidi badala ya kuangalia hali halisi ya kesi ilivyo. Hivi wao hawajui kuwa polisi wanapenda kukomoa watu na wakati mwingine kuwa wanawababmbikizia wananchi kesi. Hivyo wanapenda watu kusota rumande.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu ni kuhusu Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kufika kule Zanzibar. Pamoja na Mheshimiwa Waziri amesema kuwa ataleta Muswada wa Sheria hapa Bungeni ili tuweze kuiwezesha Tume hiyo iweze kufika na kufanya kazi zake Zanzibar, lakini hakusema ni lini Muswada huo utaletwa. Kwani suala hili ni muhimu sana kwani Zanzibar kuna uvunjwaji mkubwa wa haki za binadamu na haujafanyiwa kazi. Hivyo tunaomba Muswada huo uletwe haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nasema ahsante sana.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumpongeza Waziri wa Katiba na Sheria kwa kuwasilisha vizuri hotuba yake ya makadirio ya matumizi kwa Wizara yake kwa mwaka wa fedha 2006/2007. Pia napenda kumpongeza Naibu Waziri wa Wizara hiyo pamoja na watendaji wote wa Idara na Taasisi zilizoko chini ya Wizara hii kwa michango yao mbalimbali katika kutekeleza majukumu yao ya kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na shukrani na pongezi zangu kwa Wizara hii nina maoni yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (kama ilivyorekebishwa) imetoa haki na uhuru wa kila mtu kupata haki ya kisheria kama ilivyo kwenye kifungu 30(3) ya Katiba hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu yeyote anaedai kuwa sharti lolote ....... au katika sheria yoyote inayohusu haki yake au wajibu wake limevunjwa, linavunjwa au inaelekea linavunjwa na mtu yeyote popote katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anaweza kufungua shauri katika Mahakama Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria hii haitekelezwi vizuri nchini kwa sababu zifuatazo:-

Kwanza, hakuna mtu anayeweza kufungua shauri la madai bila kulipa ada ya shauri hilo. Utaratibu huu unanyima haki ya msingi kwa wale ambao hawawezi kuwa na uwezo wa kulipa ada. Nafahamu kuwa *poor litigants.* Wamepewa mwanya wa *waiver of suit courts fees* lakini hali halisi ni kuwa mfumo nzima ni mrefu *(waiver)* na wenye mzunguko *(complicated).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Watanzania wengi wanaishi vijijini ambako hakuna Mahakama hata wale walio karibu na Mahakama za Mwanzo, nafasi ya kuwakilishwa na wanasheria kama vile Mawakili haipo kwa sababu sheria zilizopo zinakataza Mahakama hizo kutumiwa na Mawakili, badala yake wananchi wanalazimika kusafiri hadi kwenye Mahakama za Wilaya au Mahakama ya Hakimu Mkazi ambazo pia zipo Mjini. Hii ina maana kuwa ili upate haki lazima haki hiyo ifuate kwa kuisafiria na endapo mtu hana uwezo (fedha) basi mtu huyo ndiyo mwisho wa kupata haki hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, uzoefu umeonyesha kuwa mashauri mengi huchukua muda mrefu hadi kumalizika. Hii ni kinyume na ukweli kuwa haki ya mtu lazima ipatikane kwa wakati kwani ikumbukwe kuchelewesha haki ni kunyima haki, *the justice delayed is justice denied.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maoni hayo hapojuu ningependa sasa kufikisha ujumbe kwa Serikali, Wizara ya Katiba na Sheria kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Wizara ya Katiba na Sheria inajua kuwa Wilaya ya Tandahimba haina Mahakama ya Wilaya na hivyo wananchi kukosa haki ya kimsingi ya kupata haki ya kisheria? Je, ni lini Wilaya hiyo itapatiwa haki hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, zile Mahakama za Mwanzo za Mnyawa, Mihambwe na Litehu ambazo hazina Mahakimu, Wizara/Serikali itawaambia nini wananchi wa maeneo hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Wizara/Serikali inatambua kuwa haki hii ya kisheria ina vipingamizi vingi kiasi cha Watanzania waishio vijijini kuhitaji kujigharamia mno ili wapate? Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua tatizo hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kwa kuiunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

**MHE. AMEIR ALI AMEIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima na uwezo wa kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa hotuba aliyoitoa katika Bunge lako Tukufu ambayo imenipa muamko wa kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichangie mchango wangu mdogo tu katika Wizara hii hasa kwa vile mambo mengi ninayotaka kuchangia yamejieleza kwa ufasaha katika kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Idara ya Mahakama bado sijaridhika na uendeshaji wa kesi kwa sababu kesi zinachelewa sana na ndiyo sababu wananchi wanakata tamaa na kuondosha amani na Mahakama zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na kuwa kazi ya Ujaji ni ngumu sana na inahitaji utulivu, akili, busara nyingi, lakini pia inatakiwa kuwe na ubinadamu wa kuwahurumia wananchi walioleta malalamiko yao ambayo yanataka kutolewa maamuzi ya kisheria yanachukua muda mrefu sana kufuatilia na mwisho anashindwa kuendeleza suala lake kutokana na kesi yake kupigwa tarehe kila siku na wakati mwingine suala lake linaweza kumuingizia hasara kubwa kuliko vile alivyotegemea na kuamua kusamehe na ndiyo maana watu wengi wanaojishuku wenyewe na hawaoni maana ya kwenda Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii haiwasaidii walioleta kesi tu, bali hata husababisha walalamikiwa kukaa mahabusu kwa muda mrefu hasa kwa wale wanaokosa zamana na kusababisha mlundikano wa mahabusu katika magereza yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kuliona hili na kulipatia ufumbuzi wa kina ile kiwarejeshee wananchi imani zao katika Mahakama zetu n a waache kutumia sheria mikononi mwao na kulileteа Taifa hasara kubwa kwa sababu adhabu inayotolewa na wananchi huwa haitizami Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo naiunga mkono hoja asilimia mia moja. Ahsante.

**MHE. MANJU S. O. MSAMBYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii adimu kutoa mchango wangu katika hoja tajwa hapo juu. Napenda nieleze wazi kuwa napata kigugumizi kuunga hoja hii. Nasema hivi kwa sababu zifuatazo:-

Kwanza, jalada la kitabu cha hotuba ya Wizara tunayo maeneo yafuatayo, haki sawa kwa wote na kwa wakati. Inaniwia vigumu kuamini kama kweli Wizara inasimamia haki, kwa wakati ndio kabisa nakuwa na mashaka makubwa. Haviingii akilini inapotokea shauri linapelekwa mbele ya Mahakama tangu Januari 2003 hadi leo halijaanza kusikilizwa, achilia mbali kutolewa hukumu. Ili kuthibitisha kauli hii nakuambatanishia barua ya mlalamikaji kwa Msajili wa Wilaya, Mahakama Kuu Dodoma ya Oktoba 6, 2005. Bahati mbaya zaidi barua hiyo wala haikujibiwa. Hii ikimaanisha kuwa hata Msajili wa Mahakama hiyo hayuko tayari kuona haki ikitendeka kwa wakati. Kwa kielelezo hiki narudia kusema kuwa inaniwia vigumu kuunga hoja hii mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua wazi kuwa shauri likiwa Mahakamani halishughulikiwi mahala pengine hadi pale hukumu itapokuwa imetolewa au shauri hilo kuondolewa Mahakamani. Sina nia ya kulijadili swala hili Bungeni, bali nataka Mheshimiwa Waziri unieleze haki sawa kwa wote na kwa wakati wapi kwa shauri la tangu Januari, 2005. Mbaya zaidi shauri hili linahusu mirathi ambayo ingefanya warithi kupata fedha iliyo benki kwa nia ya kuendesha maisha.

Pili, napenda kuiomba Wizara ione umuhimu wa kutenda haki katika Mahakama za Mwanzo. Jimbo la Kigoma Kusini lenye Kata 12 ambazo zinatenganishwa na uwanda wa nchi kavu na ule wa mwambao wa Ziwa Tanganyika. Jambo la kusikitisha ni kwamba wapo Mahakimu watatu ambao wanafanya kazi isivyoridhisha kwani inachukua watu kwenye vituo zaidi ya miezi sita na pengine hata mwaka kabla mashauri yao hayajasikilishwa. Hali hii kweli inaweza kuwa Wizara inasimama utoaji wa haki sawa kwa wote na kwa wakati? Naomba niseme hapana. Haiwezekani watu wangojee mashauri yao kusikilizwa kwa muda mrefu halafu utuambie kuwa ni haki sawa kwa wote na kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, yapo mashauri ya watuhumiwa wa makosa ya mauaji ambayo yamekaa Mahakamani muda mrefu wakati upelelezi ukiwa tayari umekamilika. Kwa nini hayasikilizwi mashauri hayo? Jibu la mkato ambalo Wizara au

Idara ya Mahakama hutoa mara kwa mara ni kutokuwapo Majaji wa kutosha au uhaba wa Majaji. Nashindwa kukubali hoja hii kwani Majaji wanaosikiliza kesi za uchaguzi wanatoka wapi? Mara tu baada ya uchaguzi kesi zote husikilizwa haraka na uamuzi/hukumu kutolewa. Hivi Serikali/Wizara/Mahakama inataka kusema kuwa Majaji wanasikiliza kesi za uchaguzi huwa na elimu na taaluma tofauti na wale wanaotakiwa kusikiliza kesi za mauaji na zinginezo? Kama jibu ni hapana, kwa nini zile za uchaguzi ziwe zinasikilizwa kwa wakati. Hivi Wizara kwa hali hiyo niliyobainisha inaweza kusema kuwa haki sawa kwa wote na kwa wakati, ipo katika Idara ya Mahakama?

Nne, wapo watu ambao tayari wamehukumiwa kunyongwa. Wamesota magerezani kwa muda mrefu na kwa hali hiyo hatma yao inakuwa mashakani. Hali hii inawapa adhabu ya ziada wahukumiwa hao. Hivi Wizara imeweza kwa namna gani kumshauri mwenye mamlaka ya utekelezaji wa hukumu ya kifo? Angefaa ashauriwe awabatilishe hukumu kutoka kifo kwenda kifungo cha maisha au kuwaachia huru kama atavyoona inafaa. Wizara haielekei kuwa ilifanya hivyo maana hatujawahi kuelezwa kama wapo waliobatilishiwa hukumu. Hivi hali hii inaonesha kuna dalili za haki sawa kwa wote na kwa wakati?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo niliyoeleza hapo juu hayanipi motisha kuunga hoja mkono. Naomba kuishia hapo nikisubiri majibu ya kina katika haya niliyoeleza hapo juu.

**MHE. JOHN M. SHIBUDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia fursa hii kukushukuru kwa kunipatia fursa ya kuchangia kwa maandishi katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria kuhusu Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napongeza hotuba nzuri ya Wizara hii ya Katiba na Sheria. Wahenga husema kila kinachong'ara kina mhunzi. Hivyo nawapongeza viongozi wakuu wote wa Wizara hii kwa kutambua kwamba Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, Mbunge, ni hazina kubwa kwa Taifa letu katika kuchochea maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kumtambua Naibu Waziri Mheshimiwa Mathias Chikawe, ambae ni maarufu kwa uzalendo wake kwa maslahi ya nchi yetu. Napenda pia kumtambua Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Johnson Mwanyika, ambaye ni nuru ya tumaini kwa haki za Watanzania. Aidha, naomba pongezi zangu ziwafikie wote viongozi wa taasisi kuu za sheria na watumishi wote wa mamlaka ya Haki na Sheria Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutambua na kukiri Wizara hii inafanya kazi nzuri sana ya kuboresha malengo ya haki za jamii. Hivyo naomba Serikali itoe ufafanuzi kuhusu kuwatendea haki sungusungu walioko mahabusu kwa muda mrefu bila kujua hatma zao kwa kunijibu maswali yafuatayo:-

(a) Je, Serikali inaweza kuunda Kamati ya kuchambua kusadikika kuwepo makosa ama kubainisha kutokuwapo hatia ili sungusungu waliokaa mahabusu kwa maudhui ya bado uchunguzi kwa muda mrefu unaendelea wapate haki ya kuwa huru.?

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Pamekuwepo na jitihada za kupambana na kesi bandia kwa mujibu wa uelewa wa kijamii dhidi ya wafugaji wa ng'ombe, je, Serikali inaweza kuunda Tume ya kusukuma kasi ya kupatikana ukweli ili wafugaji waliotuhumiwa waelewe hatma zao?

(c) Wahenga husema umoja ni nguvu. Hivi karibuni Wizara ya Usalama wa Raia inategemewa kuleta Muswada wa Polisi jamii kitu ambacho naweza kusema ni asilia ya mfumo wa sungusungu, je, sheria ya nchi hii inatambua mchango wa sungusungu ili palipo na makosa ya kiufundi katika utekelezaji wa wajibu wa sungusungu hawa nao wafaidike na huruma ya sheria ya nchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naomba kujua iwapo Serikali imekamilisha ujenzi wa hoja ya kuwa na Kadhi Mkuu Tanzania Bara na iwapo pana subira ya kuboreshwa azma hii. Je, Mheshimiwa Waziri ana kauli gani kuhusu maudhui ya kuwepo Kadhi Mkuu na wajibu wake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijahitimisha naomba kauli ya Mheshimiwa Waziri kuhusu lini atatembelea Jimbo la Maswa ili aje ahitimishe kauli ya kionekanacho kwa macho huaminika kwa fikra za maamuzi ya kutendwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya kupatiwa ufumbuzi napenda kusema ufumbuzi huo utakuwa boresho mahsusi kwa kuwa mimi kutamka naunga mkono hoja ni ukweli wangu. Ahsante na naunga mkono hoja.

**MHE. MWAJUMA HASSAN KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kutoa mchango wangu katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria kwa hotuba yake. Baada ya hayo sasa naomba nianze kuchangia katika maeneo ya Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama ni chombo mama katika nchi yetu. Chombo hiki ndicho kinachopelekea wananchi kuishi hali ya kufuata sheria. Pamoja na umuhimu wa chombo hiki, bado kuna udhaifu mkubwa. Pamoja na kuwa ni chombo kinachotekeleza sheria pamoja na haki za binadamu, ongezeko la mjao wa watuhumiwa na wafungwa magerezani kunatokana na ukosefu wa Mahakimu na Majaji. Serikali inapaswa itatue tatizo hili kwani kuwaweka watu rumande kwa dhana, halafu ukachelewa kusikiliza kesi ni kwenda kinyume cha haki za binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, iko haja Serikali iwaandalie utaratibu maalumu Mahakimu na Majaji wetu kuwaweka katika mazingira mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumuacha Hakimu usoni mwa mtu alie mhukumu jana ama atakaye mhukumu kesho, hili inaweza kuzua neno, ama Hakimu kushindwa kufanya kazi yake, kwa kupokea rushwa ama kuhofu. Kumweka Hakimu vijijini ni kumfanya ateswe na watu wa familia ya mhukumiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu haki za akina mama na watoto. Serikali inafaa ione iko haja ya sheria hii itazamwe kwani akinamama ndio wanaobebeshwa majukumu makubwa katika kuwaenzi watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu walemavu. Kwa kweli walemavu wanasikitisha sana na si kwa ulemavu wao bali ni majina wanayopewa na Watanzania wazima. Kumwita mlemavu jina kutokana na ulemavu wake ni kinyume cha sheria. Ni vyema sasa Serikali iwawekee sheria wenzetu hawa.

**MHE. VUAI ABDALLA KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza sina budi kumpongeza Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, kwa hotuba nzuri aliyoitayarisha kwa ushirikiano na viongozi wa Wizara yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama ya Tanzania ni chombo kimoja wapo kati ya mhimili mitatu ya dola, kinastahili kutenda haki na kusimamiwa na Jaji Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kupitia Mahakama iwe ikifanya haki na Mahakimu watende haki wasicheleweshe kesi, wasipokee rushwa kwani bado ya hali hii inasikitikiwa na wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kesi za jinai na madai naomba ziendeshwe vizuri, kusiwe na malalamiko ya wananchi. Kwa haki Mahakama zifanye na tujali kila mtu ana haki sawa za binadamu.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nichukue nafasi kumshukuru Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanazofanya tangu wateuliwe kushika nyadhifa zao. Aidha, nawapongeza kwa kuandaa bajeti nzuri ya Wizara hii. Pamoja na hayo napenda kuchangia kwenye maeneo machache kama ifuatavyo:-

Kwanza uhaba wa majengo na uchakavu wa Mahakama za Mwanzo. Wilaya ya Mbozi yenye takribani watu 600,000 sasa ina Mahakama chache sana za Mwanzo. Kwa mfano Tarafa ya Igamba yenye idadi kubwa sana ya watu takribani watu wapatao 180,000 ina Mahakama tatu tu za Mwanzo na huhudumiwa na Hakimu mmoja tu. Mahakama hizo ziko katika Kata za Igamba, Itaka na Msia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii si kwamba inamfanya Hakimu ashindwe kufanya kazi zake kwa ufanisi na kwa muda, lakini pia huchelewesha haki za watuhumiwa. Si jambo la ajabu kuona kesi ndogo ya madai inachukua muda mrefu kuisha kwa sababu tu Hakimu yupo mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishauri Wizara kama ifuatavyo, moja Wizara ikarabati jengo la Mahakama ya Mwanzo Igamba ambalo liko kwenye hali mbaya sana. Pili, Wizara ijenge jengo lingine la Mahakama Kata ya Itaka kwani lililopo ni dogo sana na limechakaa sana. Naomba pia ieleweke kwamba Kata ya Itaka ni kubwa sana, ina idadi ya watu wanaokadiriwa kufikia 60,000. Pia kiwango cha makosa ya madai ya jinai, ardhi ile kiko juu sana, hali hii hufanya sehemu hiyo kuwa na kesi nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo ujenzi wa jengo kubwa na la kisasa ni muhimu sana. Tatu, Wizara ipeleke Hakimu mwingine angalau mmoja ili awe na kituo kimoja cha kazi kuliko ilivyo sasa ambapo hakimu mmoja aliyepo hulazimika kutembelea au kufanya kazi katika maeneo matatu. Nne, Wizara pia iwape Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo, usafiri ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa urahisi zaidi. Tano, Wizara ijenge Mahakama mpya katika Kata za Isansa na Mambinzo ili kuwapa wananchi wanaoishi maeneo hayo huduma ya Mahakama kwa muda mzuri zaidi na kutolazimika kusafiri mwendo mrefu kufuata Mahakama takribani kilometa 30 hadi 50 hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti,kuhusu utunzaji wa kumbukumbu Mahakamani. Utunzaji wa kumbukumbu za kesi au utunzaji wa mafaili ya kesi kwenye Masjala za Mahakama nyingi, hasa za Mwanzo ni mbaya sana na mara kadhaa wahusika wa mafaili au wenye kesi wanapoenda Mahakamani kwa ajili ya kesi zao mara kadha huambiwa faili zao hazipatikani. Aidha, Mahakama nyingi hasa za Mwanzo, hazina vyumba maalum vya kutunza kumbukumbu hizo muhimu, hali hii husababisha mafaili mengi kupotea na hivyo kuleta usumbufu mkubwa sana kwa wahusika. Nashauri Wizara ilitambue tatizo hili na kulifanyia kazi kubwa ili kumbukumbu za kesi zitunzwe vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hiyo hapo juu isipodhibitiwa itasababisha kuendelea kuwanyima watu haki yao ya msingi, itakuwa ni kuwacheleweshа watu haki yao na wote tunajua kwamba haki iliyocheleweshwa ni sawa na haki iliyonyimwa *(justice delayed is equals to justice denied),* naomba sana hili lirekebishwe. Hali hiyo pia ikiachiwa iendelee, itaendelea kuwafanya makarani wa Mahahama wa Mwanzo na Mahakama nyingine kuendelea kudai rushwa kwa wahusika kwa kisingizio kwamba inawachukua muda mrefu kusaka faili za wahusika. Hivi kutafuta faili si kazi ya makarani? Kwa nini wanageuza kazi ya utafutaji wa mafaili kuwa mradi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ucheleweshaji wa kesi, kama nilivyosema hapo juu kwamba ucheleweshaji wa kesi ni sawa na kuwanyima wahusika haki yao ya msingi. Hivi katika hali ya kawaida inachukua muda gani mathalani kwa hakimu hususan wa Mahakama ya Mwanzo kumaliza kesi moja ndogo ya madai? Nauliza hiyo kwa sababu wakati mwingine inamchukua hakimu muda wa zaidi ya mwaka mmoja kumaliza kesi za aina hiyo. Naomba utendaji kazi wa Mahakimu upimwe kwa kesi hizi wanazozisikiliza na kuzitolea maamuzi na pia wapandishwe vyeo kwa msingi huo. Kwa kufanya hivyo kutawafanya wawajibike zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba nzuri tunaomba utekelezaji uwe pia mzuri. Naunga mkono hoja. Ahsante sana.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia maeneo yafuatayo:-

(i) Kwa vile Tume ya Kurekebisha Sheria imefanya kazi nzuri ya kuzungukia nchi nzima kutafuta maoni ya wananchi na kutoa mapendekezo ya marekebisho kadhaa na kwa kuwa kuna taarifa kuwa mapendekezo mengine yana zaidi ya miaka kumi Wizarani bila marekebisho. Husika kufanyika, je:-

(a) Ni marekebisho au mapendekezo ya sheria zipi yamewasilishwa katika miaka kumi na tano iliyopita na ambayo hayajafanyiwa kazi hadi sasa kwa majina?

(b) Ni sababu zipi za msingi zimefanya mapendekezo hayo kutofanyiwa kazi kwa kipindi chote hicho?

(c) Kwa vile sheria zingine kama shilingi 100/= za matunzo ya mtoto, *Workman's Compensation, Inheritance Ordinance, Marriage Act of 1971* ni baadhi tu ya sheria zinazogusa wananchi wengi wa kawaida na zimepitwa na wakati, ni lini sasa Serikali italeta marekebisho ya sheria hizo Bungeni ili kuondoa kero nyingi kwa wananchi wetu?

(d) Isingekuwa vema Serikali kuandaa *legislative plan* kama zinavyofanya nchi nyingi ili kuepuka ucheleweshaji wa aina hii na kuwapa nafasi Wabunge kuchambua Miswada kwa kina?

(ii) Wilaya ya Karatu sasa ni zaidi ya miaka kumi tangu imekuwa Wilaya na haina Mahakama za Wilaya. Tena kufanya mambo yawe mabaya zaidi mahabusu wa Karatu wanawekwa mahabusu Arusha na kwa kuwa Mahakama ya Wilaya iko Mji wa Mbulu, Wilaya ya Mbulu ambayo ni kilometa zaidi ya 200 toka Arusha, je, ni lini sasa Serikali itajenga Mahakama ya Wilaya Karatu na je, wakati ujenzi huo unapangwa ni kwa nini Serikali isipange/kutunga fungu kumwezesha Hakimu wa Mbulu kusikiliza kesi husika Karatu kuondoa usumbufu mkubwa unaowapata watuhumiwa kwa sasa? Nategemea kupata jibu la kina ili tusihitaji kwenda kwenye vifungu. Natanguliza shukrani za dhati.

**MHE. JUMA SULEIMAN N'HUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono hoja. Nakupongeza Mheshimiwa Waziri na wataalam wote. Hoja ya kuanzisha Mahakama ya Kadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ilani ya CCM ya mwaka 2005 ukurasa wa 132 Ibara ya 108 imesema ifuatavyo: "Kulipatia ufumbuzi suala la kuanzisha kwa Mahakama ya Kadhi Tanzania Bara." Mheshimiwa Waziri, katika hotuba yako jambo hili halikuzungumzwa kabisa, je, kuna hatua gani? Ni lini hatua zitaanza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza Serikali kwa kuboresha maslahi ya Majaji na Mahakimu. Naomba juhudi hizo ziendelee sambamba na kuangalia vitendea kazi na ofisi zake ziwekewe vifaa vya kisasa. Serikali iangalie uwezekano wa kuongeza Mahakimu na Majaji ili kupunguza mrundikano wa kesi na kesi kuchukua muda mrefu. Kuweko na muda maalum wa kusikilizwa kesi na kumalizika na kesi ambazo huwa zinachukua muda mrefu kwa upelelezi zifutwe. Naunga mkono hoja.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Waziri wa Katiba na Sheria, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote wa Wizara hii kwa kuandaa hotuba nzuri ya bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa cheti cha kuzaliwa ni haki kwa kila raia, naiomba Serikali kuweka mikakati madhubuti hasa vijijini kuhakikisha kuwa kila mtoto anayezaliwa anapata cheti cha kuzaliwa kwa kuwa vyeti vya kuzaliwa vinatolewa katika ngazi ya Wilaya, wananchi wengi wanaoishi vijijini hawana uwezo wa kufuatilia vyeti vya watoto wao Makao Makuu ya Wilaya.Wananchi wengi waliozaliwa vijijini wanahangaika sana kutafuta vyeti vya kuzaliwa kwa ajili ya kupata hati ya kusafiria na kadhalika. Naiomba Serikali kuweka mikakati madhubuti katika suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chini ya mifuko wa pamoja *(basket fund)* Wizara hii inatarajia kujenga jengo la ofisi ya Makao Makuu ya Wizara ya Katiba nan Katiba kwa mwaka huu wa 2006/2007. Katika hotuba ya Waziri jengo hilo halikutajwa litakapojengwa. Namwomba Waziri wa Wizara ya Katina na Sheria aonyeshe mfano kwa kujenga jengo la Wizara yake Makao Makuu ya Serikali yaani Mkoani Dodoma ikizingatiwa kuwa uamuzi wa Serikali kuhamia Dodoma Wizara yake pia ilihusika kwa kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kuunda Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Je, kuundwa kwa Tume hii kumewasaidiaje wananchi wa Tanzania? Je, Tume hii inawasaidiaje wananchi wanaosota Mahakamani bila sababu za maana pasipo kupata haki zao? Je, Tume hii imewahi kuwahoji watu mbalimbali walioshtakiwa/kushtaki kupata maoni yao kuhusu haki inavyotendeka/isivyotendeka katika ,ahakama zetu? Kama jibu ni ndiyo wamewasaidiaje wananchi na hasa waishio vijijini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kuangalia upya suala la Wazee wa Baraza kulipwa posho kwa wakati na pia posho hiyo iweze kukidhi japo robo ya mahitaji yao. Wazee wa Baraza wanashinda kila siku Mahakamani lakini hakuna wanachokipata hivyo wanatumia nafasi zao kuwashawishi watuhumiwa kutoa chochote kwao na kwa Mahakimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naunga mkono hoja ya Serikali.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi za dhati kwa Waziri wa Katiba na Sheria pamoja na Naibu wake kwa kazi nzuri wanayoifanya. Mchango wangu wa leo unahusu suala la Mahakimu katika Mahakama zilizopo katika Wilaya zenye mbuga za wanyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yako haina budi kuangalia upya Mahakimu wanaowapanga katika Mahakama hizi kutokana na mazingira mabaya ya rushwa yanayoweza kuwakabili. Hali hii ya rushwa inatokana na ukweli kwamba katika Wilaya hizi kumekuwepo na hali ya kutoaminiana baina ya mamlaka zinazohifadhi wanyama na

Mahakimu. Mfano katika Wilaya ya Serengeti kumekuwepo na malalamiko ya kwamba kesi za majangili wanaua wanyama zimekuwa zikipindishwa na hatimaye haki kutotendeka hali inayosababisha vitendo vya kihalifu katika mbuga za wanyama iendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Mahakimu hawa wabadilishwe au waangaliwe upya kabla ya kupelekwa katika maeneo yenye mbuga za wanyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni kuhusu wazee wa baraza, suala hili liangaliwe upya na naomba Serikali/Wizara wakati wa kujibu hoja anieleze, Serikali imejiandaaje kukabiliana na suala hili ambalo kwa kweli kitendo cha kuwalipa wazee hawa shilingi 200/= kwa kesi kinachangia kuongezeka kwa rushwa. Sheria ya Mahakama za Mwanzo inaeleza kuwa wazee hawa wa Baraza watasikiliza kesi na maoni yao yatapewa kipaumbele wakati wa hukumu. Je, suala hili Serikali haioni kwamba huu ni mwanya mkubwa wa rushwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa pia kipato au malipo hayo ya shilingi 200/= ni madogo lakini pia yamekuwa yakicheleweshwa. Naomba Serikali inieleze ina mkakati gani wa kuhakikisha kuwa suala hili la wazee hawa linaisha kwa maana kwamba walipwe kwa wakati au waongezewe kiwango cha malipo cha zaidi ya shilingi 200/= kwa kesi ili walau kupunguza mwanya wa rushwa. Naunga mkono hoja.

**MHE. EUSTACE O. KATAGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri. Napongeza kwa hotuba nzuri na uendeshaji mzuri wa shughuli za Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama Kuu ya Bukoba kwa ajili ya Mkoa wa Kagera imepata Jaji na sasa inaendeleza huduma ikiwa Mahakama Kuu kamili kuliko zamani ambapo Jaji alikuwa anatoka Mwanza. Imesaidia sana na tunashukuru sana Mheshimiwa Jaji, anajituma sana, tunamshukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jengo la Mahakama ya Wilaya ya Karagwe, haliridhishi. Tunaomba likarabatiwe na majengo kuongezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Mahakama za Mwanzo waongezewe vitendea kazi hasa *stastionaries,* mafaili, *carbon papers* na kadhalika. Naunga mkono hoja.

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Pamoja na kuunga mkono hoja, nachukua fursa hii kuipongeza Serikali ya Awamu ya Nne kwa ushindi iliyopata katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kutoa mchango wangu katika kuipongeza Wizari hii kwa mipango yake mahsusi ya utekelezaji wa programu zake

kupitia mtandao wa kompyuta. Hii inatoa chachu katika harakati za kupunguza kero na kuwapo maamuzi ya haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ina majukumu mengi na mazito yenye kugusa haki za binadamu katika maamuzi, hivyo ushauri wangu nauelekeza katika kuboresha taaluma za kisheria ili kupata Mahakimu na Majaji zaidi ili kabla watuhumiwa kukosa haki kutokana na ufinyu wa watu hao, hivyo kupelekea kusubiri foleni ya kupewa hukumu, iondoke mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii mama inapaswa iwe pia na uwiano wa karibu sana katika utendaji wake na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Wizara ya Usalama wa Raia, kwani uwiano wao wa ukaribu utasaidia sana katika kutoa haki kwa watuhumiwa katika maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi nampongeza Waziri wa Katiba na Sheria kwa maamuzi yake ya kutembelea Magereza na kujionea mwenyewe hali halisi na hatimaye kutoa mwongozo juu ya majukumu ya utoaji haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa wananchi wote wanategemea zaidi haki kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ingekuwa bora Mwanasheria Mkuu aongezewe nguvu zaidi katika mamuzi ya kisheria hasa zaidi katika maamuzi ya kisheria hasa pale katika utata wa upelelezi unaochukua muda mrefu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakimu ni watu muhimu sana katika jamii kwani wao ni waamuzi wa haki za kisheria, hivyo sio watu wote wanaopendelea Mahakimu au Majaji kwani baadhi ya watu huchukizwa na maamuzi ya kisheria hivyo ingekuwa busara kwa watu hawa kupewa ulinzi katika makazi yao ili wawe na uhakika wa maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinadharia, Tume ya Haki za Binadamu iwe kimsingi inashirikiana na Wizara hii ili kuweka ufanisi katika kufuatilia mambo na kama yapo mashirikiano haya basi yaongezwe zaidi ili huduma za kisheria ziwe pana zaidi na nyepesi kiutekelezaji.

**MHE. FETEH SAAD MGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutupa uhai, uzima, amani na utulivu wa nchi yetu, sasa kwa heshima kubwa nina furaha kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete na Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Amani Abeid Karume, kwa ushindi mkubwa walioupata katika uchaguzi Mkuu uliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nampongeza Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, Mawaziri na Waheshimiwa Wabunge wote. Pongezi maalum kwa Mheshimiwa Spika kwa kuchaguliwa na Bunge hili Tukufu kwa kishindo kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kubwa sana naomba kuchangia baadhi ya sehemu chache katika hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mahakama, pamoja na kwamba Mahakama zetu zinajitahidi katika kuendesha kesi ili kupunguza au kuondoa kabisa mrundikano wa kesi nyingi zilizoko Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nashauri kwamba bado Serikali iongeze kujengwa Mahakama zaidi na hasa zile Mahakama za chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mahakimu, sambamba na ujenzi wa Mahakama, kuna upungufu mkubwa wa Mahakimu hao. Nashauri juhudi kubwa Serikali ichukue katika kuwapata Mahakimu kwani hiyo itapunguza ule mrundikano wa mahabusu uliojaa kule magerezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Sheria ya *Parole,* nionavyo mimi, bado sheria hii haijatumika ipasavyo kwani kule magerezani kuna wafungwa wengi ambao wamekwishajirekebisha na vifungo vyao vimebakia miaka miwili au chini ya hapo. Kwa nini hawapewi fursa hiyo ya kutolewa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu wafungwa watoto wadogo, pamoja na juhudi nzuri zinazochukuliwa katika kuwatenganisha wafungwa watoto walio chini ya umri wa miaka 18 na wale watu wazima, lakini bado kuna baadhi ya magereza watoto wamo. Nashauri suala hili ni vyema likachukuliwa hatua ya haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango wangu huo mdogo, nahitimisha kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria kwa hotuba yake iliyo nzuri na ameisoma kwa ufasaha mkubwa. Aidha, nampongeza Mwanasheria Mkuu wa Serikali , Katibu Mkuu wa Wizara na watendaji wote wa Wizara kwa juhudi zao wanazozifanya kwa Wizara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matumaini yangu mchango huu mdogo pengine utasaidia katika kupunguza yale matatizo ya mahakama zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kubwa, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Bumbwini, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichuke nafasi hii kumpongeza Waziri, naibu Waziri na Katibu Mkuu kwa maandalizi mazuri ya kufikisha bajeti hii hapa Bungeni. Pia niwapongeze watendaji wote chini ya Jaji Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katiba ya Jamhuri ya nchi yetu inatambua mihimili mitatu, Bunge, Serikali na Mahakama. Vyombo hivi vinategemeana sana na vya muhimu kwa maisha na maendeleo ya binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Misungwi imeshindwa kukamilika kutokana na kupungukiwa na nguzo moja muhimu ambayo ni Mahakama. Hatuna Hakimu wa Wilaya tangu Wilaya hii ianzishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wamelifikisha kwa Mheshimiwa Rais na kuahidi kulishughulikia katika kipindi cha uongozi wake wa awamu ya kwanza mwaka 2005/2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi mbalimbali imekuwa ikiendelea kujengwa/kupelekwa katika Wilaya zilizo na huduma na kuachwa Misungwi bila masaada wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana nilikamata kifungu na kutaka ufafanuzi, Mheshimiwa Waziri wa wakati huo alinihakikishia kuwa wangechukua hatua, lakini hakuna chochote. Je, ahadi hiyo ya Waziri ilikuwa kulidanganya Bunge au vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi wa kina katika majumuisho ili wananchi wa Misungwi wajue hatma yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo cha kutopewa hadhi ya kuwa na Mahakama yao, nyumba za kupanga zipo na pia ni vyema akateuliwa na kupunguza malalamiko yanayowapata wananchi kufuata huduma Wilayani Kwimba ambako ni mbali sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Serikali ihakikishe huduma hii muhimu inapatikana Wilayani mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nasubiri ufafanuzi wa hoja yangu na naunga mkono hoja.

**MHE. ANIA S. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kwa maandishi. Nampongeza Waziri na Naibu Waziri na watalaamu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya sheria za nchi yetu Tanzania hazifutwi au kutekelezwa na hazina tafsiri sahihi na zinawaonea wananchi kwa kuwa hawazijui. Kuna umuhimu wa kuzitafasili ili zifanye kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kero nyingine ni kurundikana kwa mahabusu. Ni vema sheria ziangaliwe upya ili kupunguza mrundikano katika magereza yetu. Kuna kesi nyingi sio za lazima mtu kukaa mahabusu muda mrefu, mfano kupigana au mtu kufanya

fujo sambamba na kuongeza Majaji na Mahakimu nchini na kuangalia mishahara, makazi na vitendea kazi ili kuwapa mazingira bora ya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Tume hii iangaliwe upya. Sheria hii inakandamiza demokrasia. Sasa hivi tumo katika mfumo wa vyama vingi, sheria inayompa mamlaka Rais kuteua Tume ya Taifa ya Uchaguzi, inakandamiza na kumnyima haki Mtanzania ambaye ameingia katika kinyang'anyiro cha kugombe Urais pale ambapo hakufanyiwa haki na Tume hiyo kuipeleka Mahakamani na pia Katiba inalinda sheria hii kwa kuwa nanukuu; "Hakuna Mahakama yenye mamlaka kuchunguza jambo lolote lililotolew na Tume ya Uchaguzi katika kutekelea madaraka yake kwa mujibu wa sheria hii." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni ukwiukaji wa haki za binadamu, naomba kuwasilisha.

**MHE. KHADIJA SALUM AL-QASSMY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mungu kwa kuniwezesha kujikita katika kutoa mchango wangu kwa Wizara hii nyeti ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Waziri, Naibu Waziri na watendaji wake wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia mambo muhimu kuhusu Katiba ya nchi yetu. Katiba ibadilishwe ili ikidhi haja ya mfumo wa vyama vingi vya siasa kwani katiba hii ya leo ina mfumo wa chama kimoja cha siasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunataka kuleta vyama vingi, Serikali ilitafuta maoni mbalimbali kutoka kwa wananchi kwa kupitia *white paper* na matokeo yake 20% walikubali vyama vingi na 80% walikataa vyama vingi na Serikali kwa nia njema wakawapa wachache .

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba Katiba ibadilishwe japo watu wachache ndio wanaotaka vitumike vigezo vile vile vya *white paper*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba elimu ya kujua sheria ya nchi yetu itolewe ili watu wetu waelewe kwani watu wengi hawajui sheria na hutenda kosa bila ya kujua kama hilo ni kosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria inayomlinda mke iangaliwe upya kwani mwanamke anapata taabu sana. Mwanaume humpiga mke wake au mwanamke mpaka akaamuua au kumkata kwa mapanga . Kwa hiyo, sheria iongezwe makali ipate kuwalinda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na nashukuru.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri, *AG, DPP* na watendaji wengine wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri pamoja na vikwazo vingi vinavyowakabili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, motisha ndogo, watumishi wengi na hasa wanasheria katika ofisi za *AG* na *DPP,* mishahara yao pamoja malipo mengine kwa ajili ya kukimu matumizi ya simu za kazi, *risk allowance* hazitolewi.

Kwa unasaba huu watumishi hawa wanapunguzwa *morale* zao katika kazi zao. Matokeo yake watumishi hawa hutumia ofisi za *AG* na *DPP* kwa ajili ya kujifunza na kupata uzoefu na baadaye kuhamia sekta binafsi, kwa hiyo *AG* na *DPP* wanaendelea kupoteza watumishi wazuri. Wanaobakia ni wachache na hawawezi kutimiza kazi zao kwa wakati kwani zina wazidi kimo, nashauri maslahi yao yaongezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ucheleweshaji wa kesi. Kesi nyingi huchelewa kutolewa maamuzi kutokana na sababu nyingi, miongoni mwa sababu hizo ni upungufu wa watendaji katika ofisi za *AG* na *DPP.* Aidha, ucheleweshaji wa kesi nyingi unatokana na upungufu wa Mahakimu katika ngazi mbalimbali pamoja na uchunguzi wa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti,ushauri wangu ni kuwa Serikali ichukue hatua za makusudi na za haraka kukabiliana na matatizo hayo.

Kuhusu hali ya majengo na samani za Mahakama. Majengo mengi ya Mahakama pamoja na samani zake ni chakavu sana. Aidha, vitendea kazi vingine kama *stationery,* magari (usafiri) ama ni vichakavu au havipatikani kabisa. Kwa mnasaba huu, kesi nyingi hucheleweshwa na mapungufu haya. Ushauri ni kuwa Serikali ichukue hatua za makusudi ili kukabiliana na matatizo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzishwa kwa nafasi ya Kadhi Tanzania, Serikali iendelee kufanya utafiti wa kina kuhusu suala la kuwa na Kadhi ambaye atashughulikia kesi za waislamu kwa mujibu wa taratibu ya dini yao bila kuvunja Katiba ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa asilimia mia moja.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti,hongera Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri na uwasilishaji mzuri Bungeni. Ushauri wangu ni huu ufuatao:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kongwa tuna Mahakama ya Wilaya ya kisasa. Tunashukuru Serikali katika kukamilisha jengo hilo hapakujengwa nyumba ya Hakimu wa Wilaya, tunaomba nyumba hiyo ijengwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Mahakama za Mwanzo chakavu sana za enzi za ukoloni, zinahitaji ukarabati mkubwa. Mahakama hizo ni pamoja na ukarabati mkubwa, Mahakama hizo ni pamoja na Sagara, Mlali, Pandambili, Zoissa, Mkoka na Kongwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba ujenzi wa Mahakama ya Mwanzo Kibaigwa mashauri ni mengi sana pale. Naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa misingi ile ile ya kutoa kipaumbele cha maendeleo kwenye Mikoa na Wilaya za pembazoni mwa nchi na maeneo yaliyo nyuma kimaendeleo na kwa vile Wilaya ya Ludewa ni moja ya maeneo ya aina hiyo basi katika magari 36 yatakayonunuliwa kwa ajili ya wakaguzi wa Mahakama za Mwanzo basi Wilaya ya Ludewa ipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitapenda kujibiwa kama Ludewa itapata gari au lah na kama jibu ni hapana nipewe maelezo kwa sababu gani.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, kwa kazi nzuri anayofanya tokea ateuliwe na Mheshimiwa Rais kuongoza Wizara nyeti. Nampongeza pia Naibu Waziri na Katibu Mkuu wa Wizara hii ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwasilisha kilio cha wananchi wa Singida kuwa uhaba mkubwa wa Mahakimu upo ufumbuzi wa *Magistrates* katika Mahakama za Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti,Wilaya ya Iramba hakuna hata *magistrate* mmoja, wa Manyoni yupo mmoja tu na Wilaya ya Singida ina upungufu wa zaidi ya *Magistrates* watatu au wanne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mahakama za Mwanzo hali ni mbaya zaidi kwa sababu upungufu wa Mahakimu wa Mwanzo ni mkubwa zaidi ya Mahakimu saba. Hivyo waliopo wanafanya kazi katika mazingira magumu sana kwani kesi ni nyingi na wanapata lawama nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama ya Mwanzo Mungaa, Puma, Misughawa na Kata nyinginezo hazima Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo, hivyo Mahakimu wachache waliopo wakati mwingine wanazunguka kwenda kusikiliza kesi katika Mahakama hizo, hali ambayo ni hatari na sio salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa usafiri pia haupo hivyo Mahakimu wanapanda mabasi, ma - *land rover* pamoja na washitakiwa na hivyo kuhatarisha usalama wa Mahakimu hao. Vipi hakimu anamhukumu mtu na kisha apanda naye gari moja kwenda mjini au kwingineko?

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Mahakama zenyewe ni mbovu sasa Mahakama za Mwanzo za Mkoa wa Singida ni za tokea ukoloni. Zinahitaji matengenezo au ukarabati, naomba Mahakimu waongezwe na wapatiwe usafiri na vile vile Mahakama zenyewe zikarabatiwe. Naunga mkono hoja.

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Mwenyekiti, uendeshaji wa kesi na kupunguza kero za wananchi kuhusu utoaji haki. Katika ukurasa wa 26, Mheshimiwa Waziri ameeleza kuwa kati ya kesi za madai 933 Mahakama Kuu ni kesi 284 tu zimeshughulikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia upo mtizamo wa wananchi kuwa kesi zenye maslahi ya wananchi wengi mara nyingi hazipewi umuhimu wa kwanza kusikilizwa na hata zikisikiliwa hisia ni kuwa kesi hizo zinashindwa. Aidha, kesi hizo zinahusu vijiji na taasisi za umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi maalum, kwa kuwa Kanuni zetu hazituruhusu kuzungumzia kesi zilizoko Mahakamani, natoa ombi maalum kuwa Shauri Na. 22 la mwaka 2005 linalohusu fidia ya shamba liitwalo *Babati Sisal Estate* lisikilizwe mapema iwezekanavyo kwa kuwa inagusa sana wananchi wengi na ujenzi wa taasisi za Serikali. Naomba kukukabidhi kumbukumbu chache ili zikusaidie kulielewa shauri hilo.

Kuhusu upungufu wa Mahakimu, kwa mwenendo wa sasa wa Serikali kuajiri Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo wachache kama 100 na Mahakimu Wakazi 70 (ukurasa wa 46) Sekta ya Sheria haitaweza kupunguza kero za wananchi kwa kiwango kikubwa. Hivyo ni muhimu Serikali iweke mikakati maalum kama vile kuongeza vyuo vya Mahakama na kutafuta utaratibu mwingine wa namna ya kuongeza Majaji ambao ni wachache mno. Ikumbukwe kuwa idadi ya watu inaongezeka kwa kasi kubwa na hivyo hivyo mahitaji ya Mahakimu na ya wananchi nayo kuongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Babati ina Mahakama za Mwanzo tisa ambazo ni Babati, Bonga, Gallapo, Gidas, Magugu, Mwada, Dareda, Bashnet na Ufana. Ni Mahakimu watatu tu wa Mwanzo kati ya tisa, Mahakama sita hazina Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Waziri kwenye jedwali la pili ukurasa wa 69 ameeleza kuwa majengo ya Mahakama ya Mwanzo ya Bonga yamejengwa/kukarabatiwa. Sawa, lakini hadi leo hakuna Hakimu. Tafadhali naomba kufahamu Mahakama hii ambayo ina jengo ni lini sasa itapata Hakimu ili ili ianze. Nitapenda kufahamu wakati wa majumuisho ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri.

Mradi wa *Quick Start,* Mkoa wa Manyara ulikuwa na ufadhili wa mradi huo ambao kata hivyo haukufanikiwa hadi sasa. Kwa kuwa wananchi wa Babati walichanga fedha kwa ajili ya Mahakama za Mwanzo na Wilaya. Napenda kufahamu ni fedha kiasi gani zilichangwa, zipo wapi, zinafanya nini na nini hatma ya mpango uliokuwepo wa *Quick Start* ambao ulitakiwa kuwa wa mfano katika maboresho ya sekta ya sheria.

Kuhusu posho za wazee wa Mahakama. Kumekuwepo na malalamiko hadi sasa juu ya ulipaji wa posho za wazee. Aidha, inaonekana kuwa hakuna *transparency* ya kutosha fedha zinapopelekwa Wilayani na hiyo kusababisha wazee hao kulalamika kila mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kuwa fedha zinapopelekwa kwa malipo hayo kupitia *(OC)* matumizi ya kawaida ni vema ziwekwe kwenye matangazo ili wazee hao wajue kama fedha zipo au hazipo ili kuondoa wazee hao kuwalaumu Mahakimu Wafawidhi bila sababu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza utaratibu wa kuboresha huduma na kwa kuanza kutenga kazi za mwendesha mashtaka ya jinai na za upelelezi na utaratibu wa kuandaa programu ya upunguzaji wa mrundikano wa kesi. Pia napongeza utaratibu wa Kamati za Kusukuma kesi *(Case Flow Management Committee).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na namtakia Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote kheri.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Waziri wa Katiba na Sheria, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara hii kwa maandalizi na uwasilishaji mzuri wa hotuba ya Bajeti ya mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa mchango wangu katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania kuwa Makao Makuu ya *The African Court of Justice and Human Rights.* Natoa pongezi kwa wote walioshiriki kutoa hoja na kusimamia hoja hadi wanachama wa Umoja wa Gambia kuridhia Tanzania kuwa Makao Makuu ya Mahakama hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa Mheshimiwa Waziri awafahamishe Watanzania juu ya hatua ambazo Serikali imechukua kuwezesha Mahakama hiyo hapa Tanzania kupata majengo ya kuwezesha Mahakama hiyo kuanza kufanya kazi.

Kuhusu ushiriki wa Wizara katika kutoa ushauri kwa Watalaam wa Wizara mbalimbali kuhusu mikataba. Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria ameeleza kwamba Wizara yake inashirikiana na wataalamu wa Wizara mbalimbali katika majadiliano na kuandaa rasimu za taarifa muhimu kuhusu mikataba ya utekelezaji wa majukumu ya Serikali. Hivi sasa kumekuwa na malalamiko mengi sana kuhusu mikataba mbalimbali ambayo inakandamiza uchumi wa Tanzania kwa mfano mkataba wa uzalishaji na mauzo ya umeme kati ya *IPTL* na *TANESCO* kwa niaba ya Serikali na pia malalamiko dhidi ya mikataba kati ya Serikali na makampuni ya madini kuhusu uvunaji na malipo ya madini. Ili kudhihirisha kasoro zinazolalamikiwa hata Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne, ametoa agizo kuangaliwa upya kwa mikataba hiyo. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kulielezea nini Taifa juu ya ushiriki wa maofisa wa Wizara ya Katiba na Sheria katika kutoa ushauri katika mikataba hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapungufu katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi na ukarabati wa majengo ya Mahakama ngazi za Wilaya. Kumekuwa na malalamiko mengi katika ngazi ya Wilaya kwa kutoshirikishwa kwa maofisa wa Mahakama za Wilaya katika utekelezaji wa ujenzi au ukarabati wa majengo ya Mahakama katika Wilaya zao.

Tenda za ujenzi zimekuwa zikisimamiwa na mkoa na uteuzi wa Mkandarasi hufanyika wakati mwingine bila hata Mkandarasi kutembelea na kuona hali ya majengo yanayohitaji ukarabati. Mara nyingi matokeo yake ni kukarabati maeneo ambayo siyo muhimu sana na kuacha yale ya lazima zaidi. Hata mara nyingine uchaguzi wa maeneo ya ujenzi wa Mahakama ngazi ya Kata kufanywa na Mkoa bila kuwashirikisha viongozi wa Wilaya. Ni vema Mheshimiwa Waziri akatazama kwa kina malalamiko hayo na kufanya marekebisho kuhusu taratibu za matumizi ya fedha kwa kazi za ujenzi mpya na ukarabati hasa katika Wilaya ya Muheza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ucheleweshaji wa malipo ya fedha zinazopitia Mahakamani. Kuna ucheleweshwaji mkubwa sana wa fedha zinazolipwa kupitia Mahakama zetu. Baadhi ya malipo hayo ni kama fedha za mirathi, licha ya kukamilishwa kwa hatua zote muhimu kuwezeshwa fedha za mirathi kulipwa malipo yanacheleweshwa kwa muda mrefu hadi kufikia hatua wananchi kukata tamaa kuendelea kufuatilia mali yao hiyo na mwisho wa yote wananchi kujiuliza fedha hizo baada ya wao kukata tamaa kuzifuatilia zinaenda wapi. Nashauri Mheshimiwa Waziri atazame hali hiyo na kujaribu kuona Wilaya zipi bado zinashikilia fedha za wananchi kwa muda mrefu bila kuwalipa? Naunga mkono hoja.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, kwanza kabisa naomba tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kutupa uzima na hivyo kukutana ndani ya Jumba hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti pili, nakushukuru kwa kunipatia fursa hii ili niweze kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria iliyowasilishwa hapa asubuhi ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nitumie fursa hii kumshukuru sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali aliyenitangulia Mheshimiwa Andrew John Chenge, kwa misingi aliyoiweka na ambayo imeniwezesha kuyatekeleza majukumu yangu vyema. Namshukuru kwa ushirikiano ambao ameendelea kunipatia hadi hivi sasa. *(Makofi)*

Aidha, nawashukuru viongozi walioteuliwa kuiongoza Wizara, Mheshimiwa Dr. Mary Nagu na Naibu Waziri, Mheshimiwa Mathias Chikawe, ambao tunaendelea kufanya kazi kwa ushirikiano mkubwa na wa karibu. Kwa ushirikiano huo natumaini tutaweza kulisukuma gurudumu la maendeleo na utekelezaji wa majukumu ya Wizara yetu kwa ari, nguvu na kasi mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuwapongeza Mheshimiwa Angel Anold Kileo, Mheshimiwa Nathalia Kimaro na Mheshimiwa Edward Piter Kangwa, kwa kuteuliwa kwao hivi karibuni kuwa Majaji wa Mahakama ya Rufaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nijielekeze katika hoja iliyowasilishwa kwa umahiri na ufasaha mkubwa na Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria. Nitamke kwanza kwa kusema naiunga mkono kwa asiliamia mia moja. *(Makofi)*

Mimi katika mchango wangu ambao utakuwa mfupi tu, kwa sababu nitajielekeza katika kutoa maelezo katika hoja zilizotolewa ambazo ni za kisheria. Hoja zenyewe ni hizi zifuatazo:-

Mheshimiwa Lucas Selelii, alitaka kupatiwa ufafanuzi kuhusu uhai wa Bunge hili baada ya kuchelewa kuanza kazi baada ya Uchaguzi Mkuu uliopita. Kwa mujibu wa Ibara ya 65(1) ya Katiba ya nchi, maisha ya Bunge ni miaka mitano kama alivyoeleza Mheshimiwa Lucas Selelii. Ibara ya 65(2) inaeleza maana ya maneno, maisha ya Bunge kwamba ni ule muda ambao Bunge limeitishwa kukutana kwa mara ya kwanza baada ya Uchaguzi Mkuu na kuishia tarehe ya kuvunjwa Bunge kwa ajili ya kuwezesha uchaguzi mwingine kufanyika. Hata hivyo, muda wa Bunge jipya kuanza kutekeleza majukumu yake utatetegemea mazingira ya namna Bunge lilivyovunjwa.

Kwa mujibu wa Ibara 90(ii), Bunge linaweza kuvunjwa ama kwa kuisha muda wake wa miaka mitano au wakati wowote katika miezi kumi na mbili ya mwisho wa uhai wake isipokuwa kama Spika atakuwa amepewa taarifa rasmi inayopendekeza kuundwa kwa Kamati Maalum ya kuchunguza Rais kwa mujibu wa Ibara hii.

Kwa hiyo, Rais ana mamlaka ya kuamua tarehe ya uchaguzi. Kama Rais akiamua tarehe ya uchaguzi kwamba iwe mwezi Oktoba, mwaka huo ambao utahusika Ibara ya 90(ii) inamruhusu kufanya hivyo. Kwa hiyo, uchaguzi siyo lazima ufanyike mwezi Desemba, kama ambavyo uchaguzi uliopita umefanyika. Ibara ya 90(ii) inampa Mheshimiwa Rais uwezo wa kuvunja Bunge katika muda wa miezi kumi na mbili kabla ya muda wake kuisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba pia nielezee juu ya hoja zilizotolewa na Wabunge waliochangia hoja za Waheshimiwa Mawaziri wengine, Mheshimiwa William Kusila alichangia katika Makadirio ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuhusu masharti magumu ya dhamana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masharti ya dhamana yameainishwa katika Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai Sheria Na. 9 ya mwaka 1985. Hakimu amepewa mamlaka ya utashi ya kuangalia mazingira ya kesi iliyo mbele yake. Kwa mfano, mshtakiwa awe na uwezo wa kuhudhuria Mahakamani anapohitajika kufanya hivyo na pili, usalama wa mshtakiwa. Hata hivyo, kama masharti ya dhamana yataonekana ni magumu mshtakiwa anaruhusiwa kuomba rufaa kwenye Mahakama ya juu zaidi. Dhamana ni haki ya mshtakiwa ingawa ni kweli kwamba haruhusiwi kupewa dhamana katika baadhi ya makosa yale makubwa kama mauaji ya makusudi au uhaini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, akiomba rufaa kwenda Mahakama ya juu, Mahakama ile inaweza kufanya masahihisho kuhusiana na dhamana hiyo, masharti aliyopewa ya dhamana yanaweza kufanyiwa masahihisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juu ya Sheria ya *Parole* ifanyiwe marekebisho ili kupanua wigo wa *Parole* na Sheria ya Huduma ya Jamii yaani *Community Service Act* irekebishwe. Hii pia ilichangiwa na Mheshimiwa William Kusila, Mbunge wa Bahi na Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, Mbunge wa CHADEMA, Viti Maalum Kigoma alichangia pia hotuba ya Waziri wa Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhumuni ya Sheria ya *Parole* Sura ya 400, chapisho la mwaka 2002 ni kuwaachia huru wafungwa ambao wamejirekebisha na ambao wamekaa magerezani zaidi ya miaka minne ili kupunguza msongamano wa magereza. Sheria hii ilitungwa mwaka 1994. Hivyo bado ni mpya. Aidha, Sheria ya Huduma za Jamii *(Community Service Act)* Sura ya 219 chapisho la mwaka 2002 ambayo ina shabaha ya kutoa adhabu mbadala ya kifungo cha nje kwa kufanyakazi za jamii. Utaratibu huu pia unapunguza msongamano wa wafungwa magerezani. Maoni ya Wizara ni kwamba sheria hizi mbili zinapanua wigo kwa hatua za kupunguza msongamano.

Pia Mheshimiwa William Kusila alitoa hoja ili kukabiliana na ongezeko la vitendo vya ubakaji. Sheria ya Makosa ya Kujamiiana ifanyiwe marekebisho. Wizara itafanyia utafiti na kufanyia kazi kwa kushirikiana na wadau ikiwa ni pamoja na Mheshimiwa Mbunge. Lakini hili nina hakika kwamba Waziri wangu wa Katiba na Sheria atalizungumzia kwa kirefu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kesi zinazowahusu watu waliowekwa mahabusu kuchukua muda mrefu, hili lilichangiwa na Mheshimiwa Diana Chilolo, Mbunge wa Singida, Viti Maalum, CCM na Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, CHADEMA, Viti Maalum Kigoma akichangia pia hotuba ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama inasikiliza kesi kulingana na utaratibu wa kisheria uliopo. Kesi zote ambazo upelelezi umekamilika zinasikilizwa mara moja. Aidha, utaratibu wa kusikiliza kesi unasimamiwa na Kamati ya kusukuma kesi ambazo ziko kwenye ngazi ya Wilaya, Mkoa, Kanda na Kitaifa. Wajumbe wa Kamati hizi ni kutoka Mahakama, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Polisi na Magereza. Sambamba na maelezo hayo, kesi zinazokaa Mahakamani zaidi ya siku 60 huwa zinafutwa kisheria, hiyo lakini inategemea kwamba mshtakiwa ndiye aombe kwamba kesi hiyo ifutwe mbele ya Mahakama, labda kama anawakilishwa na Wakili hii haiwezi kutupa matatizo kwa sababu Wakili wake anajua kwamba kama kesi imekaa kwa muda wa siku 60 tangu ianze kupelelezwa basi anaweza kuiomba Mahakama iweze kufuta kesi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kitengo cha uandikishaji wa vizazi na vifo ihamishiwe Idara ya Uhamiaji ili kudhibiti uhamiaji haramu. Hii ilichangiwa na Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, Mbunge wa CHADEMA, Viti Maalum Kigoma wakati akichangia hotuba ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa mwneyekiti, Serikali imeiwezesha Ofisi ya Kabidhi Wasii Mkuu kwa kuifanya kuwa Wakala wa Serikali ili kuiwezesha kufanya kazi kwa ufanisi zaidi na kuwa na taarifa muhimu za uraia na kuiwezesha Idara ya Uhamiaji kutoa vitambulisho vya uraia. Kwa hiyo, tunafikiri kwamba kwa sasa hivi wakati haujafika wa kuihamisha Idara hiyo kuipeleka kwenye Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Sheria ya uandikishaji wa vizazi na vifo ipitiwe upya. Wizara inaafikiana na hoja hiyo, hilo suala litafanyiwa kazi na lipo katika mkakati wa mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine linahusu Muswada wa *Nationality* kulikuwa na mchango hapa uliwasilishwa hapa Bungeni. Hili lilichangiwa na Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, Mbunge wa CHADEMA, Viti Maalum na Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, Mbunge wa Singida Kaskazini. *(Makofi)*

Kuhusu Tume ya Kurekebisha Sheria imekwisha wasilisha taarifa ya utafiti huo, nawahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba suala hili litashughulikiwa na Serikali ya awamu hii na endapo wadau wataona kwamba ni vema ije hapa Bungeni tutaileta ili muweze na nyie kuijadili na kama mtaona kwamba itafaa mtaipitisha iwe sheria ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuwabambikiza kesi wananchi. Hili imechangiwa na Mheshimiwa Abdul Marombwa, Mbunge wa Kibiti. Kitendo cha kuwabambikiza watu kesi ni ukiukaji wa haki za binadamu. Pale ambapo malalamiko ya ubambikizaji wa kesi yanapotolewa Mkurugenzi wa Mashtaka huondoa mashtaka. Askari yeyote anayebainika kubambikiza kesi anapaswa kushughulikiwa na mamlaka

husika. Kwa hiyo, mtu yeyote ambaye anafikiri kwamba ndugu yake ama jamaa yake amebambikizwa kesi basi tunamwomba aende kwenye Ofisi za Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambazo ziko kwenye Kanda kumi na moja hivi, ili aweze kutoa taarifa. Ukishatoa taarifa kwenye Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wataifanyia kazi na kuhakikisha kwamba malalamiko uliyoleta kama kweli mtu amewekwa ndani kinyume cha sheria anahakikisha kwamba haki inatendeka na huyo mtu anaachiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Majaji na Mahakimu wanawajibika kwa nani hususan pale wanapotoa maamuzi yanatoa haki? Hili limetolewa na Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mbunge wa Matemwe, CCM.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Majaji na Mahakimu wana kinga ya kisheria wanapotoa hukumu Mahakamani. Aidha, upande ambao haukuridhika na hukumu ya Jaji au Hakimu unatakiwa kuomba rufaa katika Mahakama ya juu zaidi na kama hajaridhika inaomba tena rufaa Mahakama Kuu. Kama mtu umeanzia kesi yake kwenye Mahakama ya Mwanzo kama hukuridhika na hukumu iliyotolewa na Hakimu Mahakama ya Mwanzo, unaweza kuomba rufaa kwenda kwenye Mahakama ya Wilaya na kama hukuridhika na Mahakama ya Wilaya unaweza kuomba rufaa kwenda Mahakama Kuu. Kama hukuridhika na Mahakama Kuu unaweza kuomba rufaa tena kwenda kwenye Mahakama ya Rufaa.

Kuhusu Sheria ya Ununuzi Serikalini *(Public Procurement Act)* ifanyiwe marekebisho. Hii imetolewa na Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mbunge wa Kibaha Mjini. Rai yake imepokelewa, aidha, tunamwomba Mheshimiwa Mbunge atusaidie kuainisha maeneo halisi ya sheria hiyo inahitaji marekebisho. Tunamkaribisha aje atuletee maeneo halisi ambayo anaona yana matatizo ili tuweze kufanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge na Mahakama limetiwa mfukoni na Serikali kwa miaka 40. Mheshimiwa Juma Suleiman Nh’unga, akichangia hotuba ya Makadirio ya Bajeti ya Mipango ya Serikali. Mgawanyo wa madaraka baina ya mihimili mitatu ya dola imekuwa ikizingatiwa kwa muda wa miaka 40, dhana kwamba imetiwa mfukoni inaweza kuwa imetokana na wajibu alionao Waziri wa Kazi katika Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kuwasilisha Bajeti ya Bunge, Bungeni na Waziri wa Katiba na Sheria kwa upande wake kuwakilisha Bajeti kwa upande wa Mahakama. Kazi hii ni ya Utawala na uwajibikaji wa kisera. Wala haipaswi kuchukuliwa kuwa ni kuweka mfukoni mihimili hiyo ya dola.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba nimalizie kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kutoa mchango wangu kuhusu hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kutoa mchango wangu kuhusu Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria. Napenda kumalizia kwa kusema kwamba, naiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. Naomba Waheshimiwa Wabunge, muendelee kutuunga mkono na kutupa

yale ambayo tumewaomba, muyaadhinishe katika bajeti hii ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuungana na Waziri wa Katiba na Sheria, alivyozungumza leo asubuhi kwa kutoa shukrani zangu na pongezi kwa viongozi wote ambao wamechaguliwa na kuteuliwa katika nyadhifa zao mbalimbali, baada ya Uchaguzi Mkuu uliopita mwaka 2005. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu kwa dhati kabisa, nimshukuru Mheshimiwa Rais wetu Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuniteua mimi kuwa Naibu Waziri wa Wizara hii nyeti na kunipa nafasi hii ya kushiriki katika kutoa mchango wangu mdogo katika Serikali hii ya Awamu ya Nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa shukrani zangu za pekee kwa wananchi wa Jimbo la Nachingwea, ambao wamenipa heshima kubwa ya kunichagua kuwa mwakilishi wao humu Bungeni. Nawaahidi kuwa, nitafanya kazi nao kwa nguvu na akili zangu zote ili kuleta maendeleo katika Wilaya yetu ya Nachingwea.

Aidha, napenda kumshukuru Mheshimiwa Edgar Maokolo-Majogo, ambaye ndiyo aliyenitangulia kuwa Mbunge wa Jimbo letu kwa muda wa miaka 30 iliyopita, kwa ushauri wake mzuri. Mwisho, napenda kuwashukuru ndugu, jamaa na marafiki, ambao kwa namna moja au nyingine, wameniwezesha kusimama hapa leo hii. Lakini napenda niwataje watu wane, ambao wamenisaidia sana katika mchakato huu. Wote katika watu hawa ni wanawake, wa kwanza kabisa ni mama yangu, Mama Prisca Chikawe, huyu alikuwa kampeni meneja wangu wakati wa Uchaguzi Mkuu na mshauri wangu mkuu. Wa pili, dada yangu anaitwa Diana Chikawe, ambaye alikuwa dreva aliniendesha wakati wote wa kampeni, tukizunguka Wilaya ya Nachingwea. Wa tatu, mke wangu Profesa Amandina Lihamba, ambaye amenipa *support* kubwa na uvumilivu mkubwa. Lakini wa mwisho na siyo kwa umuhimu ni Mheshimiwa Dr. Mary M. Nagu, kiongozi wangu ambaye amenisaidia na anaendelea kuniongoza vizuri sana katika utekelezaji wa majukumu yangu kama msaidizi wake mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea kutoa mchango, naomba kwanza niseme kwamba, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri mia kwa mia. *(Makofi)*

Naanza sasa kwa mchango uliotolewa na Mheshimiwa Herbert J. Mntangi, Mbunge wa Muheza, yeye alitaka kujua kwamba, Serikali inalishughulikiaje suala la kupatikana kwa majengo kwa ajili ya Mahakama ya Afrika na kuhusu suala la ufanisi wa wanasheria katika mikataba limezungumzwa sana na Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yake. Hali ya sasa imeanza kuboreshwa kwa kuwapatia mafunzo maalum, wanasheria wetu kuhusu mikataba. Waheshimiwa Wabunge, wameitaka mikataba iletwe Bungeni. Napenda kurejea mikataba inayopaswa kuletwa hapa Bungeni ni ile ambayo kwa masharti yake, inataka iridhiwe na Bunge kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e), kwa mfano Mkataba wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Mkataba wa *SADC*.

Aidha, suala hili ni sharti lizingatie mgawanyo wa madaraka. Shughuli hiyo kwa mujibu wa ibara ya nne ya Katiba ya utendaji, ambayo Serikali ndiyo inasaini Mikataba hii. Pili, Mikataba hii ina vipengele vyenye lengo la kulinda siri za kibiashara *(trade secrets)*, zinazowekwa humu ndani. Sasa itakuwa vigumu kuileta Mikataba hiyo ambayo idara moja ya Serikali imeingia na mtu binafsi, halafu ikasambazwa hadharani. Itakuwa mna-*breach* ule Mkataba wenyewe.

Ipo Mikataba ambayo inatakiwa kuletwa humu ndani kuridhiwa, nayo inafahamika na ni masharti ya Mikataba hiyo. Lakini Mikataba hii ya kibiashara baina ya Idara ya Serikali, labda Wizara fulani na shirika la nje, kuileta humu ndani, sasa ule uwajibikaji wa Serikali mbele ya Bunge unakuwaje, maana Bunge litakuwa limeshautazama Mkataba limeuridhia/ Sasa ikitokea Mkataba huo ukaonekana umepinda, nani ataiuliza Serikali?

Nafikiri Bunge lina wajibu wa kusubiri Serikali ifanye, ikikosea ama ikienda vibaya au ikienda vizuri pia waisifu. Lakini kuleta Mkataba hapa halafu ukasema Bunge sasa ridhieni, huo siyo Mkataba wa nchi kwa nchi, Mkataba wa kibiashara tu wa kawaida. Kwa hiyo, tunadhani si sawa kuleta Mkataba ndani ya Bunge uridhiwe, haikatazwi kwa Wabunge kuwa na Mikataba hiyo hata kidogo, lakini haiwezi kuletwa humu ndani ya Bunge. Bunge mna taratibu zenu za kudai vitu hivyo, kuna sheria zinazowaruhusu kudai vitu hivi, lakini si ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nazungumzia michango ambayo imetolewa na Mheshimiwa Eustace O. Katagira, yeye alizungumzia majengo ya Mahakama ya Wilaya Karagwe. Ni kweli jengo la Mahakama ya Wilaya ya Karagwe ni bovu na mpango wa Serikali ni kujenga jengo lingine badala ya kurikarabati lililopo. Pia alizungumzia vitendea kazi katika Mahakama za Mwanzo. Upatikanaji wa vitendea kazi kwenye mahakama hizo umepewa kipaumbele kwenye bajeti ya mwaka huu na mtaona katika jedwali kwenye bajeti tumeonesha haya.

Halafu Mheshimiwa Prof. Idris A. Mtulia na Mheshimiwa Prof. Raphael B. Mwalyosi, wote wamezungumzia juu ya ya uhaba wa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo. Ni kweli tuna uhaba mkubwa wa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo, sasa hivi tunahitaji mahakimu zaidi ya 397 ili tukamilishe kila mahakama kuwa na hakimu. Kwa hiyo, uhaba huo upo, lakini hatua zinachukuliwa na Serikali kutatua tatizo hili la uhaba wa mahakimu, tunawasomesha katika vyuo vyetu mbalimbali ili tuweze kuwagawa katika hizo sehemu ambazo zina uhaba. Uhaba huo tunaukubali kweli upo.

Mheshimiwa Prof. Idris A. Mtulia pia aliomba Wilaya ya Rufiji ipatiwe gari kwa ajili ya Mahakama ya Wilaya hiyo. Wilaya ya Rufiji ina Hakimu nafikiri anaitwa Bwana Muhidin Matitu. Aidha, Makao ya Wilaya hiyo ya Utete ambapo Hakimu huyo anaishi, kutokana na kesi zilizopo Kibiti, analazimika kutembelea Kibiti pia. Mahakama ya Tanzania, imeanzisha mpango wa kununua magari ya ukaguzi kwenye Mahakama zote za Wilaya kwa mwaka huu wa fedha Wilaya zote zitapata magari.

Mheshimiwa Dr. Luka J. Siyame, yeye amezungumzia ujenzi wa Mahakama ya Mwanzo Msangano na alizungumzia pia Wilaya ya Mbozi kupatiwa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo. Kweli kuna upungufu mkubwa wa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo, kama nilivyosema hapo mwanzo, mwaka huu wa fedha, tunakusudia kuajiri mahakimu 100 wa Mahakama za Mwanzo na Wilaya ya Mbozi ni moja ya Wilaya ambazo zitapatiwa Mahakimu. Nawapongeza wananchi wa Msangano kwa moyo wao, mahakama hiyo, itaingizwa kwenye mpango endelevu wa ujenzi na ukarabati wa majengo ya Mahakama za Mwanzo ili iweze kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, alitoa hoja kwamba, Mahakimu watende haki na kutochelewesha kesi. Naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa, kesi zinazoshughulikiwa na Mahakama, zinasikilizwa kwa mujibu wa Sheria. Aidha, ni azma ya Serikali kuwa kesi zote zisikilizwe na kutolewa maamuzi haraka iwezekanavyo na kwa haki na hii hasa ndiyo *motto* yetu katika Wizara, haki sawa kwa wote kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vifaa kwa ajili ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar, kwa kweli naona hili si suala la Bunge hili.

Mheshimiwa Aziza S. Ally na Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, walizungumzia kuhusu kupunguza kesi mahakamani na kuongeza kasi ya kusikiliza kesi. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, suala kuharakisha kesi ni la kisheria na si matakwa ya hakimu. Aidha, ili kuhakikisha kesi haichelewi, Serikali inaweka utaratibu wa kuwa na Kamati za kusukuma kesi kwenye ngazi za Wilaya, Mkoa, Kanda na Kitaifa. Wajumbe wa Kamati wanatoka Mahakama, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Polisi na Magereza. Kamati hizi zimefanya kazi, zimesaidia sana kupunguza msongamano wa kesi katika sehemu nyingi hususan Dar es Salaam, Mkoa wa Ruvuma na kwingine na sasa zinafanya kazi nchi nzima.

Mheshimiwa Stephen J. Galinoma, Mheshimiwa Job Y. Ndugai na Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, wao walizungumzia ujenzi na ukarabati wa majengo ya Mahakama za Mwanzo katika sehemu zao. Tunao mpango, Serikali kwa kupitia Mahakama ya Tanzania, imeanzisha mpango endelevu wa ujenzi na ukarabati wa majengo ya Mahakama za Mwanzo kwa awamu na ni azma ya Serikali kuwa, majengo yote ya Mahakama za Mwanzo yatajengwa au kukarabatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wachangiaji walikuwa wengi, nagusia suala ambalo alizungumzia Mheshimiwa Philip S. Marmo, alisema Mahakama za Wilaya na Mahakama za Mwanzo, zinasikiliza migogoro ya ardhi. Kwa sasa kisheria Mahakama za Mwanzo hazina uwezo wa kusikiliza migogoro ya ardhi. Kwa hiyo, Serikali inafuatilia matatizo na matukio yaliyojitokeza kwenye Wilaya ya Mbulu ili kujua kama Mahakama za Mwanzo za Wilaya hizo bado zinasikiliza migogoro ya ardhi. Uchunguzi huo utasaidia kubaini utendaji kazi wa Hakimu wa Wilaya na Hakimu wa Mamlaka ya Mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Juma Suleiman Nh'unga, alitaka mahakama zipatiwe vitendea kazi vya kisasa, pia alitaka tuongeze idadi ya majaji na

mahakimu. Serikali inafahamu umuhimu wa kuwa na vitendea kazi vya kisasa katika mahakama za ngazi zote. Serikali imekuwa ikinunua vitendea vya kisasa, zikiwemo kompyuta, kwa awamu kwa ajili ya mahakama mbalimbali. Katika mwaka huu wa fedha, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali imetenga fedha kwa ajili ya ununuzi huo. Aidha, kwa mwaka huu wa fedha, Mahakimu Wakazi 100 wataajiriwa na Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo 100 pia wanatarajiwa kuajiri.

Mheshimiwa Juma A. Njwayo, amesema Wilaya ya Tandahimba haina Mahakama ya Wilaya na pia alikuwa anataka Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo. Wilaya ya Tandahimba, imeshatoa kiwanja kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama ya Wilaya katika wilaya hiyo. Kati ya mahakimu 100 wa Mahakama za Mwanzo watakaoajiriwa, Wilaya ya Tandahimba itakuwa moja ya wilaya ambayo itapatiwa Mahakimu.

Mheshimiwa Siraju J. Kaboyonga, yeye alizungumza kuhusu hali duni ya majengo na samani za mahakama. Tunamshukuru Mheshimiwa Mbunge kwanza, kwa ushauri wake, Serikali inaendelea kuchukua hatua za kukabiliana matatizo ya uchakavu wa majengo na upatikanaji wa samani na hata magari.

Mheshimiwa Feteh Saad Mgeni, alitoa ushauri kuwa Serikali iongeze ujenzi wa mahakama hasa za mwanzo, pia tuajiri mahakamu zaidi kupunguza mlundikano wa kesi uliopo. Serikali inashukuru ushauri huu na tunamwahidi hali yetu ya kifedha itakapokuwa nzuri, tutaendelea kufanya ajira hizo na kujenga mahakama hizo. Tunamshukuru kwa ushauri wake huu.

Mheshimiwa Lucas L. Selelii, aliungumzia kuhusu mhasibu wa mahakama aliyeiba fedha za mirathi, Hazina imekwishatoa kibali cha kuandika fedha hizo kuwa ni upotevu. Mahakama imekwishaanza kuwalipa warithi wa mirathi hiyo, ni vyema walalamikaji wakawasiliana na Mahakama ya Wilaya ya Tabora ili walipwe fedha zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nitazungumzia hoja nne kama muda utaniruhusu. Hoja ya kwanza kwa ujumla ilikuwa ni uhaba na uchakavu wa majengo ya mahakama. Ilizungumzwa na wengi kama nilivyosema, Mheshimiwa Eustace O. Katagira, Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, Mheshimiwa Dr. Luka J. Siyame, Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Mheshimiwa Stephen J. Galinoma, Mheshimiwa Juma A. Njwayo, Mheshimiwa Siraju J. Kaboyonga na Mheshimiwa Feteh Saad Mgeni. Maelezo ni kama niliyoyatoa kwamba, kweli Wilaya zote hizo hazina mahakimu tuna mpango endelevu wa kupata mahakimu katika kila Wilaya.

Mheshimiwa Paul P. Kimiti, alizungumzia kuhusu adhabu ya kifo, alisema kwa vile watu wanapewa adhabu hiyo halafu haitekelezwi, akashauri kwamba, pengine adhabu hii ingefutwa. Mwenye mamlaka ya mwisho kuhusu adhabu ya kunyongwa ni Mheshimiwa Rais, kwa mujibu wa sheria za nchi na utaratibu wa utekelezaji wa adhabu ya kifo ni mrefu na unamhusisha Mheshimiwa Rais, ambaye sheria ndiyo imempa ridhaa hiyo. Suala la kufuta au kubakia kwa adhabu ya kifo ni jambo linalohitaji mjadala wa Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru Mheshimiwa Naibu Waziri. Nawaarifu tu Waheshimiwa Wabunge kwamba, hii baridi mnayoiona humu ndani, tumekwisha agiza kwamba irekebishwe kidogo. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naona bado nina bahati ya wewe kukalika Kiti na nina hakika hiyo ni baraka kubwa sana. Nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuhitimisha hoja niliyoiwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu leo asubuhi. Naomba nianze kwa kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote, waliochangia kwa kuzungumza humu Bungeni, wale waliochangia kwa maandishi leo hii na pia wale waliochangia kuhusu masuala mbalimbali yanayoigusa Wizara wakati walipokuwa wakizungumza na kujadili Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na pia katika Wizara nyingine.

Mingi ya michango hiyo imekuwa yenye kuiunga mkono hotuba yangu, niwezalo ni kuwashukuru sana nyote, ambao mmeunga mkono hoja ya Wizara yangu na nina hakika katika manufaa ya kuleta haki zaidi ndani ya nchi, hakutakuwa na mtafaruku zaidi na mtanipitishia fedha ambazo nimepangiwa na Serikali ili tuongeze haki ndani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nianze kwa kuwatambua Wabunge wote waliochangia. Walichangia kwa kuzungumza Bungeni ni kama ifuatavyo: Mheshimiwa Pindi H. Chana, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Fatma Mussa Maghimbi, Msemaji Mkuu wa Upinzani kwa Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa William H. Shellukindo, Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, dada yangu, Mheshimiwa Tatu M. Ntimizi, Mheshimiwa Anna M. Komu, Mheshimiwa Lucas L. Selelii, Mheshimiwa Gosbert B. Blandes, Mheshimiwa Juma Suleiman Nh’unga, Mheshimiwa Mwanne I. Mchemba, mtani wangu na mdogo wangu, ambaye nina hakika sasa anatambika ili hii hoja ipite, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mheshimiwa Johnson P. M. Mwanyika, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na hatimaye Mheshimiwa Mathias M. Chikawe, Naibu Waziri wa Katiba na Sheria. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa maandishi ni wengi kidogo na ni kama ifuatavyo: Mheshimiwa Eustace O. Katagira, Mheshimiwa Prof. Idris A. Mtulia, Mheshimiwa Aziza S. Ally, Mheshimiwa Dr. Lucas J. Siyame, Mheshimiwa Jacob D. Shibiliti, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Philip S. Marmo, Mheshimiwa Stephen J. Galinoma, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, Mheshimiwa John P. Lwanji, Mheshimiwa Juma A. Njwayo, Mheshimiwa Manju S. O. Msambya, Mheshimiwa Juma H. Killimbah, huyu tena ni mtani wangu mwingine, Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa na Mheshimiwa Siraju J. Kaboyonga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa Juma Suleiman Nh’unga, Mheshimiwa Feteh Saad Mgeni, Mheshimiwa Herbert J. Mntangi, Mheshimiwa Omar S.

Kwaangw', Mheshimiwa Lucy B. Msafiri, Mheshimiwa Ania S. Chaurembo, Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, Mheshimiwa Khadija Salum Shamis, Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Mheshimiwa Nuru A. Bafadhili, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Emmanuel J. Luhahula, Mheshimiwa Hemed Mohammed Hemed, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mheshimiwa James D. Lembeli, Mheshimiwa Sigifrid S. Ng'itu, Mheshimiwa Wilson M. Masilingi, Mheshimiwa Prof. Raphael B. Mwalyosi, Mheshimiwa Bujiku P. Sakila na Mheshimiwa Haji Juma Sereweji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa Clemence B. Lyamba, Mheshimiwa Martha M. Mlata, mtani mwingine, Mheshimiwa Damas P. Nakei, Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo, Mheshimiwa Dr. Zainabu A. Gama, Mheshimiwa Felister A. Bura, Mheshimiwa Dr. Harrisson G. Mwakyembe, Mheshimiwa Lucy T. Mayenga, Mheshimiwa Mkiwa A. Kimwanga, Mheshimiwa Felix N. Kijiko, Mheshimiwa William M. Ngeleja, Mheshimiwa Mohamed H. Missanga, mtani tena, Mheshimiwa Mwajuma Hassan Khamis, Mheshimiwa Anastazia J. Wambura, Mheshimiwa John M. Shibuda, Mheshimiwa Yono S. Kevela, Mheshimiwa Guido G. Sigonda, Mheshimiwa Dorah H. Mushi, Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya na Mheshimwa Zuleikha Yunus Haji. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge waliozungumzia masuala ya Wizara yangu wakati wakichangia hoja ya Wizara nyingine na Waziri Mkuu ni kama ifuatavyo: Mheshimiwa Juma Suleiman Nh'unga, Mheshimiwa Siraju J. Kaboyonga, Mheshimiwa Lucy T. Mayenga, Mheshimiwa John P. Lwanji, Mheshimiwa Charles M. Kajenge, Mheshimiwa Balozi Getrude I. Mongella, Mheshimiwa Dr. Harrisson G. Mwakyembe, Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, Mheshimiwa Suzan A. J. Lyimo, Mheshimiwa Meryce M. Emmanuel, Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa, Mheshimiwa Dr. Zainabu A. Gama, Mheshimiwa Hassan Rajabu Khatib, Mheshimwia Kheri Khatib Ameir, Mheshimiwa William J. Kusila, Mheshimiwa Mhonga S. Ruhwanya, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mheshimiwa Lazaro S. Nyalandu, Mheshimiwa Abdul J. Marombwa na Mheshimiwa Paul P. Kimiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, amenisaidia sana kutoa maelezo juu michango iliyotolewa kuhusu masuala ya kisheria. Napenda kukubaliana naye kwa michango yake, nilimwomba awe anamjibu Mbunge mmoja mmoja. Pia Naibu Waziri, amenisaidia sana katika kutoa maelezo kuhusu michango mingi iliyotolewa kuhusu masuala ya kisheria na pia yale ya kisheria yenye kuhitaji muono wa kisiasa, namshukuru na yeye amejaribu kupitia hoja za Wabunge mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati yetu ya Katiba, Sheria na Utawala, kwa mawazo yao mazuri sana, ambayo nina hakika tukiyazingatia, yataboresha sana utendaji ndani ya Wizara yangu na katika sekta nzima na nina waahidi kufanya hivyo. Ninaishukuru Kamati kwa ushirikiano wao wakati wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nianze kujielekeza katika maeneo ya jumla, lakini kabla sijafika huko, ninaomba vile vile niishukuru Kambi ya Upinzani, kupitia kwa Mheshimiwa Fatma Mussa Maghimbi, kwa maoni yao ambayo ni ya ushauri na sijaona mtafaruku wowote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema katika hotuba yangu, Sekta ya Sheria inagusa kila sekta katika jamii, kiuchumi, kijamii hata kisiasa. Shughuli zote za nchi zinahitaji na zinategemea sheria, taratibu za kisheria na utawala bora na pia juhudi za kupunguza umaskini, hutegemea sana amani, utulivu na uhakika wa usalama wa maisha na mali za wananchi. Upatikanaji wa mambo hayo ni lazima uendane na ustawi wa mazingira ya utawala, unaotokana na utawala wa sheria. Wakati mwingine amani na utulivu vikiwepo, baadhi ya watu huchukulia kuwa vipo kwa sababu viliumbwa kuwepo.

Napenda nieleze wazi kuwa, amani tuliyonayo ni kwa sababu ya kuenguka kwa misingi ya haki katika uongozi wa nchi yetu. Uendeshaji wa nchi bila kuzingatia misingi ya haki na sheria, waweza kusababisha kuvunjika kwa amani kama ilivyo katika nchi nyingine za Afrika. Amani haipo na hata shughuli zote za maendeleo zinakwama, hivyo umuhimu wa sekta hii katika jamii ni mkubwa sana na ndio maana, sijashangaa nilivyopata maoni mengi na wengine wakiwa wakali sana humu ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama pia nilivyoeleza katika hotuba yangu na kama baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walivyogusia, bajeti ya Wizara yetu bado ni ndogo ikilinganishwa na mahitaji. Hata hivyo, Serikali inalitambua hilo na ndio maana kila mwaka, imekuwa ikiipa kipaumbele Wizara kwa kuongeza fungu la bajeti kama tulivyoonesha katika jendwali namba moja la hotuba yangu na asubuhi nilieleza. Nawaombeni sana Waheshimiwa Wabunge, mpitishe makisio ya Wizara yangu kwa mwaka huu na bila shaka bajeti itaendelea kuongezeka kadiri mfuko wa Taifa utakavyoruhusu. Hata hivyo, napenda kusema kwamba, haki ambayo naizungumzia ni ile ambayo inazingatia haki kwa upande mmoja na wajibu kwa upande mwingine. Kama ilivyo kwa mpiga kasia, akipiga kasia lake upande mmoja tu wa mtumbwi wake, mtumbwi hautasogea kwenda mbele, bali utazunguka hapo hapo alipo. Hivyo, haki ninayoizungumzia ni ile inayozingatia kasia inayopigwa pande zote mbili za mtumbwi.

Sasa naomba kuchangia katika maoni yaliyotolewa na Wabunge kwa ujumla, kwani kama nilivyosema, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, wamejitahidi sana kugusia hoja ya kila Mbunge kwa kutaja majina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwanza, nitambue Wabunge katika maeneo ambayo wameyachangia kusudi wajue kwamba, hata kama nitatoa hoja kwa ujumla, nitakuwa nimewataja. Waliochangia kuhusu ucheleweshaji wa kesi ni pamoja na Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, Mheshimiwa Bujiku P. Sakila, Mheshimiwa Ania S. Chaurembo, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa Eustace O. Katagira na Mheshimiwa Dr. Luka J. Siyame.

Eneo la pili ambalo limechangiwa ni kuhusu uchakavu wa majengo, waliochangia ni Mheshimiwa Stephen J. Galinoma, Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Mheshimiwa Godfrey

W. Zambi, Mheshimwia Siraju J. Kaboyonga, Mheshimiwa Feteh Saad Mgeni, Mheshimiwa Lucy B. Msafiri na Mheshimiwa Mohamed H. Missanga.

Kuhusu nidhamu na uwajibikaji, waliochangia ni kuhusu nidhamu na uwajibikaji ndani ya sekta hususan kwenye mahakama, ni pamoja na Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, Mheshimiwa Tatu M. Ntimizi, Mheshimiwa Suzan A. J. Lyimo, Mheshimiwa Bujiku P. Sakila na Mheshimiwa Nuru A. Bafadhili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wengine waliendelea kuchangia juu ya upungufu wa Majaji na Mahakimu, nao ni pamoja na Mheshimiwa Juma Suleiman Nh'unga, Mheshimiwa Sigifrid S. Ng'itu, Mheshimiwa Juma A. Njwayo, Mheshimiwa Mohamed H. Missanga, Mheshimiwa Jacob D. Shibiliti, Mheshimiwa Hemed Mohammed Hemed, Mheshimiwa Dr. Luka J. Siyame, Mheshimiwa James D. Lembeli na Mheshimiwa Jacob D. Shibiliti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia kuhusu uhaba wa maslahi, vitendea kazi, nyumba bora na mazingira mazuri kwa watumishi wa kada ya sheria ni pamoja na Mheshimiwa Siraju J. Kaboyonga, Mheshimiwa Prof. Idris A. Mtulia, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis na Mheshimiwa Riziki Omar Juma.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, samahani kidogo, dakika moja tu kama unaweza kukaa, nina tangazo kidogo.

Waheshimiwa Wabunge, nafurahi kulitangazia Bunge kwamba, Mheshimiwa Spika, amesharudi safari yake ya Arusha. Kwa hiyo, nachukua fursa hii sasa kumkabidhi rasmi shughuli inayoendelea. *(Makofi)*

*(Hapa Spika, Mheshimiwa Samuel J. Sitta - Alikalia Kiti)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana. Mnasalimiwa si tu kutoka Arusha, ni Oldonyo Sambu. Mheshimiwa Waziri, tafadhali endelea.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwamba umewahi hoja yangu, kwa hiyo, leo nimebarikiwa kuwa na Mwenyekiti na wewe Mheshimiwa Spika. Lakini pole kwa safari.

Nilikuwa nawaelezea Waheshimiwa Wabunge, ambao walichangia kuhusu uhaba wa maslahi, vitendea kazi, nyumba bora na mazingira mazuri kwa watumishi wa kada ya Sheria na katika Mahakama.

Hao ni pamoja na Mheshimiwa Siraju J. Kaboyonga, Mheshimiwa Prof. Idris A. Mtulia, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Mohamed H. Missanga, Mheshimiwa Mwajuma Hassan Khamis, Mheshimiwa Eustace O. Katagira, Mheshimiwa Juma Suleiman Nh'unga, Mheshimiwa Prof. Raphael B. Mwalyosi, Mheshimiwa Prof. Idris Ali Mtulia, Mheshimiwa Dr.

Wilbrod P. Slaa, Mheshimiwa Ruth B. Msafiri, Mheshimiwa Ania S. Chaurembo, Mheshimiwa Bujiku P. Sakila na Mheshimiwa Mkiwa A. Kimwanga. *(Makofi)*

Kuhusu marekebisho ya Sheria aliyechangia ni Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, naomba nijibu hoja hizi kwa ujumla na ninaomba kumhakikishia Mheshimiwa Herbert J. Mntangi kama alivyomhakikishia Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba, Serikali inashughulikia suala la kupatikana kwa majengo kwa ajili ya Mahakama ya Afrika. Kwanza ni heshima kuwa na Mahakama na kwa hiyo hatutasita kupata nyumba ambayo inastahili hadhi ya Mahakama hiyo.

Mheshimiwa Spika, napenda kulielezea Bunge lako Tukufu kwamba, ni kweli mazingira ambapo Mahakama yetu inafanyia kazi si mazuri na kwa hiyo, imechangia katika mambo mengine ambayo kwa kweli hayapaswi kuyasemea Mahakama. Pamoja na matatizo hayo ni kuwa na nafasi ya majengo finyu kwa ngazi zote za Mahakama. Serikali inajitahidi kupitia fedha zake za maboresho, pamoja na kutenga fedha kila mwaka katika bajeti yake ya Wizara ya Katiba na Sheria, kujenga majengo kwa ajili ya Mahakama za Mwanzo hadi Mahakama ya Rufaa.

Kuhusu vitendea kazi, ni kweli kabisa kwa mfano, Majaji wetu na Mahakimu wanalalamikiwa sana kwamba, wanachelewesha kesi kwa sababu kwanza wao ni wachache sana, kwa ngazi zote Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufaa. Lakini leo nikiwasilisha hotuba yangu, nimesema kwamba, Mheshimiwa Rais ametoa kibali cha kuajiri Majaji wengine 20. Nina hakika ajira ya hao Majaji itapelekea kesi kwenda kwa kasi zaidi na kuhusu vitendea kazi, tutajitahidi sana kama ilivyoelezwa na Naibu Waziri, pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Tutaboresha vitendea kazi ikiwemo vilevile na vyombo vya kisasa vya kuweza kurekodi uendeshaji wa kesi ili Hakimu asipate shida ya kuandika.

Wanaandika *pages* nyingi sana na wakati mwingine kwenda kurejea inakuwa kazi kubwa na mkono unachoka. Majaji wetu wengi sana wamekuwa wakijitahidi, lakini kwa sababu ukilinganisha idadi yao na vitendea kazi na kesi walizonazo, wamekuwa wakikumbwa na matatizo ya kuambiwa kwamba, wanakula rushwa, lakini kumbe sababu ni mazingira wanamofanyia kazi na uchache wao, ndiyo unapelekea kwamba wanaonekana kwamba hawatendi kazi zao kama inavyostahili. Nina hakika tutakapoboresha vitendea kazi na watakapokuwa na maeneo mazuri ya kufanyia kazi na idadi yao kuongezeka, hata hayo mengine yanayosemwa yatafutika moja baada ya jingine.

Kuhusu maslahi, ni kweli Sekta ya Sheria imekumbwa na maslahi madogo, ukilinganisha na wanasheria wengine, ambao wako kwenye soko na wengi wangependa kuwa wanasheria wa kujitegemea, kwa sababu kule kuna maslahi makubwa. Kwa hiyo, wale wanaofanya kazi Serikalini, kwa hakika wamejitolea na inataka moyo na inataka kujituma sana. Serikali itajitahidi sana kutambua juhudi ya wanasheria wetu, ambao

bado wamebakia Serikalini na kila mwaka inapowezekana, itaongeza mishahara yao ili hali zao na maslahi yao yawe bora zaidi.

Mheshimiwa Spika, nina hakika, maboresho ndani ya Sekta ya Sheria yatasaidia sana katika kuboresha utaalam wa watumishi ndani ya Sekta nzima, wakiwemo Mahakimu na Wanasheria wetu, ambao wanafanya kazi katika Mazingira magumu na kwa utaalamu mdogo, ukilinganisha na kazi ambazo wanazifanya na wale ambao wako nje ya Serikali.

Kuhusu msongamano wa Magereza, tumejaribu kufanya kila linalowezekana, kupitia magereza na kwa mfano katika Mkoa wa Dar es Salaam au Kanda ya Dar es Salaam, Jaji Mfawidhi na wale wote wanaohusika, walitembelea magereza yetu na wakajaribu kubuni namna ya kupunguza au kuharakisha kesi, kusudi mlundikano upungue. Kwa hakika ulipungua na juhudi hizo sasa zinatapakaa katika nchi nzima, nina hakika pamoja na kuongeza idadi ya Mahakimu na Majaji, sasa mlundikano utaanza kupungua.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba niliongelee suala ambalo Waheshimiwa Wabunge waliliongelea, nalo linahusu Mahakama ya Kadhi.

Mheshimiwa Spika, suala la Mahakama ya Kadhi, liko ndani ya Ilani ya Uchaguzi na kwa sababu liko ndani ya Ilani ya Uchaguzi, kwa hakika lazima litafanyiwa kazi, hilo ni la uhakika. Serikali inatambua mchango wa Tume ya Bunge, kuhusu uanzishwaji wa Mahakama ya Kadhi, linaloendelea hivi sasa ni kuongeza wigo au kupanua wigo wa mapokeo ya maoni zaidi ya kurutubisha suala linalohusu uanzishwaji wa Mahakama ya Kadhi na mimi ninawahakikishia kwamba, mchakato huu utaendelea kwa manufaa ya wale wote wanaohusika na kwa manufaa ya Taifa letu. Pale ambapo tutafikia mahali ambapo sasa tutafikiri kwamba, linaweza kuja hapa Bungeni, hatutasita kufanya hivyo, lakini kila jambo zuri Waheshimiwa Wabunge, linahitaji kufanyiwa kazi na linahitaji subira, ninaomba subira yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sheria 40 za Tume ya Nyalali na ambazo zimepitiwa na Tume ya Kurekebisha Sheria na mapendekezo yote yamefanyiwa kazi na kuletwa Serikalini. Ni kweli kabisa kuna Sheria 28, ambazo zimefanyiwa marekebisho na marekebisho hayo yametokana na mapendekezo ya Tume ya Kurekebisha Sheria. Sheria nyingine zilizobaki ni zile ambazo zinaihusu Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba niongelee suala ambalo akina mama wenzangu, wameliongelea kwa uchungu, nalo linanihusu mimi. Wabunge wengine wasifikiri kwamba, *we are more sentimental,* lakini nitajaribu kujielekeza kwenye maudhui ya suala lenyewe, ni Sheria ya Ndoa, Mirathi, Sheria ya Watoto, pamoja na Sheria ya Matunzo ya Watoto.

Wizara yangu ikishirikiana na Wizara yetu ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na tukishirikiana vilevile na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, kwa sababu nao

wana jukumu hapa, tutaendeleza mchakato huu na kuhakikisha kwamba, tunaleta sheria mpya au kurekebisha ili kurekebisha hali ilivyo hivi sasa. *(Makofi)*

Nina hakika kwamba, sote hata kama ni kina baba, wanawahusu watoto, wasingetaka mama zao, dada zao au watoto wao wa kike wapate tabu. Sheria hizi zinahusu watu wote kwa mfano, Sheria ya Mirathi haihusu wanawake peke yake, inahusu watoto ambao ni wa baba vilevile na inahusu watoto wa kiume vilevile. Kwa hiyo, kwa hakika itaendeleza mchakato huo kwa kasi na ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, wakati ambapo alikuwa anapongezwa na Jumuiya ya Wanawake Tanzania, alisema na aliudhihirishia umma wa Watanzania, wakiwemo wanawake kwamba, Sheria hizi nilishawahi kuzifikisha kwenye Baraza la Mawaziri na mchakato wake utaongezewa kasi, ari na nguvu mpya.

Mheshimiwa Spika, sasa nakwenda kwenye suala ambalo Ndugu yangu, Mheshimiwa Lucas L. Selelii, anasema ameshikilia shilingi, lakini nina hakika atanihurumia baada ya kutoa maelezo ambayo nina hakika yatamridhisha, nalo ni suala la Sungusungu.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka kwamba, jana Waziri wa Usalama wa Raia, alisema kwamba, wanafikiria kuanzisha Polisi Jamii na mimi nina hakika tumepata uzoefu kutokana na vikundi hivi kama vya Sungusungu, ambavyo vitapelekea kuboresha hili suala la Polisi Jamii. Kwa hiyo, nashukuru sana maeneo yale ambayo yalikuwa na Sungusungu. Napenda kusema kwamba, palipo na utata ama tuhuma dhidi ya usungusungu, waliokaa mahabusu muda mrefu, kwa vile tuna Kamati za kusukuma kesi, naomba Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wanaohusika, wapeleke malalamiko ya wananchi ili yahakikiwe na Kamati hizo na ikibidi, wengine tunaohusika tujulishwe ili tuoe namna ya kuharakisha na Sungusungu hawa wasiendelee kukaa mahabusu bali watendewe haki.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kubambikizwa kesi wafugaji. Wanaobambikizwa kesi ni wengi sana, si wafugaji pekee, lakini kwa sababu mimi natoka kwenye jamii ya wafugaji, ninajua wafugaji wengi kwa sababu wamejielekeza zaidi kwenye ufugaji, wengi hawakwenda shule, lakini sasa wanakwenda shule na kwa hiyo, unaweza ukakuta kwamba wengi hawaelewi lugha ya Kiswahili na ikawa ni rahisi kueleweka kwamba wamebambikizwa kesi, kumbe wao wameshindwa kujieleza vizuri.

Vyovyote vile itakavyokuwa, suala la kubambikizwa kesi, siyo jambo zuri, naomba nitoe rai kwa Waheshimiwa Wabunge, wasingojee vikao hivi vya Bajeti au vya Bunge, bali wajaribu kupeleka malalamiko hayo panapohusika na katika Wizara yetu ili tuone namna ya kurekebisha hali hii ya kubambikizwa kesi wananchi wetu na siyo wafugaji tu, hata wale wengine ambao wanabambikizwa kesi. Si jambo jema na kwa hiyo, tunaomba tushirikiane tena kwa ile ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya, kurekebisha hayo mambo kwa kushirikiana na Waheshimiwa Wabunge. Naomba kuwaeleza kwamba, tuko kwenye jahazi moja. Mimi sitasita kushirikiana nanyi na kama mimi niko tayari kushirikiana nanyi, basi naomba nanyi mshirikiane nami.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mikataba ya Sheria, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ambaye ni Mwanasheria, amelielezea suala hili vizuri na vilevile Naibu Waziri wangu alilirudia. Kwa kweli nakubaliana nao kwamba, lazima kuwe na mgawanyo wa madaraka. Nafikiri Waheshimiwa Wabunge, hatutakubali madaraka yetu ya Bunge yachukuliwe na mtu mwingine, hatutakubali na tutalalamika. Vilevile Mahakama hawatakubali madaraka yao yanyang'anywe na Mhimili mwingine na kwa hiyo *Executive* nayo ingetaka ifanye majukumu yale ambayo ni ya kwake, kwa madaraka iliyopewa ili watakapokuwa wamekosea mahali au watakapokuwa wameenda kwa bahati mbaya mrama, basi kuwe na mwingine ambaye atahoji. Kwa sababu utakapokuwa umeingia jikoni, haitakuwa rahisi kuhoji kazi ambayo umeifanya wewe.

Mheshimiwa Spika, naamini kwamba, kama kuna Mkataba wowote ambao una utata, Bunge lako Tukufu likitaka kuupitia, sidhani katika madhumuni ya kuhoji kama *Executive* itakataa, lakini kuna utaratibu ambao utafuatwa. Kwa sababu kwa misingi ya biashara, biashara inayofanywa na Tanzania inafanywa na nchi nyingine, sasa tukimwaga mchele mbele ya kuku wengi, itakuwaje? Kwa hiyo, ninarudia tena kusema kwamba, kuna watu wanasema hapa siyo hadhara, lakini mikutano yetu inatangazwa kwa vyovyote vile ama siyo, lakini kwa utaratibu ambao unakubalika, kama kuna jambo ambalo ni la maslahi ya Taifa, sidhani kama Serikali ama *Executive,* itakataa Bunge lisiangalie hilo jambo. Kwa hiyo, naomba tuendelee kushirikiana, *Executive* nayo inataka maslahi ya Taifa yazingatiwe na maslahi ya Taifa kupitia Mikataba hii itazingatiwa.

Katika hotuba yangu nilieleza kwamba, kulikuwa na mapungufu ambayo sasa tunayaangalia kwa makini sana ili tuyaondoe kwa upande wa Wanasheria na Wataalamu wengine wanaohusika katika Sekta zinazohusika mathalani Madini, *TANESCO* na kwingine, ili tusirudie yaliyotokea hapo awali.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba niende walikoongelea Mikataba ile ya kuridhia. Hili ni jukumu la Serikali kuleta Mikataba ya kuridhia. Serikali itaongeza kasi ya kuangalia Mikataba hiyo na hii iletwe kwa wakati muafaka katika Bunge lako kwa kuridhia na mimi nina hakika ili tuheshimike mbele ya ulimwengu ni budi tuweze kuleta Mikataba hiyo kuridhia ili na sisi tusiwe kisiwa ndani ya Ulimwengu huu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Ripoti ya Jaji Nyalali. Ripoti iliibua matatizo yanayokwamisha utoaji wa haki na ripoti hiyo ndiyo msingi wa kuwepo Programu ya Kuboresha Sekta ya Sheria, ambapo kuna maeneo mengi ambayo niliyaelezea katika hotuba yangu, lakini kwa kupitia maboresho haya ya Sekta ya Sheria, nina hakika tutaboresha majengo ya Mahakama na maeneo mengine ya Sekta ya Sheria, tutaongeza idadi ya watumishi wakiwemo Majaji na Mahakimu, tutaongeza utalaamu na tutaboresha vitendea kazi. Kwa sasa ni Jaji Nyalali ni Marehemu. Ningerudia tena kutambua juhudi za Marehemu Jaji Nyalali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sheria ya Kujamiiana, sasa hili ni lingine la akina mama, yaani hili ni letu, lakini nina hakika makosa ya kujamiiana hayaathiri akina mama peke yao, bali yanaathiri na wanaume. Suala la ubakaji ni nyeti, tumepokea lawama kutoka kwa watu wengi, wapo wanaodhani kuwa Sheria ni kali sana na wapo ambao

wanadhani kuwa Sheria haitendi haki, labda inatoa hukumu ambayo si kali sana, lakini ambalo nalijua na ambalo pengine linahusu pande zote mbili ni pale ambapo Sheria hii, imewanyima Mahakimu uhuru wa kutoa adhabu kulingana na makosa. Nikisema hivyo, siyo tu kwamba imenyima uhuru wa kutoa adhabu hiyo ya chini, imewanyima Mahakimu vilevile kutoa adhabu ya juu kulingana na makosa yenyewe. Sasa ninaomba nitambue kwamba pengine kuna sababu ya kurejea Sheria hii ili kwanza, tuwape Mahakimu uhuru zaidi, kama kosa ni kubwa zaidi ya ile adhabu ya miaka 30 basi wawe na uhuru wa kutoa adhabu kubwa zaidi. Lakini kama kosa ni dogo, kama la kukonyeza, basi na wao waweze kutoa hukumu ambayo inalingana na kukonyeza na siyo kubaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, akina mama wote wanatambua kwamba, wakati Sheria hii ya kujamiiana inaletwa hapa Bungeni, mimi kwa wakati ule ndiyo niliyekuwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Wanawake na Watoto na nilishabikia sana, nikaambiwa kwamba, pengine ni *mjahidina* wa hii Sheria. Nawahakikishia kwamba, sisi sote tunataka wabakaji wapate adhabu stahili, sisi wote tunataka wale wanaobaka watoto wadogo kwa imani ambazo mimi sizielewi, wapate adhabu wanayostahili, sasa msinihukumu kwa hili na mimi mwanangu hule wa kiume akitaka kumkonyeza yule anayempenda, naye asipewe adhabu ya miaka 30 na watoto wenu vilevile. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ninachoomba kwenu ninyi ni kwamba, ni kweli Sheria inataka rejea ili Mahakimu wapewe uhuru wa kuweza kuona kosa hili linastahili adhabu hii na ili tusing'ang'anie kwenye adhabu ya miaka 30 peke yake, inaweza kwenda juu au kwenda chini. Nafikiri mtakubaliana na mimi na nasema kwamba, kwa kweli mimi sina sululu na wabakaji na nilijibu swali ndani ya Bunge hili kwamba, pengine haitoshi tu adhabu kwa sababu nataka niwaambie kwamba, wahalifu walio wengi magereza sasa hivi ni wa makosa haya. Kwa hiyo, ninaomba wazazi wote wajaribu kuwalea watoto, waone ubakaji ni kitu kibaya na kinachotoa utu wa binadamu.

Lakini zaidi ya hivyo, tuendelee na elimu, tuwe jamii ambayo inaheshimika na jamii ambayo inajali utu wa binadamu. Nina hakika jamii ikikubali hili, hatutakuwa na wabakaji na kwa sababu tumewafunga watu miaka 30, bado kesi zinaongezeka, nina hakika tunahitaji kazi kubwa zaidi katika eneo hilo.

Sasa kuhusu ukeketaji, Waheshimiwa Wabunge, mimi ni Mbunge wa Jimbo la Hanang na mengine ni magumu sana kuyaongea kuhusu ukeketaji. Lakini ukeketaji ni *operation*, ambayo haina umuhimu na kungekuwa na sababu ya ukeketaji kungekuwa na hospitali za kupeleka watu kukeketwa. Sasa nitakaloweza kusema ni kwamba, Sheria ya Makosa ya Kujamiiana vilevile imetoa adhabu ya makosa kama haya ya ukeketaji, lakini nasema pengine elimu ni bora zaidi, kwa sababu tutakuwa na jela ngapi za kupeleka watu ambao wanaamini kukeketa ni muhimu? Mimi nitakuwa mstari wa mbele, kwa kusaidiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto katika kueneza elimu hii, ili wazee ambao elimu yao ilikuwa ndogo, waache shughuli hiyo ya ukeketaji na tuwape shughuli nyingine za kiuchumi waweze kuendesha maisha yao.

Mheshimiwa Zuleikha Yunus Haji, aliongelea juu ya Mfuko wa Walemavu na akasema Mfuko huo upo na kwa sababu haupo katika Wizara ya Katiba na Sheria,

utakuwepo kwenye Wizara nyingine na kwa hiyo ni suala la Serikali, nitalifuatilia. Tutasaidiana na Serikali kuona kwamba, Mfuko huu kama upo, basi ufanye kazi ambayo ulistahili kufanya na tuufufue na tuuchangamkie, kwa sababu walemavu wetu wanavyoteseka, sisi kama nchi na kama jamii, tunapoteza heshima tunayostahili. Nakuahidi Mheshimiwa Zuleikha Yunus Haji, mimi binafsi nitalifuatilia lakini kama pia Waziri wa Katiba na Sheria, vilevile ndani ya Serikali nitajaribu kuona Wizara ambazo zinahusika ili walemavu waweze kutendewa haki wanayostahili.

Mheshimiwa Spika, jana tulikwenda katika Gereza la Isanga na kulikuwa na malalamiko kwamba, kulikuwa na Wamasai watatu, ambao walikamatwa kule Ngorongoro au Serengeti, wakahukumiwa kwa sababu hawajui Kiswahili fasaha na kwa hiyo watakuwa wamehukumiwa sijui ni kwa bahati mbaya. Lakini tulikwenda na Mbunge wa Ngorongoro, ambaye ndiye anahusika na watu hawa, wakatoa maelezo yao wakasema walikata rufaa nje ya muda wa rufaa na kwa hiyo, wameomba sasa wasikilizwe rufaa yao nje ya muda wa rufaa. Kama kibali kitatolewa, lakini nawaomba wanaohusika wafuatilie, mahakama huwa haziendi kutafuta kesi mpaka wapate watu ambao wanazipeleka hizo kesi. Kwa hiyo, nawaomba wale wanaohusika, wajaribu kufuatilia na mimi mwenyewe vilevile pamoja na Mbunge, tutajitahidi kufanya hivyo.

Lakini vilevile Mheshimiwa Mbunge alikuwa na kesi nyingine ya uvunjaji wa Haki za Binadamu katika Mbuga ya Ngorongoro au Hifadhi ya Ngorongoro kwamba, kuna watu ambao walijikuta wako kwenye Mbuga, sasa wanaondolewa na kwa hivyo mali zao labda zimepotea na huo ni uvunjaji wa Haki za Binadamu. Suala hili nitalifuatilia, kwa sasa sina taarifa kamili na nitakuwa sitendi haki, kujibu mambo ambayo sina taarifa nayo.

Mheshimiwa Spika, pale nilipoanza kutoa shukrani, nilisema nashukuru sana upande wa Upinzani kwa ushirikiano wao na kwamba mimi nachukulia Upinzani kama kioo, asubuhi ukiondoka nyumbani inabidi uangalie uso ili uone kama uso wako ni mzuri. Kwa hiyo, Upinzani unatusaidia na Upinzani ni suala ambalo limekubalika ndani ya Taifa letu. Kwa hiyo, naomba nigusie masuala ambayo walikuwa wameyaleta kupitia hotuba yao, lakini kama muda hautatosha, watanisamehe kwa sababu mengi ambayo yamo humu vilevile nimeyaongelea kwa ujumla katika hoja zile za ujumla.

Wapinzani waliongea kuhusu kuongeza Kanda za Mahakama Kuu kutoka 11. Nataka niwaeleze kwamba, kwa sasa kuna Kanda 13 na bado pengine kama kutakuwa na mahitaji Kanda zitaongezeka. Kama nilivyosema katika hotuba, lengo ni kuwa na Mahakama Kuu kila Mkoa. Kwa mwaka huu wa fedha, ujenzi wa Mahakama Kuu Shinyanga, utaaza wakati ule wa Kagera unakamilika. *(Makofi)*

Wameongelea vilevile uhaba wa Majaji na Mahakimu, unaosababisha kuchelewa kuamuliwa kwa kesi. Kama nilivyoeleza katika hotuba na katika maelezo yangu, Wizara inalitambua tatizo la upungufu wa Mahakimu na Majaji na imekuwa ikichukua hatua za kuongeza idadi yao kutegemea na upatikanaji wa nafasi za kufanyia kazi na vitendea kazi. Vilevile wameongelea kupatiwa mafunzo Watumishi wa Idara ya Mahakama, hususan Mahakimu na Makarani. Nataka niwaambie kwamba, Lushoto iko pale kwa ajili

hiyo na tutajitahidi kuwapeleka katika vyuo vingine ili waweze kutekeleza wajibu wao ipasavyo.

Sasa kuhusu vitabu vya Sheria kusambazwa katika Mahakama, hadi sasa Sheria mbalimbali muhimu zilizopo katika Toleo la Sheria zilizofanyiwa urekebu hadi mwaka 2000, zimesambazwa karibu katika Mahakama zote nchini. Pia kwa msaada wa *USA,* tuliendesha semina kwa Mahakimu wote wa Mahakama za Mwanzo nchini na wakati wa semina hizo Mahakimu wote hao waligawiwa Sheria zote muhimu, zinazotumika katika Mahakama hizo.

Wapinzani waliongelea vilevile utaratibu wa usuluhishi muafaka au *ADR* kutotumika katika Mahakama zetu. Utaratibu huu wa *ADR* kwa sasa unatumika katika Mahakama za ngazi zote, isipokuwa Mahakama za Mwanzo. Napenda kulihakikishia Bunge hili Tukufu kwamba, utaratibu huo umeonesha mafanikio makubwa katika kupunguza kesi za madai. Kila kesi ni lazima ipitie utaratibu huu na hivyo hakuna siku maalum ya kufanya usuluhishi kama ilivyokuwa hapo awali.

Hoja nyingine ilikuwa inahusu Kamati za Kusukuma Mashauri au *Case Flow Management.* Kamati hizi ambazo hukaa angalau mara nne kwa mwaka, zimeonesha vilevile mafanikio makubwa katika kuharakisha upelelezi wa kesi na usikilizaji wa kesi zilizokwama, kwa sababu moja ama nyingine. Baada ya Kamati ya Kitaifa kuundwa na kuanza kufanya kazi mwaka 2005, sasa Kamati hizi zinafanya kazi kuanzia ngazi ya Taifa hadi Wilaya.

Mheshimiwa Spika, Wapinzania vilevile walileta suala la kukamilisha upelelezi wa kesi ndani ya siku 60 kutotumika. Suala hili ni la kisheria na limekuwa likitumika kikamilifu na kesi nyingi tu zimeweza kufutwa chini ya kifungu cha Sheria kinachohusika, yaani kifungu cha 225 cha Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai ya Mwaka 1995.

Wapinzani vilevile walisema Mahakama imekuwa inachelewa kutoa nakala za hukumu kwa wakati. Mahakama imekuwa ikijitahidi kuboresha utendaji wake wa kununua vifaa na vitendea kazi, ikiwa ni pamoja na kompyuta kama ilivyoelezwa, nina hakika hali bado si nzuri sana lakini kwa vyovyote vile imeboreka.

Mheshimiwa Spika, ufafanuzi kuhusu suala la *Legal Sector Reform,* suala hili limezungumziwa kwa kirefu katika hotuba yangu. Tumekwisha kuingia katika makubaliano ya awali na wafadhili na kwa hiyo, maboresho ya Sekta ya Sheria yameanza.

Pili, tuna Mradi wa MKUMBITA, ambao utaboresha uendeshaji wa mashauri ya biashara, tunategemea programu hii itaboresha maeneo mengi ya Sekta ya Sheria. Kwa hiyo, kwa maelezo zaidi, naomba Mheshimiwa Fatma Mussa Maghimbi au Kambi ya Upinzani, ikitaka tunaweza tukawapa bila matatizo yoyote.

Kuhusu Toleo la Sheria zilizofanyiwa urekebu, Toleo 2002 kuchapishwa Afrika Kusini na siyo kwa Mpiga Mchapa Mkuu wa Serikali. Shughuli ya uchapishaji ni kweli ilifanywa kwa msaada wa wafadhili, chini ya utaratibu wa *tender* ya Kimataifa na Kampuni ya *Duty* ya Afrika Kusini, ndiyo iliyoshinda *tender* hiyo. Mimi ni mmoja wa wale ambao naamini, kufanya kazi zetu au shughuli zetu za kibiashara humu nchini ni vizuri. Naomba basi, makampuni yetu na vyombo vingine vya biashara, vichangamkie *tender* hizo kwa sababu ndiyo utaratibu wa siku hizi. Sasa kama haku-*tender,* inakuwa vigumu sana hasa inapohusu fedha za wafadhili. Walisema kwamba, kuna makosa mengi, lakini mimi nasema tumepiga hatua. Tuna hizo sheria ambazo zimewekwa pamoja, sasa kama kuna makosa ya *typing* au kuna makosa madogo madogo, hilo tutalifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ununuzi wa Jengo la Ubalozi wa Tanzania nchini Italy na madai ya kughushi na wizi wa fedha. Suala hili lipo katika hatua za uchunguzi na hivyo nitawasiliana na Wizara inayohusika. Nina hakika wakati muafaka utakapofika, wataeleza. Kwa kweli hili si la Sekta ya Sheria au la Mahakama, kwa sababu bado halijafika Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uimarishaji wa Ofisi ya Kabidhi Wasii Mkuu, napenda kuwaambia kwamba, sasa Ofisi ya Kabidhi Wasii imekuwa ni Wakala na kwa sababu ni Wakala itajitegemea zaidi na ipewe rasilimali zaidi za kuboresha shughuli zake. Mimi nakubaliana kwamba, uandikishaji wa watoto wetu kwa suala la uraia na mahitaji mengine ni muhimu sana na najua katika maeneo mengine, ambayo yana majukumu ya Wakala huu, yatakuwa yanaboreka. Kwa hiyo na mimi pamoja na kwamba, sasa Wakala utajitegemea, tutaupa ushirikiano wa karibu sana ili uweze kutenda kazi zake kwa ubora zaidi kuliko ilivyo Ofisi ya Kabidhi Wasii.

Mheshimiwa Spika, nimeongelea suala la makosa ya uchapishaji katika Toleo la Sheria kwa hiyo, sina sababu ya kulirudia.

Mheshimiwa Spika, uandaaji wa sheria katika lugha ya Kiingereza, ambazo baadhi ya Watanzania hawazielewi. Wizara inatambua umuhimu wa kuandika sheria za nchi yetu kwa lugha ya Kiswahili, ambayo ndiyo lugha ya Taifa. Sheria zetu zinaandaliwa kwa Kiingereza na zinapaswa kutafsiriwa kwa Kiswahili. Serikali itaendelea kutafsiri sheria kama tulivyosema, tumetafsiri tayari Sheria ya Mazingira na Sheria ya Ardhi. Tutaendelea na juhudi hiyo ili wananchi wetu wazijue sheria hizi na wazitumie ili kupata haki zao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuridhia na kutoa taarifa kuhusu utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa ya Haki za Binadamu, hili nimelizungumzia katika hotuba yangu na tunalitekeleza na ninaahidi tutaendelea kulitekeleza. Tutaongeza jitihada katika kutekeleza suala hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuridhia Mikataba mbalimbali, tutaendelea kutafakari Mikataba mbalimbali na kuridhia yote ambayo ina manufaa kwa nchi yetu na baada ya kufanya maandalizi yote muhimu yanayohitajika kabla ya kuridhiwa.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mapendekezo ya Ripoti ya Tume ya Kurekebisha Sheria, nimeeleza kwamba, tumepokea mapendekezo na bado tunaendelea kupokea mapendekezo ya Tume ya Kurekebisha Sheria. Katika hotuba yangu, nimeeleza ni mapendekezo yapi ambayo tumeyapokea, lakini hizi *dual citizenship* tunazifanyia kazi na yale mengine yote tunayafanyia kazi. Ila ninachoweza kuahidi ni kwamba, tutajitihadi kuongeza kasi ili tusicheleweshe sana mapendekezo haya na yasije yakapitwa na wakati.

Mheshimiwa Spika, lingine lilihusu kwa nini Sheria inamlinda mwanamke hadi anapofikia umri wa miaka 18. Hili lililetwa na rafiki yangu Mheshimiwa Mwanne I. Mchemba. Ninachoweza kusema ni kwamba, nafikiri wanawake wote wanalindwa na sheria, lakini ni kweli wale walio chini ya umri wa miaka 18 ni watoto na watoto wanahitaji uangalizi wa kila mtu ikiwemo sheria. Kwa hiyo, ninachoweza kusema ni kwamba, sheria zetu zinaangalia watu wote, lakini watoto wanapewa uangalizi zaidi kwa sababu wao wenyewe hawawezi kujilinda.

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa kuheshimu maamuzi ya Tume ya Nyamuma, Serikali ilianzisha chombo hiki kwa nia thabiti na hakina nia ya kupuuza mapendekezo yake. Yapo mapendekezo mengi ambayo yamewahi kutolewa na Tume ya Haki za Binadamu, yakatekelezwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Nyamuma, Serikali ilikwishalitolea maelezo kwa kirefu hapo awali. Aidha, suala hili hivi sasa liko Mahakamani na mimi nafikiri hairuhusiwi kulizungumzia. Lakini ninachoweza kusema ni kwamba, kila wakati Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, itakapoleta ushauri wake, tutajitahidi kuufanyia kazi ushauri ambao unaletwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu watumishi wa Tume ya Kudumu ya Uchunguzi katika Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Waheshimiwa Wabunge, walijua kwa nini kuna watumishi ambao siyo Wanasheria.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Haki za Binadamu ina haki za kisheria na haki nyinginezo. Kwa hiyo, naamini tunahitaji Wanasheria kama tunavyohitaji wataalamu wengine, ila tutahakikisha kwamba, kunakuwa na Wanasheria wengi zaidi ili waweze kufanya kazi zao vizuri, kwa sababu mambo mengi yanahitaji tafsiri ya sheria.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuhamasisha Serikali kuridhia Mikataba mbalimbali ya kinabinadamu, tutaendelea kufanya hivyo bila kusita.

Mheshimiwa Spika, kuhusu muda wa mkataba wa ajira ya Makamishna wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na idadi ya Makamishna. Kimsingi muda wa Makamishna wa Tume kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni miaka mitatu, ambayo inaweza kuongezwa kwa miaka mitatu mingine.

Mheshimiwa Spika, kila nchi ina utaratibu wake kuhusu muda wa Makamishna wake, kulingana na mazingira yanayohusika. Kipindi cha miaka sita kinatosheleza. Hata

hivyo, Serikali itaangalia utaratibu wa kuwezesha Makamishna walioingia pamoja, kutoondoka wote kwa wakati mmoja ili Tume isiwe inaanza kazi upya kila wakati.

Mheshimiwa Spika, kuhusu idadi ya Makamishna, Serikali bado inaamini kuwa idadi ya Makamishna saba inatosheleza na uwiano wake unaridhisha. Aidha, Sheria ya Tume inaruhusu pia kuajiriwa kwa Makamishna Wasaidizi, ambao idadi yao haikutajwa. Pamoja na Makamishna, Tume inao watumishi ambao wana taaluma mbalimbali katika Sekretarieti, kwa ajili ya kufanya uchunguzi na uchambuzi wa malalamiko mbalimbali na kuwashauri Makamishna wetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maamuzi ya Tume kupata nguvu ya Kimahakama kuhusu kifungu 28(2)(3). Mpaka sasa tafsiri sahihi ya vifungu hivyo, haijatolewa ufafanuzi na Mahakama ya Rufani ya Tanzania. Baada ya Rufaa ya Kesi ya Nyamuma kuwasilishwa mbele ya Mahakama hiyo, mara watakapotoa tafsiri, hatua zinazostahili zitafuata.

Mheshimiwa Spika, nimejaribu kugusia hoja nyingi za Waheshimiwa Wabunge na zile hoja ambazo Naibu Waziri amezungumzia na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Nafikiri tutakuwa tumegusia kama si hoja za Waheshimiwa Wabunge wote, nina hakika tutakuwa tumegusa hoja nyingi. Mimi naahidi kama Mawaziri wengine na vilevile kama wewe ulivyoelekeza kwamba, tunapotoa ahadi ya kutoa maelezo hayo kwa maandishi, hatudanganyi na mimi binafsi Waziri wa Katiba na Sheria, nitahakikisha kwamba, maelezo hayo ya kimaandishi nitawapa na nitajitahidi kama inawezekana kabla ya kumaliza Kikao cha Bunge hili, tutawapa kwa sababu maelezo ndiyo haya ambayo yapo hapa, tutayatoa kwa wingi ili kila Mheshimiwa Mbunge, ayapate pamoja na wale waliouliza maswali.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hayo, sasa narudia tena kutoa shukrani zangu za dhati, kwa wale wote waliotoa hoja na wale ambao wamepigia makofi. Nawaombeni na ninawasihi kwa wale ambao maelezo hayajatosheleza, ikibidi sana, sitakataa kusimama kwenye Kamati ya Matumizi wakati wa kupitisha mafungu. Lakini hata nje ya Bunge hili, mimi niko tayari, si tu kutoa maelezo, bali kushirikiana katika kurekebisha hali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawaomba Waheshimiwa Wabunge, wapitishe mafungu yote kwenye Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru sana na ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 40 - Mahakama**

| | | |
|---|---|---|
| Kif. 1001 - *Administration and General* … … | Sh. | 13,868,050,100/= |
| Kif. 2001 - *High Court* .. … … … … … … | Sh. | 1,188,849,200/= |
| Kif. 2002 - *Court of Appeal Dar es Salaam* … | Sh. | 724,693,600/= |
| Kif. 2003 - *Arusha Zone* … … … … … … .... | Sh. | 954,130,100/= |
| Kif. 2004 - *Dar es Salaam Zone* … … … … | Sh. | 1,873,431,800/= |
| Kif. 2005 - *Dodoma Zone* … … … … … … | Sh. | 818,981,700/= |
| Kif. 2006 - *Mbeya Zone* … … … … … … | Sh. | 1,781,398,000/= |
| Kif. 2007 - *Mtwara Zone* … … … … … … | Sh. | 753,137,000/= |
| Kif. 2008 - *Mwanza Zone* … … … … … … | Sh. | 1,295,962,400/= |
| Kif. 2009 - *Tabora Zone* … … … … … … | Sh. | 1,673,712,200/= |
| Kif. 2010 - *Tanga Zone* … … … … … … | Sh. | 664,012,500/= |
| Kif. 2011 - *Primary Courts* … … … … … … | Sh. | 4,622,751,500/= |
| Kif. 2012 - *District Courts* … … … … … … | Sh. | 4,529,296,000/= |
| Kif. 2013 - *Kagera Zone* … … … … … … … | Sh. | 733,319,200/= |
| Kif. 2014 - *Ruvuma Zone* … … … … … … | Sh. | 775,270,800/= |
| Kif. 2015 - *Moshi Zone* … … … … … … … | Sh. | 708,952,900/= |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 41 – Wizara ya Katiba na Sheria**

Kif. 1001 - *Administration and General* … … … Sh. 2,277,859,400/=

**MHE. DR. WILBOD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza. Niko kwenye *Vote* 41, *Programme* ya 10, *Sub-vote* 1001, kifungu kidogo cha 250100, mshahara wa dada yangu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, mshahara ni wa Waziri sio wa dada yako. *(Kicheko)*

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo mawili madogo. La kwanza, ni la kuweka *record* sawa tu. Wakati wa kujibu hoja, Mheshimiwa Naibu Waziri, alisema suala la Mikataba haliwezekani likaletwa kwenye hadhara. Lakini nataka kusema tu Bunge si hadhara, Bunge ni chombo kinachofanya kazi kwa niaba ya wananchi na pale inapokuwa lazima Mkataba wowote ufike Bungeni, haufiki hadharani. Nadhani tumeapa na kwa hiyo, tunajua namna ya kutunza siri. Nilitaka kutoa maelezo ya kuweka sawa hiyo *record*, liweze kutolewa kwamba, je, pale ambapo Bunge linahitaji kujadili kitu fulani na ikatumika Kamati yetu ni kwa nini kauli kama hizo ziendelee kutumika? Ni mara mbili au tatu, kauli hiyo imeendelea kutumika. Tunataka kuwa na uhakika, Bunge liweze kupewa haki yake linapotaka kusimamia masuala haya ya Mikataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili katika mchango wangu asubuhi na katika mchango wa maandishi vilevile nilikuwa nimeuliza kuhusu mapendekezo mbalimbali ya marekebisho ya sheria, yaliyokwisha kupelekwa Wizarani. Kuna mapendekezo yalipelekwa yana zaidi ya miaka 10 na kuna vitu ambavyo vinagusa wananchi. Mojawapo ni hili la shilingi 100 kwa matunzo ya watoto ni la tangu miaka ya uhuru, mpaka leo matunzo ya mtoto ni shilingi 100. Mapendekezo hayo yako Wizarani kwa muda mrefu. Leo *workman's compensation,* mtu ameuawa na tembo kwa mfano, kule kwangu wanauawa wengi, mtu anapata fidia ya shilingi 50,000 na fidia ya juu sana ni 100,000, ziliwekwa miaka ya 60. Nimeuliza je, mapendekezo haya yaliyowasilishwa Wizarani na yamekaa kwa muda mrefu, sasa ni lini yataletwa Bungeni ili Bunge hili liweze kupitia sheria hizo kwa mujibu wa utaratibu na kwa mujibu wa mabadiliko ya kiuchumi, ambayo nchi yetu sasa imeingia? Nataka nipate maelezo tu.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu hoja ya Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, ambaye ni kaka yangu kweli. Mshahara wa Waziri ukienda kwake, hatutakuwa na hasara. Kuhusu Mikataba, hii nilifikiri nimeweka *record* vizuri. Kwa sababu mimi nimelitoea maelezo, nikasema kwamba, nia na madhumuni ni kuweka ile *separation of powers* na kwa hiyo kama hili linakubaliwa kimsingi, kazi ya Bunge kuhoji, bado iko pale pale ama sivyo. Mkitaka kujua juu ya Mkataba Fulani, nikasema taratibu zinatatumika ili muweze kutekeleza hilo jukumu la kuhoji kama ilivyo jukumu la Bunge na kwa hiyo, *record* hii sasa iwe sawa na kwamba, Bunge si hadhara ni kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuhusu mapendekezo yaliyoletwa na Tume ya Kurekebisha Sheria, mpaka sasa mapendekezo yameletwa mengi. Naomba hii idadi nitampa nikiwa ofisini, nimetaka niletewe lakini bahati mbaya, sikuipata mpaka nilipofika hapa. Lakini kila wanapoleta marekebisho, Serikali inayafanyia kazi. Kwa mfano, kuhusu Sheria ya Watoto na *Affiliation Act,* ile ya matunzo ya watoto ni kweli mimi kama mama na Mheshimiwa Anna M. Komu alisema kwamba, shilingi 100 kweli hata lita ya maziwa haiwezi kununua na kwa hiyo, ni ya zamani. Sasa ama tunarekebisha sheria hii ya *Affiliation* au ya matunzo ya watoto au kuna ile inayoitwa *currency points,* ambazo Waziri anaweza kila wakati kurekebisha *amount* ambayo imetajwa kwenye sheria. Kwa hiyo, naomba sana hili kwa kweli limeleta matatizo kwa wengi, lakini ni sheria ambayo iko mbioni kuletwa kwa marekebisho au kuleta sheria mpya, pamoja na hii *currency points.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuhusu *workman's compensation* ile iko Wizara ya Sheria, lakini nayo ni hivyo hivyo, inahusu *compensation* inayotolewa ni kidogo mno. Kwa hiyo, nitashirikiana na wale wengine wanaohusika, nao waongeze kasi kusudi hizi sheria ambazo tayari zimeshafanyiwa kazi na mapendekezo kuwasilishwa Wizarani, ziwasilishwe kwa marekebisho. Nafikiri kaka yangu sasa atanihurumia, watoto wangu wasife njaa. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *Vote* 41, *Programme* 10, *Sub-vote* 1001, kifungu kidogo cha 250100. Nataka nipate maelezo juu

ya usiri wa Mikataba. Ukishasema mtu aingia Mkataba na Serikali ya Tanzania, tayari ni *Public* si *Private*. Kwa hiyo, hakuna sababu kwa nini mikataba kama hiyo, ambayo inaingiwa na Serikali ya Tanzania, isiwe wazi kwa watu wote na mambo ya kushirikisha Bunge sio lazima tushirikishwe Bunge katika kikao kama hiki. Lakini Bunge pia lina Kamati mbalimbali, zinaweza zikaangalia jambo ambalo lina uzito wa Kitaifa. Sifikiri kwamba, ni vyema Bunge hili lifanywe tu kama daktari wa *post-mortem* kuwa, tunaangalia kitu kimeshaharibika. Ni vizuri kama kuna jambo ambalo linatuhusu sisi sote na Rais alisema wadau wetu ni watu wote wa *public* ya Tanzania, basi hili jambo la usiri lisije likawa kinga ya kufanya maovu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka nipate maelezo juu ya hili. Kama tumezungumza kushirikishwa, sasa hivi tunataka kushirikishwa katika kuangalia Mikataba ambayo tayari imekuwa mibovu na Serikali imesema ni mibovu ya *IPTL,* Mambo ya Madini na mambo mengine, nyumba za Serikali na vitu chungu mbovu. Kwa hiyo, hiyo ni *post-mortem*. Lakini pia kuna mambo mengine ambayo Serikali inaweza kuamua. Labda inataka kuamua kuuza reli, inataka kuamua kuuza mashamba ya Wilaya nzima au inataka kuhamisha watu kwa sababu ya madini na vitu kama hivyo. Kwa hiyo, kuna vitu ambavyo ni mtambuka. Ni vizuri kwa maoni yangu usiri huo usiwe kinga ya kufanya maovu. Nataka nipate maelezo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, sasa hili la mwisho inaonekana umetoa maoni. Umenichanganya hapo kwa sababu la kwanza linahusu usiri baada ya Serikali kuingia Mikataba, umedai upate maelezo. Hili la pili, la kusema watu washirikishwe kabla hata ya Mkataba kuingiwa, umetoa maoni. Sasa sijui, lakini namwaachia Waziri ili aweze kusema kwa yote mawili, maana yake haujaridhika inaelekea.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa John M. Cheyo, kwa kutaka apate ufafanuzi huu, pengine na wote wataelewa hili suala vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, suala la kwanza ni ule msingi wa *separation* ya *power.* Nashukuru sana imeonekana Waheshimiwa Wabunge, wamelielewa vizuri kwamba, kazi ya kuingia mikataba ndani ya Serikali ni ya *Executive,* lakini Bunge linaweza kuhoji pale ambapo linafikiri ni kwa maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuhusu kuhoji, kuna utaratibu wa Bunge ambao niliueleza kwamba, inaweza ikawa kupitia kwenye Kamati inayohusika au Kamati ambayo wewe mwenyewe utaitaka iweze kuhoji mikataba hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuhusu usiri, mimi nilikuwa Meneja Mkuu na kwa hiyo nimehusika katika mambo ya biashara. Hata mshindani wako kujua *cost per unit* au gharama ya kutengeneza bidhaa yenyewe tu, inatosha kukuondoa wewe kwenye soko. Kwa hiyo, kuna mambo mengine mengi, ambayo yanahusika kwenye hii mikataba, ambayo nasema hatuingii sisi wenyewe kwenye hiyo Mikataba, kuna nchi nyingine pengine ina maslahi na mikataba hiyo ambayo tunaingia. Kwa hiyo, kwa

kupitia taratibu zilizowekwa za Bunge, *Executive* au Serikali, haijakataa Bunge kuhoji jambo ambalo ni la manufaa kwa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuhusu ushiriki, ndiyo nasema mambo kama hayo ambayo vilevile kutawanya hayatakuwa kwa maslahi ya Taifa na kwa kuzingatia ule msingi wenyewe kwamba, kazi fulani ni ya *Executive*, kazi nyingine ni ya Bunge na kazi nyingine ni ya Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa John Cheyo kama pengine atahitaji maelezo zaidi ni kwa nini inakuwa hivyo, basi sisi wote tunaohusika ndani ya Serikali tupo tutaelezana na kama kuna haja ya majadiliano, tutaendelea mpaka hili jambo lipate muafaka. Ahsante sana.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sina matatizo na Serikali kuingia Mkataba. Tatizo ambalo naliona ni *issue* ya usiri. Hii *issue* ya usiri, *Procurement Act* yenyewe inasema, chochote Serikali itakachoingia lazima kiwe *open tender*. Sasa kama kitu kimekuwa ni *open tender*, tena tunavyoelekea kwenye hii *globalization, tender* zote hizi zinaweza kuwa hata kwenye *internet,* ili watu wote wajue kuwa huyu amesema hivi, huyu ameomba hiki, huyu ame-*tender* namna hii. Sasa *issue* ya kuwa na Mkataba na Serikali kuwa siri, kuwa watu wote wasifahamu kuna nini, inatoka wapi, *public is public* au *definition* hiyo kwa Waziri ni tofauti labda? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mimi nadhani kinachojitokeza hapa, hakiwezi kuamuliwa hapa kwenye Kamati ya Matumizi. Ni dhahiri kabisa kwamba, Waheshimiwa Wabunge, tunahitaji semina kuhusu Mikataba. Kwa sababu Mikataba ni ya aina nyingi sana. Ipo Mikataba ambayo haina wasiwasi kabisa, wala haiwezi kuwa siri, siyo tu kwa Waheshimiwa Wabunge na sio siri hata kwa wananchi. Lakini ipo Mikataba ambayo kwa aina yake, haiwezi kuwa hivyo. Sasa tukijaribu hapa kwenye Kamati ya Matumizi tufikie aina fulani ya muafaka, nadhani haitakuwa sahihi. Kwa hiyo, napendekeza kwa Mheshimiwa Waziri, katika wakati unaofaa na tusichelewe sana hili jambo lisiendelee kutupa shida, basi ifanyike semina angalau ya siku moja, watu watoe madukuduku yao. *(Makofi)*

**MHE. MANJU S. O. MSAMBYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *Vote* 41, *Programme* 10, *subvote* 1001, kifungu kidogo kabisa 250100 – Mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, alipokuwa anajibu hoja, kwanza ali-*skip* hoja yangu. Lakini alipokuwa anajibu hoja ya mirathi alieleza kwamba, atahakikisha sheria hii ya mirathi, anaichangamkia kwa kasi mpya na kubwa ili iweze kukidhi mazingira ya sasa. Lakini Mheshimiwa Waziri, wakati akijibu suala la Chifu Kadhi, amesema mambo mazuri hayataki haraka. Lakini hoja ya kuwa na Chifu Kadhi Tanzania, imeanza tangu mwaka 1998. Hivi Sera ya Serikali kuhusu suala hili, inasema uharaka au ukaribu unatakiwa uchukue muda gani?

Mheshimiwa Waziri, kwa kauli yake ameshaonesha kwamba, suala la Chifu Kadhi ni zuri. Sasa litachukua muda gani ili Watanzania hasa wale ambao wanatakiwa wafaidike na kuwa na huduma ya Chifu Kadhi, wapate huduma hiyo? Hilo ni la kwanza. La pili, naelewa kabisa, kwa Kanuni za Bunge suala likiwa Mahakamani halitakiwi kujadiliwa kwenye chombo kingine chochote mpaka hukumu ya suala hilo iwe imetolewa au suala hilo liwe limeondolewa Mahakamani. Asubuhi nilimpa Mheshimiwa Waziri *document* hii.

*(Hapa Mheshimiwa Mbunge alionesha document husika ndani ya Bunge)*

**MHE. MANJU S. O. MSAMBYA:** Sikutaka *document* hii katika kujibu aizungumzie kama inavyoshughulikiwa Mahakamani. Lakini nilitaka nielewe na bahati nzuri Mheshimiwa Job Y. Ndugai, alikuwa ameshika kiti chako, aliwatambulisha watu hapa Bungeni leo asubuhi, akataja viongozi wengi sana wa kutoka Idara ya Mahakama hapa Dodoma. Sasa suala hili liko Mahakamani Dodoma, sitaki Mheshimiwa Waziri atoe jibu kwamba, litaamuliwa hivi, litaamuliwa vile. Nataka kufahamu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri.

Hili la mirathi vile vile, nasema wazi kwamba, nina maslahi nalo, linanihusu. Kesi iko Mahakamani tangu Januari, 2003 na kwa bahati nzuri, kwenye kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri, kuna sentensi moja nzuri sana inasema: "Haki sawa kwa wote na kwa wakati." *(Makofi)*

Hivi hii haki itatolewa lini na watoto wa marehemu ambao hii dhuluma inataka kufanyika au imeshafanyika, wameibiwa fedha Benki na Benki imetoa ushirikiano?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, hebu keti kwanza. Hili la pili, siwezi kuliruhusu. Kwa sababu mahali pa kupata ufafanuzi, hapawezi kufungwa fungwa kati yenu na Waziri. Unaulizia kitu ambacho hutaki yeye ataje kesi yenyewe, asitaje wale wanaohusika ni kina nani kwa sababu itaathiri msingi mwingine. Sasa tutalizungumziaje kwenye Kamati ya Matumizi kukapata ufafanuzi? (*Makofi)*

**MHE. MANJU S. O. MSAMBYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki kubishana. Kitu ambacho nilikuwa nimefunga ni suala likiwa Mahakamani halijadiliwi Bungeni. Lakini nilikuwa naeleza *issue* hii kucheleweshwa tangu mwaka 2003.

**MWENYEKITI:** *Issue* ipi, iliyo Mahakamani?

**MHE. MANJU S. O. MSAMBYA:** Ndiyo.

**MWENYEKITI:** Alaah!

**MHE. MANJU S. O. MSAMBYA:** Samahani kidogo Mwenyekiti, mtu huyu ameandika barua kwa Msajili wa Mahakama akilalamika kucheleweshwa kwa mchakato wote. Upelelezi umekamilika, watu wa pande zote zinazohusika, wanafika Mahakamani

lakini kila siku kesi inaahirishwa wala haijaanza kuzungumzwa, ndilo nililokuwa nazungumza. Hilo la pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu …

**MWENYEKITI:** Tumalize hilo la pili kwanza. La pili bado siliruhusu.

**MHE. MANJU S. O. MSAMBYA:** Mimi nadhani nimemaliza.

**MWENYEKITI:** Wewe umemaliza lakini mimi siliruhusu. Kwa sababu linaathiri misingi muhimu kabisa. Hakuna namna yoyote tunayoweza kuendelea na jambo hilo, ila wewe mwenyewe kama mwakilishi wa wananchi na una maslahi nalo pia kama unavyosema, ukikaa na Mheshimiwa Waziri nina hakika atalifanyia kazi.

Lakini jambo lililojifunga hatuwezi kuwajua ni nani, kesi namba ngapi na haiwezi kutamkwa humu kwa maana ya kanuni zetu za Bunge, haliwezi hata kidogo kupatiwa ufafanuzi tutakuwa tunawaonea tu Serikali. Lakini la kwanza la Kadhi ni suala la Sera, naruhusu lijibiwe na ulikuwa unaanza la tatu, hilo nakuruhusu kama nalo litakuwa katika msitari.

**MHE. MANJU S. O. MSAMBYA:** Sawa. Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tatu au la pili sasa maana hilo lingine limefutwa kwa amri yako. *(Makofi/Kicheko)*

Suala la pili, Mheshimiwa Waziri alipokuwa anajibu na mimi nilieleza kwa maandishi na wengi wameeleza, watu waliohukumiwa kwa makosa ya mauaji, wamehukumiwa kunyongwa, hukumu imetolewa na bado hukumu ile haijatekelezwa. Mheshimiwa Waziri, amesema mwenye mamlaka ya kutengua hukumu ni Mheshimiwa Rais. Lakini watu hawa wamekaa jela, hukumu zimetolewa hakuna hatua inayochukuliwa. Je, Waziri au vyombo vinavyotakiwa kuchukua hatua, vimemshauri vipi Mheshimiwa Rais ili hawa watu wasiendelee kuteseka magerezani, maana wanapata adhabu mbili; wanangojea adhabu ile ambayo waliyohukumiwa, adhabu haitekelezwi. Kwa hiyo, wanakuwa na adhabu ya kisaikolojia. Ilikuwa ni hilo Mheshimiwa Mwenyekiti.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Manju S. O. Msambya, kwa kutaka ufafanuzi wa masuala mawili na lile lingine liko Mahakamani na kwa hiyo hatuwezi kuliongelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mahakama ya Kadhi, nilijitahidi sana kutokutumia neno halitaki haraka, nilitumia neno subira. Nikasema kwamba, Tume ile ya Bunge, imefanya kazi na tumeshukuru sana tumeipokea kazi iliyofanyika na suala lenyewe linahitaji kupata maoni zaidi na tutalishughulikia. Nilieleza kwenye jibu langu la awali kwamba, suala hili lipo kwenye Ilani ya Uchaguzi na kwa sababu liko kwenye Ilani ya Uchaguzil bahati nzuri muda wenyewe unajulikana kwambal katika miaka mitano hii, litashughulikiwa. Mimi pamoja na wale wote wanaohusika, tutalishughulikia na wakati muafaka ukifika, tutalileta hapa. Bado naomba subira yenu na sijasema kwamba, halihitaji haraka.

Sasa kuhusu swali la pili la watu waliohukumiwa kunyongwa na kwamba mwenye maamuzi ya mwisho ni Mheshimiwa Rais, nimelipokea, nitalifanyia kazi na nitaendelea kumshauri Mheshimiwa Rais. Lakini ni kweli mwenye maamuzi ya mwisho ni Mheshimiwa Rais.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, *Vote* 41, *Programme* 10, *subvote* 1001, *item* 250100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nikushukuru kwa kulifupisha suala la tenda, kwa sababu hata mimi nilikuwa nataka nilizungumzie, lakini nina suala lingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bunge lililopita, kwa mara ya mwisho tulipokuwa tunafanya marekebisho ya Katiba tulikuwa tunazungumzia suala la asilimia 30 ya Wabunge wa Viti Maalum Wanawake. Naomba nili-*underline* hilo. Bahati mbaya tulipomaliza kupitisha marekebisho haya tukagundua hii ilikuwa ni *oversight* ya Serikali na Wabunge, kwa hiyo ni makosa ya *oversight,* ilikuwa si kwa makusudi. Tukagundua kwamba, asilimia 30 iliyotamkwa ndani ya Katiba haikuwa asilimia 30, tulikuwa tunataka asilimia 30 ya Wabunge

**MWENYEKITI:** Samahani Mheshimiwa Mbunge, nimekusikia vizuri unasema Bunge lilikosea; ndivyo unavyosema? Sasa kama Bunge lilikosea unamhoji Waziri ufafanuzi au?

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nirudie tena, inawezekana Kiswahili changu cha Kingoni hakifai.

Nasema tulipomaliza kushughulikia Marekebisho ya Katiba, tulikuja kugundua kulikuwa na *oversight,* bahati nzuri nimetumia neno hilo kati ya Serikali na sisi Wabunge, *oversight*. Sisi Wabunge Wanawake tukamwona Waziri Mkuu aliyepita, tukasema hii asilimia 30 ukifanya marekebisho si asilimia 30. Tukafanya mahesabu, Waziri Mkuu aliyepita akakiri, kweli ilikuwa *oversight,* akatumia neno hilo hilo. Akaomba basi kwa sababu muda umekwisha, tunaomba mapema tu Bunge lijalo, tulizungumzie hili ili ile asilimia 30 ya Wabunge wa Viti Maalum ya humu kwenye Katiba haisemi asilimia 30 ya Wabunge wote, inasema asilimia 30 ya Wabunge kifungu (a) ambayo ni wa Majimbo, kifungu (c) ambao ni Wabunge wa Baraza la Wawakillishi, halafu kifungu (d) kinazungumzia Mwanasheria Mkuu, kifungu (e) kinazungumzia Wabunge walioteuliwa na Rais na kifungu (f) kinazungumzia Spika, iwapo atakuwa sio Mbunge. Kwa maana hiyo, haikuzungumzia Wabunge wote. Kwa mfano, sasa hivi tuna Wabunge 329 kama sikosei. Kwa maana hiyo kwa namba hii, inamaanisha Wabunge wa Viti Maalum kwa *total number* hii, tungekuwa na Wabunge nafikiri karibu 98 au 99, maana yake *point* saba ni zaidi ya nusu. Lakini sasa hivi tuko ..

**MWENYEKITI:** Idadi halisi Kikatiba ni 324.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** 324 Sawa. Ahsante Mwenyekiti. Kwa maana hiyo, ukifanya mahesabu sasa hivi Wabunge 75 wa Viti Maalum kwa nia ile ambayo tumeizungumzia na kwa nia ile tuliyemwona Waziri Mkuu haipo. Kwa hiyo, mimi nilikuwa naomba nisaidiwe, je, Waziri atalishughulikia kwa wakati gani?

**MWENYEKITI:** Muda umeisha. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu marekebisho ya Katiba na kwamba asilimia 30 haijafikiwa kimahesabu, tumelipokea, tutalifanyia kazi. Kama ni kweli, kwa vyovyote vile, nafikiri sitaweza kusema lingine ni kwamba, litafanyiwa kazi. Lakini naomba nitumie muda huu kusema kwamba, akina mama wala asilimia 30 haitutoshi, twendeni majimboni ili tuwe asilimia 50. *(Makofi)*

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Lakini vile vile mimi nakupongeza kwa jinsi ambavyo umetoa uamuzi mzuri, kuhusu suala hili la Mikataba kwa sababu na hilo nilikuwa nalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Vote* 41, *programme* 10, *subvote* 1001, kifungu kidogo cha 250100 – Mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nikichangia kwa mdomo hapa Bungeni, pamoja na mengine nilisema kwa uchungu sana, suala la ndugu zetu walinzi wa jadi, ambao wako katika maeneo ya Kanda ya Ziwa na Mikoa ya Magharibi hasa Mikoa ya Shinyanga, Tabora na Mwanza.

Nimezungumza kwa uchungu, watu hawa ambavyo wengi wao hasa viongozi wako magerezani, wamekamatwa baada ya vijana wao au watu wa kawaida au kundi la watu kufanya makosa katika utendaji haswa wanapopambana na majambazi au wezi wa mifugo, inatokea makosa kweli. Lakini nikasema kwamba, viongozi hawa wamewekwa ndani kwa muda mrefu, hawapelekwi Mahakamani, hawafanywi chochote, bado wamewekwa ndani kwa miaka mitano au sita. Waziri alipojibu hapa, akajibu kwamba, zipo Kamati za Wilaya za Mkoa, lakini leo ni miaka sita hizo Kamati zipo zimeshindwa na mimi nikaona mtu ambaye angeweza kusema ni Serikali, mwenyewe yuko hapa hapa.

Kama kweli hawa watu wana hatia, wangepelekwa Mahakamani, lakini kwa sababu ushahidi haupo, hawapelekwi Mahakamani. Serikali inaona kigugumizi gain, kutamka hawa watu waondolewe nje ya Mahakama, kama upelelezi utakamilika basi tunaweza kuwachukua kwa sababu ni viongozi ambao wanajulikana, wana makazi yao na wana maeneo yao watolewe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa watu wamefanya kazi nzuri sana, hakuna anayebisha kazi waliyoifanya. Tena wanafanya kazi ya kujitolea, wanajitolea na maisha. Sasa Waziri anapoturudisha tena Wilayani bila kutoa tamko la dhahiri, bado sijakubaliana naye. Naomba tamko la Serikali litoke dhahiri, ili watu hawa watolewe.

**MWENYEKITI:** Nadhani unaomba ufafanuzi, kwa nini tamko halitolewa, hudai kwenye Kamati ya Matumizi kwamba, tamko litolewe, unadai ufafanuzi. Nimekuelewa na ndiyo hilo.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana na namshukuru Mheshimiwa Lucas L. Selelii, kutetea watu wake ndiyo kazi ya Ubunge. *(Makofi)*

Sasa nilimwomba wakati ule, malalamiko haya au taarifa hizi, zipelekwe kwenye ile *Case Flow Management Committee.* Lakini zaidi ya hivyo, namwomba Mheshimiwa Lucas L. Selelii, aniletee taarifa na orodha ya hao ili tuifanyie kazi ili watu hao watendewe haki. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lucas L. Selelii hujaridhika tena?
**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli sijaridhika.
**MWENYEKITI:** Umemwelewa Mheshimiwa Waziri?

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Nimemwelewa lakini sijaridhika.

**MWENYEKITI:** Anasema waorodheshwe halafu aletewe, hili linaonekana kama zoezi maalum, nadhani baada ya hapo ndiyo tutajua jibu. Lakini sijui.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaridhika. Nimemwelewa vizuri sana. Kitu ambacho sijaridhika mimi ni mwakilishi wa Jimbo la Nzega peke yake, sio mwakilishi wa Wilaya ya Nzega, ni Jimbo la Nzega. Lakini viongozi hawa wako katika Mikoa mitatu; Shinyanga, Mwanza na Tabora, sina uhakika Musoma. Sasa je, ananipa ruhusa nikafanye kazi ya Serikali mimi! Amesema hapa hapa kazi ya Serikali ni nyingine na sisi Wabunge kazi yetu ni nyingine. Serikali ina mtandao wa kutosha wa kujua hizo taarifa wangapi wako magerezani wanajua, si wamewaweka kwenye magereza wao wenyewe! Leo mimi Mbunge wa Nzega, niende mpaka Shinyanga, Musoma, hili ndilo sijaridhika! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado nataka maelezo. Nahitaji maelezo watamke hapa hapa watu hao waondolewe.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza na mimi najiunga na Waziri wa Katiba na Sheria, kumpongeza sana Mheshimiwa Lucas L. Selelii, kwa kutetea watu wake.

Pili, Serikali tunatambua na kupongeza kazi nzuri inayofanywa na Sungusungu. Lakini hata kama tutatenda haki tukisema tutoe kauli kwamba, Sungusungu yeyote aliye na kesi leo mahakamani iondolewe, tutakuwa hatufanyi Utawala Bora na hatufuati Utawala wa Sheria. Bado tunarudi pale pale, kama Mheshimiwa Lucas L. Selelii anawajua hao wa Nzega na mwingine anawajua hao wa Shinyanga na mwingine anasema

wako Musoma, basi tuletewe orodha ile halafu tutaichambua, tutaifanyia kazi, ndipo tutakapofanya maamuzi. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 - *Finance and Accounts* … … Sh.278,822,900/=
Kif. 1003 - *Policy and Information Services* … Sh.68,557,500/=
Kif. 2001 - *Administrator General* … … Sh. 680,569,700/=
Kif. 2002 - *Public Prosection* … … Sh. 2,334,621,900/=
Kif. 2003 - *Legislative Drafting* … … Sh.544,658,200/=
Kif. 3001 - *Civil and International Affairs* … Sh.483,206,100/=
Kif. 4001 - *Constitutional Affairs* … … Sh.498,902,300/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 55 – Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora**

Kif. 1001 - *Administration and General* … Sh.2,938,178,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 59 – Tume ya Kurekebisha Sheria**

Kif. 1001 - *Administration and General…* … Sh.785,972,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 64 – Mahakama ya Biashara**

Kif.1001 - *Administration and General* .... … ... Sh.857,138,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 90 – Mahakama ya Ardhi**

Kif.1001 - *Administration and General* … … Sh.813,311,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 40 – Mahakama**

Kif. 1001 - *Administration and General* … … Sh.800,000, 000/=
Kif. 2001 - *High Court* … … … ...... Sh. 700,000,000/=
Kif. 2002 - *Court of Appeal* … … ...... .... .... Sh. 200,000,000/=
Kif. 2011 - *Primary Court* … … … ... .... Sh. 1,800,000,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2012 - *District Courts* … ... .... ...... Sh.360,001,000/=

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ukurasa wa 33 *Vote* 40, *suvote* 2012 - *District Courts* na kipengele cha 6310 - *Construction of District Court Buildings* ambayoni shilingi 360,001,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kufahamu tu ufafanuzi kwamba, wenzetu wa Tandahimba wanajengewa Mahakama mpya. Wilaya ya Tandahimba ilianza pamoja na Wilaya ya Ruangwa, Mkoani Lindi. Sasa je, kifungu hiki ni pamoja na Wilaya ya Ruangwa ambayo ilianza siku moja na Wilaya ya Tandahimba?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Fatma A. Mikidadi, kwa kutaka kujua kama Mahakama ya Wilaya ya Ruangwa itajengwa kama ilivyojengwa Mahakama ya Wilaya ya Tandahimba. Nataka kumhakikishia kwamba, kupitia maboresho ya Sekta ya Sheria au kupitia bajeti ya Serikali, Mahakama ya Wilaya ya Ruangwa itakuwa katika mpango wa kujengwa. Kama sio mwaka huu na kwa sababu amesimama, basi nitashirikiana na Mahakama kuona kwamba na Wilaya ya Ruangwa, inapata Mahakama, kwa sababu Wilaya zile mpya zinapewa kipaumbele.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuuliza swali dogo. Wakati nachangia hotuba ya Waziri asubuhi, niliongelea suala zima la ujenzi wa Mahakama ya Sikonge, *Vote* 40, *subvote* 2012 - *Districts Court,* kifungu kidogo 6310 *Construction of District Court Buiildings.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu ufafanuzi kidogo, pamoja na majibu mazuri sana aliyokuwa amejibu Mheshimiwa Waziri na amenifurahisha nilichangia mengi. Naomba ufafanuzi kidogo je, hii Mahakama ya Sikonge, kwa kipindi hiki itakuwepo au itapewa kipaumbele? Kwa sababu wananchi wanateseka sana kule Sikonge kutoka Sikonge kwenda Tabora Mjini kwa ajili ya kesi, wengi wanaachia njiani haki zao na hawawezi kupata haki kwa sababu hawana uwezo wa kusafiri kwenda huko. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri, anisaidie ufafanuzi kwa hili, je, Sikonge imo kwenye kifungu hiki? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Kabla sijamwita Mheshimiwa Waziri kujibu, nataka kuwapongezeni Waheshimiwa Wabunge, naona vitabu hivi sasa mnaanza kuvielewa. Mnakifuata kifungu, sio kushika tu mshahara.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Mwanne I. Mchemba, Mbunge wa Viti Maalum Tabora. Kwanza, kwa kunipa nafasi ya kumshukuru sana kwa michango yake mizuri na kunikumbusha suala hili, ambalo kutokana labda na ufinyu wa muda, hatukuweza kwenda Wilaya hadi Wilaya.

Katika maelelzo yangu ya awali, nilisema kwamba, sasa hivi katika kuboresha utendaji wa Mahakama, tunajenga au tunakarabati Mahakama za ngazi zote. Nia ya Serikali ni kuwa na Mahakama katika Wilaya zote. Tumeorodhesha Wilaya zile ambazo zinanufaika na maboresho ya Sekta ya Sheria lakini Mahakama vile vile ina utaratibu wake wa kila mwaka wa kuweza kujenga au kukarabati Mahakama za Wilaya. Mahakama ya Wilaya ya Sikonge, haikuwa kwenye maboresho ya Sekta ya Sheria, tutaona inaingia kwenye utaratibu ule wa Mahakama, ambao kila mwaka wanatengewa fedha za ujenzi au ukarabati wa Mahakama.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2013 – *Kagera Zone* ..... ..... ....... ....... Sh.500,000,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 41 – Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba**

Kif. 1001 - *Administration and General* .... .... Sh.11,894,140,000/=
Kif. 4001 - *Constitutional Affairs* .... ..... ...... Sh. 75,000,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa naKamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 55 – Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora**

Kif. 1001 - *Administration and General* ..... ..... Sh..260,000,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 64 - Mahakama ya Biashara**

Kif. 1001 - *Administration and General* ..... ..... Sh.233,000,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Matumizi, imepitia Makadirio ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila ya mabadiliko. Hivyo, naomba kutoa hoja kwamba, sasa Bunge lako Tukufu liyakubali Makadirio hayo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naafiki

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka 2006/2007 yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nina machache tu ya kusema. Kwanza, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Mbunge wa Kongwa. Taarifa nilizonazo na kule viwanja vya ndege nilikuwa natazama, anavyofanya kazi nimevutiwa sana na nadhani wote mmeridhika na kazi aliyoifanya.

La pili, nilikuwa naomba kufafanua tu, jana baadhi ya Mawaziri walinishangaa niliposema kwamba, tunahitaji yale majibu kwa maandishi. Nadhani wamezoea ule utaratibu kwamba, maandishi maana yake unamjibu mmoja mmoja peke yake. Kwa utaratibu mpya tulionao ni kwamba, *Hansard* inachukua yale yanayozungumzwa na ile michango iliyotolewa kwa maandishi na Ofisi ya Bunge ina haki ya kuyapata hayo

majibu. Kwa hiyo, mimi nilidhani tafsiri yake ni dhahiri kabisa kwamba, kutakuwa kama ni *matri*x, masuala yote ambayo hayakujibiwa, kutakuwa kama na kijitabu kutoka kila Wizara, kikiorodhesha yale ili yakiwa ya Wabunge wengi badala ya kumjibu mmoja mmoja itakuwa ni elimu kwetu wote, kwa sababu mjadala huo ulikuwa ni wa Bunge. Ndiyo maana nilisema tunavyotarajia kwenye Mkutano wa Tano tuweze kupata muhtsari tu wa majibu yenyewe, *in matrix form*.

Mbunge fulani aliuliza kuhusu hili, jibu lake ni hili basi. Kwa hiyo, inakuwa ni pamoja. Lakini kusema kila Mheshimiwa Waziri, atakuwa anaandika barua kwa Mbunge mmoja mmoja kwanza, Spika hatajua kwamba yamejibiwa, halafu tunaweza kuingia kwenye mgogoro kama mtu anakuja kusema hajajibiwa na Ofisi haijui kama alijibiwa. Huo ndio ufafanuzi wangu, nadhani ni kazi ya kawaida. Nimefarijika kwamba, nimeongea na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula amesema yeye kazi yake iko tayari na ataweza kuwasilisha kwa namna hii niliyoizungumza. Kwa hiyo, kwa ufafanuzi huo nadhani Waheshimiwa Mawaziri mmenielewa, hizi ndiyo taratibu mpya za ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya. Kwa hiyo, twende hivyo.

Mwisho, napenda kuwashukuru sana Mheshimiwa Kaika S. Telele, Mheshimiwa Michael L. Laizer na Mheshimiwa Christopher O. Ole-Sendeka, tuliofuatana pamoja mpaka Oldonyo Sambu na nilifurahi sana kwamba, kule kwa wenzetu waliokuwa kwenye mkutano wamefurahi kwamba, Spika hakwenda peke yake na kwa sababu tulikwenda nao, basi mimi nimefarijika sana.

Baada ya kusema hayo, sasa naliahirisha Bunge kabla ya muda wake hadi kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 01.35 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Ijuma Tarehe 28 Julai, 2006 Saa Tatu Asubuhi)*